

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Kumi – Tarehe 21 Aprili, 2022

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu!

NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI
WA UMMA NA UTAWALA BORA:**

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, (Utumishi na Utawala Bora) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

**MHE. DKT. THEA M. NTARA - K. n. y. MWENYEKITI WA
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA
MITAA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais, (Utumishi na Utawala Bora) kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, pamoja na maoni ua Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge leo ni siku ya Alhamis kwa kawaida ilikuwa tuwe na maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu leo yupo Dodoma na yupo Bungeni lakini maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu leo hayatakuwepo, kwa sababu baada ya kumaliza hotuba yake wakati ule amepata changamoto kidogo ya sauti, kwa hiyo siyo kwamba anaumwa lakini sauti yake kidogo imepotea kwa hiyo leo hataweza kuzungumza hapa ndani. Kwa hiyo tutaendelea na ratiba yetu. Katibu!

NDG. EMMANUEL MPANDA– KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 82

Hitaji la Watumishi wa Afya – Kituo cha Afya Itaka

MHE. JULIANA D. SHONZA aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka Watumishi wa Afya wa kutosha katika Kituo cha Afya cha Itaka?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI Mheshimiwa Dkt. Dugange majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuajiri na kuwapeleka watumishi katika vituo vya kutolea huduma za

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

afya kote nchini ambapo katika ajira za mwaka 2020/2021 Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi ilipelekwa watumishi 17 na kati yao watumishi Wawili walipelekwa Kituo cha Afya Itaka.

Mheshimiwa Spika, katika ajira za watumishi wa kada za afya 7,612 zilizotangazwa wiki hii, Kituo cha Afya Itaka kitapewa kipaumbele. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Juliana Shonza swali la nyongeza.

MHE. JULIANA D. SHONZA: Mheshimiwa Spika, nashukuru.

Kwanza nianze kwa kuishukuru Serikali kwa sababu imetupatia fedha zaidi ya Shilingi Milioni 300 kwa ajili ya ujenzi wa wodi za upasuaji pamoja na wodi za akina mama katika kituo cha afya cha Itaka.

Je, Serikali sasa inatuhakikishieje kwamba ujenzi huu utakapokamilika watatupatia Daktari wa upasuaji ikizingatiwa kwamba mpaka sasa hatuna Daktari wa upasuaji lakini kituo kile cha afya cha Itaga kinahudumia Kata takribani Tano kwa maana ya Kata ya Harungu pamoja na Nambizo. Kwa hiyo nilitaka kufahamu *commitment* ya Serikali kwamba itatuletea lini Daktari wa upasuaji?

Mheshimiwa Spika, swali la pili mamlaka ya Mji mdogo wa Mlowo una wakazi takribani 100,000 lakini katika hali ya kusikitisha mpaka sasa hivi hatuna Kituo cha Afya pale na sasa hivi ninavyoongea tayari wananchi wamefyatua tofali zaidi ya 150,000 vilevile mamlaka ya Mji imetoa eneo heka kumi...

SPIKA: Mheshimiwa Juliana Shonza uliza swali.

MHE. JULIANA D. SHONZA: Mheshimiwa Spika, naomba kufahamu sasa ni lini Serikali itatuletea fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha Mlowo?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Juliana Daniel Sh onza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Shonza kwa namna ambavyo anawasemea wananchi wa Mkoa wa Songwe pia kwa namna ambavyo anaendelea kuwapa ushirikiano Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Songwe akiwepo Mheshimiwa Mwenisongole Mbunge wa Jimbo la Mbozi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa jengo la upasuaji katika Kituo cha Afya cha Itaka na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge baada ya jengo lile kukamilika tutapeleka Daktari ambaye atatoa huduma za upasuaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili kuhusiana na Kata ya Mlowo kuwa na wananchi wengi na haina kituo cha afya nina imani kwamba Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo aliwasilisha vipaumbele vya Kata Tatu za kimkakati nasi tutakwenda kufanya tathmini na kuona kama Mlowo iko katika orodha hiyo basi tutatafuta fedha ili tuweze kujenga kituo cha afya. Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Minza Mjika swali la nyongeza.

MHE. MINZA S. MJIKA: Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kuuliza swali.

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Simiyu tuna Wilaya Tatu ambazo zina upungufu wa watumishi wa afya. Wilaya ya Meatu, Bariadi na Maswa.

Je, ni lini Serikali itapeleka watumishi wa kutosha?

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Minza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli katika Halmashauri hizi za Mkoa wa Simiyu kuna upungufu wa watumishi kama ilivyo kwenye Halmashauri nyingine zote hapa nchini, mpango wa Serikali ni kuendelea kuajiri watumishi kwa awamu na ndiyo maana ajira 7,612 zimetangazwa na Halmashauri hizi pia zitapewa kipaumbele katika kuwapelekea watumishi hao. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Japhet Hasunga swali la nyongeza.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri katika Kata ya Nanyara pale Songwe pana kituo cha afya ambacho kimejengwa takribani zaidi ya miaka minne sasa na hakina wafanyakazi kabisa wa kutosha.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba inapeleka wafanyakazi katika kituo hicho cha afya?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Japhet Hasunga Mbunge wa Vwawa kama ifuatavyo:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, katika kituo hiki cha Nanyara ambacho kimekamilika zaidi ya miaka Minne iliyopita kina watumishi wachache, nimhakikishie kwamba mpango ni kuhakikisha tunapeleka watumishi ambao angalau watakidhi mahitaji ya kituo cha afya na hivyo tutahakikisha tunapeleka watumishi katika kituo hiki ili waweze kutoa huduma bora za afya. Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Deus Sangu swali la nyongeza.

MHE. DEUS C. SANGU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii.

Katika Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga mpaka sasa tuna uhaba wa watumishi wa kada ya afya 660. Je, Serikali ina mpango gani wa kuleta watumishi katika kada hii ya afya?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Deus Sangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kipaumbele cha Serikali kwenye vituo vyote vya afya vilivyokamilika vinavyotoa huduma na ambavyo vinatarajiwa kuanza kutoa huduma ni kupeleka watumishi ili viweze kutoa huduma. Ndiyo maana kuna ajira ambazo zimetangazwa. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge mkakati wa Serikali ni kuhakikisha watumishi wanakwenda kwenye kituo hicho pia na tutahakikisha watumishi wanakwenda kutoa huduma za afya pale. Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava swali la nyongeza.

MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA: Mheshimiwa Spika, ahsante kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Je, ni lini Serikali itapeleka watumishi wa kutosha katika Wilaya ya Kishapu, vituo vya afya vya Mwahalanga, Dulisi na Kishapu?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika majibu yangu ya awali kwamba mkakati wa Serikali ni kuendelea kuajiri, vituo hivi vya afya ambavyo vina upungufu wa watumishi vitapelekewa watumishi kwenye ajira hii pia kwenye ajira zinazofuata. Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Pallangyo swali la nyongeza.

MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na mimi kunipa nafasi niulize swali la nyongeza nalo liko hivi.

Mheshimiwa Spika, baada ya wafadhili waliokuwa wanaendesha kituo cha afya Momela kujiondoa watumishi pia ambao walikuwa wanalipwa na wale wafadhili Afrika waliondoka. Sasa hivi huduma zimedorora; Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka watumishi na wataalam kwa ajili ya kufanya huduma zikae vizuri? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Pallangyo, Mbunge wa Arumeru Mashariki, kama ifuatavyo:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba kuna upungufu wa watumishi katika kituo hicho cha afya na nimhakikishie kwamba tutaendelea kupeleka watumishi pale ili waendeleo kutoa huduma za afya na tutaangalia katika ajira hizi na zinazofuata ili tuhakikishe kwamba kituo kile kinatoa huduma bora kwa wananchi.

SPIKA: Mheshimiwa Anatropia Theonest, swali la nyongeza.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Halmashauri ya Kyerwa ina vituo vya afya Vitatu licha ya kuwa na wakazi zaidi ya 600,000. Napenda kujua tayari kituo cha afya cha Kamuli kimekamilika changamoto imekuwa vifaatiba na Madaktari.

Ni lini madaktari watapelekwa ili hicho kituo kiweze kuongezeka na kusaidia kupunguza adha kwa wananchi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Anatropia Theonest Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vituo vyote ambavyo vimekamilika na ndio maana jana wakati tunapitisha bajeti hapa tunashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kupitisha bajeti ya Wizara hii ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI ambayo kwa kiasi kikubwa kwenye sekta ya afya tumeweka ununuzi wa vifaatiba pia na ajira za watumishi.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika kituo hiki cha afya katika Halmashauri ya Kyerwa pia tutahakikisha kinapata vifaatiba na watumishi ili kianze kutoa huduma bora zaidi za afya kwa wananchi. *(Makofi)*

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mheshimiwa Agnes Hokororo swali la nyongeza.

MHE. AGNES E. HOKORORO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Serikali ina mpango gani wa kupeleka watumishi katika kituo cha afya Lukuledi ambacho kinakamilika ambacho kitahudumia Kata zaidi ya Tano?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Agnes Hokororo Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kituo cha afya hiki cha Lukuledi ambacho amekitaja Mheshimiwa Mbunge ni miongoni mwa vituo ambavyo vitapelekewa watumishi ili viendelee kutoa huduma bora za afya. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakipa kipaumbele kituo cha afya hiki?

SPIKA: Mheshimiwa Yahaya Massare swali la nyongeza.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Bajeti iliyopita tulipitisha kwamba tutajengewa hospitali 28 za Halmashauri, mojawapo ikiwa Halmashauri yangu ya Itigi. Je, ni lini sasa Serikali itapeleka pesa katika ujenzi wa hospitali hiyo ya Wilaya?

SPIKA: Swali la msingi linahusu watumishi sasa Mheshimiwa Massare ninakupa nafasi uliza kuhusu watumishi kwenye Jimbo lako.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kipo Kituo cha afya Rungwa ambacho tunaendelea na ujenzi na hakijasajiliwa kama kituo cha afya na watumishi ni wa zahanati. Je, sasa Serikali iko tayari kupeleka watumishi kwa Kituo hiki cha Afya cha Rungwa?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Yahaya Massare, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kituo hiki cha afya ambacho kinaendelea na ujenzi baada ya kukamilika tutafanya mpango wa kuhakikisha kwamba tunapeleka watumishi ili kianze kutoa huduma za afya. Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi Mbunge wa Malinyi sasa aulize swali lake.

Na. 83

Ujenzi wa Barabara wa Lupiro – Malinyi – Kilosa kwa Mpepo – Londo Mpaka Lumecha KM 296

MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itajenga walau kilometa chache barabara ya Lupiro – Malinyi – Kilosa kwa Mpepo – Londo mpaka Lumecha kilometa 296?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi Mbunge wa Malinyi, kama ifuatavyo: -

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, Serikali imepokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge na itaanza kujenga kilometa chache chache za barabara ya Lupiro – Malinyi – Kilosa kwa Mpepo hadi Londo mpaka Lumecha yenye urefu wa kilometa 296 hasa kwa kuanza na maeneo korofi ili barabara hii iweze kupitika kwa urahisi wakati wote wa mwaka. Aidha, Serikali itaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

SPIKA: Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi swali la nyongeza.

MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali lakini barabara hiyo ambayo anaizungumzia kwa sasa kuna dharura kwa maana ya mawasiliano yamekatika baina ya Malinyi na Morogoro Mjini.

Je, Wizara iko tayari kuiongezea *TANROADS* Mkoa fedha na kuielekeza ku-*attend* dharura hii? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi Mbunge wa Malinyi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara ya Malinyi ni kati ya wilaya ambazo ziko chini na hii barabara mvua nyingi zinazonyesha milimani zinapita huko, kwa hiyo kuna changamoto kubwa ya mvua kupita juu ya barabara. Kwa kulitambua hilo nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Serikali imeliona na mpango kwanza ni kuongeza fedha kwa maana ya bajeti ili tuweze kuinua hiyo barabara na kuongeza makalavati sehemu ambazo maji mengi yanapita. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Cecil Mwambe swali la nyongeza.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Barabara ya Lupio – Malinyi- Kilosa kwa Mpepo- Londo mpaka Lumecha ina umuhimu sana sawasawa na ilivyo barabara ya Masasi -Nachingwea - Liwale- Lupilo - Malinyi mpaka Kilosa inaunganisha Mkoa wa Lindi na Mtwara. Nini mkakati wa Serikali kuunganisha kipande hiki cha barabara ili kuwasaidia wakazi wa Mkoa wa Mtwara na Lindi kufika Dodoma kirahisi? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cecil Mwambe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara hii iko kwenye mpango wa Serikali kuijenga, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kadri Serikali inavyopata fedha barabara hii itajengwa ili kurahisisha mawasiliano kati ya Wilaya hizo mbili. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Dennis Londo swali la nyongeza.

MHE. DENNIS L. LONDO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, barabara hii ya Londo -Lumecha ni muhimu sana lakini inayofanana na barabara ya Londo ni barabara ya kutoka Kilosa mpaka Ulaya kwenda Mikumi.

Je, ni lini Serikali inaenda kuanza ujenzi wa barabara hii? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dennis Londo, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara hii ilishaanza kujengwa na tuna mpango wa kuendeleza. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba azma ya Serikali ni kuunganisha barabara inayounganisha barabara ya Dodoma – Morogoro kwenda Mikumi ili iweze kujengwa yote kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mipango ipo na bado tutaendelea kuikamilisha hiyo barabara kwa kiwango cha lami. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mrisho Gambo swali la nyongeza.

MHE. MRISHO M. GAMBO: Mheshimiwa Spika, kwa sababu changamoto ya barabara kwenye Jimbo la Malinyi inafanana na changamoto ya barabara kwenye Jimbo la Arusha Mjini. Naomba kuuliza swali kwa Mheshimiwa Naibu Waziri. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara kutoka kwenye *airport* ya Kisongo mpaka eneo la Kilombero kwa sababu barabara hiyo inasababisha mafuriko sana kwenye Kata ya *Unga Limited*, Osinyai na Sombetini?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mrisho Gambo, Mbunge wa Arusha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya kutoka Kisongo kwenda Kilombero ni barabara ambayo ipo kwenye mpango na tayari usanifu unaendelea ili kukamilisha na kuweza kuijenga kwa kiwango cha lami na kuondoa changamoto kwa wakazi wa Arusha ambayo wanaipata sasa hivi. Ahsante.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Kingu, swali la nyongeza.

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naomba kujua ni lini Serikali itatekeleza ujenzi wa Barabara ya Singida- Sepuka-Ndago mpaka Kizaga yenye urefu wa kilomita 95 ambayo imeahidiwa kwenye Ilani zote za Uchaguzi 2015 -2020 na 2020 - 2025 lakini mpaka leo barabara hii halijaanza?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kingu, Mbunge wa Singida, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoiandisha ni kweli imeainishwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi na ni azma ya Serikali kuijenga hii barabara kwa kiwango cha lami kama ilivyoahidiwa. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mipango ipo na katika utekelezaji wa Ilani wa miaka hii mitano nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii itajengwa kadiri fedha itakavyopatikana. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Daniel Sillo Baren, swali la nyongeza.

MHE. DANIEL B. SILLO: Mheshimiwa Spika, ahsante; je, Serikali itaanza lini ujenzi wa Barabara ya Dareda - Bashnet mpaka Dongobesh kwa kiwango cha lami?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

nyongeza la Mheshimiwa Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara hii iko kwenye mpango na naomba tu tusebiri bajeti kwamba barabara hii Dareda - Dongobesh Serikali ina mpango wa kujenga kwa kiwango cha lami. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Cecilia Paresso, swali la nyongeza.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kumekuwa na ahadi ya muda mrefu sana ya ujenzi wa kiwango cha lami barabara ya kutoka njia panda Oldiani-Mangola mpaka Matala Lalago ambayo inaunganisha Mkoa wa Arusha na Mkoa wa Simiyu.

Je, ni lini Serikali angalau hata kwa vipande itaanza kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara hii itaanza kujengwa kwa vipande, lakini barabara itakayoanza kujengwa ni ya Babati kuja Mbulu - Hydrom kwenda Sibiti kwa kiwango cha lami na tutaanza sehemu ya Mbulu kuja Hydrom na hiyo aliyoitaja tutaanza baada ya muda kwa sababu ni barabara ambayo zinaenda *parallel*. Kwa hiyo tumeamua tuanze kwanza hii ya Babati - Mbulu - Hydrom kwenda Sibiti halafu barabara aliyoitaja itafuata. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Daniel Awack, swali la nyongeza.

MHE. DANIEL A. TLEMAI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Barabara aliyoitaja ya Mbulu- Singida ni tofauti na barabara ambayo ameuliza muuliza swali ambayo inatoka njia panda ambayo inaelekea Mangola ambayo inaelekea Matala ambayo inaelekea Lalago ambayo pia imeunganisha Mkoa wa Arusha na Mkoa wa Simiyu. Sasa ni lini Serikali itatoa majibu sahihi ya barabara hiyo kuanza kama alivyotoa majibu ya barabara ya Mbulu-Singida?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Awack, Mbunge wa Babati, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ziko barabara mbili ambazo nazifahamu kutokea Babati. Aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge na niliyoitaja ni barabara ambazo zinakwenda *parallel* na zinakwenda kukutana mbele. Nimesema Serikali imeamua kujenga kwanza Barabara ya Serengeti *bypass* ambayo inaanzia Babati – Mbulu - Haydom kwenda Sibiti. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya kuanzia Ifakara -Kihansi- Madeke mpaka Njombe? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum Morogoro, kama ifuatavyo:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja Serikali itaanza kujenga kadiri fedha itakapopatikana. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Shaaban Shekilindi, swali la nyongeza.

MHE. SHABAN O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Kwanza nishukuru Serikali kwa kututengea fedha za nusu kilomita kwa Barabara ya Magamba kwenda Mlalo na Barabara ya kutoka Magamba kwenda Mlola. Hata hivyo, mara nyingi tumekuwa tukiomba kwamba tuongezewe kilometa tano, je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza kilometa tano ambazo tumeziomba? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shekilindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara hii tumeamua kujenga kwa awamu na naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kupitia Ofisi ya Meneja wa *TANROAD* wa Mkoa wa Tanga, barabara hii tutaenda kujenga kwa awamu kadiri fedha zitakapopatikana. Kwa hiyo tutaendelea kujenga kwa vipande vipande mpaka tukamilishe hizo kilomita tano. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Vita Kawawa swali la nyongeza.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Mheshimiwa Naibu Waziri alikuja kuitembelea Barabara yetu ya Mtwara Pachani - Nalasi na tulitoa ushauri kwamba kuna sehemu ya vipande vipande ambavyo ndivyo korofi vinasababisha watu kulala njiani. Je, Serikali ushauri wetu wa kututengenezea vile vipande korofi

wameweka utaratibu gani ambavyo havizidi hata kilomita 10, vipande vile korofi korofi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vita Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara hii nimeitembelea, barabara ambayo ndio inapita kwa wananchi. Mpango wa Serikali kama walivyoshauri Waheshimiwa Wabunge wa Jimbo hasa la Namtumbo na Tunduru tumewaagiza Meneja wa Mkoa wa Ruvuma waweze kuainisha maeneo yote korofi na madaraja korofi ili tuweze kuyatengeneza na kuondoa changamoto ya barabara hii kukatika kupitika kwa mwaka mzima.

SPIKA: Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya, swali la nyongeza.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Je, ni lini Barabara kutoka Kitai-Rwanda-Litui mpaka Ndumbi itanza kujengwa kwa kiwango cha lami?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, Mbunge wa Nyasa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara hii tayari iko kwenye hatua za awali na nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sasa hivi tunakamilisha usanifu wa kina na baada ya kukamilika usanifu wa kina kwa barabara hii ya kutoka

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Litui kwenda hadi Ndumbi na mpaka Nyasa tutaanza kujenga kwa kiwango cha lami. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaelekea kwenye Wizara ya Madini, Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mbunge wa Rorya, sasa aulize swali lake.

Na. 84

Uchimbaji wa Dhahabu Eneo la Utegi

MHE. JAFARI W. CHEGE aliuliza:-

Je, ni lini uchimbaji wa madini ya dhahabu utaanza katika eneo la Utegi, Tarafa ya Girango?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mbunge wa Rorya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Madini imeendelea kutoa leseni za utafutaji wa Madini nchini. Katika Eneo la Utegi kuna leseni za utafutaji wa madini za Kampuni ya *North Mara Gold Mine Limited na ABG Exploration Limited*. Kwa sasa kampuni hizi zinaendelea na utafutaji wa madini katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, uchimbaji wa madini hutegemea kukamilika kwa mafanikio kwa zoezi la utafutaji wa madini ambalo huhusisha shughuli za kijiolojia. Aidha, shughuli hizi huchukua gharama kubwa na muda mrefu. Kwa msingi huo, eneo la Utegi linatarajiwa kuanza uchimbaji baada ya utafiti

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kukamilika na kuonekana kwa mashapo yenye kutosheleza kuanzisha uchimbaji kwa faida. Aidha, Serikali kupitia Tume ya Madini inafuatilia kwa karibu shughuli za utafutaji wa madini zinazofanyika nchi nzima.

SPIKA: Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, swali la nyongeza.

MHE. JAFARI W. CHEGE: Mheshimiwa Spika, nimshukuru Waziri kwa majibu mazuri pamoja na kwamba hayajaleta sana matumaini kwa wananchi. Pamoja na majibu haya nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza nataka nijue tu kwamba pale utafiti utakapokamilika nini nafasi ya wachimbaji wadogo kupewa nafasi kuchimba madini kwenye eneo lile?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, nataka nijue maeneo yanayozunguka eneo la Utegi kama Kowak, Mika na maeneo mengine nini nafasi ya kuanza utafiti kwenye maeneo yale ili eneo litakapokamilika utafiti wa awali kwenye eneo la kwanza iendane sambamba na eneo la pili na haya maeneo mengine?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mbunge wa Jimbo la Rorya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala zima la upatikanaji wa maeneo ya machimbo ya madini kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi hutegemea kukamilika kwa utafiti. Utafiti unapokuwa umekamilika na kwa jinsi ambavyo utafiti huo huchukua gharama kubwa na kampuni zinazofanya utafiti huu ni kampuni kubwa zenye uwezo wa uchimbaji mkubwa, sisi kama Wizara tuna mamlaka ya kumegua eneo ambalo wachimbaji wadogo wanaweza wakakatiwa, waweze nao kupata maeneo yao

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ya kuchimba kama ambavyo sera yetu inasema kwamba lazima tuwape wachimbaji wadogo maeneo ya kuchimba.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, swali lake hilo la kwanza la wachimbaji wadogo kupatiwa maeneo ya kuchimba linachukuliwa kwa uzito mkubwa na tutawahakikishia kwamba watapewa maeneo.

Mheshimiwa Spika, maeneo ambayo anayazungumzia kwamba ni lini utafiti huo utakamilika na kuweza kuanza uchimbaji, ni wazi kwamba utafiti ndio utakaotupa jibu kwamba ni lini uchimbaji utanza katika maeneo hayo.

SPIKA: Mheshimiwa Kuchauka, swali la nyongeza.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kutokana na ripoti ya *GST*, Wilaya ya Liwale imeonekana kuwa na madini mengi sana ya dhahabu, kito na *sapphire*. Tayari wawekezaji wako kule na wachimbaji wadogo wameshaanza kazi, lakini Wilaya ya Liwale haina Ofisi ya Madini pale, matokeo yake wale wachimbaji wadogo na wawekezaji wengine wanakwenda Tunduru kuuzia madini. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuweka ofisi pale Liwale ili kuwarahisishia wachimbaji wadogo kupeleka madini yao Tunduru badala ya kuuzia Liwale?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kuchauka, Mbunge wa Liwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sisi Wizara ya Madini tumeendelea kujenga masoko ya madini na kuanzisha vituo vya kuuza na kununua madini katika maeneo yote yenye madini nchini. Kwa hiyo nimhakikishie kwamba ni swala la muda tu katika mzunguko wetu kadiri mapato yanavyoruhusu, tutafika huko

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Liwale na tutajenga soko na tutahakikisha kwamba wachimbaji wake walioko huko wana masoko ya kuuzia madini yao kwa bei iliyo sahihi na bila kupunjwa na mtu yeyote.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, swali la nyongeza.

MHE. IDDI K. IDDI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nataka kumuuliza Naibu Waziri kumekuwa na *RL* nyingi kwa maana ya leseni zilizoshikiliwa na Serikali katika Halmashauri ya Msalala Kata ya Ntobo. Sasa ni lini Serikali itaachia maeneo haya ili wachimbaji wadogo wadogo wa Jimbo la Msalala waweze kutumia haki yao ya msingi kuchimba katika maeneo yale?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Madini, napenda kumjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba maeneo yote yaliyoshikiliwa na Serikali au maeneo yote ambayo yameshikiliwa na kampuni kubwa za utafiti wa madini ambayo anaomba au anadai ni lini watarudishiwa wananchi. Watarudishiwa wananchi pale ambapo utafiti utakamilika au sisi tumebaini kama Wizara kwamba watumiaji wake hawana mpango wa kuyatumia na hivyo tutaweza kukaa nao na kuyarejesha Serikalini tuweze kuwekea utaratibu wa kupewa wadau au wawekezaji ambao wako tayari kuwekeza.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dunstun Kitandula, swali la nyongeza.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ili niulize swali moja dogo la nyongeza. Jiwe la rubi lenye uzito wa kilo 2.8 lipo kwenye maonyesho kwa sasa Dubai na jiwe hili linasadikika linatoka Tanzania na kwamba siku chache zijazo kutakuwa na mnada wa kuuza jiwe hili. Je, kama nchi tunanufaika vipi na mnada huo? (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Kitandula, Mbunge wa Mkuranga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli mnamo tarehe 13 Aprili, 2022 Wizara ya Madini ilipata taarifa kupitia mitandao ya kijamii kwamba kuna jiwe la madini ya rubi lenye uzito wa kilo 2.8 na ambalo linadaiwa kuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 120, sawa na zaidi ya bilioni 240 za Kitanzania ambalo limepewa jina la Bad All Hamal na ambalo linakwenda kuwekwa mnadani ndani ya siku 30 baada ya mfungo wa mwezi Mtukufu wa Ramadhan na jiwe hilo kudaiwa kwamba limetoka Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mara baada ya kupata habari hizi Wizara ya Maliasili imechukua hatua za haraka kutafuta kama habari hizi ni za kweli na kama kweli jiwe hili kweli limetoka Tanzania na kwa sababu jiwe hili limeshavuka mipaka liko kwenye nchi nyingine, taarifa hizi sasa tunazozikusanya ili tuweze kutoa taarifa sahihi katika Bunge lako Tukufu zinahusisha Nchi ya Dubai na tayari Ubalози wetu uliopo Dubai na sisi tunafanya mawasiliano kufuatilia ukweli na uhalisia wa thamani ya jiwe hili. Pia baada ya ufuatiliaji wa awali tumebaini kwamba mmiliki halali au tuseme sasa wa jiwe hilo yuko nchini Marekani katika Jimbo la California na mawasiliano naye pia tumeshafanya tangu jana. Hivyo sasa suala hili linazidi kupanua wigo wake kidiplomasia kwamba linahusisha nchi tatu; Nchi ya Tanzania, Dubai na Marekani.

Mheshimiwa Spika, nikuhakikishie tu kwamba tutakapokuwa tumepata nyaraka za usafirishaji wa jiwe hili kama kweli limetoka Tanzania tukapata nyaraka zinazoonyesha thamani na asili ya hili jiwe kwamba limetoka wapi. Tutakapokuwa tumepata na nyaraka za mauzo kati ya mmiliki wa sasa na wa hapo awali, sisi tutaleta taarifa katika Bunge lako Tukufu za uwepo wa jiwe hili na kama ni la kwetu, niwahakikishie Watanzania kwamba haki yao haitapotea sheria, kanuni na taratibu zetu zitatumika

kuhakikisha kwamba rasilimali hii inakwenda kunufaisha Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, sisi Wizara ya Madini tunaendelea kuwahakikishia Watanzania kwamba tumesimama imara kudhibiti na kusimamia rasilimali madini kwa manufaa ya nchi yetu. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Dunstan Kitandula ni Mbunge wa Mkinga, kutoka Tanga, Mheshimiwa Ally Mchungahela, swali la nyongeza.

MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Nina swali linalofanana na hilo. Kule Lupaso kwenye Kijiji cha Matemwe, kunafanyika uchimbaji: Je, Serikali inafahamu kwamba kuna uchimbaji unaendelea pale?

Je, uchimbaji ule unanufaisha vipi Halmashauri na Serikali kwa ujumla?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, naomba nikiri kwamba sina hakika na tuko tayari baada ya Bunge hili nikutane na Mheshimiwa Mbunge na watendaji wetu tuweze kujua na kufuatilia kuhusu machimbo hayo. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, tunakushukuru kwa majibu hayo kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Sasa Waheshimiwa Wabunge, tunaenda Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 85

Mpango wa Kuzalisha Mbegu Bora za Parachichi

MHE. SHALLY J. RAYMOND aliuliza:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Je, Serikali ina mpango gani wa kuzalisha Mbegu bora za Parachichi aina ya Hass na kuzigawa kwa wakulima kwa bei nafuu?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli miche ya parachichi katika baadhi ya maeneo imekuwa ikiuzwa kwa bei kati ya shilingi 5,000 hadi shilingi 6,000 ambapo baadhi ya wananchi wanashindwa kumudu, kwani ekari moja inahitaji miche siyo chini ya 70 na kwa ekari 10 utahitaji shilingi 3,500,000 kwa ajili ya miche tu iwapo bei ya mche ni shilingi 5,000.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali kupitia *TAR* inatarajia kuanza uzalishaji wa miche ya parachichi milioni 20. Miche hiyo itauzwa kwa bei ya ruzuku ya chini ya shilingi 2,000. Aidha, katika kudhibiti ubora wa wazalishaji binafsi, Serikali kupitia Taasisi ya Uthibiti Ubora wa Mbegu (*TOSCI*) imeanza usajili wa wazalishaji wa miche ya parachichi nchini. Pia katika kuhakikisha usimamizi bora wa zao hili, Serikali inatarajia kuzindua mwongozo wa uzalishaji wa zao la parachichi.

SPIKA: Mheshimiwa Shally Raymond, swali la nyongeza.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa nimekuwa nikifuatilia sana mbegu za parachichi katika Bunge hili kwa kipindi kirefu; na kwa kuwa leo nimeambiwa itazalishwa miche milioni 20 ya ruzuku; na kwa kuwa wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro ikiwemo Siha, Hai, Rombo, Mwanga, Same na Moshi Vijijini, wote wanasubiri miche hiyo kwa hamu, naomba kujua, mgao wetu ni miche mingapi kwa hii awamu itakayotoka? (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa parachichi lina wadau wengi sana, naomba pia kufahamu, Serikali imejiunganishaje na wadau hao ili kupata soko la uhakika la parachichi ambalo ni *perishable*, kwa kipindi hicho ambacho kipo na kinachoendelea katika soko la nje na ndani? Naomba kufahamu. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa namna anavyowapigania wakulima wa parachichi katika Mkoa wa Kilimanjaro. Katika maswali yake; la kwanza, mgao utatokana na mahitaji. Siyo rahisi sana kutamka hapa Bungeni kwamba nitapeleka miche mingapi katika Mkoa wa Kilimanjaro, lakini mahitaji yataamua miche mingapi iende katika Mkoa wa Kilimanjaro. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge avute Subira, tukianza zoezi hili, najua tutakuwa pamoja, yale mahitaji ya wakulima Mkoa wa Kilimanjaro tutahakikisha kwamba tunayafikia ili wakulima waendeleo kulima kwa tija. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili kuhusu soko la uhakika, katika eneo ambalo tumelifanyia kazi la utafutaji wa masoko katika mazao yetu ni pamoja na parachichi. Hivi sasa tarehe 25 Novemba, 2011 Mamlaka ya Afya ya Mimea India walitupatia kibali cha kupeleka parachichi India, na hivi sasa wakulima wetu wameanza kupeleka parachichi India. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile tunauza parachichi yetu Afrika ya Kusini. Pia tunakamilisha mazungumzo na China juu ya *phytol-sanitary*, tutaanza pia kupeleka parachichi yetu pia China. Hivi sasa ninavyozungumza, wazalishaji wetu

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wadogo wadogo wameshapata masoko ya uhakika kule Hispania na Marekani pia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu masuala ya soko, soko la uhakika lipo, isipokuwa tulikuwa tuna changamoto moja ambayo tumeshai-*address* hivi sasa, ilikuwa ni lazima zao letu *li-meet international standard*, na hivi sasa tunayo maabara yetu pale Arusha ambayo tumeiboresha na hivi sasa tumepata *accreditation* ambayo ni namba 17025. Kwa hiyo, zao lolote ambalo linatoka Tanzania hivi sasa lina uhakika soko nje ya mipaka ya Tanzania. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Deo Mwanyika, swali la nyongeza.

MHE. DEODATUS P. MWANYIKA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuniona niulize swali dogo la nyongeza. Pamoja na kugawa mbegu bure ambapo tunashukuru, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba wananchi hasa wakulima wadogo wadogo wanapata utalam hasa kwenye maeneo ya dawa na magonjwa yanayoshambulia zao hili la parachichi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Deodatus Mwanyika kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema pale awali katika majibu yangu ya msingi, zao la parachichi ambalo ni dhahabu ya kijani tunalipa kipaumbele kikubwa na tunakuja na mkakati madhubuti wa kuhakikisha tunawasaidia wakulima wetu kuanzia huduma za ugani mpaka upatikanaji wa pembejeo na waweze kuzalisha kwa tija. Nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba ni zao ambalo tunalipa kipaumbele na tutahakikisha kwamba wakulima wetu wanapata elimu ya kutosha na kanuni bora za kilimo ili waweze kulima kwa tija. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mheshimiwa Neema Mwandabila, swali la nyongeza.

NEEMA G. MWANDABILA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Naibu Waziri amekiri kwamba kuna uzalishaji holela wa miche hii ya maparachichi na katika mikoa inayolima parachichi, Songwe pia ni mkoa mmoja kati ya mikoa inayolima parachichi: Ni nini mkakati wa utoaji elimu kwa wananchi na wakulima ili waweze kuepukana na hawa matapeli, wazalishaji wa hizi mbegu? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Neema Mwandabila, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kupitia mwongozo ambao tutautoa, utatoa mfumo mzima wa upatikanaji wa miche bora na yenye kuleta tija kwa wakulima wa parachichi na hivyo itaondoa changamoto iliyopo hivi sasa ambapo katika baadhi ya maeneo kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi, kuna chongomoto ya upatikana wa miche bora ya parachichi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kupitia mwongozo huu wa *TOSCI*, maana yake utakuwa ndiyo mwongozo utakaomfanya mkulima yeyote wa Tanzania ambaye anataka kulima parachichi ataufuata na itakuwa ni sehemu salama kwake kwa sababu ni taasisi ya Serikali ambayo itafanya kazi hii ya kuhakikisha kwamba wakulima wote wanapata miche bora.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Asia Halamga, swali la nyongeza.

MHE. ASIA A. HALAMGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa kumekuwa na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

changamoto kubwa sana ya upatikanaji wa mbegu za shayiri. Je, Serikali haioni sasa haja ya kuanzisha kituo cha uzalishaji wa mbegu katika shamba la *NAFCO* lililoko Wilaya ya Hanang?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, majibu kwa kifupi.

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, naomba tu kumwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba shamba la Bassotu kama Wizara, tunaligeuza kuwa ni *center of excellence* kwa ajili ya kuzalisha ngano na shairi.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Halima James Mdee, swali la yongeza.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, kigezo cha bei ya mche kinatokana na umri wa mche, kwa sababu hata sasa hivi kuna miche bora kabisa inapatikana kwa shilingi 3,000. Sasa swali langu; Serikali imetumia kigezo gani; ama itatumia kigezo gani cha umri, ili huo mche wa shilingi 2,000 usiwe tofauti na miche ya sasa ambayo inauzwa shilingi 3,000 kwa sababu umri wake ni mdogo?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Halima Mdee, mkulima wa parachichi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, zao hili la parachichi ni zao ambalo hivi sasa limeanza kukimbiliwa na wakulima wengi sana kwa sababu limeleta soko la uhakika na vilevile watu wameanza kunufaika kwa kiwango kikubwa sana.

Kuhusu suala la miche ambayo tutaizalisha, ni kweli liko suala la umri wa miche, lakini ni lazima tunanzie sehemu. Sehemu yenyewe ni kwamba, uzalishaji wetu wa miche kama nilivyosema, ni ule ambao tunaamini kabisa wakulima wa parachichi kupitia miche ambayo tutaizalisha chini ya vituo

vyetu vya *TARI*, ambavyo itakuwa ni ya ndani ya muda mfupi pia, wapate kwa bei hiyo hiyo ambapo miche ile mingine ya muda mrefu imekuwa ikiuzwa.

Mheshimiwa Spika, lengo letu kubwa ni kuhakikisha kwamba, ni lazima tuanzie sehemu, lakini mbele tutaboresha kuhakikisha ya kwamba, basi wakulima wetu wawe wana bei ambayo ni *standard*, ambayo kila mmoja anaweza akai-*afford* na mwisho wa siku tunaongeza tija katika kilimo chetu cha parachichi na hasa katika eneo ambalo Mheshimiwa Mbunge analima huko. (*Makofi*)

SPIKA: Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa wananchi wa Jimbo la Hai, wamehamasika sana kulima zao hili la parachichi na zao la kahawa: Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa ruzuku ili wakulima hawa waweze kufanya kazi hii kwa ufanisi? Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, Mbunge wa Hai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi, kutokana na umuhimu wa zao hilo la parachichi, Serikali tumedhamilia kuweka ruzuku ya kutosha ili kuwafanya wakulima waendeleo kulima kwa tija na kupata miche hii kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mkoa wa Kilimanjaro, tunashirikiana pia na wadau kama Africado na wadau wengine kama vile *KEDA* kule Rombo ambao pia kwa pamoja tunafanya kazi ya uzalishaji wa parachichi. Tumesema katika bajeti ya mwaka 2022/2023, tutazungumza

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kuhusu ruzuku ambayo tumeitenga kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wakulima hawa wanapata miche kwa bei nafuu.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na kwamba Serikali imetafuta masoko, na masoko kweli yanaonekana, lakini kuna shida kubwa sana ya vifungashio vya parachichi kwa ajili ya export. Serikali imejipangaje kujenga kiwanda kwa ajili ya kutengeneza vifungashio hivyo, kwa maana kwa sasa tunategemea Kenya ndio wanaotuletea?

SPIKA: Ahsante sana. Swali la vifungashio litajibiwa kama swali la msingi. Mheshimiwa Prof. Ndakidemi, swali la nyongeza.

MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa. Matunda ya parachichi ya kisasa hushambuliwa sana na magonjwa aina ya *fungus* na wadudu kama vile inzi wa matunda.

Je, Serikali imejipangaje kuja kusaidia wakulima kupambana na changamoto hii? (*Makofi*)

SPIKA: Hilo nalo litajibiwa kama swali la msingi. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; Mheshimiwa Ussi, Salum Pondeza Mbunge wa Chumbuni, sasa aulize swali lake.

Na. 86

Wizara ya Elimu kuwa na majengo yake Zanzibar

MHE. USSI SALUM PONDEZA aliuliza: -

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Je, ni lini Serikali itajenga majengo ya Wizara ya Elimu Zanzibar ili kutoa huduma kwa wakati na kupunguza gharama za kukodi Ofisi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge Chumbuni, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Zanzibar kuna Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, yenye majengo yake, ambayo ina Idara ya Elimu ya Juu inayoongozwa na Mkurugenzi kwa lengo la kuhakikisha kuwa wanafunzi wa elimu ya juu wanapata huduma. Vilevile, zipo Taasisi za Elimu ya Juu zinazotoa huduma kwa wanafunzi kama vile; Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Taasisi ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Karume, Taasisi ya Sayansi ya Bahari (*IMS*) na Tume ya Taifa Sayansi na Teknolojia (*COSTECH*).

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kujenga ofisi katika maeneo mbalimbali nchini kwa lengo la kusogeza huduma za elimu karibu na wananchi kulingana na upatikanaji wa fedha. Aidha, ni nia ya Serikali kuhakikisha kuwa kila Taasisi ya Umma inakuwa na majengo yake kwa lengo la kupunguza gharama za kukodi ofisi. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Ussi Pondeza, swali la nyongeza.

MHE. USSI SALUM PONDEZA: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri, kwanza nilikuwa na maswali mawili ya nyongeza. Kutokana na mpango huu ambao majibu yake

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ya Serikali ambayo ameelezea nataka nimuulize Zanzibar inanufaikaje na mradi huu wa *High Education Economic*?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, napenda kumwuliza, Serikali ina mpango gani sasa wa kuzipandisha hadhi *campus* za *UDSM* na Mwalimu Nyerere ili ziwe Chuo Kikuu ili kuondosha tatizo hili? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ussi Pondeza, Mbunge wa Chumbuni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali yetu ilipata mkopo, kutoka Benki ya Dunia wenye thamani ya zaidi ya Dola za Marekani milioni 425. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge katika mkopo huu, Serikali imetenga zaidi ya Dola milioni 20 kwa ajili ya Chuo chetu cha Taifa cha Zanzibar, kwa ajili ya uongezaji wa miundombinu pamoja na usomeshaji wa wafanyakazi katika eneo lile. Kwa hiyo, eneo hili tunakwenda kulifanyia maboresho makubwa sana kuhakikisha kwamba tunakuwa na miundombinu ya kutosha; na Zanzibar ni mnufaika mkubwa wa mikopo hii pamoja na vyuo vingine vya elimu ya juu nchini.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili, ameulizia kuhusiana na suala la kupandisha hadhi *campus* zetu. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu, hivi sasa Serikali kupitia mkopo huu wa *HIT*, tunakwenda kuboresha miundombinu katika vyuo vyetu vikuu na taasisi mbalimbali za elimu ya juu nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hatuna dhamira ya kupandisha hadhi *campus* hizi mbili pamoja na *campus* nyingine za vyuo zilizokuwepo pale mpaka miundombinu pamoja na watumishi waweze kutosheleza mahitaji tunayoyahitaji hivi sasa. Nashukuru sana. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yao kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

MHE. JERRY W. SILAA: Mheshimiwa Spika, jambo la dharura.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nilete matangazo kwenu baada ya kipindi chetu cha maswali kutoka kwa Wabunge na majibu kutoka Serikalini. Nitaanza na matangazo yanayohusu wageni waliopo hapa Bungeni. Kwanza, tunaanza na wageni walioko katika jukwaa langu.

Tunao wageni wa Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kutoka ofisi ya Rais, Utumishi, na Ofisi ya Rais Ikulu, na hawa ni Dkt. Laurean Ndumbaro, Katibu Mkuu Utumishi. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye pia Dkt. Moses Kusiluka ambaye ni Katibu Mkuu Ikulu; karibu sana. Tunaye pia Bwana Xavier Daudi, ambaye ni Naibu Katibu Mkuu, Utumishi; karibu sana. Tunaye pia CP Salum Hamduni, ambaye ni Mkurugenzi Mkuu TAKUKURU; karibu sana. Tunaye pia Mheshimiwa Jaji Sivangilwa Mwangesi ambaye ni Kamishna wa Maadili; karibu sana. Tunaye pia Brig. Gen. Andrew Chakila, ambaye ni Mratibu Msaidizi Mkuu – Baraza la Usalama la Taifa; karibu sana. Tunaye pia Mhandisi John Nzulule, ambaye ni Afisa Mtendaji Mkuu *TGFA*; karibu sana. Tunaye Bwana Mathew Kirama, ambaye ni Katibu Mtendaji Tume ya Utumishi wa Umma; karibu sana. *(Makofi)*

Hawa wameambatana na Wakurugenzi na watendaji wa waandamizi wa taasisi zilizo chini ya ofisi hiyo. Kama nao wako humu ndani, basi wanaweza kusimama; karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye Mgeni wa Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye ni msanii wa mipasho, au michambo kutoka Jiji Dar es Salaam, na huyu ni Ndugu Swalehe Jumanne Nassoro, maarufu... *(Makofi)*

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Ngoja nirudie sijamaliza kutambulisha naona ameshaka tayari, haya huyu ndugu Swalehe Jumanne Nassoro, ambaye ni msanii wa mipasho, huyu ni maarufu kama Dkt. Kumbuka Majaliwa. Karibu sana Bungeni. *(Makofi)*

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

SPIKA: Ee! Mheshimiwa Waziri Mkuu inaonekana mgeni wako maneno yake yamesikika sehemu nyingi, naona kuna watu wanamsaidia hapa ndani kusema. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, ambao ni kaka yake na Rafiki yake kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 26 wa Mheshimiwa Zuberi Kuchauka ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotokea Liwale Mkoa wa Lindi. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni nane wa Mheshimiwa Joseph Mkundi, ambao ni wanafunzi kutoka Chuo cha VETA, Mkoa wa Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, ambao ni wadogo zake kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Festo Sanga, ambaye ni mdogo wake kutoka Makete Mkoa wa Njombe. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Amsabi Mlimi, ambaye ni Mkuu wa Idara ya Mazingira, Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti ndugu Victor Rutonesha. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni ambao wamelitembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, kwanza ni wageni 85 na walimu 15

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kutoka shule ya Sekondari Mji Mpya ya Morogoro Mjini. Karibuni sana wanafunzi na walimu Bungeni, tunaamini mtapata fursa ya kujifunza. *(Makofi)*

Pia tunao wanafunzi 41 na walimu sita kutoka Shule ya Marangu *Hills Academy* ya Marangu, Kilimanjaro, wakiongozwa na Mwalimu Mkuu wa Shule h iyo Mwalimu Thomas Malulu. Karibuni sana wageni wetu Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge lipo jambo lingine la kukumbushana. Wapo Waheshimiwa Wabunge ambao wanatumia vishikwambi vya Wabunge wenzao kuwasilisha aidha hoja, maswali au michango yao ya maandishi. Sasa ukipeleka huo mchango maana yake mchango ule unatambulika kama ni wahuyo mwenye kishikwambi. Mchango unaokuwa umepeleka unaingia kwa jina la yule mwenye kishikwambi, kwa sababu vishikwambi hivi ofisi ya Bunge imevisajili kwa jina la mhusika aliyepewa.

Kwa hiyo, kama Mbunge anachangamoto na kishikwambi chake, basi azungumze na wataalam wetu ambao huwa wanazunguka humu Bungeni muda wote ili wamsaidie. Lakini usitumie kishikwambi cha Mbunge mwingine kupeleka taarifa upande wa Bunge, kwa sababu taarifa zinazokwenda huko zinaenda kama za huyo Mbunge mwenye kishikwambi ulichotumia wewe.

Hapa nimeletewa mchango wa maandishi ambao umetolewa na Mheshimiwa Mbunge kwa kutumia kishikwambi cha Mbunge mwingine. Sasa kwa sababu leo ndio nimetoa hili tangazo wacha nisiwataje, niwaache, isijeonekana wanaazimana vishikwambi humu ndani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tujizuie tusifanye hivyo kwa sababu hata maswali ukipeleka maana yake ataitwa Mbunge mwenye kishikwambi ndiyo swali litapangwa ni la kwake, kumbe ni la kwako wewe, na ukifikiri kwamba sisi tumejua kwamba ni swali lako kwa hiyo tujitahidi kufanya hivyo.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Jambo lingine ambalo napaswa kulizungumzia ni kwamba, Waheshimiwa Wabunge jana tumehitimisha bajeti ya ofisi ya Rais, TAMISEMI, na Wabunge wote hapa tumeipitisha kwa kadri ya kanuni zetu na alipata nafasi Mheshimiwa Naibu Spika ya kuwapongeza. Sasa wakati hoja ile ikiletwa mezani kuna makosa ambayo yalifanyika, makosa ya kiuchapaji, na sasa Mheshimiwa Waziri jana hapa alifanya marekebisho lakini sasa kwa mujibu wa taratibu zetu, yale marekebisho hayawezi kuingia moja kwa moja kwenye taarifa rasmi za Bunge. Kwa sababu taarifa rasmi ni Bunge ni taarifa za kudumu lazima zikae kwa usahihi ndiyo maana huwa tunakumbushwa hapa.

Kwa muktadha huo nimepokea barua kutoka kwa Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, ambaye ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, akinijulisha kwamba siku ya tarehe 14 Aprili, 2022 alipokuwa akiwasilisha hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Rais TAMISEMI kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 katika eneo la utekelezaji wa bajeti ya ofisi ya Rais TAMISEMI kwa mwaka wa fedha, 2021/2022 sehemu ya huduma za ustawi wa jamii alisomakwamba:-

Ofisi ya Rais TAMISEMI imefanya ununuzi wa pikipiki 68 aina ya boxer zenye thamani ya shilingi milioni 789.9 kwa ajili ya maafisa ustawi wa jamii.

Hivyo Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, anaomba kutoa taarifa kwamba idadi ya pikipiki 68 inayotajwa kwenye hotuba yake si sahihi na ilitokana na makosa ya kiuandishi. Usahihi ni kwamba pikipiki 68 zimenunuliwa na wadau kwa gharama shilingi milioni 227.50 ambao walikuwa wanatekeleza mradi wa *USAID* kizazi kipya katika baadhi ya halmashauri, katika mikoa 21 ambazo zilinunuliwa na kusambazwa mwezi Septemba, 2021. Kufuatia kununuliwa kwa pikipiki hizo, ofisi ya Rais TAMISEMI iliona umuhimu wa kuongeza ununuzi wa pikipiki 200 aina ya *boxer*, ambapo ununuzi upo katika hatua za mwisho; lengo ikiwa ni kutosheleza mahitaji ya maafisa ustawi wa jamii nchini. Pikipiki hizo zinanunuliwa kwa kutumia fedha za mpango wa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

maendeleo kwa ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya UVIKO - 19 ambazo zitagharimu shilingi milioni 562.40. pikipiki hizo zitasambazwa kwenye maeneo ambayo hayakupata mgao wa awali wa pikipiki.

Hivyo basi, ili Bunge letu liwe na kumbukumbu sahihi za suala hili Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, awasilishe nakala za hotuba na vitabu vya bajeti zenye marekebisho yaliyowasilishwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI. (*Makofi*)

Pia Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*) zifanyiwe marekebisho kwa kufuta kilichosemwa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, wakati akitoa hotuba yake Bungeni na kuweka maelezo haya niliyoyasoma mpaka sasa.

Kwa hiyo, kwa maagizo haya maana yake Mheshimiwa Waziri atatuletea nakala tepe ili tubadilisha zile zilizoko kwenye vishikwambi vyenu ili nanyi mkae na taarifa iliyo sahihi, lakini pia kwa upande wa Bunge tutarekebisha zile Taarifa Rasmi za Bunge kwa ajili ya vizazi vijavyo huko baadaye vitakavyokuwa vinasoma taarifa zetu ziwe zimekaa sawasawa.

Baada ya maelezo hayo, Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na ratiba yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Jerry Silaa alisimama kwamba kuna hoja ya dharura.

HOJA YA DHARURA

MHE. JERRY W. SILAA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Ninasimama kwa Kanuni ya 54 ambayo inatoa nafasi ya Bunge kusimamisha shughuli zake zilizoko kwenye ratiba kujadili jambo la dharura.

Mheshimiwa Spika, tumeona kwenye vyombo vya habari jana, na sisi wengine tumepigiwa simu na vijana wengi kutoka kwenye majimbo yetu. Lipo tangazo limetoka jana

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

linalotoa katazo la vijana wanaojishughulisha na shughuli za uendeshaji wa bado boda na bajaji kuingia katikati ya Jiji la Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vijana hawa wamejajiri, na wote tunafahamu kuwa tatizo la ajira ni tatizo kubwa kwenye nchi yetu. Vijana wanaoendesha boda boda na bajaji hawafanyi hivyo kwa kupenda bali kwa kujikimu wao na familia zao. wako Wabunge wengi humu ndani huwa wanawasemea vijana hawa, na kwenye kampeni zetu ndio wanatangulia mbele kwenye mikutano yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi niliona Mbeya wakikukaribisha, na boda boda ndio walikuwa wanaongoza msafara wako katika sherehe za kukukaribisha baada ya kuwa Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo imetokea Dar es Salaam lakini naamini tukilikalia kimya, kesho litatokea Mbeya, Arusha, Dodoma, na maeneo mengine. Nikuombe, kama itakuridhia na kama hoja hii itaungwa mkono na Wabunge, tusimamishe ratiba ya Bunge tujadili maslahi mapana ya vijana hawa.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja huwa haitolewi katika ngazi hii, tuwe tunaenda vizuri; ni mpaka nikisharidhika na maelezo yake ya awali ndipo nampa fursa ili sasa aeleze kwa upana halafu ndiyo anatoa hoja. Kwa hiyo, ngazi hii huwezi kuunga mkono hoja kabla mimi sijasema kama hilo jambo ni la dharura au hapana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge amesimama Mheshimiwa Jerry William Silaa akitupeleka kwenye Kanuni ya 54 na kwamba kuna jambo la dharura ambalo limejitokeza siku za jana, na kwa mujibu wa maelezo yake anasema yeye mwenyewe ameona kwenye chombo cha Habari kwa sababu yupo hapa Dodoma na jambo hili limetokea Jiji Dar es Salaam. Kwamba limetolewa katazo ambalo Mheshimiwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Jerry hajasema ni nani aliyetoa hili kataza la boda boda kuingia katikati ya jiji.

Sasa katikati ya jiji; hivi bado ni Jiji la Dar es Salaam au ni Jiji la Ilala likiwa Mkoani Dar es Salaam, lakini kwa hiyo sasa ametupeleka hapa akitaka Bunge tuahirishe shughuli ambazo tunazo leo ama kwa muda fulani ili tuweze kujadili hoja hii ya hawa vijana wetu ambao wamejajiri kwenye eneo hili la kuendesha boda boda. Kanuni yetu ya 54 huwa inabidi isomewe pamoja na kanuni ya 55 kwa sababu ndiyo inayoweka masharti ya jambo hilo kuona kama jambo hilo ni la dharura au hapana. Sasa masharti hayo sitayasoma, lakini labda niwasomee Fasili ya Nne ya Kanuni ya 55 inasema jambo lolote litahesabiwa kuwa ni lenye maslahi kwa umma iwapo utatuzi wake unategemea hatua zaidi kuliko zile za utekelezaji wa kawaida wa sheria peke yake.

Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Waziri Mkuu yuko hapa, kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni lakini pia mtendaji huko kwenye Serikali, Waheshimiwa Mawaziri mko hapa jambo hili mlíchukue, kwa sababu kama mmeweka katazo; tunafahamu makatazo huwa yako mengi, Mbunge wa Kigoma, Mheshimiwa Assa Mekanika pia alinieleza kwamba kule kwao kuna magari fulani hivi ya usafiri yamekatazwa kutumika kwa sababu sijajua sababu vizuri lakini ni kwamba hayo ndiyo magari yanayoweza kutumika kwa barabara za Kigoma. Sasa magari kama hayo nayo yamewekewa katazo. *(Makofi)*

Nadhani Waheshimiwa Wabunge tukubaliane jambo hili Serikali ikalifanyie kazi kwa upana wake kwa maeneo yote ambayo yametolewa makatazo. Kwa hiyo, kwa upande wa Dar es Salaam katazo hilo la boda boda lakini pia upande wa Kigoma nimeambiwa hayo magari yale madogo kabisa, yanaitwa mchomoko, kitu kama hicho; yamekatazwa, sasa kule hakuna usafiri mwingine zaidi ya hayo magari. Sasa ukiweka katazo unataka wananchi wasafiri kwa namna gani.

Kwa hiyo, hayo yote mawili myatazame na pia mwongozo mtakatoa utaleta mwelekeo mzuri wa maeneo

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mengine, makatazo ya namna yanavyotolewa basi kuwe na taarifa fulani hivi ambazo sisi wawakilishi wa wananchi tutakuwa tunazielewa wote kwa pamoja kwa sababu tunatamani wananchi wetu waendeleo na shughuli zao za maendeleo lakini wakati huo huo kama Serikali kuna jambo inataka kulifanya kwenye hayo maeneo ambayo itahatarisha usalama wa hawa watu basi tunaweza pia kuelezana kuliko kuchukua tu haya maamuzi wakati mbadala haujapatikana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Serikali mlichukue hilo, Mheshimiwa Jerry Silaa, hili litafanyiwa kazi kwa utaratibu wa kawaida kwa hiyo siyo jambo la dharura.

Katibu!

NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais ,
Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa
Mwaka wa Fedha 2022/2023**

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja za Serikali; nimuite sasa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Jenista Joakim Muhagama.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA
UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika...

*(Hapa Wabunge walimshangilia Mhe. Jenista J. Muhagama
– Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa
Umma na Utawala Bora)*

SPIKA: Mheshimiwa Jenista inaonekana hii hotuba yako Waheshimiwa Wabunge wameshasoma wameshaelewa na wanataka kuipitisha leo. Karibu Mheshimiwa Jenista. *(Kicheko)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kuiunga mkono hatuba yetu kabla sijamaliza kuisoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Usemi iliyochoambua ofisi ya Rais ya Ikulu, Sekretarieti ya Maadili ya Umma, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, Tume ya Utumishi wa Umma na Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka ya Taifa, Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, aidha naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Mpango wa Utekelezaji na Makadirio ya Fedha kwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kutujalia afya njema. Ninaomba pia kumshukuru sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Imani yake kubwa kwangu kwa kuiteua kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, pia namshukuru sana kwa Imani yake kwa Mheshimiwa Deogratius Ndejembu, kwa kumteua kuwa Naibu Waziri na kuendelea kufanya kazi ndani ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, namshukuru pia Mheshimiwa Rais kwa safu nzuri ya watendaji wa Serikali ndani ya ofisi yangu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu Samia Suluhu Hassan kwa kutimiza mwaka mmoja wa utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa mafanikio makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amedhihirisha kwamba yeye ni kiongozi bora, muadilifu, mzalendo, mchapa kazi, mcha Mungu na mwenye nia na maono makubwa ya kuleta ustawi wa Taifa na maendeleo kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ameonesha dhamira na nia thabiti ya kuboresha Utumishi wa Umma nchini na Utawala Bora, kwani hata alipohutubia Bunge la Kumi na na Mbili kwa mara ya kwanza alisisitiza kuwa Serikali anayoiongoza itaendelea jitihada za kuimarisha maadili, nidhamu, uzalendo, uchapakazi na uwajibikaji katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, naomba nirejee kuwa alitoa ahadi ya kusimamia haki na stahiki za Watumishi wa Umma na Watendaji serikalini ili kuongeza ari ya kufanya kazi kwa bidii na kukuza uwajibikaji wa hiari katika Utumishi wa Umma. Ofisi ya Rais yangu na watendaji wote tunaendelea kumthibitishia Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba tutaendelea kusimama na kutembea katika maono hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa namna anavyomsaidia Rais. Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa uongozi wake shupavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kusimamia na kuratibu kazi za kila siku za Serikali na utendaji wa Serikali Bungeni. *(Makofi)*

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, naomba kwa dhati kabisa nikupongeze wewe mwenyewe kwa kuwa mwanamke wa pili kushika uongozi wa Mhimili huu wa Bunge. Pia, nampongeza sana Naibu Spika ambaye ameungana nawe kuchaguliwa kwa kishindo kikubwa mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza wenyeviti wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nawapongeza wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Bunge, Katibu wa Bunge pamoja na watumishi wote wa Bunge kwa ustadi mkubwa wa kusaidia kuendesha Bunge letu tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu ya Awamu ya Sita inaendelea kufanya kazi kwa umoja, hivyo kwa namna ya pekee sana niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri wenzangu wote, Naibu Mawaziri na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais ili kuweza kumsaidia. Kipekee namshukuru Mheshimiwa George Mkuchika Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais pamoja na Mheshimiwa Innocent Bashungwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa mashauriano na mashirikiano yao makubwa kwangu ndani ya Ofisi ya Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa dhati naishukuru sana tena sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya USEMI chini ya Mwenyekiti wake mahiri kabisa Mheshimiwa Abdallah Chaurembo, Mbunge wa Mbagala na Makamu wake Mheshimiwa Dennis Londo, Mbunge wa Mikumi, pamoja na Wajumbe wote wa Kamati kwa ushirikiano na maelekezo na ushauri wao ambao wamekuwa wakiutoa kwa Wizara yangu, kwa Makadirio ya Fedha na utekelezaji wake kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na Mpango wa Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Nawashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii adhimu kumshukuru Balozi Hussein Katanga - Katibu Mkuu Kiongozi, nimshukuru pia Dkt. Kusiluka - Katibu Mkuu - Ikulu; Dkt. Laurean Ndumbaro - Katibu Mkuu Ofisi ya Rais,

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Menejimenti ya Utumishi wa Umma na ndugu yangu, Ndugu Xavier Daudi - Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Niwashukuru pia Makamishna, Watendaji Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi na Watumishi wote Ofisi ya Rais, Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kazi nzuri ambazo wameendelea kuzifanya kwa ustawi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kuwashukuru sana waajiri wote wa Taasisi zote na Mashirika yote ya Umma nchini na Watumishi wa Umma kwa kuendelea kutekeleza wajibu wao kwa ufanisi, uzalendo pamoja na imani yao kwa uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita ambao umeiwezesha Serikali kutekeleza majukumu yake ya kuwahudumia wananchi.

Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Peramiho, kwa kuendelea kunipa ushirikiano wakati wote ninapoendelea kuwawakilisha. Vile vile, naishukuru familia yangu kwa ushirikiano kwa sala na maombi yao kwangu katika kutekeleza majukumu haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 tuliwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, maombi ya fedha kwa ajili ya kutekeleza mipango inayoiwezesha Ofisi yangu kukidhi mazingatio ya kiseru na ya kimkakati.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tupo mbele ya Bunge lako Tukufu ili kutoa Taarifa ya Utekelezaji wa shughuli zilizoombewa fedha kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na kuwasilisha mapendekezo ya Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mafungu yote niliyoyataja kwa mwaka wa fedha 2021/2022 iliidhinishiwa jumla ya shilingi 727,932,861,000 ikiwa shilingi 544,574,460,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 183,358,401,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. *(Makofi)*

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, ninaomba Kiti chako kiridhie kutokana na muda nisisome utekelezaji wote wa kazi za Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Hata hivyo, kwa kuwa Ofisi yangu ndiyo yenye dhamana ya kuomba fedha ili kuwezesha utendaji kazi wa kila siku wa Ofisi ya Rais Ikulu pamoja na kusimamia masuala ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ujumla. Ninaomba nieleze mafanikio na mageuzi makubwa japo machache kwa uchache kati ya mengi yaliyosimamiwa na Ofisi ya Rais, Ikulu kwa kuongozwa na Mheshimiwa Rais mwenyewe na utekelezaji wa Ofisi yangu kwenye masuala ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka, 2021/2022 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia kupitia uongozi wa Rais utalii umeweza kuongezeka sana katika Taifa letu na hivi karibuni tumeshuhudia juhudi kubwa ya Rais ya kukuza utalii kupitia Filamu yetu mpya ya *Royal Tour*.

Vilevile, tumeshuhudia kupitia uongozi wa Rais mahusiano ya kidiplomasia na hasa katika Uchumi na Mahusiano ya Kikanda vimeimarishwa kwa kiasi kikubwa. Tumeshuhudia uwekezaji na uingizaji wa mitaji mikubwa nchini ili kuongeza fursa za ajira umeongezeka. Tumeshuhudia demokrasia imeweza kuimarika katika Taifa letu na mapambano dhini ya Ugonjwa wa COVID – 19 yameweza kuimarishwa. Tumeweza kuimarisha miundombinu ya huduma za kijamii na kiuchumi kote nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo yote mapambano dhidi ya rushwa yameonesha kuimarika, ambapo kwa mujibu wa taarifa ya *Transparency International* ya Mwaka, 2021 iliyotoka mwezi Februari, 2022 kupitia kiashiria cha *Corruption Perception Index* inaonesha kuwa Tanzania imeendelea kufanya vizuri kwa kushika nafasi ya 87 kati ya nchi 180, ikiwa imepanda kwa nafasi Saba ikilinganishwa na nafasi ya 94 ya mwaka, 2020. Kwa mafanikio haya Tanzania imeshika nafasi ya Pili kwa mapambano dhidi ya rushwa kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, pia, utafiti wa *World Justice Project* iliyotumia kiashiria cha *The Rule of Law Index*, inaonesha kuwa mwaka 2020 Tanzania iliendelea kufanya vizuri kwa mwaka wa pili mfululizo, katika kudhibiti matumizi mabaya ya madaraka kwenye mihimili ya Utawala, Mahakama na Bunge. Kushika nafasi ya 93 kati ya nchi 128 duniani ikiwa ni nchi ya kwanza kwa nchi za Afrika Mashariki na nafasi ya 13 kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Mheshimiwa Spika, Vilevile, utafiti wa Taasisi binafsi ya *Research on Poverty Alleviation (REPOA)* ulitolewa mwaka, 2022 unaonesha Tanzania inafanya vizuri katika kukabiliana na tatizo la rushwa. Serikali kupitia *TASAF* imeendelea na kazi ya utambuzi wa kaya masikini, uhaulishaji wa fedha za ukuzaji wa uchumi katika kaya ili kupunguza umasikini wa kipato, kuinua ubora wa maisha na ustawi wa jamii na utawala bora pamoja na uwajibikaji. Mpaka kufikia mwezi Machi, 2022 jumla ya kaya 1,992 zenye watu 9,960 zimejitoa kwa hiari katika mpango wa *TASAF* baada ya kuhitimu na kaya 158,262 zenye watu 791,310 zinaendelea kujihitimisha katika kipindi cha kukua kiuchumi kupitia *TASAF* na kuanzia mwezi Mei 2022 watapewa miezi sita ya kusubiri kuondolewa kwenye mpango wa *TASAF*, hizo ni juhudi kubwa za Serikali kupitia Ofisi ya Rais. (*Makoff*)

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha uwajibikaji wa hiari pamoja na kuzingatia haki na stahiki za Watumishi wa Umma, Serikali kupitia bajeti ya mwaka, 2021/2022 imefanya mambo makubwa kati ya hayo ni pamoja na haya nitakayoyasema:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imepandisha madaraja na vyeo watumishi 190,781 wenye sifa stahiki, Serikali imeshatoa kibali kingine kabla ya Mwaka wa Fedha, 2021/2022 haujaisha itapandisha vyeo na madaraja watumishi wengine 92,619;

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshalipa madeni na malimbikizo ya mishahara ya watumishi 65,394;

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imeweza kuwabadilisha kada na vyeo watumishi 19,386. Kabla ya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mwaka wa Fedha wa 2021/2022 haujaisha itawabadilisha kada na vyeo watumishi wengine 6,026 na kufanya jumla ya watumishi 25,412 ambao watabadilishwa vyeo na kada zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali katika mwaka wa fedha 2021/2022 imetoa kibali cha ajira za watumishi 44,096 ambapo ajira mpya ambazo zimekwishatolewa mpaka sasa ni 11,492 na Serikali imekwisha kutangaza ajira nyingine 32,604 ambazo utaratibu wa ajira umeanza na utakamilika kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha 2021/2022 na ninasema ni mwezi Juni, 2022.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele kwa nafasi hizo kimewekwa kwenye elimu, afya pamoja na sekta nyingine muhimu zenye uhitaji. Tumeshuhudia katika kipindi hiki kilichopita Serikali pia imepunguza kodi ya mishahara *(PAYE)* kutoka asilimia Tisa mpaka asilimia Nane.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2022/2023 una mambo mengi muhimu ya kuzingatiwa. Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023, umezingatia nyaraka muhimu za Serikali, ikiwemo Dira ya Maendeleo, Ilani ya Uchaguzi na Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa nitoe taarifa ndani ya Bunge lako Tukufu kwa Mpango huu wa mwaka 2022/2023, nieleze katika Taasisi zote na Ofisi mbalimbali ambazo ziko ndani ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Ikulu na Taasisi zake, tukianza na Ofisi ya Rais. Ikulu itaendelea kutoa ushauri kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika masuala ya muendelezo wa ujenzi wa demokrasia, siasa, uchumi, jamii, sheria, diplomasia, mawasiliano na habari, uhusiano wa kikanda, kimataifa na ushauri mwingine kwa lengo la kumsaidia Mheshimiwa Rais.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Ikulu itaendelea kuboresha Ikulu ya Chamwino kwa kujenga ukumbi wa mikutano (*multipurpose hall*) na baadhi ya ofisi ambazo zinahitajika. Ofisi ya Rais, Ikulu itaendelea kuratibu mkakati wa Kitaifa wa Tatu dhidi ya rushwa na kukamilisha mkakati mpya wa Nne wa kupambana na rushwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na haya majukumu machache niliyoyasema, Ofisi ya Rais, Ikulu imejipanga kutekeleza majukumu 19 kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na ninaomba Waheshimiwa Wabunge waangalie ukurasa wa 38 na ukurasa wa 39 wa hotuba yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) imejipanga kutekeleza majukumu yafuatayo kwa uchache: -

Mheshimiwa Spika, kwanza, itakuwa ni kuhuisha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini, Na. 11 ya mwaka, 2007 ili iendane na mazingira ya sasa ya kuzuia na kupambana na rushwa nchini.

Mheshimiwa Spika, pia itaendelea kufanya utafiti na uchambuzi wa mifumo ya utendaji na utoaji wa huduma katika sekta za umma na binafsi ili kubaini maeneo yenye mianya ya rushwa, lengo ikiwa ni kuzuia rushwa ili isitendeke.

Mheshimiwa Spika, vilevile itaendelea kufuatilia matumizi ya fedha za umma katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa fedha zinazopitishwa na Bunge kwa kuimarisha kitengo cha *Public Expenditure Tracking* ama kwa kifupi (*PET*).

Mheshimiwa Spika, TAKUKURU pia itaendelea kufanya ufuatiliaji wa kina na uchambuzi wa maboresho ya mifumo ya malipo Serikalini (*MUCE*), ili kuziba mianya ya ufujaji wa fedha za umma na rushwa katika Serikali za Mitaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, TAKUKURU itakamilisha ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu - Dodoma. TAKUKURU imejipanga

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kutekeleza majukumu 13 pamoja na hayo niliyoyasema na ninaomba Waheshimiwa Wabunge waangalie hotuba yangu ukurasa wa 40-41.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Taasisi ya Uongozi. Taasisi ya Uongozi imejipanga kutekeleza *program* maalum ya mafunzo ya uongozi kwa Wanawake Viongozi Waandamizi na Viongozi wanaochipukia. Lakini vilevile Taasisi hii imejipanga kutoa mafunzo kwa Viongozi wa Bodi za Mashirika ya Umma nchini, ili kuimarisha usimamizi na utendaji kazi wa mashirika hayo katika viwango na ubora unaotakiwa. Pamoja na kazi hizo mbili Taasisi ya Uongozi imejipanga kutekeleza majukumu 12 kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kama inavyojionesha katika ukurasa wa 41 na 42 katika hotuba yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya MKURABITA imejipanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, kuendelea na urasimishaji na uendelezaji wa biashara 7,000 katika mamlaka Saba za Serikali za Mitaa Tanzania Bara na vilevile, imejipanga kuendeleza na kurasimisha biashara katika upande wa pili wa Muungano (Zanzibar). Taasisi hii pia pamoja na kujenga vituo vya urasimishaji biashara nchini, itaendelea pia na ujenzi wa masijala za ardhi katika pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Spika, Taasisi yetu ya MKURABITA imejipanga kutekeleza majukumu 10 pamoja na haya niliyoyasema na ninaomba Waheshimiwa Wabunge kwa Mwaka huu wa Fedha, 2022/2023 waangalie ukurasa wa 43 na 44 katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*) umejipanga kufanya zoezi la utambuzi wa kaya 186,500 kwenye Mamlaka 142 za utekelezaji ambazo zimeachwa katika vijiji, mitaa na shehia kwa sababu mbalimbali. Pamoja na kutambua na kuhakiki hali za ustawi wa maisha kwa kaya za walengwa 713,350.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, *TASAF* itaendelea kuhaulisha ruzuku kwa kaya maskini 1,279,325 zilizokidhi vigezo katika kuingia katika kipindi cha pili cha Mpango. *TASAF* pia itaendelea kuunda vikundi vya kuweka na kukopa katika mamlaka 82 na jumla ya wanachama 240,000 watafikiwa.

Mheshimiwa Spika, kazi zilizopangwa kufanywa na *TASAF* zitakuwa Tisa pamoja na nilizosema na zinaenda kuonekana ukurasa wa 44 na 45 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Ndege za Serikali utaendelea na ujenzi wa awamu ya pili wa karakana ya Ndege za Serikali, katika Kiwanja cha Kimataifa cha Mwalimu Julius Nyerere. Pia utaendelea kutoa huduma za usafiri wa anga kwa Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, shughuli zilizopangwa na Wakala huu wa Ndege za Serikali, majukumu yatakuwa ni Nane kwa Mwaka wa Fedha unaokuja na majukumu hayo yameainishwa vizuri kwenye ukurasa wa 45 na 46 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza Mpango wa Mwaka wa Fedha wa 2022/2023 Fungu 20 - Ofisi ya Rais - Ikulu, inaomba kiasi cha Shilingi 29,828,203,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Aidha, Fungu 30 -Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri inaomba kiasi cha Shilingi 741,299,267,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi na Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma imeweka vipaumbele vikuu viwili ambavyo ni kuongeza matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma kwa taasisi na kwa wananchi ili kuweza kuwafikia kwa urahisi. Vilevile, imejipanga kuimarisha uwajibikaji wa pamoja miongoni mwa viongozi wa umma na hasa katika suala la viongozi kukinzana kunakopelekea shughuli za maendeleo kutokutekelezwa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Sekretarieti ya Maadili kwa Viongozi itakwenda katika maeneo ya Halmashauri kukutana

na Madiwani na Watendaji wa Halmashauri ili kuwapatia mafunzo yanayokidhi masuala ya maadili katika utendaji kazi wao wa kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge hili linatokana na migogoro mingi ya Madiwani na baadhi ya Watendaji wa Halmashauri, tuna kila sababu ya kuiondoa kwa sasa. Pamoja na majukumu haya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma imejipangia jumla ya majukumu Tisa kwa Mwaka wa Fedha, 2022/2023 kama ilivyo katika ukurasa wa 46 na ukurasa wa 47 katika hotuba yetu.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa 2022/2023 Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma imetengewa jumla ya Shilingi 12,730,049,000 kwa Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Taasisi zilizo chini yake itaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kuhakikisha kuwa utumishi wa umma unaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya utawala bora na kwamba sera, sheria, kanuni na taratibu mbalimbali za utumishi wa umma zinazingatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma itahakikisha inasimamia utawala wa watumishi wa umma, mikataba ya utendaji kazi Serikalini, orodha ya mishahara katika utumishi wa umma na maadili ya watumishi wa umma. Pia, itahakikisha mipango ya uendelezaji rasilimali watu katika utumishi wa umma inafanyika kwa ubora.

Mheshimiwa Spika, Ofisi itaandaa na kusimamia miundo, mifumo ya utendaji kazi na uboreshaji wa utoaji huduma kwa utumishi wa umma, pamoja na kuhakikisha kunakuwa na uwajibikaji wenye uwazi na uwajibikaji wa hiari. Kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma imejipanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mahitaji makubwa ya ajira nchini, Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma imepanga kutoa ajira nyingine mpya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

30,000, kwa kada mbalimbali na kuwapandisha vyeo watumishi 120,210 na kubadilisha vyeo watumishi wengine 8,080 waliotengewa nafasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo hili tunalifanya ili kukidhi kiu ya Watanzania na Waheshimiwa Wabunge ya ukosefu wa watumishi wengi katika kada zile muhimu kama afya, elimu na kada nyingine zinazotaka watumishi.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma itaendelea kuchambua na kuhakiki madai na malimbikizo ya mishahara ya watumishi wa umma na katika mwaka wa bajeti wa 2022/2023 tumetenga fedha za Kitanzania Shilingi 103,883,257,000 ili kuhakikisha kwamba malimbikizo ya mishahara kwa watumishi wa umma yanaendelea kulipwa na tunasafisha *data* zote za madai hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha utendaji kazi kwa utumishi wa umma tutaendelea kuimarisha na kuboresha miundombinu ya TEHAMA kwa ajili ya kuwezesha utendaji kazi wa mifumo mbalimbali ya kiutendaji. Tutaboresha mfumo wa mishahara, tutaboresha mfumo wa uwazi wa upimaji kazi kwa watumishi wa umma yaani *PEPMIS* na tutaboresha mfumo wa uwazi wa kimkataba kwa taasisi za Serikali na mashirika ya umma yaani *PIPMIS* na tutaendelea kuboresha mfumo wa kufanya ufuatiliaji wa hali ya utumishi na utawanyiko wake nchini. Tutaendeleza kuimarisha mfumo wa e-mrejesho ili kupata mrejesho wa utendaji kazi wa Serikali kutoka kwa watumishi na Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka huu wa fedha tutaanza kujenga mfumo mpya wa *biometric attendance*, ili ku-*control* mahudhurio ya watumishi wa umma katika maeneo mbalimbali ya kazi. Tutaendelea kuziwezesha taasisi za umma kuandaa mipango ya rasilimali watu na mipango ya urithishaji madaraka na mipango ya mafunzo, lakini vilevile tutaendelea kusimamia mikataba ya ushirikiano wa kimataifa na kikanda ili kuhakikisha kuwa watumishi wa umma

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wanapata fursa za ajira katika taasisi ambazo Tanzania ni mshiriki.

Mheshimiwa Spika, tutaendelea kukamilisha mfumo jumuisi wa ufuatiliaji na tathmini Serikalini tukishirikiana na wadau mbalimbali utakaounganisha mifumo ya ufuatiliaji na tathmini iliyoko katika taasisi zote za umma ili kuboresha utendaji kazi na uwajibikaji Serikalini. Tutaendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa tano la Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma katika kuhakikisha kwamba, ofisi yetu inapata ofisi ya kudumu eneo la Mtumba, Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma tumejipanga majukumu 48 kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Angalia ukurasa wa 47 na 53.

Mheshimiwa Spika, Chuo Cha Utumishi wa Umma kimepokea maelekezo na kujipanga kutekeleza agizo la Serikali la kutoa mafunzo ya awali (*Induction Course*) kwa watumishi wapya wote ambao watakuwa wanaingia kwenye ajira nchini kuanzia mwaka ujao wa fedha, lakini vilevile Chuo cha Utumishi wa Umma kitaendelea kupanua majengo ya *campus* kwenye maeneo mbalimbali nchini na kitajenga ukumbi wa wazi hapa Dodoma kwa ajili ya kuendeleza utoaji wa mafunzo kwa watumishi wa umma hapa Dodoma. Chuo cha Utumishi wa Umma kimejipanga kufanya majukumu 12 kwa mwaka wa fedha unaokuja. Angalia ukurasa wa 53 na 54 wa Taarifa yangu.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Serikali Mtandao itaendelea kuiunganisha mifumo ya taasisi za Serikali kwenye mfumo wa kuwezesha mifumo ya Serikali kuwasiliana na kubadilishana taarifa (*Government Enterprise Service Bus*), pia kusimamia hali ya usalama wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA Serikalini. Itaendelea kujenga mifumo itakayoboresha utoaji wa huduma wa taasisi mbalimbali za Serikali katika utumishi wa umma. Hapa tumeweka kipaumbele cha ujenzi wa mfumo wa kusimamia mikopo ya asilimia 10 katika Halmashauri zetu zote nchini.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali Mtandao wataendelea kujenga na kukamilisha mfumo wa kusimamia usambazaji wa mbolea nchini na mfumo wa taarifa za soko la ajira na vilevile mfumo wa usimamizi wa vyama vya ushirika. Mifumo hii yote tutashirikiana na Wizara na sekta husika katika kujenga. Pamoja na majukumu hayo eGA wamepangiwa majukumu mengine 10. Angalia ukurasa wa 54 na 56 wa taarifa yangu.

Mheshimiwa Spika, Watumishi *Housing Investment*. Taasisi hii imepewa jukumu la kuhakikisha inajenga nyumba 1,000 hapa Dodoma, lakini tumeiagiza taasisi hii kuweka kipaumbele cha ujenzi wa nyumba kwenye halmashauri za wilaya mpya ambazo zina mahitaji ya nyumba za watumishi ambayo ni makubwa. Vilevile taasisi hii imepewa majukumu mengine nane kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kama inavyoonekana katika ukurasa wa 56 na 57.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Fungu la Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma linaomba kuidhinishiwa jumla ya fedha za Kitanzania 47,611,581,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Sekretarieti ya Ajira itaendelea kusimamia michakato ya ajira, lakini itaendelea kuimarisha Ofisi ya Sekretarieti ya Ajira Zanzibar ili kusimamia michakato ya ajira za Muungano.

Mheshimiwa Spika, Sekretarieti ya Ajira vilevile itaanza ujenzi wa mfumo mpya wa usaili wa mchujo kwa njia ya mtandao (*Online aptitude test*). Mfumo huu Waheshimiwa Wabunge utasaidia kuondoa kadhia ya kuwakusanya watoto wa Kitanzania eneo moja na sasa *interview* za awali zitafanyika katika maeneo ya mikoa hukohuko ambako vijana wengi wa Kitanzania wapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha Sekretarieti ya Ajira itaanza ujenzi wa mfumo mwingine mpya wa kupima haiba za wasaili (*psychometric testing system*), ili

kutambua haiba na tabia za wasailiwa na kubaini uwezo unaostahili kujengwa kwa waajiriwa wapya, lakini mfumo huu hautakuwa ni kigezo cha kuwakatalia vijana wa Tanzania kupata ajira. Katika kutekeleza majukumu haya ya Sekretarieti ya Ajira nchini katika utumishi wa umma, imetengewa fedha za kitanzania shilingi 8,721,849,000 kwa Miradi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma; kwa mwaka wa fedha ofisi hii imepanga kufanya ukaguzi wa kina katika taasisi mbalimbali za Serikali na kaguzi hizo zitakuwa za kawaida na kaguzi maalum. Vilevile Tume ya Utumishi wa Umma imepanga kuandaa mfumo wa TEHAMA kwa ajili ya kuongeza ufanisi kwenye kushughulikia rufaa na ukaguzi katika rasilimali watu na kuendeleza ujenzi wa jengo la Ofisi za Tume, Makao Makuu Dodoma. Maelezo zaidi ya majukumu nane yanaonekana ukurasa wa 58 mpaka 59. Tume ya Utumishi wa Umma imepangiwa fedha za Kitanzania Sh.5,681,824,000 kwa fedha za kawaida na fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka imepangiwa kufanya kazi kubwa ya kuimarisha uhifadhi wa kumbukumbu na nyaraka katika teknolojia ya kisasa kwa kuingiza nyaraka katika mfumo wa kidijitali na kuhifadhi kumbukumbu za nyaraka katika mfumo wa kidijitali. Ili kuweza kupata maelezo zaidi ya kazi 13 ambazo zimepangwa kufanywa na Idara ya Kumbukumbu ya Nyaraka ninaomba Waheshimiwa Wabunge waende ukurasa wa 59 mpaka ukurasa wa 60 wa hotuba ya kitabu change.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Kumbukumbu ya Nyaraka za Taifa inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi 4,914,791,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, itaendelea kuimarisha uwezeshaji wa vyombo vinavyosaidia kwenye maamuzi ya nchi, usalama na kuimarisha vita dhidi ya rushwa. Maadili

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kwa viongozi wote na watumishi wa umma yanatarajiwa kujengwa na kuchangia ipasavyo kwenye ujenzi wa nchi na kuleta tija ya rasilimali watu na ufanisi katika matumizi ya rasilimali fedha na rasilimali nyingine nchini. Kati ya mambo ambayo Serikali itayapa kipaumbele ni usimamizi thabiti wa warasilimali watu na rasilimali fedha kwa kusisitiza uwajibikaji wa hiyari katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya mafungu yote yaliyo chini ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, imelenga kuwa na utumishi wa umma unaotoa huduma bora kwa haraka na staha, ukizingatia Katiba, sera, sheria, kanuni, taratibu na miongozo katika kujenga imani zaidi kwa wananchi na kuendana na kauli ya Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Amiri Jeshi Mkuu aliyoitoa tarehe 22 Aprili, wakati akihutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bunge la 12 aliposema maneno yafuatayo, naomba niyanukuu:

“Tutawapima viongozi na watumishi wa umma kwa namna wanavyotimiza majukumu yao, hatutawaonea aibu viongozi na watumishi wazembe, wezi na wabadhirifu wa mali za umma. Tutaendeleza pia na juhudi za kupambana na rushwa kwenye utumishi wa umma. Wajibu wa watumishi wa umma ni lazima uendane na haki zao”. Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, katika kuendana na wakati jitihada zaidi tutaziweka kwenye kujenga uwezo wa mifumo ya kimenejimenti na utoaji wa huduma, ikiwemo matumizi sahihi na salama ya fursa zinazopatikana katika utoaji wa huduma kwa njia ya TEHAMA ndani ya Serikali. Hivyo tunataka kujenga utumishi wa umma wa kidijitali nchini.

Mheshimiwa Spika, napenda kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa, kama Waziri mwenye dhamana ya menejimenti ya Utumishi wa Umma, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiye mwenye dhamana kuu katika ofisi yangu. Hivyo, basi amekuwa akisisitiza dhamira yake ya kushughulikia haki na maslahi ya watumishi wa umma ikiwa ni pamoja na mishahara stahiki kwa watumishi wa umma. Hivyo, kabla ya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kuomba fedha kwenye Bunge lako hili Tukufu naomba kueleza kuwa kilio cha maslahi na motisha kwa watumishi wa umma kinaangaliwa kwa jicho pendwa sana na Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Amiri Jeshi Mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza kwa kina utekelezaji wa majukumu kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na mipango ya bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, sasa naomba kuwasilisha rasmi mapendekezo ya maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kwa muhtasari, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Fungu 20 – Ofisi ya Rais, Ikulu. Matumizi ya Kawaida tunaomba jumla ya Sh.29,828,203,000.

Mheshimiwa Spika, Fungu 30 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri. Matumizi ya Kawaida tunaomba jumla ya shilingi 577,206,673,000 na Matumizi ya Miradi ya Maendeleo tunaomba jumla ya shilingi 164,092,594,000. Katika fungu hili tunaomba jumla ya fedha za Kitanzania shilingi 741,299,267,000.

Mheshimiwa Spika, Fungu 33 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Matumizi ya Kawaida tunaomba fedha za Kitanzania shilingi 9,260,049,000 na Matumizi ya Miradi ya Maendeleo tunaomba shilingi 3,470,000,000. Na jumla tunaomba shilingi 12,730,049,000.

Mheshimiwa Spika, Fungu 32 – Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Tunaomba Matumizi ya Kawaida shilingi 39,541,381,000 na Matumizi ya Miradi ya Maendeleo tunaomba shilingi 8,070,200,000. Jumla tunaomba shilingi 47,611,581,000.

Mheshimiwa Spika, Fungu 67 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma. Matumizi ya Kawaida tunaomba shilingi 5,063,849,000. Matumizi ya Miradi ya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Maendeleo tunaomba shilingi 3,658,000,000. Jumla ya fedha tunaomba shilingi 8,721,849,000.

Mheshimiwa Spika, Fungu 94 – Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma. Matumizi ya Kawaida tunaomba shilingi 5,681,824,000 na Matumizi ya Miradi ya Maendeleo tunaomba shilingi 300,000,000. Jumla tunaomba shilingi 5,981,824,000.

Mheshimiwa Spika, Fungu 04 – Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa. Matumizi ya Kawaida tunaomba shilingi 3,504,791,000 na Matumizi ya Miradi ya Maendeleo tunaomba shilingi 1,410,000,000. Jumla tunaomba jumla ya fedha ya Kitanzania shilingi 4,914,791,000.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, jumla kuu ya Bajeti ninayoiomba kwa mafungu yote yaliyoko chini ya Ofisi ya Rais Ikulu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka 2022/2023, ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jumla ya Matumizi ya Kawaida ni shilingi 670,086,770,000 na jumla ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo ni shilingi 181,000,794,000. Jumla Kuu ya Mafungu yote ni shilingi 851,087,564,000.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wenzangu, mwisho, naomba niwashukuru sana kwa ushirikiano ambao mmekuwa mkiipatia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mimi na Mheshimiwa Naibu Waziri tutaendelea kuwa wanyenyekevu kwanza kwa mamlaka na Serikali yetu, lakini vilevile kwenu Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuwa tunaamini kabisa ninyi Wabunge wenzetu mmekuwa ni wasimamizi wa karibu wa utumishi wa umma katika maeneo yenu. Tunaomba kuwakaribisha katika kila jambo la ushauri, maoni na mapendekezo; Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora itakuwa wazi kwenu ninyi Wabunge wote kwa niaba ya wananchi wote wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalize kwa kuwashukuru sana kwa kunisikiliza na naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA, MHESHIMIWA JENISTA J. MHAGAMA (MB) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2022/2023 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa iliyochambua bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu (Fungu 20 na 30); Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma (Fungu 33); Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (Fungu 32); Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma (Fungu 67); Tume ya Utumishi wa Umma (Fungu 94); na Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa (Fungu 04); Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/22. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Mpango wa Utekelezaji na Makadirio ya Fedha kwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2022/23.

2. Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kutujalia amani na utulivu ambavyovimetuwezesha kutekeleza majukumu ya kuongoza Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na kuwahudumia wananchi pamoja na kutuwezesha kukutana kwa ajili ya kupokea utekelezaji wa Ofisi yangu na kutafakari malengo yajayo katika mkutano huu wa saba wa Bunge la 12. Kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani yake kubwa kwangu kwa kuiteua kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Pia, namshukuru Rais

kwa imani yake kwa Naibu Waziri wangu Mheshimiwa Deogratus Ndejemi, Mbunge wa Jimbo la Chamwino kwa kumbakiza katika nafasi yake na ndani ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Pia, namshukuru Rais kwa safu nzuri ya Watendaji wa Ofisi yangu ambao amewaidhinisha.

3. Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii, kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kutimiza mwaka mmoja kazini kwa mafanikio makubwa ya utendaji wa kazi yanayoonekana katika sekta mbalimbali nchini. Rais wetu amedhihirisha kuwa yeye ni kiongozi bora, muadilifu, mzalendo, mchapakazi, mcha Mungu, mwenye nia na maono makubwa ya kuleta ustawi wa taifa na maendeleo kwa Watanzania.

4. Mheshimiwa Spika, naomba pia nimpongeze Rais wetu kwa azma yake ya dhati ya kuboresha Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Dhamira hiyo aliionesha wakati akilihutubia Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Aprili, 2021 mara baada ya kuapishwa kuwa Rais. Alisema na anaendelea kutekeleza kwa vitendo dhamira yake ya kuwa, Serikali anayoingoa itaendeleza jitihada za kuimarisha maadili, nidhamu, uzalendo, uchapa kazi na uwajibikaji. Pia, aliahidi kusimamia haki na stahiki za Watumishi wa Umma na Watendaji serikalini ili kuongeza ari ya kufanya kazi kwa bidii na kukuza uwajibikaji wa hiari katika Utumishi wa Umma. Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inaahidi kuendelea kufanya kazi kwa bidii, nidhamu, uadilifu, weledi na uzalendo wa kitaifa ili kuendana na kasi ya Serikali ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

5. Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa namna anavyomsaidia Rais kutekeleza majukumu ya kuiletea maendeleo nchi yetu. Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Zanzibar

na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa uongozi wake shupavu na nia yake thabiti ya kuleta maendeleo Zanzibar.

6. Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kusimamia na kuratibu kazi za kila siku za Serikali na utendaji wa Serikali Bungeni kwa umahiri mkubwa. Pamoja na kumsaidia vyema Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kullitea Taifa letu maendeleo.

7. Mheshimiwa Spika, naomba nikupongeze wewe binafsi kwa kuwa mwanamke wa pili kushika uongozi wa Mhimili huu wa Bunge. Pia, nampongeza Naibu Spika ambaye ameungana nawe kuchaguliwa kwa kishindo katika nafasi za kuliongoza Bunge letu Tukufu. Tunategemea kuwa umakini, weledi, busara na hekima kubwa mliyodhihirisha katika nafasi mlizokuwa nazo zitaendelea kukua zaidi mnapotekeleza wajibu wenu katika nafasi hizi kubwa zaidi. Pia, nawapongeza Wenyeviti wa Bunge kwa kusimamia kwa ustadi wa hali ya juu kazi waliyopewa ya kuongoza vikao vya Bunge letu, kwa hakika mmekuwa msaada mkubwa sana katika uendeshaji wa Bunge kwa ujumla.

8. Mheshimiwa Spika, naomba pia kuwapongeza Mawaziri wenzangu wote wa Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuendelea kupewa nafasi ya kuwatumikia Watanzania, hasa kutekeleza Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025.

9. Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Abdallah Chaurembo, Mbunge wa Mbagala na Makamu wake Mheshimiwa Dennis Londo, Mbunge wa Mikumi, pamoja na Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri mzuri walioutoa wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2021/22 na Mapendekezo ya Mpango wa Utekelezaji na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha

kwa Mwaka wa Fedha 2022/23. Maoni, ushauri na ushirikiano wa Kamati umetuwezesha kuboresha utendaji kazi wa Ofisi yangu na maandalizi ya hotuba hii.

10. Mheshimiwa Spika, nawashukuru Balozi Hussein A. Kattanga, Katibu Mkuu Kiongozi; Dkt Moses M. Kusiluka, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Ikulu; Dkt. Laurean J. Ndumbaro, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Bw. Xavier M. Daudi, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Makamishna, Watendaji Wakuu wa Taasisi; Wakurugenzi na Watumishi wote wa Ofisi ya Rais Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kazi nzuri wanazozifanya katika kutekeleza majukumu yanayoiwezesha Ofisi kufikia malengo yake, ikiwa ni pamoja na kukamilisha Hotuba hii kwa wakati. Aidha, napenda kuwashukuru waajiri na watumishi wote wa Umma kwa kutekeleza wajibu wao kwa ufanisi, uzalendo pamoja na imani yao kwa uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita ambao umeiwezesha Serikali kutekeleza majukumu yake ya kuwahudumia wananchi.

11. Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda kuzishukuru Nchi Wahisani na Washirika wa Maendeleo ambao wamechangia jitihada zetu za kuleta maendeleo kwa wananchi. Hivyo, nachukua fursa hii kuwashukuru na kuwataja wachache ambao ni:- Jamhuri ya Watu wa China, Japan, Uingereza, India, Jamhuri ya Korea, Marekani, Sweden, Australia, Umoja wa Ulaya, Norway, Finland, Uswisi, Malaysia, Misri, Singapore, Cuba, Thailand na Ireland. Vile vile, nayashukuru Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa ambayo ni: Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia (WB), OFID-OPEC Fund for International Development, Foreign Commonwealth Development Office (FCDO), KOICA, GIZ, USAID, SIDA, UNDP, Jumuiya ya Madola, JICA, UNICEF, ILO, WFP, UN Women, Global Fund, Mfuko wa Fedha wa Kimataifa (IMF) na Taasisi ya Bill and Melinda Gates Foundation.

12. Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Peramiho kwa kuendelea kunipa ushirikiano wakati wote ninapoendelea kuwawakilisha. Vile vile,

naishukuru familia yangu kwa ushirikiano wanaonipa na kwa dua zao wakati wote ninapotekeleza majukumu yangu.

13. Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa natoa pole kwa Watanzania wenzetu, Viongozi na Watumishi wa Umma waliopotelewa na ndugu zao kutokana na sababu mbalimbali zilizojitokeza katika kipindi hiki. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awape faraja wote ili waendeleo kujenga Taifa letu.

14. Mheshimiwa Spika, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan kwa mikakati yake bora ya kupambana na UVIKO 19 kwa kuhimiza wananchi wote ikiwemo watumishi wa umma kupata chanjo. Aidha, Rais ametumia fursa ya UVIKO kupata fedha za kuiletea maendeleo nchi yetu. Natumia nafasi hii kutoa rai kwa watumishi wa umma kuendelea kuchukua tahadhari za kujikinga.

15. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/22 tuliwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu, maombi ya fedha kwa ajili ya kutekeleza mipango kazi inayowezesha Ofisi yangu kwa mazingatio ya kisera na kimkakati. Kwa mara nyingine tupo mbele ya Bunge lako Tukufu ili kutoa Taarifa ya Utekelezaji wa shughuli tulizoombea fedha kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 pamoja na kuwasilisha mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/23.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MWAKA WA FEDHA 2021/22

16. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2021/22 ulizingatia miongozo ya kitaifa ambayo ni Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025, Maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, Hotuba ya Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa kuhutubia Bunge la 12 pamoja na maelekezo yake mbalimbali. Aidha, utekelezaji umezingatia Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano Awamu ya Tatu (2021/22 - 2025/26), unaoitaka Tanzania iwe na Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu.

OFISI YA RAIS - IKULU NA TAASISI ZAKE

17. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Fungu: 20 Ofisi ya Rais, Ikulu iliidhiniwa **Shilingi 24,557,764,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Machi, 2022 **Shilingi 18,339,003,333.31** zilipokelewa na kutumika.

18. Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza majukumu yake, katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Fungu 30 Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri inayojumuisha taasisi zilizo chini ya Ikulu, iliidhiniwa **Shilingi 639,780,318,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 467,921,917,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 171,858,401,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2022 **Shilingi 491,351,852,318.92** zilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo **Shilingi 368,574,043,260.92** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 122,777,809,058** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Yafuatayo ni maelezo kwa kila taasisi:-

A: OFISI YA RAIS- IKULU

19. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Ikulu imeendelea kuongoza, kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali. Katika kipindi cha mwezi Julai, 2021 hadi Machi, 2022, kazi zifuatazo zilitekelezwa:-

(i) Ushauri umeendelea kutolewa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika masuala ya Siasa, Uchumi, Jamii, Sheria, Diplomasia, Mawasiliano na Habari, Uhusiano wa Kikanda, Kimataifa na ushauri mwingine kwa lengo la kumsaidia Rais kufanya maamuzi;

(ii) Ushauri umeendelea kutolewa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu ratiba ya kila siku;

(iii) Huduma zimeendelea kutolewa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na familia yake;

(iv) Mikutano 25 ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ilifanyika, ambapo nyaraka 43 zilichambuliwa. Mikutano 10 ya Kamati

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Maalum ya Makatibu Wakuu (IMTC) ilifanyika na nyaraka 20 zilichambuliwa na ushauri kutolewa. Mikutano miwili ya kazi ya Kamati ya Makatibu Wakuu ilifanyika ambapo mada tano ziliwasilishwa na kujadiliwa. Mikutano mitano ya Baraza la Mawaziri ilifanyika ambapo nyaraka 21 zilijadiliwa na kutolewa maamuzi. Aidha, mikutano minne ya Kamati ya Katiba na Bunge ya Baraza la Mawaziri ilifanyika ambapo miswada 13 ilijadiliwa;

(v) Kumbukumbu za Mikutano ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu na Baraza la Mawaziri ziliandaliwa na kusambazwa kwa wakati kwa wahusika. Aidha, ufuatiliaji na tathmini ya Maamuzi ya Baraza la Mawaziri ulifanyika na taarifa ya utekelezaji wake iliandaliwa;

(vi) Ziara ya Maafisa wa Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri kutembelea Mradi wa Bwawa la Kuazalisha Umeme la Julius Nyerere na Uhifadhi katika mbuga za Ngorongoro, Loliondo na Serengeti ilifanyika ili kuona hali halisi ya utendaji na kushauri ipasavyo;

(vii) Mafunzo kuhusu utayarishaji na uwasilishaji wa Nyaraka za Baraza la Mawaziri kwa Menejimenti za Wizara tano za Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; Ofisi ya Rais – Ikulu; Wizara ya Afya; Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yalifanyika;

(viii) Mkutano wa Waratibu wa Shughuli za Baraza la Mawaziri (CLOs) katika Wizara zote ulifanyika mwezi Machi, 2022 Mkoani Singida;

(ix) Vitabu vya Taarifa za Utekelezaji wa Kazi na Shughuli za Baraza la Mawaziri na Kamati zake kwa kipindi cha pili cha Serikali ya Awamu ya Nne (mwaka 2010 – 2015) na kipindi cha kwanza cha Serikali ya awamu ya 5 (2015 – 2020) vinaandaliwa;

(x) Mafunzo ya kujenga uwezo kuhusu utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu (NACCSAP III) yamefanyika kwa Kamati za Kudhibiti Uadilifu za Taasisi 86

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(zinazojumuisha Sekta ya Umma, Sekta Binafsi, na Asasi za Kiraia CSOs);

(xi) Tathmini ya utekelezaji wa Awamu ya Tatu ya Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa imefanyika ambapo rasimu iliyoboreshwa ya taarifa ya tathmini inafanyiwa uchambuzi kabla ya kuwasilishwa Serikalini;

(xii) Uratibu na uendeshaji wa mikutano ya Makatibu Wakuu na Waratibu wa Programu za Maboresho umefanyika na kuwezesha kikao cha Katibu Mkuu Kiongozi na Makatibu Wakuu wanaosimamia utekelezaji wa Programu za Maboresho katika Sekta ya Umma kufanyika. Vile vile, mikutano mitatu (3) ya Waratibu wa Programu za Maboresho imefanyika ili kuimarisha usimamizi, uongozi na umiliki wa mchakato wa maboresho katika sekta ya umma nchini;

(xiii) Mkutano wa uhamasishaji baina ya Idara ya Utawala Bora na Maboresho, Menejimenti ya TPSF pamoja na AZAKI umefanyika ili kuhamasisha Sekta Binafsi kuzingatia malengo ya Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na kuishirikisha katika tathmini. Aidha, majadiliano na viongozi wa dini (TEC, BAKWATA na CCT) kuhusu utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa kwa lengo la kukusanya maoni umefanyika;

(xiv) Taarifa mbili (2) za utekelezaji za robo mwaka za Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu (NACSAP III) zimeandaliwa. Aidha, maandalizi ya awali ya Mfumo wa Kielektroniki wa Ufuatiliaji na Tathmini wa NACSAP III yamefanyika;

(xv) Ziara za ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa zimefanyika katika Mikoa ya Shinyanga, Simiyu, Mara, Dar es salaam, Pwani na Singida. Aidha, ziara za ufuatiliaji wa Utekelezaji wa maboresho zimefanyika katika Mikoa ya Dar es salaam, Pwani, Arusha, Manyara, Singida, Tabora na Katavi;

(xvi) Rufaa 222 za Watumishi wa Umma, Mamlaka ya Nidhamu na Waajiri zilichambuliwa na kutolewa uamuzi na Rais na

Katibu Mkuu Kiongozi ambapo wahusika walijulishwa. Aidha, malalamiko 587 ya Watumishi wa Umma na wananchi wengine yalichambuliwa na kutolewa maelekezo;

(xvii) Majibu na ushahidi umetolewa kwenye kesi za madai tatu (3) kuhusu watumishi wa Umma na wananchi wengine zilizoko Mahakama Kuu zinazopinga uamuzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au Katibu Mkuu Kiongozi zilitolewa kwa kushirikiana na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali; na

(xviii) Ujenzi wa Ikulu ya Chamwino umeendelea kufanyika na umefikia asilimia 94. Aidha, ukarabati wa baadhi ya majengo katika Ikulu ya Dar es Salaam umefanyika ukihusisha pia upakaji rangi wa majengo na ukuta.

B. TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA (TAKUKURU)

20. Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura ya 329. Majukumu hayo ni kuchukua hatua stahiki za kuzuia na kupambana na rushwa kwenye sekta ya umma, mashirika na sekta binafsi, ikijikita zaidi katika kuzuia vitendo vya Rushwa kwa watumishi wa umma na sekta binafsi na wananchi kwa ujumla.

21. Mheshimiwa Spika, juhudi zinazochukuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na **Mhe. Samia Suluhu Hassan** katika kukabiliana na vitendo vya rushwa nchini zimeleta mafanikio makubwa kwa kuongeza nidhamu, uadilifu na uwajibikaji katika nyanja mbalimbali zikiwemo za utumishi wa umma, biashara, uwekezaji, ukusanyaji mapato na matumizi ya madaraka na fedha za umma. Mafanikio haya yamejengea Serikali uwezo imara wa kukuza uchumi na kuongeza kasi ya utoaji huduma bora kwa umma.

22. Mheshimiwa Spika, matokeo ya tafiti zilizofanywa na taasisi mbalimbali za kitaifa, kikanda na kimataifa kuhusu hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kupambana na rushwa

zimedhihirisha kuwa Tanzania inafanya vizuri katika kudhibiti vitendo vya rushwa na ufasidi nchini. Taarifa ya **Transparency International** ya mwaka 2021 iliyotoka Februari, 2022; kupitia Kiashiria cha *Corruption Perception Index* inaonesha kuwa Tanzania imeendelea kufanya vizuri kwa kupata **alama 39** na kushika **nafasi ya 87** kati ya nchi **180**, ikiwa imepanda kwa **nafasi 7** ikilinganishwa na **alama 38** katika nafasi ya **94** ya mwaka 2020. Kwa mafanikio haya Tanzania imeshika nafasi ya pili kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Pia, Utafiti wa **World Justice Project (WJP)** unayotumia kiashiria cha *“The Rule of Law Index”* unaonesha kuwa kwa mwaka 2020, Tanzania iliendelea kufanya vizuri kwa mwaka wa pili mfululizo katika kudhibiti matumizi mabaya ya madaraka kwenye mihimili ya utawala, mahakama na bunge kwa kushika **nafasi ya 93** kati ya nchi **128** duniani, ikiwa ni nchi ya kwanza kwa nchi za Afrika Mashariki na **nafasi ya 13** kwa nchi za kusini mwa jangwa la Sahara. Vilevile, utafiti wa taasisi binafsi ya **Research on Poverty Alleviation (REPOA)**, uliotolewa mwezi 2022 unaonesha kuwa Tanzania inafanya vizuri katika kulikabili tatizo la rushwa na kuwa imepungua katika kipindi cha **miezi 12** iliyopita.

23. Mheshimiwa Spika, Serikali imeongeza nguvu kwenye kudhibiti rushwa na ufasidi nchini kwa kuweka msisitizo kwenye eneo la uzuiaji rushwa. Katika kipindi cha mwezi Julai, 2021 hadi Machi, 2022, baadhiya kazi zilizotekelezwa ni zifuatazo:-

(i) Kazi 370 za uchambuzi wa mifumo zilifanyika katika maeneo mbalimbali yakiwemo:

a) Upatikanaji, usambazaji na udhibiti wa bidhaa za afya;

b) Usimamizi wa ajira, mitihani na fedha za utafiti/ushauri katika Vyuo Vikuu vya Umma nchini;

c) Usimamizi wa mitihani katika vyuo vya kati;

d) Ufanisi wa mfumo wa huduma za ununuzi Serikalini; na

e) Rushwa ya ngono katika ajira na upandishwaji vyeo katika sekta ya elimu. Kutokana na kazi hizo, hatua zimechukuliwa

ikiwani pmaoja na kushauri Mamlaka husika namna ya kudhibiti mianya ya rushwa katika maeneo hayo.

(ii) Warsha vikao 161 vya wadau kujadili matokeo ya kazi za utafiti, ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za umma katika miradi ya maendeleo na uchambuzi wa mifumo kwa lengo la kuweka mikakati ya kudhibiti rushwa vilifanyika. Aidha, kazi 38 za ufuatiliaji wa utekelezaji wa maazimio ya kuziba mianya ya rushwa yatokanayo na vikao vya wadau zilifanyika katika maeneo mbalimbali yakiwemo: udhibiti wa rushwa ya ngono katika Chuo Kikuu cha Dodoma na utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi nchini;

(iii) Ufuatiliaji wa utekelezaji wa Miradi ya maendeleo 597 yenye thamani ya **Shilingi** trilioni 4.7 umefanyika katika sekta za Afya, Maji, Fedha, Elimu, Kilimo, Ujenzi na Viwanda kwa lengo la kuhakikisha miradi hiyo inatekelezwa kama ilivyopangwa na thamani ya fedha inapatikana. Kati ya miradi hiyo, miradi 81 yenye thamani ya **Shilingi** bilioni 43 ilibainika kuwa na mapungufu mbalimbali katika utekelezaji hivyo watekelezaji wake walishauriwa namna bora ya kutekeleza miradi hiyo kupitia vikao kazi na mingine inaendelea kufanyiwa uchunguzi ili hatua stahiki zichukuliwe;

(iv) Elimu kuhusu madhara za rushwa na juhudi za Serikali za kudhibiti Rushwa na kupata uungwaji mkono ilitolewa kwa umma kupitia njia mbalimbali zikiwemo semina 2,178, mikutano ya hadhara/mijadala 2,269, vipindi vya redio na televisheni 278, maonesho 236 na taarifa kwa umma 56 kupitia vyombo vya habari. Aidha, habari/makala 394 ziliandaliwa kwa ajili ya wavuti na jarida la TAKUKURU;

(v) Elimu kuhusu rushwa ilitolewa kwa vijana walio shuleni na vyuoni ambapo Klabu za wapinga rushwa 4,371 zilifikiwa ili kujenga kizazi cha vijana wenye maadili na wanaochukia rushwa. Aidha, Skauti wamejengewa mazingira ya kushirikishwa kwenye mapambano dhidi ya rushwa ambapo Mwongozo wa Wawezeshaji wa Kufundisha Vijana wa Skauti Kuzuia na Kupambana na Rushwa umezinduliwa na kusambazwa nchini kote kwa lengo la kuwajengea uwezo

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wawezeshaji wa Skauti namna ya kutoa elimu kwa vijana wa Skauti kuhusu namna ya kuzuia na kupambana na rushwa;

(vi) Uelimishaji Umma umefanyika kupitia mitandao ya kijamii kwa kutoa matangazo 2,415 dhidi ya rushwa yaliyoandaliwa na kusambazwa kwenye mitandao ya Twitter, Facebook na Instagram. Aidha, TAKUKURU Online TV imerusha jumla ya habari 32 na kufanikiwa kuwafikia wananchi wengi kwa gharama nafuu;

(vii) Kesi 865 za tuhuma dhidi ya rushwa na uufisadi ziliendeshwa mahakamani zikiwemo kesi mpya 305. Aidha, kesi 338 ziliamuliwa mahakamani ambapo kesi 191 watuhumiwa walipatikana na hatia na kuhukumiwa kifungo au kulipa faini na kesi 147 watuhumiwa wake hawakupatikana na hatia na kuachiwa huru. Kesi 527 bado zinaendelea mahakamani **KIAMBATANISHO NA. 1 Uk. 137**;

(viii) **Shilingi** bilioni 1.42 zimeokolewa kutokana na operesheni mbalimbali za uchunguzi uliofanyika kote nchini. Aidha, Taasisi kwa kushirikiana na mamlaka nyingine imewezesha kutaifisha na kurejesha Serikalini fedha na mali zenye thamani ya **Shilingi** bilioni 6.3 na dola za kimarekani 1,468,364 ambazo zinahusisha fedha, nyumba tano (5), viwanja sita (6) na magari saba (7);

(ix) Mapitio ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya mwaka 2007 yamefanyika katika ngazi mbalimbali za maamuzi na kuainisha mapungufu ya kisera yanashughulikiwa na Ofisi ya Rais kama msimamizi wa Sera na mengine yanafanyiwa kazi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Sheria inahuishwa ili iendane na hali ya sasa ya kiuchumi na kijamii pamoja na dhamira ya Serikali ya kudhibiti rushwa nchini;

(x) Mfumo wa TEHAMA wa ndani ya TAKUKURU umeimarishwa kwa kuunganisha Ofisi mpya za makao makuu zilizopo eneo la Nanenanena Area D katika jiji la Dodoma kwenye mtandao wa Taasisi. Aidha njia za mawasiliano katika mikoa 28 na wilaya 13 zimeboreshwa kwa lengo la kurahisisha mtiririko mzuri wa majalada, upatikanaji wa takwimu na mawasiliano

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kutoka ngazi za Wilaya, Mikoa na Makao Makuu. Vile vile, mfumo wa masijala wa kielektroniki wa Ofisi (e-Office) ambao unaboresha utendaji kazi ndani ya Taasisi umewekwa na kuanza kutumika;

(xi) Watumishi wa TAKUKURU 406 wamepatiwa mafunzo ya kuwajengea uwezo ili kuongeza weledi wa kutekeleza majukumu kwa ufanisi;

(xii) Kazi ya ujenzi wa Ofisi ya TAKUKURU Makao Makuu Dodoma umefikia asilimia 38 mbapo kazi inayoendelea ni ufungaji wa maboksi ya mbao (form work) kwa ajili ya kumwaga zege ghorofa ya kwanza;

(xiii) Taratibu za kuwapata wakandarasi kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo ya Ofisi za TAKUKURU Mkoa wa Kilimanjaro, Morogoro na Iringa na Wilaya za Mvomero, Kilolo, Kongwa, Liwale na Kiteto zimekamilika; na

(xiv) Taratibu za kuwapata wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa ukuta katika Ofisi za TAKUKURU Wilaya ya Chamwino, Ruangwa na ujenzi wa karakana ya magari, Dodoma zimekamilika.

C. TAASISI YA UONGOZI

24. Mheshimiwa Spika, Taasisi ya UONGOZI imeendelea kuwa Kituo cha utaalum wa hali ya juu cha kuendeleza Viongozi Barani Afrika kwa kuanzia na Tanzania, Ukanda wa Afrika Mashariki na hatimaye Afrika kwa ujumla. Walengwa ni Viongozi Waandamizi waliopo na wanaojitokeza wakiwemo wanasiasa, watumishi wa Serikali na Mahakama. Katika kipindi cha mwezi Julai, 2021 hadi Machi, 2022 kazi zifuatazo zilitekelezwa:-

(i) Kozi 46 za muda mfupi zimetolewa kwa viongozi 2,759 wakiwemo Mawaziri na Manaibu Waziri wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mawaziri na Makatibu Wakuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Uongozi ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Maafisa Waandamizi na Makamanda wa Mikoa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wa Jeshi la Polisi la Tanzania, Maafisa Maandamizi wa Mamlaka ya Kodi Tanzania. Utekelezaji huu ni zaidi ya lengo la kutoa kozi fupi 14 kwa sababu ya ongezeko la mahitaji ya mafunzo;

(ii) Maafisa Waandamizi 43 kutoka Wizara, Taasisi na Mashirika ya Umma, Taasisi za Kiraia na Taasisi Binafsi wamepatiwa mafunzo katika ngazi ya stashahada ya uzamili. Mafunzo yalihusu moduli saba ambazo ni Ujuzi wa Fedha kwa Watendaji, Uongozi wa Matokeo, Ubunifu, Maendeleo Endelevu, Usimamizi wa Rasilimali watu wa Kimkakati, Mawasiliano ya Kimkakati na Maadili. Moduli hizi zilitolewa kama ilivyopangwa. Mafunzo hayo ni ya awamu ya tano ya Programu ya Stashahada ya Uzamili inayoendeshwa kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Aalto cha nchini Finland;

(iii) Maafisa Waandamizi 85 kutoka Wizara, Taasisi na Mashirika ya Umma, Taasisi za Kiraia na Taasisi Binafsi wamepatiwa mafunzo katika ngazi ya cheti ikiwa ni utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Programu ya Uongozi ngazi ya Cheti inayotolewa kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Aalto cha nchini Finland;

(iv) Mikutano mitatu 930 ya kitaifa iliyohusu masuala ya uongozi na maendeleo endelevu iliandaliwa kama ilivyopangwa. Mikutano hiyo ilihudhuriwa na viongozi 1,157 wakiwemo Viongozi wa Umma, Vyuo Vikuu, Taasisi za Utafiti, Taasisi za Kiraia, Taasisi Binafsi, viongozi wastaafu, wanazuoni na wanafunzi wa vyuo vikuu;

(v) Utafiti tumizi ulifanyika katika maeneo matatu kati ya manne yaliyopangwa kufanyika kwa mwaka. Utafiti huu ulihusu:-

(a) Tathmini ya utekelezaji wa dhana ya ushiriki wa watanzania kwenye miradi ya kimkakati na matokeo yake nchini Tanzania;

(b) Tathmini ya utekelezaji wa sheria kuu mbili za kimkakati ambazo ni Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusiana na Umiliki wa Maliasili ya Mwaka 2017; na Sheria ya Mapitio na Majadiliano Kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba Inayohusu Maliasili ya Mwaka 2017;

(c) Tathmini ya athari za kimazingira na za kijamii zinazotokana na ujenzi wa Reli ya Kisasa kipande cha tano kutokea Mwanza mpaka Isaka.

(vi) Vipindi vine (4) vya mahojiano na viongozi waandamizi na wataalam iliandaliwa kama ilivyopangwa. Mahojiano hayo yanahusu masuala ya Uchumi wa kijani Barani Afrika, Ujumuisho katika masuala ya Fedha Barani Afrika, Uchumi wa Buluu na Nishati Mbadala. Vipindi hivi vilirushwa kwenye runinga na kuwekwa kwenye tovuti ya Taasisi ya UONGOZI na mitandao ya kijamii kwa lengo la kubadilishana taarifa, maarifa na uzoefu. Vipindi hivi vinaonekana Bara zima la Afrika;

(vii) Ushauri wa kitaalamu ulitolewa kwa TASAF katika kupitia Mpango Mkakati wa Pili. Aidha, Taasisi kwa kushirikianana Ofisi ya Waziri Mkuu imeratibu na kushiriki kuandaa Mwongozo wa Kutengeneza Sera Nchini;

(viii) Kutumia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kushirikisha umma katika kujadili masuala ya Uongozi na Maendeleo endelevu; na

(ix) Machapisho saba juu ya masuala ya Uongozi na Maendeleo Endelevu yameandaliwa na kutolewa.

D. MPANGO WA KURASIMISHA RASILIMALI NA BIASHARA ZA WANYONGE TANZANIA (MKURABITA)

25. Mheshimiwa Spika, Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) umeendelea kutekeleza jukumu la kuandaa na kusimamia mfumo wa kitaifa wa umiliki wa rasilimali na uendeshaji wa Biashara nchini unaotambulika na kukubalika kisheria. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, MKURABITA imetekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Vituo Jumuishi vitano vya Urasimishaji na Uendelezaji Biashara vimeanzishwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa za Shinyanga, Moshi, Tarime, Rungwe na Sumbawanga kwa kufanya ukarabati wa majengo katika maeneo hayo;

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(ii) Urasimishaji na uendelezaji biashara umefanyika kwa kutoa mafunzo ya Urasimishaji wa Biashara kwa wafanyabiashara 2,042 katika Manispaa za Shinyanga (1095) na Moshi (947). Aidha, Wafanyabiashara 1,210 wamesajili biashara zao na kuanza kufanya biashara katika Mfumo rasmi, Wafanyabiashara 470 wamefungua akaunti za benki na Wafanyabiashara 255 wamejiunga na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii;

(iii) Ujenzi wa Masjala 12 za Ardhi za Vijiji umekamilika katika Mamlaka saba za Serikali za Mitaa ambazo ni Masasi (2), Newala (2), Chamwino (1), Moshi (2), Meru (2), Mbarali (1), Itigi (1) na Nachingwea (1). Ujenzi wa Masjala 10 za Ardhi za Vijiji umefikia katika hatua za umaliziaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa za Kibiti (1), Mvomero (1), Nachingwea (1), Sumbawanga (1), Makete (2), Kalambo (1) na Mwanga (3)

(iv) Urasimishaji wa Waendesha Bodaboda umefanyika kwa kutoa mafunzo kwa Waendesha Bodaboda 3,993 katika Halmashauri tatu za Jiji la Dodoma (2,639), Manispaa za Shinyanga (605) na Moshi (749). Kati ya hao waliopata mafunzo, Waendesha Bodaboda 2,720 wamepata leseni za usafirishaji na udereva ambapo Jiji la Dodoma ni 1,650, Manispaa za Shinyanga ni 350 na Moshi ni 720. Aidha, jumla ya mikopo ya **Shilingi** 841 imetolewa kwa Waendesha Bodaboda 909 ambapo shilingi Milioni 554 zimetolewa na Halmashauri zao kutoka fungu la asilimia 10 kwa Vijana na **Shilingi** milioni 287 zimekopeshwa na Benki za CRDB na NMB;

(v) Hatua za awali za uanzishwaji wa vituo jumuishi viwili vya urasimishaji wa biashara katika Wilaya ya Kusini - Unguja na Chakechake - Pemba zimefanyika ili kupata maeneo kwa ajili ya uanzishwaji wa vituo husika. Aidha, jumla ya wafanyabiashara 50 wamepata mafunzo na kusajili biashara zao;

(vi) Mafunzo kuhusu fursa na matumizi ya kiuchumi ya Hati za Haki Milki za Kimila yametolewa kwa wakulima 2,400 wa mashamba yaliyorasimishwa katika Halmashauri za Wilaya za Mufindi (395), Kilolo (220), Sikonge (507), Butiama (210), Moshi

(706), Rufiji (147) na Kibiti (215). Aidha, mafunzo kwa wakulima 58 wa jamii ya kifugaji yametolewa na mizinga 30 ya nyuki imetolewa;

(vii) Urasimishaji wa ardhi mjini umefanyika kwa kuandaa Hati miliki 3,083 katika Mamlaka 4 za Serikali za Mitaa za Chamwimo, Babati, Tunduma, na Makete. Aidha, jumla ya Hati Miliki 1,152 katika Halmashauri za Chamwimo (328), Babati (120), Tunduma (338) na Makete (366) ziko tayari kutolewa kwa wananchi;

(viii) Ufuatiliaji na Tathmini ya shughuli za urasimishaji ardhi umefanyika Tanzania Bara katika Halmashauri za Jiji la Arusha, Wilaya za Makete, Momba, Kiteto, Meru na Halmashauri za Mji mdogo wa Tandala na Tunduma, wilaya ya Uyui na manispaa ya Tabora kwa lengo la kubaini matokeo na vikwazo vya uendeleu wa urasimishaji ardhi na biashara kwenye Halmashauri hizo.

Aidha, kwa upande wa Zanzibar, ufuatiliaji na tathmini umefanyika katika Wilaya sita za Wete, Mkoani, Chakechake, Mjini, Magharibi A na Magharibi B kwa nia ya kubaini upatikanaji wa mikopo kwa kutumia fursa za urasimishaji wa ardhi na biashara; na

(ix) Vipindi 14 vya redio na runinga kuhusu utekelezaji wa shughuli za urasimishaji vimezalishwa na kurushwa hewani kupitia TBC Taifa na TBC1. Aidha, baadhi ya taarifa na maudhui ya vipindi vilivyozalishwa yameendelea kutolewa kwa njia ya runinga kupitia baadhi ya vipindi vya taarifa za habari ikiwemo ARIDHIO na vipindi vya Harakati.

E. MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII (TASAF)

26. Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii umeendelea kutekeleza Awamu ya Tatu ya TASAF kwa kuyapa kipaumbele maeneo ya Ukuzaji wa uchumi na kupunguza umaskini wa kipato; Kuinua ubora wa maisha na ustawi wa jamii; na Utawala bora na uwajibikaji. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, Mfuko wa Maendeleo Jamii (TASAF) umetekeleza kazi zifuatazo:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(i) Uhakiki wa awali wa Kaya umefanyika katika Mamlaka 186 za utekelezaji. Jumla ya Kaya 886,724 zilihakikiwa ambapo kaya 781,342 zimekidhi vigezo vya uhakiki wa awali wa kuendelea kuwepo katika Kipindi cha Pili cha Mpango na kaya 105,382 zimeboreka kiuchumi ambapo zimepewa muda wa kujiandaa ili kutoka kwenye mpango na kujitegemea kiuchumi;

(ii) Utambuzi na uandikishaji wa kaya maskini kwa Vijiji/Mitaa/Shehia ambazo hazikufikiwa na Mpango wa Kipindi cha Kwanza umefanyika na umekamilika katika Mamlaka zote 186 ambapo Mitaa/Vijiji/Shehia 7,217 vimefikiwa na jumla ya Kaya 602,672 zimetambuliwa. Kati ya hizo, Kaya mpya 498,091 ziliandikishwa na hivyo kufanya Mpango kuwa na Kaya za Walengwa 1,279,325;

(iii) Ruzuku ya **Shilingi** bilioni 213 ilihawilishwa kwa kaya 1,279,325 zilizokidhi vigezo vya kuingia katika Kipindi cha Pili cha Mpango kutoka maeneo yote ya utekelezaji 184 kwa Tanzania Bara na Pemba na Unguja kwa Zanzibar. Maelezo ya mgawanyo wa Ruzuku hiyo yapo katika **KIAMBATANISHO NA. 2 UK. 138 - 148**;

(iv) Miradi 2,674 ya Kutoa Ajira za Muda kutoka katika mamlaka za utekelezaji 51 imeibuliwa na jamii. Miradi hii ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji na inatoa Ajira ya Muda kwa kaya 253,117. Kufikia Machi, 2022, jumla ya **Shilingi** bilioni 16.14 zimeshalipwa kwa Walengwa kama Ujira. Pia mafunzo ya usimamizi wa miradi yamefanyika kwa wawezeshaji 1,399 kutoka mamlaka 51 za utekelezaji zinazotekeleza miradi kwa mwaka 2021/2022. Mgawanyo wa Miradi hiyo imeoneshwa katika **KIAMBATANISHO NA. 2 UK. 138 - 148**;

(v) Miradi 550 imeandaliwa na kutekelezwa ambapo miradi mitatu (3) kati ya hiyo yenye thamani ya **Shilingi** 321.21 milioni imekamilika wakati mingine 547 yenye thamani ya **Shilingi** bilioni 16.0 ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Miradi hiyo itawezesha upatikanaji wa huduma za elimu, afya, maji, mazingira, barabara za vijijini na miradi ya ujasiriamali kwa wananchi wanaoishi maeneo husika. Aidha, jumla ya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wataalam 120 kutoka mamlaka 44 za utekelezaji wamepatiwa mafunzo ya uwezeshaji na usimamizi wa miradi. Maelezo zaidi yapo katika **KIAMBATANISHO NA. 2 Uk. 138 - 148;**

(vi) Jumla ya Vikundi 2,385 viliundwa vyenye wanachama 30,255 (wanawake 26,977 na wanaume 3,278), kwenye mamlaka 10 za utekelezaji. Wawezeshaji 269 walipatiwa mafunzo ya uundaji wa vikundi vya Kuweka Akiba na Kuwekeza. Mafunzo yamefanyika kwa wawezeshaji 59 wa kitaifa yanayohusu uhamasishaji na uundaji wa vikundi, uwekaji kumbukumbu za taarifa za fedha, usimamizi wa mikopo na utatuzi wa migogoro. Kiasi cha **Shilingi** bilioni 2.25 kama ruzuku ya vikundi imetolewa kwa walengwa 4,884 wa mamlaka za utekelezaji za Bagamoyo na Chalinze kwa ajili ya miradi ya ujasiriamali;

(vii) Idadi ya mamlaka za utekelezaji zilizoingizwa katika malipo ya njia ya Kielektroniki imeongezewa hadi kufikia mamlaka za utekelezaji 122. Njia hii ya malipo inawezesha fedha kutumwa moja kwa moja kwa Mlengwa kupitia mitandao ya simu, Benki kwa namba ya NIDA) na kumfikia kwa haraka na kupunguza gharama za uendeshaji. Asilimia 19 ya walengwa katika maeneo hayo wameanza kupokea fedha kwa njia ya kielektroniki na uhamasishaji unaendelea ili kuandikisha walengwa zaidi kutumia mfumo huu wa malipo;

(viii) Mifumo ya Teknolojia, Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ya utunzaji wa kumbukumbu za walengwa, uendeshaji na utoaji taarifa iliendelea kuboreshwa na kuimarishwa. Mfumo wa kuwasilisha na kupokea malalamiko umeendelea kutumika katika maeneo yote ya utekelezaji. Mifumo ya TASAF imeunganishwa na mifumo mingine ya kitaifa kama vile NIDA na Malipo ya Serikali Mtandao (Government Electronic Payment Gateway – GePG). Aidha, utengenezaji wa Mfumo wa Ukusanyaji wa Taarifa za Walengwa kwa kutumia vifaa vya kidijitali ‘tablets’ ili kuondokana na matumizi ya karatasi ulikamilika na kutumika kwenye uhakiki na utambuzi wa kaya. Mfumo huu ni rahisi na unapunguza gharama za ukusanyaji na uingizaji wa takwimu;

(ix) Tathmini ya msingi ya Kipindi cha Pili cha Mpango imefanyika katika Maeneo ya Utekelezaji 32 ambapo Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (OCGS) zilihusika. Aidha, tafiti mbalimbali zimefanyika na kuonesha jinsi Mpango unavyowanufaisha walengwa ambapo jumla ya **Shilingi** bilioni 3.5 zimetumika kwa kazi hizo; na

(x) Mapitio ya pamoja ya Timu ya Serikali na Wadau wa Maendeleo kuhusu utekelezaji wa shughuli za Mpango yamefanyika katika vipindi vitano vya Julai, 2021 mpaka Februari, 2022. Taarifa zote za mapitio zimeonesha utekelezaji wa Mpango unaendelea vizuri na unawasaidia walengwa kuondokana na umaskini na kuwajengea uwezo wa kiuchumi na kuwaendeleza watoto katika afya na elimu bora. Wadau wa Maendeleo wameahidi kuendelea kushirikiana katika utekeleza wa mpango. Aidha, wadau hao wameahidi kushirikiana na Serikali katika kuongeza muda wa utekelezaji kwa miaka miwili ili kufidia muda uliopotea kutokana na kuchelewa kuanza kwa utekelezaji.

F. WAKALA YA NDEGE ZA SERIKALI

27. Mheshimiwa Spika, Wakala ya Ndege za Serikali ina jukumu la kutoa huduma ya usafiri wa anga kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Viongozi wengine Wakuu wa Kitaifa. Wakala ilianzishwa ili kuboresha huduma na kuimarisha usalama wa usafiri wa ndege kwa viongozi wanaotumia huduma hizo.

28. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, Wakala wa Ndege za Serikali ilitekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Ukarabati na upanuzi wa karakana ya Ndege za Serikali awamu ya kwanza katika Uwanja wa Ndege Julius Nyerere umefikia asilimia 60 na kazi itakamilika ndani ya mwaka huu wa fedha;

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(ii) Huduma za usafiri wa anga zimetolewa kwa Viongozi Wakuu wa Kitaifa;

(iii) Gharama za bima za ndege pamoja na bima za Wanaanga zililipwa;

(iv) Wakala imeendelea kuratibu ununuzi wa ndege na kusimamia mikataba ya ukodishwaji wa Ndege za Serikali kwa Kampuni ya Ndege ya Tanzania (ATCL);

(v) Matengenezo makubwa ya Ndege mbili aina ya Gulfstream 550 na Fokker 50 zinazowahudumia Viongozi Wakuu wa Kitaifa yamefanyika kwa mujibu ya kalenda ya matengenezo iliyotolewa na watengenezaji; na

(vi) Mafunzo ya kisheria kwa wanaanga 31 yamefanyika ili kuhuisha leseni zao.

OFISI YA RAIS, SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

29. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/22, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ilitengewa **Shilingi 9,216,921,000.00**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 7,366,921,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 1,850,000,000.00** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2022 kiasi cha **Shilingi 5,273,418,955.38** kimepokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizi, **Shilingi 5,198,908,955.38** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 74,510,000.00** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

30. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Matamko ya viongozi wa Umma kuhusu rasilimali na madeni yapatayo 14,020 kati ya 15,522 yamepokelewa ikiwa ni sawa na asimilia 90.3 ya matarajio hadi kufikia Desemba, 2021;

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(ii) Malalamiko 115 ya ukiukwaji wa maadili dhidi ya Viongozi wa Umma yalipokelewa na kuchambuliwa. Kati ya malalamiko hayo, malalamiko 66 yalihusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na malalamiko 49 hayakuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma hivyo yalipelekwa kwa taasisi husika;

(iv) Uhakiki wa matamko ya rasilimali na madeni kwa viongozi wa umma na mgongano wa masilahi umefanyika kwa viongozi 425. Kati yao, viongozi wanaume ni 302 na wanawake ni 123. Kati ya viongozi waliohakikiwa asilimia 11 ya viongozi walibainika kuwa na dosari katika matamko. Aidha, viongozi asilimia moja watafanyiwa uchunguzi wa kina na viongozi ambao tuhuma zitathibitika watafikishwa kwenye Baraza la Maadili;

(v) Elimu kwa Viongozi wa Umma 3,180, Watumishi wa Umma 5,629 na Wananchi 1,386 kuhusu jinsi ya kujiepusha na mgongano wa masilahi na kuishi kwa kuzingatia kiapo cha Ahadi ya Uadilifu;

(vi) Klabu 143 za Maadili zenye wanachama 4,000 zilianzishwa katika shule za msingi na sekondari. Klabu 33 zilitembelewa kwa lengo la kukuza na kuendeleza maadili miongoni mwa wanafunzi na wanachama wa klabu. Lengo la klabu hizi ni kukuza na kuendeleza vijana katika kuzingatia maadili na kujiandaa kuwa Viongozi wa kesho;

(vii) Mapitio ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya mwaka 1995 yamefanyika katika ngazi mbalimbali za maamuzi na yanafanyiwa kazi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali; na

(viii) Ujenzi wa jengo la Ofisi ya Makao Makuu na Kanda ya Kati Dodoma la Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma umefikia hatua ya ghorofa ya tano ambayo ni sawa na asilimia 55.

**OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA
UTAWALA BORA NA TAASISI ZAKE**

A. MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA

31. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2021/2022, Fungu 32 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma: inayojumuisha taasisi zilizochini yake iliidhinishwa jumla ya **Shilingi 45,869,114,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizi, **Shilingi 38,219,114,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 7,650,000,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

32. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Machi, 2022 kiasi cha **Shilingi 33,727,642,021.89** kimepokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo **Shilingi 30,664,972,854.79** zilikuwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 3,062,669,167.10** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

33. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma pamoja na Taasisi zake imeendelea kutoa huduma kwa kuzingatia misingi ya utawala bora. Aidha, watumishi wa Umma wanawajibika na kutekeleza majukumu yao ya msingi kwa bidii, uadilifu, weledi na maarifa na kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu.

34. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2021 hadi Machi, 2022 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma pamoja na Taasisi zake ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Ujenzi wa Mfumo mpya wa Usimamizi wa Utendaji Kazi kwa Watumishi wa Umma (PEPMIS) umeanzishwa ili kuondokana na changamoto za usimamizi wa utendaji kazi zilizojitokeza katika utekelezaji wa mfumo wa awali wa OPRAS, ambao haukuakisi hali halisi ya utendaji kazi wa watumishi hali iliyoleta hisia za kupendeleana au kuoneana na kutokutumika kwa matokeo ya utendaji kazi katika kufanya maamuzi ya kiutumishi. Mfumo mpya wa PEPMIS utakuwa ni wa kielektroniki na utaondokana na matumizi ya makaratasi. Pia utaongeza uwazi katika usimamizi wa watumishi na kuondoa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

upendeleo na uonevu katika upimaji wa utendaji wa watumishi. Utaweka mifumo ya ufuatiliaji wa utendaji kazi wa watumishi kwa kuzingatia malengo yaliyowekwa na yanayopimika. Mifumo huu pia utahamasisha uwajibikaji wa hiari na kurahisisha upatikanaji wa taarifa za utendaji kazi wa watumishi;

(ii) Ujenzi wa Mfumo mpya wa Usimamizi wa Utendaji kazi katika ngazi ya Taasisi (PIPMIS) umeanzishwa. Mfumo huu ni makubaliano ya kimaandishi kati ya Serikali na Taasisi ya Umma kuhusu malengo ambayo Taasisi husika itayatekeleza katika kipindi cha mwaka mmoja. Makubaliano hayo yatakuwa kati ya viongozi wakuu wa Taasisi na Viongozi wao wanaowasimamia katika masuala ya kisera na utendaji wa kila siku. Malengo yaliyomo ndani ya mikataba yatakuwa na vigezo, shabaha na viashiria vitakavyotumika katika utendaji wa taasisi kila mwaka. Utekelezaji wa Mfumo wa PIPMIS utaongeza uwajibikaji katika utekelezaji wa sera, mikakati na vipaumbele vya taasisi, sekta na taifa kwa ujumla; kuimarisha utamaduni unaojali matokeo; na kuleta matumizi bora ya rasilimali za umma. Manufaa haya yatatokana na kuwepo kwa vigezo na viashiria vya kupima utendaji wa taasisi katika maeneo hayo, kulinganisha na kushindanisha utendaji wa taasisi na kutoa Tuzo za utendaji mzuri kila mwaka;

(iii) Maelekezo ya Rais kuhusiana na utendaji wenye matokeo katika sekta ya Umma yametekelezwa kwa kuanza kuandaa Mifumo mipya miwili ambayo ni PEPMIS na PIPMIS kwa lengo la kuimarisha dhana ya utendaji unaojali matokeo; kutoa huduma bora kwa wananchi; na kuongeza uwajibikaji wa viongozi na watumishi katika Taasisi za Umma;

(iv) Mfumo wa Tathmini ya Hali ya Rasilimaliwatu katika taasisi za umma umesanifiwa, umejengwa na kuanza kutumika mwezi Machi, 2022 katika kukusanya, kuhakiki na kuonesha mgawanyo na mtawanyiko wa watumishi ili kubainisha mahitaji ya watumishi kwenye taasisi zote za umma;

(v) Mafunzo ya matumizi ya Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Malipo ya Mishahara (HCMIS) yamefanyika kwa Maafisa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Masuuli; Wakuu wa Idara za Utawala/Utumishi; Maafisa Utumishi/ Utawala; Wakaguzi wa Ndani na Wahasibu;

(vi) Uhakiki wa watumishi kwenye Taasisi za Umma 150 pamoja na usafirishaji na uboreshaji wa taarifa za kiutumishi na mishahara kwenye Mfumo wa HCMIS umefanyika ili kuhakikisha kunakuwa na matumizi bora ya Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma;

(vii) Usimamizi wa Mfumo mpya wa HCMIS umefanyika katika Taasisi 541 ambazo zimeanza kutumia mfumo huo na kuhakikisha huduma za mfumo zinapatikanaji wakati wote. Vile vile, watumiaji wapya 558 kutoka katika Taasisi 241 walisajiliwa kwenye mfumo;

(viii) Maafisa TEHAMA na Maafisa wanaoshughulikia malalamiko 675 kutoka taasisi zilizo Kanda ya Kaskazini, Nyanda za Juu Kusini, Magharibi, Kati, Ziwa na Kanda ya Kusini wamepatiwa mafunzo ya utekelezaji wa mfumo wa kidijitali wa e-Mrejesho na Sema na Waziri wa UTUMISHI;

(ix) Uimarishaji na uboreshaji wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA umefanyika ili kurahisisha utendaji kazi na utoaji wa huduma. Vile vile, ununuzi wa vitendea kazi na mahitaji muhimu ya TEHAMA ikiwemo mifumo, programu, kompyuta, printa, skana, simu, umefanyika ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo ya matumizi bora na salama ya mifumo na vifaa vya TEHAMA;

(x) Uhuishaji wa Mkakati wa Taifa wa Serikali Mtandao wa mwaka 2021-2026 unaendelea ambapo rasimu ya mkakati imekamilika na hatua za mwisho za uidhinishaji zinafuatiliwa. Vile vile, rasimu ya kwanza ya Mkakati wa Serikali wa Kujilinda na Majanga ya Kimtandao ya Mwaka 2017 imeandaliwa na kukamilika. Ukusanyaji wa maoni kutoka kwa wadau ili kuboresha Mkakati huu unaendelea;

(xi) Uratibu wa uanzishwaji wa Vituo vitatu vya Huduma Pamoja (One Stop Centres) umefanyika ambapo Vituo 2 vya Huduma Pamoja vimeanzishwa katika Ofisi za Shirika la Posta

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Dar es Salaam na Dodoma. Vile vile, Mwongozo wa kusimamia utekelezaji wa Mradi wa Huduma Pamoja umeandaliwa na kuanza kutumika mwezi Desemba, 2021. Mwongozo huo umeainisha majukumu ya wadau muhimu katika mradi huo;

(xii) Uratibu wa uanzishwaji wa Mradi wa Tanzania ya Kidijitali umefanyika ambapo nyaraka zote za Mradi zimekamilika na mradi umeanza kutekelezwa mwezi Septemba, 2021. Utekelezaji wa maeneo ya mradi yanayohusu masuala ya Serikali Mtandao unaendelea kuratibiwa;

(xiii) **Watumishi 190,781** wenye sifa stahiki wamepandishwa vyeo/madaraja;

(xiv) Madeni ya mishahara ya **Watumishi wa Umma 65,394** yenye thamani ya **Shilingi 91,087,826,006.34** yamelipwa;

(xv) Watumishi wa Umma 19,386 wamebadilishwa kada;

(xvi) Vibali vya **ajira mpya na mbadala kwa nafasi 12,336** vimetolewa;

(xvii) Taasisi za Umma 42 zimewezeshwa kuandaa Mipango ya Rasilimaliwatu, Taasisi 44 zimewezeshwa kuandaa Mipango ya Urithishanaji Madaraka na Taasisi 8 zimewezeshwa kuandaa Mipango ya Mafunzo ili kuhakikisha wanakuwepo watumishi wa umma wenye sifa stahiki na weledi katika nafasi zote kwenye utumishi wa umma;

(xviii) Miundo ya Wizara 22 na Taasisi za Umma 28 imekamilishwa na kuidhinishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwasilishwa kwenye Wizara na Taasisi husika kwa ajili ya utekelezaji. Vile vile, Miundo ya Taasisi 35 imechambuliwa na imepitishwa na Kamati ya Rais ya Utekelezaji (PIC) na kuwasilishwa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya kupata idhini ya utekelezaji. Aidha, uchambuzi wa miundo ya Taasisi 80 umefanyika na ipo kwenye hatua ya kujadiliwa kwenye vikao vya Kamati ya Rais ya Utekelezaji (PIC) na miundo ya Wizara

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

tatu zilizofanyiwa marekebisho inafanyiwa mapitio ili kukidhi mabadiliko ya hati idhini;

(xix) Mapitio ya Sheria na Miongozo ya Kiutumishi yamefanyika kwa lengo la kuboresha utendaji kazi pamoja na kutoa miongozo ya kuimarisha Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Shughuli hizo zilikusisha ukamilishaji wa marekebisho ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003; Kutafsiri Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma za Mwaka 2009 kutoka lugha ya Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili; Uandaaji wa Waraka wa Mkuu wa Utumishi wa Umma Na. 2 kuhusu Utaratibu wa Matumizi, aina na Stahili za Magari kwa Viongozi katika Utumishi wa Umma; na Waraka wa Utumishi Na. 1 wa mwaka 2022 kuhusu Utaratibu wa Watendaji Wakuu wa Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma kuhudhuria Vikao vya Menejimenti za Wizara Mama;

(xx) Marekebisho ya Kanuni za Kudumu Katika Utumishi wa Umma za Mwaka 2009 yamefanyika na mchakato wa tathmini ya Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ya Mwaka 2008 umeanzishwa;

(xxi) Masharti ya kazi ya viongozi wa umma walio katika nafasi za kisiasa yameandaliwa na kutolewa;

(xxii) Taasisi 20 za Umma zimefanyiwa ufuatiliaji wa namna ya kutekeleza miongozo ya anuai za jamii mahali pa kazi. Aidha, imeandaliwa Rasimu ya Mwongozo wa ujumuishaji wa masuala ya jinsia katika Utumishi wa Umma;

(xxiii) Taarifa ya utekelezaji wa Mkataba wa Afrika wa Maadili na Misingi ya Utumishi wa Umma na Utawala (*The African Charter on Values and Principles of Public Service and Administration*) imeandaliwa;

(xxiv) Sera za Usimamizi wa Rasilimali watu katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) zimepitwa na kuhuishwa;

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(xxv) Miundo ya Maendeleo ya Utumishi ya Kada mbalimbali zilizo chini ya Wizara 22 na Wakala za Serikali na Mashirika ya Umma 47 imehuishwa;

(xxvi) Utawala wa Utumishi wa Umma umeendelea kufanyika kwa kuchakata mahitaji ya vibali kwa Waajiri na watumishi mbalimbali ikiwemo vibali vya uhamisho (4,405), kushikizwa (36), kuazimwa (1,490) na vibali (384) vya likizo bila malipo;

(xxvii) Uwianishaji na uoanishaji wa mishahara na mipango ya motisha katika Utumishi wa Umma umeendelea kufanyika ikiwemo kuandaa Mwongozo wa Posho na Masilahi katika Utumishi wa Umma kwa lengo la kuoanisha masilahi katika utumishi wa Umma na kuhisha Miundo ya Mishahara ya Wakala za Serikali na Mashirika ya Umma 47;

(xxviii) Maombi ya vibali mbalimbali yameshughulikiwa ikiwemo vibali 959 vya uteuzi ili kujaza nafasi za uongozi, vibali 830 vya kukaimu nafasi za uongozi na vibali 665 vya ajira za mikataba, ili kuimarisha uwepo wa viongozi wenye sifa stahiki, weledi na maono ya utumishi wa umma pamoja na kuimarisha ufanisi wa utendaji kazi;

(xxix) Taasisi za Umma 16 zimewezeshwa kuandaa Mahitaji ya Watumishi wa Umma ili kupata uwiano mzuri wa watumishi katika kutekeleza majukumu ya Taasisi husika;

(xxx) Upatikanaji wa fursa za mafunzo 216 ya muda mrefu na mfupi zinazotolewa na Wadau wa Maendeleo umeratibiwa kwa lengo la kuwaongezea watumishi wa umma ujuzi na maarifa katika utekelezaji wa majukumu. Kati ya fursa hizo, nafasi za mafunzo 67 ni za mafunzo ya muda mrefu kutoka Jamhuri ya Watu wa China, nafasi 24 kutoka Serikali ya Korea na nafasi za mafunzo 125 ni za mafunzo ya muda mfupi kutoka Serikali ya Korea, Malaysia, Thailand na China;

(xxxi) Utoaji wa mafunzo elekezi kwa Viongozi 59 ambao ni Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala wa mikoa ya Tanzania Bara umeratibiwa ili kuwajengea uwezo katika usimamizi na utoaji wa maamuzi ya kimkakati;

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(xxxii) Usimamizi wa Mikataba ya Ushirikiano wa Kimataifa na Kikanda umefanyika ili kuhakikisha kuwa watumishi wa umma wanapata fursa za ajira katika taasisi ambazo Tanzania ni mshirika. Nafasi 13 za ajira kutoka Jumuiya ya Madola, UNEP, UNWTO, ICGRL, SADC, AFDB na nafasi katika Jopo la Wataalamu wa Umoja wa Mataifa kushughulikia masuala ya Sudan zilipokelewa kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na kutangazwa ili wataanzania wenye sifa waweze kuomba;

(xxxiii) Uratibu na ufuatiliaji wa ajira za wageni katika Utumishi wa Umma na Miradi ya Kimkakati umefanyika ambapo vibali 391 vyenye msamaha wa ada vimetolewa kwa wataalam wa kigeni kufanya kazi katika Utumishi wa Umma na Miradi mbalimbali ya kimkakati;

(xxxiv) Watumishi wa Umma 1,772 kutoka Taasisi za Umma 38 wamejengewa uelewa kwa kupatiwa mafunzo kuhusu Uzingatiaji wa Maadili ya Utendaji kazi katika Utumishi wa Umma;

(xxxv) Taasisi za Umma 15 zimefanyiwa ufuatiliaji wa uzingatiaji wa maadili ya Utendaji kazi katika Utumishi wa Umma. Pia, Mfumo wa Ushughulikiaji wa Malalamiko ya Wananchi katika Utumishi wa Umma umefuatiliwa;

(xxxvi) Kampeni za uimarishaji wa uzingatiaji wa maadili kwenye taasisi za umma na vyama vya Kitaaluma zimefanyika kupitia Kikao kazi ambapo walishiriki 40 kutoka taasisi za Umma walihudhuria;

(xxxvii) Wananchi wamehabarishwa kuhusu huduma zitolewazo na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na namna ya upatikanaji wake ambapo taarifa 72, matukio 447 katika picha, makala fupi za mwendo (Video clips) 114, makala mbili za mwendo (documentary) na nakala 27 za Gazeti la Serikali zenye taarifa za kiutumishi zililotolewa kwa umma kupitia magazeti, televisheni, redio, mitandao ya kijamii ya watu binafsi, mitandao ya kijamii ya ofisi na tovuti ya ofisi;

(xxxviii) Ujenzi wa jengo la ghorofa tano la Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora umeanza na umefikia hatua ya ghorofa ya tatu; na

(xxxix) Huduma zimeendelea kutolewa kwa Viongozi Wakuu wa Kitaifa (Wastaafu 11 na wajane 7) kwa mujibu wa sheria.

B. CHUO CHA UTUMISHI WA UMMA (TPSC)

35. Mheshimiwa Spika, Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania kilianzishwa ili kutoa mafunzo, ushauri, kufanya utafiti tumizi na kutoa machapisho mbalimbali katika nyanja za Uongozi, Menejimenti na Utawala. Chuo kinaendesha mafunzo ya muda mfupi kwa Watumishi wa Umma yanayolenga kuwajengea uwezo katika nyanja za utawala, usimamizi wa utendaji kazi za kila siku, menejimenti pamoja na uongozi. Mafunzo hayo hutolewa katika hatua ya awali kwa watumishi wapya wa umma, (induction) hatua ya kati kwa Maafisa Waandamizi na Maafisa Wakuu, hatua ya juu kwa Viongozi wa Umma wanaochipukia na mengine kulingana na mahitaji ya wadau wa Chuo. Mafunzo yote hayo yanalenga kuboresha utendaji kazi katika utumishi wa umma ili kuleta tija na ufanisi katika huduma zinazotolewa kwa umma. Vile vile, Chuo kinasaidia Serikali kukuza Sera za Utamaduni wa kujifunza na kusaidia utumiaji wa teknolojia miongoni mwa watendaji katika kutekeleza majukumu yao.

36. Mheshimiwa Spika, Chuo kinatoa mafunzo ya muda mrefu katika ngazi za Astashahada, Stashahada na Shahada katika nyanja za Utunzaji wa Kumbukumbu, Uhazili, Menejimenti ya Rasilimaliwatu, Ununuzi na Ugavi, na Utawala wa Umma. Chuo cha Utumishi wa Umma ndicho chuo pekee hapa nchini kinachotoa shahada ya Uhazili.

37. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake Chuo kina Kampasi sita zilizoko kwenye Mikoa ya Dar es Salaam, Tabora, Mtwara, Singida, Tanga na Mbeya. Pia, Chuo kinatoa huduma za mafunzo kwa njia ya mtandao kupitia kituo cha mafunzo kwa njia ya mtandao kilichopo Dar es Salaam - TPSC Global Learning Centre (TGLC).

38. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 shughuli zifuatazo zimetokeleza:

(i) Watumishi wa Umma 1,102 walipatiwa mafunzo ya kujiandaa kufanya Mitihani ya Utumishi wa Umma hiyo ni sawa na asilimia 157 ya Watumishi waliolengwa;

(ii) Watumishi wa Umma 5,722 wamepatiwa mafunzo yahasuyo Uongozi na Maendeleo; pamoja na Manejimenti na Usimamizi wa Ofisi katika Taasisi za umma, sawa na asilimia 78 ya lengo la mwaka. Kati yao watumishi 4,398 walipatiwa mafunzo kwa njia ya ana kwa ana na watumishi 1,024 walipatiwa mafunzo kwa njia ya mtandao;

(iii) Mafunzo ya Awali yalitolewa kwa Watumishi wa Umma wapatao 721 sawa na asilimia 28 ya lengo la mwaka, pia hamasa kwa waajiri ilitolewa kwa waajili kuwasisitiza kupeleka watumishi kupata mafunzo ya awali mara baada ya kuajiriwa;

(iv) Wanafunzi 10,598 walidahiliwa katika ngazi ya Shahada ya Kwanza, Stashahada na Cheti, kwa ajili ya mafunzo ya muda mrefu katika fani za utunzaji wa kumbukumbu, uhazili, TEHAMA, utunzaji wa fedha za umma, na Menejimenti ya Rasilimaliwatu, usimamizi wa ununuzi wa umma, uongozi na utawala bora;

(v) Maandiko ya ushauri katika maeneo tano ya kitaalamu yameandaliwa na kuwasilishwa kwa wateja. Aidha, shauri katika maeneo matano ya kitaalam katika Menejimenti ya Utumishi wa Umma sawa na asilimia 83 ya lengo ulitolewa;

(vi) Watumishi 40 wa Chuo cha Utumishi wa Umma wamewezeshwa kujenga uwezo katika taaluma mbalimbali, kama ifuatavyo: Shahada ya uzamivu 5, Shahada ya uzamili 6 na mafunzo ya muda mfupi watumishi 29;

(vii) Ujenzi wa majengo katika Kampasi ya Singida awamu ya kwanza unaohusisha ujenzi wa Maabara za Kuchapa (*Typing Labs*) umefikia asilimia 55. Mradi huu utakamilika kufikia Juni 30, 2022. Mradi wa Tanga utaanza baada ya taratibu za

umilikishaji wa eneo kukamilika. Aidha, mradi wa ujenzi wa katika Kanda ya Ziwa utanza baada ya miradi ya Singida na Tanga kumamilika; na

(viii) Maeneo ya ujenzi wa Kampasi za Dodoma, Tanga na kanda ya ziwa yamepatikana na taratibu za umilikishwaji wa maeneo husika zinaendelea. Aidha, ufuatiliaji wa upatikanaji wa eneo kwa ajili ya ujenzi wa Kampasi ya Mbeya unaendelea.

C. MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO (e-GA)

39. Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), ilianzishwa kwa Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya Mwaka 2019. Mamlaka ilianzishwa ili Kuratibu, Kusimamia na Kukuza jitihada za Serikali Mtandao pamoja na kuhimiza utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao kwa taasisi za umma. Mamlaka imerithi iliyokuwa Wakala ya Serikali Mtandao ambayo iliundwa kwa Sheria Na. 30 ya Wakala za Serikali, Sura ya 245 ya Mwaka 1997 na kuwa na jukumu la Kuratibu, Kusimamia na Kukuza Jitihada za Serikali Mtandao nchini bila kuwa na nguvu ya kisheria ya kuhimiza utekelezaji (kuwa chombo rekebu). Wakala ilitekeleza majukumu yake kwa kipindi cha miaka nane tangu kuzinduliwa kwake Mwezi Aprili, 2012 mpaka Mwezi Machi, 2020.

40. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai 2021, hadi Machi, 2022, Mamlaka imetekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:

(i) Mfumo maalum (Government Enterprise Service Bus, GovESB) wa kuwezesha mifumo ya Serikali kusomana na kubadilishana taarifa umesanifiwa, umejengwa na taasisi 12 zimeunganishwa. Pia, mpango kazi wa kuziunganisha Taasisi zote za Serikali zenye mifumo umeandaliwa. Aidha, viwango na miongozo imeandaliwa kuwezesha ubadilishanaji wa taarifa kuwa endelevu, wenye tija na usalama wa taarifa;

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(ii) Mifumo ya kidijitali ya kurahisisha utoaji huduma kwa umma kupitia sekta mbalimbali imesanifiwa na kujengwa kwa kushirikiana na Taasisi husika, baadhi ya mifumo hiyo ni:

(a) Mfumo wa kusimamia vyama vya ushirika - Tume ya Ushirika: Lengo la mfumo huu ni kusimamia usajili na uendeshaji wa shughuli za vyama vya ushirika nchi nzima;

(b) Mfumo wa Kusimamia Shughuli za Mamlaka za Maji – Wizara ya Maji: Lengo la mfumo huu wa pamoja ni kusimamia ankara za maji za wateja, malipo na maeneo yote yanayohusu mteja wa maji. Mamlaka za maji 71 kati ya 94 zinautumia mfumo huo. Taasisi 26 zilizobaki zitaunganishwa na mfumo huo ndani ya Mwaka wa Fedha 2022/2023;

(c) Mfumo wa Kuratibu Vibali vya Kazi nje ya nchi - Wizara ya Kazi: Lengo la mfumo huu ni kuratibu vibali vya kufanya kazi nje ya nchi;

(d) Mfumo wa Kusimamia Huduma za Wakala wa Ununuzi – GPSA: Lengo la mfumo huu ni kusimamia shughuli za usimamizi wa mafuta ya magari ya Serikali, uondoshaji wa mizigo kupitia GPSA na ununuzi wa magari ya Serikali. Mfumo huu umeanza kutumika kuanzia tarehe 1 Machi, 2022;

(e) Mfumo wa Kusimamia Stakabadhi Ghalani – Bodi ya Kusimamia Stakabadhi Ghalani: Kuandikisha na kusimamia uendeshaji wa maghala ya mazao;

(f) Mfumo wa Kupokea Mrejesho kutoka kwa wananchi – Ofisi ya Rais, Utumishi. Lengo ni kuwawezesha wananchi kuwasiliana na serikali ili kuleta malalamiko, maoni, pongezi na ushauri;

(g) Mfumo wa Kusimamia Shughuli za Wasanii – BASATA na Bodi ya Filamu (Wizara ya Michezo): Lengo la mfumo huu ni kuwezesha wasanii kuwasilisha kazi zao na kupata v i b a l i mbalimbali kutoka BASATA na Bodi ya Filamu; na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(h) Mfumo wa Kusimamia Leseni za usafirishaji – LATRA: Lengo la mfumo huu ni kusimamia shughuli za LATRA katika utoaji leseni za usafirishaji n.k.

(iii) Tathmini za Utendaji na Usalama wa Mifumo mbalimbali ya TEHAMA kwenye Taasisi za Serikali zimefanyika, mapungufu yameainishwa na kutoa ushauri juu ya maboresho; aidha ukaguzi wa mifumo ya Serikali kama inakidhi vigezo vya viwango na miongozo imefanyika na maeneo ya kuboresha yameainishwa kwa Taasisi husika kuyafanya kazi;

(iv) Mifumo Shirikishi ya TEHAMA imesimamiwa na kuboreshwa kwa lengo la kuihuisha na kuiendeleza ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia, kuboresha usalama na kukidhi mahitaji mapya ya watumiaji, mfano: GMS, MGov, e-Office, ERMS, GePG, n.k;

(v) Kusimamia, kuendesha na kuendeleza miundombinu shirikishi ya TEHAMA, mfano vituo vya kutunzia mifumo, mtandao wa mawasiliano wa Serikali (Govnet), nk;

(vi) Vituo maalum vya kuhifadhi miundombinu na mifumo ya Serikali kimtandao vimeendelea kuboreshwa ikiwa ni pamoja na kununua vifaa vinavyohitajika ili kuwezesha Government Private Cloud (GovCloud);

(vii) Usimamizi wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA ya Serikali iliyohifadhiwa kwenye vituo vya Serikali vya kuhifadhi taarifa za Serikali na Taasisi za Umma, ikiwa ni pamoja na kuongeza vitendea kazi/vifaa na masafa ya Intaneti ili kuhakikisha mifumo inafanya kazi kwa usahihi, inapunguza gharama za utendaji kazi na kuboresha utoaji wa huduma kwa Umma;

(viii) Uandaaji wa Viwango na Miongozo mbalimbali umekamilishwa ili kuiwezesha Mifumo ya TEHAMA ya kimkakati na ya kisekta kuwasiliana, pia uzingatiaji wa Viwango na Miongozo umefuatiliwa;

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(ix) Mafunzo ya Serikali Mtandao yametolewa kwa Viongozi, Wasimamizi wa TEHAMA na watumiaji wa huduma za Serikali Mtandao kwa Taasisi za Serikali ili kuongeza umiliki (ownership), uelewa katika kutumia TEHAMA, kuongeza ufanisi wa kiutendaji na utoaji wa huduma kwa wananchi; aidha, mafunzo yametolewa kwa watumishi wa Mamlaka ili kuwaongezea uwezo;

(x) Ushauri wa kitaalam na msaada wa kiufundi kwenye maeneo ya TEHAMA kwa taasisi za Serikali kuhusu uendeshaji wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA na utoaji wa huduma mbalimbali ulitolewa. Vile vile, ushauri kwenye Miradi ya TEHAMA ulitolewa ili miradi hiyo iweze kutoa matokeo yenye tija na inayozingatia viwango; na

(xi) Utafiti na ubunifu wa matumizi ya teknolojia mpya za TEHAMA katika utoaji huduma kwa umma na utendaji wa Serikali, ambapo mifumo mipya imeweza kubuniwa, mfano, mfumo wa e-Mrejesho, e-Mikutano, nk.

D. WATUMISHI HOUSING COMPANY (WHC)

41. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai 2021, hadi Machi, 2022, Watumishi Housing Company imetekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:

(i) Mpango umeandaliwa wa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa kutatua tatizo la makazi kwa watumishi kwa maeneo ya pembezoni;

(ii) Mfumo wa kuendesha Mfuko wa kukopesha (revolving fund) umeanza kutengenezwa na utasaidia ujenzi wa nyumba zenye gharama nafuu zitakazowanufaisha wafanyakazi wa kada zote;

(iii) Ujenzi wa nyumba 80 katika eneo la Njedengwa jijini Dodoma umeendelezwa; na

(iv) Upatikanaji wa kiwanja katika eneo la Mtumba karibu na Mji wa Serikali kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 1000 za gharama

nafuu umesimamiwa. Ununuzi wa viwanja namba 383, 384, 385 na 549 vyenye jumla ya mita za mraba 42,753 eneo la Chamwino - Dodoma na kiwanja namba 695 chenye ukubwa wa mita za mraba 76,774 eneo la Mtumba umefanyika. Vile vile, taarifa ya Upembuzi Yakinifu (Feasibility Study) kwa ajili ya ujenzi wa nyumba katika viwanja husika imewasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya kupata kibali cha kukopa fedha za ujenzi.

OFISI YA RAIS, SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA

42. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma ni idara inayojitegemea iliyoanzishwa kwa mujibu wa Kifungu 29 (1) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298 ili kusimamia mchakato wa ajira katika Utumishi wa Umma. Katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Fungu 67: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma iliidhinishiwa **Shilingi 3,388,771,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Machi, 2022, **Shilingi 3,238,198,766.09** zilipokelewa na kutumika.

43. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2021 hadi Machi, 2022, Sekretarieti imetekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Michakato ya ajira ilisimamiwa ili kuwezesha waajiri kupata watumishi wenye sifa zinazotakiwa kwa mujibu wa miundo ya taasisi husika, ambapo saili 13 kwa niaba ya Mamlaka za Ajira mbalimbali zimesimamiwa na waliofaulu usaili walipangiwa vituo vya kazi;

(ii) Utaalam wa masuala ya uendeshaji wa michakato ya ajira ulitolewa kwenye usaili unaoendeshwa na Taasisi zinazotumia Sheria zilizokasimiwa;

(iii) Mchakato wa ajira za Muungano umeboreshwa kwa kuongeza majukumu ya kawaida na idadi ya watumishi katika Ofisi ya Sekretarieti ya Ajira iliyopo Zanzibar;

(iv) Ujenzi wa programu ya "**Ajira Portal App**" ambayo itawaraisishia waombaji kazi kupata taarifa za ajira na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mrejesho wa michakato ya Ajira kupitia simu zao za kiganjani umekamilika na imeanza kutumika na kupunguza gharama za matangazo kwenye vyombo vya Habari na kuwafikia waombaji wengi kwa urahisi na uharaka;

(v) Utoaji wa elimu kwa Umma na matangazo kuhusu ajira umefanyika kupitia runinga za TBC, ITV na Azam Media, tovuti na mitandao ya kijamii. Elimu na matangazo hayo yalihusu majukumu ya Sekretarieti ya Ajira, ufafanuzi wa maswali na maoni ya wadau, uwepo wa nafasi za kazi, kuitwa kwenye usaili, kupangiwa vituo vya kazi pamoja na taarifa mbalimbali zinazohusiana na mchakato wa ajira na matumizi ya Mfumo wa maombi ya kazi;

(vi) Vyeti 3,328 vya waombaji kazi vilifanyiwa uhakiki kwa ushirikiano na Taasisi mbalimbali ili kubaini uhalali ambapo vyeti 3,313 kati ya hivyo vilithibitishwa kuwa ni halali ikiwa ni sawa na asilimia 99.5 na vyeti 15 vilithibitishwa kuwa sio halali ambavyo ni sawa na asilimia 0.5 ya vyeti vilivyohakikiwa;

(vii) Utafiti wa kupata mrejesho wa utekelezaji wa majukumu ya Sekretarieti ya Ajira kutoka kwa wadau wake umefanyika;

(viii) Vitendea kazi vinavyojumuisha magari mawili kwa ajili ya usimamizi wa saili mbalimbali zinazofanywa na Sekretarieti ya Ajira vimeongezwa. Vile vile, Huduma za kiutawala na kiutumishi kwa Ofisi ya Zanzibar zilitolewa; na

(ix) Ujenzi wa jengo la Ofisi za Makao Makuu ya Sekretarieti ya Ajira Dodoma umeanzishwa kwa kukamilisha utafiti wa udongo na michoro.

OFISI YA RAIS, TUME YA UTUMISHI WA UMMA

44. Mheshimiwa Spika; Tume ni chombo rekebu chenye mamlaka na wajibu wa kuhakikisha kuwa masuala ya Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma yanasimamiwa na kuendeshwa kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali kama inavyotolewa na Mamlaka.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

45. Mheshimiwa Spika: katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Tume ya Utumishi wa Umma iliidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 6,560,233,829** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Machi, 2022 kiasi cha **Shilingi 5,184,280,712.96** zilipokewa na kutumika ikiwa ni matumizi ya kawaida. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2021 hadi Machi, 2022, Tume imetekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Ukaguzi wa Rasilimaliwatu kwa Waajiri, Mamlaka za Ajira na Mamlaka za Nidhamu kwenye Taasisi 110 kati ya 150 umefanyika;

(ii) Rufaa 206 zimeshughulikiwa na kutolewa uamuzi na malalamiko 125 ya Watumishi wa Umma yalihitimishwa;

(iii) Rufaa 90 na malalamiko nane yamechambuliwa tayari kuwasilishwa mbele ya Tume kwa uamuzi;

(iv) Taarifa ya Hali ya Utumishi wa Umma na Utekelezaji wa Majukumu ya Tume kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 imeandaliwa;

(v) Maulizo 1,022 ya watumishi wa Umma, waajiri, mamlaka za ajira na nidhamu kuhusu rufaa na malalamiko yalipokelewa kwa njia mbalimbali na kushughulikiwa;

(vi) Mafunzo kwa watumishi 67 wa Tume kwa ajili ya kuwajengea uwezo kuhusu uchambuzi wa rufaa na malalamiko na ukaguzi wa Rasilimaliwatu yalitolewa. Vile vile, Mafunzo ya kuwajengea uwezo Waajiri, Mamlaka za Ajira na Mamlaka za Nidhamu kuhusu uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma yalitolewa kwa Taasisi tisa;

(vii) Uhuishaji wa Miongozo ya Tume kuhusu uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu na kuisambaza kwa Wadau ulifanyika ambapo, Mwongozo kuhusu ushughulikiaji wa masuala ya Nidhamu, Rufaa na Malalamiko umehuishwa;

(viii) Elimu kwa wadau kuhusu Sheria, Kanuni, Taratibu, na Miongozo inayosimamia Utumishi wa Umma na kuhusu

majukumu ya Tume ilitolewa kupitia vyombo vya habari, mitandao ya kijamii na tovuti ambapo vipindi sita vya Televisheni vilirushwa kupitia TBC 1, Star TV, Channel 10 na AZAM TV na vipindi vitano vya Radio vilirushwa kupitia Magic Radio, TBC Taifa na 92.6 AFM ya Dodoma;

(ix) Ukarabati wa jengo la Ofisi Dodoma baada ya kuhamia makao makuu ulifanyika; na

(x) Watumishi 74 wa Tume walielimishwa kuhusu VVU/UKIMWI, Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza mahali pa kazi na Mapambano dhidi ya Rushwa. Vile vile, huduma kwa watumishi wa Tume wanaoishi na VVU/UKIMWI na watumishi wenye mahitaji maalum zilitolewa.

OFISI YA RAIS, IDARA YA KUMBUKUMBU NA NYARAKA ZA TAIFA

46. Mheshimiwa Spika; kwa mujibu wa Sheria ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa Na. 3 ya mwaka 2002, Idara ya Kumbukumbu ya Nyaraka za Taifa ina jukumu la kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu za utunzaji kumbukumbu na nyaraka katika Taasisi za Umma. Aidha, jukumu lingine ni kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Kuwaenzi Waasisi wa Taifa Na. 18 ya Mwaka 2004 kwa kukusanya, kutunza na kuhifadhi kumbukumbu na vitu vya Waasisi wa Taifa letu (Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume).

47. Mheshimiwa Spika; katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Ofisi ya Rais - Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 4,571,018,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,571,018,000** ni matumizi ya kawaida na **Shilingi 2,000,000,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022. jumla ya **Shilingi 2,098,975,110.97** zilipokewa na kutumika. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,758,975,110.97** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 340,000,000** kwa ajili ya matumizi ya miradi ya Maendeleo.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

48. Mheshimiwa Spika; kwa kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2021 hadi Machi, 2022, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa imetekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Jumla ya nyaraka **3,224** zenye umuhimu katika historia ya Nchi yetu zimekusanywa kutoka katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 17 na Taasisi zingine za Umma tatu. **KIAMBATANISHO NA. 12 Uk. 237 - 238;**

(ii) Jumla ya majalada ya mashauri yaliyofungwa **3,192** kutoka Mahakama Kuu Kanda ya Mwanza na Kagera yamekusanywa na kuhifadhiwa katika Kituo cha Kanda ya Ziwa – Mwanza;

(iii) Mfumo wa masijala mtandao (**e-File Management System**) umewekwa katika Taasisi za Umma 24 na kufikia taasisi 140 tangu mfumo huu uanzishwe. **KIAMBATANISHO NA. 13 Uk. 239;**

(iv) Mfumo wa Utunzaji wa Kumbukumbu za Kiutendaji (**Keyword Filing System**) umewekwa katika Taasisi za Umma 27. **KIAMBATANISHO NA. 14 Uk. 240;**

(v) Ukaguzi wa hali ya utunzaji wa kumbukumbu katika Taasisi za Umma 26 umefanyika kwa lengo la kujua hali halisi ya utunzaji wake ili kubaini changamoto wanazokabiliana nazo na kuzipatia ufumbuzi. **KIAMBATANISHO NA. 15 Uk. 241;**

(vi) Mafunzo ya utunzaji wa kumbukumbu yalitolewa katika Taasisi za Umma 16. **KIAMBATANISHO NA. 16 Uk. 242;**

(vii) Taasisi tatu zimewezeshwa kutengeneza mwongozo wa utunzaji na uteketezaji wa kumbukumbu kwa mujibu wa Sheria. Taasisi hizo ni Shirika wa Uwakala wa Meli (TASAC), Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi ya Elimu ya Juu (HESLB), na Chuo cha Uongozi wa Mahakama (IJA) – Lushoto;

(viii) Ukarabati wa nyaraka zilizohifadhiwa katika Ghala Kuu la Taifa katika ofisi za Kanda ya Mashariki Dar es salaam umefanyika, ambapo nyaraka kongwe 61 zimekarabatiwa zikiwemo za uliokuwa utawala wa kikoloni wa Mwingereza (33), Government gazette (15) na Hansard (13);

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(ix) Tathimini ya majalada ya iliyokuwa Wizara ya Ushirika na Masoko zilizohifadhiwa katika Kituo cha Taifa cha Kumbukumbu Dodoma ilifanyika ili kubaini zile zenye umuhimu ili ziendelee kuhifadhiwa katika viwango stahiki na kubaini zile ambazo umuhimu wake wa matumizi umefika ukomo kwa mujibu wa Sheria;

(x) **Majalada 335** yamewekwa kwenye mfumo wa kielekroniki (Digital Records Management and Preservation System) ili kurahisisha upatikanaji wake na kwa lengo la kulinda nakala halisi za nyaraka hizo ili ziweze kudumu kwa muda mrefu; Kumbukumbu **437** za Waasisi wa Taifa (*Mwl. Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume*) zimetambuliwa, kukusanywa na kuhifadhiwa;

(xi) Vipindi viwili vimerushwa kupitia Televisheni ya Taifa (TBC) kuhusu majukumu mbalimbali ya Idara kwa lengo la kutoa elimu kwa umma; na

(xii) Uwezo wa utendaji wa watumishi wa ndani umeimarishwa, ambapo watumishi wawili waliwezesha kuhudhuria kongamano la Bodi ya Manunuzi na Ugavi (PSTB), mtumishi mmoja anaendelea na mafunzo ya muda mrefu katika shahada ya uzamili katika Sanaa ya Uchumi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Mtumishi mmoja alihudhuria mafunzo ya viwango vya uhasibu vya sekta ya umma vya kimataifa (IPSAS) yanayotolewa na Bodi ya Wahasibu (NBAA), wahudumu watatu walihudhuria mafunzo ya uhudumu yanayotolewa na Chuo cha NIP mkoani Morogoro na Watumishi wawili walihudhuria mafunzo ya ukutubi yanayoandaliwa na Bodi ya Wakutubi Tanzania.

MPANGO WA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2022/23 NA MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIWA

49. Mheshimiwa Spika, Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 umeandaliwa kwa kuzingatia, Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025, Maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 pamoja na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/

26), unaotaka Tanzania iwe na Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu. Maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 ni nguzo muhimu ya mpango unaotarajiwa kutekelezwa. Shughuli zitakazotekelezwa na kila taasisi ni kama ifuatavyo:-

OFISI YA RAIS, IKULU NA TAASISI ZAKE

A. OFISI YA RAIS – IKULU

50. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/23, Ofisi ya Rais, Ikulu imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kutoa ushauri kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika masuala ya Siasa, Uchumi, Jamii, Sheria, Diplomasia, Mawasiliano na Habari, Uhusiano wa Kikanda, Kimataifa na ushauri mwingine kwa lengo la kumsaidia Rais kufanya maamuzi;

(ii) Kutoa ushauri kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu ratiba ya kila siku;

(iii) Kutoa huduma kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na familia yake;

(iv) Kuratibu, kuandaa na kushiriki mikutano 60 ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, mikutano 40 ya Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu (IMTC) na mikutano 20 ya Baraza la Mawaziri;

(v) Kuandaa mikutano miwili ya tathmini wa mwaka kati ya Waratibu wa Shughuli za Baraza la Mawaziri wa Wizara, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na wadau wengine;

(vi) Kutoa mafunzo kuhusu utayarishaji na uwasilishaji wa Nyaraka za Baraza la Mawaziri na uchambuzi wa sera kwa Maofisa wa Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na Waratibu wa Shughuli za Baraza la Mawaziri wa Wizara;

(vii) Kuchambua na kutoa ushauri kwa Katibu Mkuu Kiongozi katika masuala ya kiuchumi, kijamii, kisheria, kiulinzi na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kiusalama, kimataifa na masuala mengine yote yanayowasilishwa;

(viii) Kufanya mafunzo na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu na Programu za Maboresho katika ngazi za Wizara, Mikoa na Serikali za Mitaa;

(ix) Kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu kwa kushirikisha wadau wa Sekta ya Umma na Binafsi; Kuandaa na Kutekeleza Mkakati mpya wa Taifa wa Mapambano Dhidi ya Rushwa;

(x) Kukamilisha tathmini ya utekelezaji wa Awamu ya Tatu ya Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa;

(xi) Kupokea na kuchambua taarifa za robo mwaka za utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Programu nyingine za maboresho;

(xii) Kuendelea kujenga uwezo wa Taasisi za Umma kuhusu uzingatiaji wa utawala bora katika kutoa huduma kwa umma;

(xiii) Kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Programu za maboresho katika ngazi za utekelezaji;

(xiv) Kupokea, kupitia na kuchambua rufaa na malalamiko ya watumishi wa umma na wananchi;

(xv) Kuendesha mikutano mitau ya Watendaji na Maafisa wa Serikali kuhusu utaratibu wa kushughulikia malalamiko na rufaa pamoja na kufuatilia utekelezaji wa maagizo mbalimbali ya Katibu Mkuu Kiongozi;

(xvi) Kufanya ziara ya ufuatiliaji wa uzingatiaji wa sheria na maelekezo yanayotolewa na Katibu Mkuu Kiongozi na Mkuu wa Utumishi wa Umma yanayohusu masuala ya Usimamizi wa utawala wa Utumishi kwenye Wizara, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(xvii) Kuratibu na kusimamia Miradi ya Maendeleo ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) na Programu ya Kujenga Uwezo wa Taasisi za Serikali Kupambana na Rushwa (BSAAT).

(xviii) Kuendelea na uboreshaji wa Ikulu ya Chamwino kwa kuanza ujenzi wa ukumbi wa mikutano (multi purpose hall) na baadhi ya ofisi; na

(xix) Kukarabati majengo ya Ikulu Ndogo za Mwanza, Tabora, Shinyanga, Lushoto Arusha na rest house moja Zanzibar.

B. TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA (TAKUKURU)

51. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/23, TAKUKURU imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kufanya utafiti na uchambuzi wa mifumo ya kiutendaji na utoaji huduma katika sekta za umma na binafsi ili kubaini maeneo yenye mianya ya rushwa na kushauri namna ya kuziba mianya hiyo;

(ii) Kufanya warsha/vikao vya kuwashirikisha wadau kuweka mikakati ya kudhibiti mianya ya rushwa na kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mikakati hiyo;

(iii) Kufuatilia matumizi ya fedha za umma katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kuhakikisha utekelezaji wake unazingatia thamani halisi ya fedha;

(iv) Kutekeleza Mkakati wa Mawasiliano wa TAKUKURU ili kujenga uwezo na uelewa kuhusu rushwa, uifisadi na juhudi za Serikali katika kupambana na rushwa kwa makundi mbalimbali katika jamii kwa kutumia njia mbalimbali za mawasiliano kuyashawishi makundi haya kuunga mkono na kushiriki katika mapambano dhidi ya rushwa nchini;

(v) Kutumia njia za mawasiliano za kimkakati kulifikia kundi la vijana ili washiriki katika shughuli zinazowajenga kimaadili na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kushiriki kupambana na rushwa ili kuwa na jamii inayochukia rushwa;

(vi) Kutumia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kubeba agenda ya mapambano dhidi ya rushwa ili kuushirikisha umma katika mapambano hayo;

(vii) Kukamilisha uchunguzi wa majalada ya tuhuma za rushwa unaoendelea pamoja na tuhuma mpya zitakazojitokeza;

(viii) Kuhuisha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya Mwaka 2007;

(ix) Kuimarisha mfumo wa TEHAMA katika taasisi ili kurahisisha na kuwezesha mtiririko mzuri wa majalada, takwimu na mawasiliano kutoka ngazi za wilaya, mkoa na makao makuu; na

(x) Kutoa mafunzo ya weledi kwa watumishi ili kuongeza ufanisi. Kujenga karakana kwa ajili ya kutengeneza magari ya taasisi ili kupunguza gharama za uendeshaji zinazotumika katika kutengeneza magari hayo;

(xi) Ujenzi wa majengo ya Ofisi za Mkoa ya Simiyu na Iringa, Ofisi za Wilaya za Momba na Nyasa pamoja na Safe house moja Dodoma;

(xii) Ujenzi wa uzio katika Ofisi nne za Wilaya ya Mpwapwa, Masasi, Namtumbo na Bahi; na

(xiii) Kufanya ukarabati mkubwa wa Ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Dodoma, Ofisi za Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Mwanza na Ofisi ya Mkuu wa TAKUKURU Wilaya ya Chato.

C.TAASISI YA UONGOZI

52. Mheshimiwa Spika, Taasisi ya UONGOZI itaendelea kujengea uwezo viongozi ili kuongeza tija katika utekelezaji wa kazi zao kwa kupitia mafunzo na semina katika Mwaka wa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Fedha 2022/23, Taasisi ya UONGOZI imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kutekeleza programu maalum ya mafunzo ya uongozi kwa Bodi za Mashirika ya Umma, Taasisi na Wakala wa Serikali kwa lengo la kuimarisha usimamizi na utendaji wa mashirika. Mafunzo haya yatatolewa kwa Bodi 40;

(ii) Kutoa mafunzo ya Stashahada ya Uzamili ya Uongozi kwa lengo la kuwajengea uwezo Viongozi 35 katika maeneo ya kufanya maamuzi ya kimkakati, kusimamia rasilimaliwatu na rasilimali nyingine na kuimarisha sifa binafsi za kiongozi;

(i) Kutoa mafunzo ya Cheti ya Uongozi kwa njia ya mtandao kwa Viongozi 50;

(ii) Kutoa mafunzo ya muda mfupi kupitia kozi 30 kwa lengo la kuwajengea uwezo Viongozi 750 katika maeneo ya Uongozi na Maendeleo Endelevu, kutokana na mahitaji na maombi ya walengwa.

(iii) Kutekeleza programu maalum ya mafunzo ya Uongozi kwa wanawake viongozi waandamizi na viongozi wanaochipukia 40 kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kufanya maamuzi ya kimkakati, usimamizi wa rasilimali za Serikali na rasilimali watu. Vile vile mafunzo haya yanalengo la kukuza vipaji vya uongozi kwa viongozi wanawake wanaochipukia;

(iv) Kuandaa mikutano sita ya kitaifa katika masuala ya uongozi na maendeleo endelevu kwa viongozi 440;

(v) Kufanya tafiti tumizi nne kuhusu masuala ya uongozi na maendeleo endelevu;

(vi) Kuandaa vipindi nane vya runinga vitakavyoshirikisha viongozi waandamizi na wataalam mbalimbali ndani na nje ya nchi, juu ya Uongozi na Maendeleo Endelevu. Vipindi hivi vitarushwa kwenye runinga, tovuti na mitandao ya kijamii na kuonekana katika Bara zima la Afrika;

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(vii) Kutumia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kushirikisha umma katika kujadili masuala ya Uongozi na Maendeleo endelevu;

(viii) Kutoa machapisho 16 juu ya masuala ya Uongozi na Maendeleo Endelevu ikiwepo Tawasifu ya Hayati Edward Moringe Sokoine, aliyekuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika awamu ya kwanza ya Uongozi;

(ix) Kutoa ushauri wa kitaalam katika maeneo yanayohusu masuala ya Uongozi na Maendeleo Endelevu; na

(x) Kuandaa michoro ya majengo na maandalizi ya awali ya ujenzi wa Kituo cha mafunzo katika Kijiji cha Kondo, Bagamoyo.

D. MPANGO WA KURASIMISHA RASILIMALI NA BIASHARA ZA WANYONGE TANZANIA (MKURABITA)

53. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/23, MKURABITA imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:

(i) Urasimishaji na Uendelezaji wa Biashara 7,000 Katika Mamlaka 7 za Serikali za Mitaa za Tanzania Bara ambazo ni Temeke, Ilemela, Sumbawanga, Korogwe, Karagwe, Bunda na Mafinga. Aidha, Urasimishaji na uendelezaji wa biashara utafanyika katika wilaya mbili za Zanzibar;

(ii) Kurasimisha na kukamilisha uandaaji Hati miliki za ardhi na kuzitoa kwa wananchi katika Mamlaka Tano za Serikali za Mitaa za Tanzania Bara za Kondoa, Kiteto, Newala, Nachingwea, Mwanga na Moshi. Aidha, kwa upande wa Zanzibar urasimishaji utafanyika katika Wilaya sita;

(iii) Kujengea uwezo wananchi 3,000 waliorasimisha rasilimali na biashara kwakuwapa mafunzo ya umuhimu wa matumizi ya Hati katika Mamlaka 6 za Serikali za Mitaa za Tanzania Bara za Kondoa, Kiteto, Newala, Nachingwea, Mwanga na Moshi;

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(iv) Kuanzisha Studio ya Matangazo ambayo itawezesha uandaaji na urushaji wa matangazo ya utekelezaji wa shughuli za MKURABITA katika Radio, Runinga na Mitandao ya Kijamii;

(v) Kufanya ufuatiliaji na tathimini ya utekelezaji wa shughuli za urasimishaji ardhi na biashara katika Mamlaka 19 za Serikali za Mitaa za Tanzania Bara ambazo ni Aidha, kwa upande wa Zanzibar, ufuatiliaji na Tathmini utafanyika katika wilaya 6;

(vi) Kuboresha Vitendea kazi kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za urasimishaji na uendeshaji wa ofisi ambapo ununuzi wa gari moja na vitendea kazi vingine utafanyika;

(vii) Kuwezesha mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi wa MKURABITA ili kuongeza ujuzi na maarifa katika utendaji wa kazi;

(viii) Kurasimisha mashamba ya wakulima wa Alizeti katika Mamlaka 3 za Serikali za Mitaa za Iramba, Chemba na Kondoa kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa alizeti ili kuongeza mchango wa Alizeti katika upatikanaji wa mafuta nchini;

(ix) Kujenga Vituo Jumuishi 5 vya Urasimishaji na uendelezaji wa biashara katika Mamlaka 5 za Serikali za Mitaa za Kigamboni, Bunda, Mpanda, Karagwe na Tunduma ambavyo vitawezesha huduma za urasimishaji kupatikana katika jengo moja; na

(x) Kujenga Masjala 3 za za Ardhi za Vijiji katika Mamlaka 2 za Serikali za Mitaa za Tanzania Bara ambazo ni Chemba, na Iramba. Kwa upande wa Zanzibar, itajengwa Masjala moja ya ardhi katika wilaya moja.

E. MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII (TASAF)

54. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/23, TASAF imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(i) Kufanya zoezi la Utambuzi wa Kaya 186,500 kwenye Mamlaka 142 za utekelezaji ambazo zimeachwa katika Vijiji/Mitaa/Shahia kwa sababu mbalimbali;

(ii) Kufanya zoezi la kuhakiki na kutambua hali za ustawi wa maisha ya Kaya za Walengwa wa Mpango zipatazo 713,350 iwapo zimeimarika kiuchumi kwa kutumia vigezo vya umaskini na utaratibu uliokubaliwa kitakwimu;

(iii) Kuendelea kuhawilisha ruzuku kwa kaya maskini 1,279,325 zilizokidhi vigezo vya kuingia katika kipindi cha Pili cha Mpango;

(iv) Kuwezesha utekelezaji wa Miradi ya Jamii ya Kutoa Ajira ya Muda kwa Kaya Maskini katika mamlaka za utekelezaji 123. Jumla ya miradi 6,900 ya Jamii na ya Kutoa Ajira za Muda itatekelezwa katika ngazi ya Vijiji/Mitaa/Shahia 6,500 na inategemewa kutoa ajira za muda kwa Walengwa 550,000;

(v) Kuwezesha Jamii kutekeleza miradi ya kuendeleza miundombinu ya huduma za jamii katika sekta mbalimbali. Jumla ya miradi 515 itatekelezwa katika Vijiji/Mitaa ya Mamlaka za Utekelezaji 43. Miradi ya mingi itakuwa katika sekta za afya, elimu, maji, mazingira na ujasiriamali;

(vi) Kuwezesha uundaji wa Vikundi vya Kuweka Akiba na Kuwekeza katika mamlaka za utekelezaji 82. Jumla ya Vikundi 24,000 vya jamii vya Kuweka Akiba na Kuwekeza vyenye wanachama takribani 240,000 vinatarajiwa kuundwa katika Mamlaka 82 za Utekelezaji kwa mwaka 2022/2023. Aidha, Walengwa 50,000 kutoka mamlaka za utekelezaji 20 waliokamilisha mipango yao ya biashara inayokidhi vigezo vilivyowekwa watapatiwa Ruzuku ya Uzalishaji mali ili kutekeleza mawazo yao ya biashara zao;

(vii) Kuongeza maeneo ya utekelezaji 39 yatakyoshiriki malipo kwa njia ya mtandao. Jumla ya mamlaka za utekelezaji 186 zinatarajiwa kukamilisha taratibu na kuingia katika malipo kwa njia ya mtandao (Benki na mitandao ya simu) kwa mwaka 2022/2023 na hivyo kukamilisha utekelezaji kwa kuziingiza Mamlaka zote za Utekelezaji nchini katika malipo ya mtandao;

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(viii) Kuimarisha Usimamizi, Ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za Mpango pamoja na matumizi ya rasilimali ili kuongeza ufanisi na uwajibikaji katika ngazi zote za utekelezaji wa Mpango; na

(ix) Kufanya Mapitio ya pamoja baina ya Timu ya Serikali na Wadau wa Maendeleo kuhusu utekelezaji wa shughuli za Mpango.

F. WAKALA YA NDEGE ZA SERIKALI

55. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/23, Wakala ya Ndege za Serikali imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kutoa huduma ya usafiri wa anga kwa Viongozi Wakuu wa Kitaifa;

(ii) Kuratibu ununuzi pamoja na kusimamia mikataba ya ukodishaji wa ndege kwa Kampuni ya Ndege ya Tanzania (ATCL);

(iii) Kulipia gharama za bima za ndege pamoja na wanaanga;

(iv) Kugharamia uendeshaji wa Ofisi na kulipia gharama za mafuta ya ndege;

(v) Kufanya matengenezo makubwa ya Ndege aina ya Gulfstream 550 inayohusumia Viongozi Wakuu kwa mujibu ya kalenda ya matengenezo inayotolewa na mtengenezaji;

(vi) Matengenezo makubwa ya injini (Engine overhaul) ya akiba ya ndege aina ya Fokker 50;

(vii) Ukarabati na upanuzi karakana ya Ndege za Serikali iliyopo katika Uwanja wa Ndege wa kimataifa wa Julius Nyerere awamu ya pili; na

(viii) Kutoa mafunzo ya kisheria kwa wanahewa kwa ajili ya kuhuisha leseni zao.

56. Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza Mpango wa Mwaka wa Fedha wa 2022/23, Fungu 20 Ofisi ya Rais, Ikulu inaomba kiasi cha **Shilingi 29,828,203,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Aidha, Fungu 30: Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri inaomba kiasi cha **Shilingi 741,299,267,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizi, **Shilingi 577,206,673,000** ni Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 164,092,594,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

57. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/23, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma imeweka vipaumbele vikuu viwili ambavyo ni kuongeza matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma kwa Taasisi na kwa wananchi ili kuweza kuwafikia kwa urahisi; na pili ni kuimarisha uwajibikaji wa pamoja miongoni mwa viongozi wa umma hasa katika suala la viongozi kukinzana kunakopelekea shughuli za maendeleo kutotekelezeka kwa wakati. Kada za viongozi zitakazojumuishwa katika eneo hili litajumuisha Wakuu wa Idara na Madiwani kutoka katika baadhi ya Halmashauri na kupatiwa mafunzo husika. Kupitia vipaumbele hivyo shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:

(i) Kupokea Tamko la Viongozi wa Umma kuhusu Rasilimali na Madeni kwa viongozi wapatao 15,522 linalopaswa kutolewa kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

(ii) Kupokea malalamiko na taarifa za ukiukwaji wa Maadili kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma kutoka kwa wananchi;

(iii) Kuchunguza tuhuma yoyote ya kuvunjwa kwa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma dhidi ya Viongozi wa Umma;

(iv) Kufanya uhakiki wa matamko ya Rasilimali na Madeni kwa Viongozi wa Umma 2,000;

(v) Kuratibu na kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Baraza la Maadili ya Viongozi wa Umma;

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(vi) Kuelimisha Viongozi wa Umma na Wananchi kwa ujumla kuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Hati ya Ahadi ya Uadilifu;

(vii) Kuandaa Taarifa ya Mwaka ya Utekelezaji wa shughuli za Sekretarieti na kuiwasilisha kwa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(viii) Kuanzisha na kuendeleza Klabu za Maadili katika shule na vyuo nchini; na

(ix) Kuendelea na kukamilisha ujenzi wa Ofisi za Makao Makuu na ile ya Kanda ya Kati Jijini Dodoma pamoja na Kuanza ujenzi kwa kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Ziwa.

58. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/23, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma imetengewa **Shilingi 12,730,049,000.00**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 9,260,049,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 3,470,000,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA TAASISI ZILIZO CHINI YAKE

59. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma Fungu 32, katika Mwaka wa Fedha 2022/23 itaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kuhakikisha kuwa Utumishi wa Umma unaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya utawala bora na kwamba Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu mbalimbali za Utumishi wa Umma zinazingatiwa. Aidha, Ofisi itahakikisha inasimamia Utawala wa Utumishi wa Umma, mikataba ya utendaji kazi Serikalini, Orodha ya Mishahara katika Utumishi wa Umma na Maadili ya watumishi wa Umma.

Pia, itahakikisha mipango na uendelezaji rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma inafanyika kwa ubora zaidi. Kwa kuzingatia pia kuwa Serikali imeingia awamu nyingine, Ofisi itaandaa na kusimamia miundo, mifumo ya utendaji kazi na uboreshaji wa utoaji huduma wa Utumishi wa Umma pamoja na kuhakikisha

kunakuwa na uwajibikaji na uwazi. Ofisi pia, itasimamia utendaji kazi na uendelezaji wa rasilimaliwatu katika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Kwa nafasi yake kama wizara mama, Ofisi itasimamia taasisi, programu na miradi iliyo chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

A. MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMMA

60. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/23, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:

(i) Kukamilisha ujenzi wa Mfumo mpya wa Utendaji kazi na Upimaji kwa Watumishi wa Umma (Public Employees' Performance Management Information System - PEPMIS) na kujengea uwezo taasisi za umma katika kutumia mfumo huu ili kuimarisha Usimamizi na Uwajibikaji wa Watumishi wa Umma;

(ii) Kukamilisha marekebisho ya Mfumo wa Utendaji kazi na Upimaji wa Taasisi za Umma kupitia mikataba ya utendaji kazi (Public Institutions Performance Management Information System - PIPMIS) na kujengea uwezo taasisi za umma wa kutumia mfumo huu ili kuimarisha Uwajibikaji wa Viongozi wa Taasisi za Umma;

(iii) Kusimamia utekelezaji wa mfumo mpya wa HCMIS katika taasisi 600 za Serikali kwa kutoa huduma za usaidizi za TEHAMA;

(iv) Kuimarisha na kuboresha miundombinu ya TEHAMA kwa ajili ya kuwezesha utendaji kazi wa mifumo na watumiaji wa mifumo;

(v) Kusimamia, kufanya ukaguzi wa usalama na ufanisi, kuendeleza, kujenga uwezo na kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mifumo ya TEHAMA ya HCMIS, PEPMIS, PIPMIS, e-HRP, Sema na Waziri wa UTUMISHI, eMrejesho, UTUMISHI Call Centre, Biometric Attendance, Watumishi Portal na Staff Assessment katika Taasisi zote za Umma;

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(vi) Kufanya tathmini ya utekelezaji wa sheria na miongozo ya Serikali Mtandao katika taasisi za Serikali;

(vii) Kuendelea na hatua za kuhuisha Mkakati wa Taifa wa Serikali Mtandao na Mkakati wa Serikali wa Kujikinga na Majanga ya Mtandao;

(viii) Kuendelea na uratibu wa ukamilishaji wa kituo kimoja cha Huduma Jamii (One Stop Centres);

(ix) Kuratibu utekelezaji wa mradi wa Tanzania ya Kidijitali (Digital Tanzania) eneo la Serikali Mtandao;

(x) Kusimamia na kuwezesha Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kutekeleza majukumu yake;

(xi) Kuendelea kuziwezesha Taasisi za Umma kuandaa Mipango ya Rasilimaliwatu, Mipango ya Urithishanaji Madaraka na Mipango ya Mafunzo ili kujenga misingi ya utekelezaji wa usimamizi wa Rasilimaliwatu utakaohakikisha kuwa wanakuwepo watumishi wa umma wenye sifa stahiki na weledi katika nafasi zote kwenye utumishi wa umma (Meritocracy) katika muda wa kati na muda mrefu;

(xii) Kuendelea na maandalizi ya Mwongozo wa Kitaifa wa Kuandaa Mpango wa Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma;

(xiii) Kuratibu upatikanaji wa fursa za mafunzo zitolewazo na washirika wa maendeleo kwa ajili ya kuwajengea uwezo na ustadi watumishi wa Umma ndani na nje ya nchi;

(xiv) Kuratibu utoaji wa mafunzo kwa viongozi katika utumishi wa umma ili kuwajengea uwezo katika usimamizi na utoaji wa maamuzi ya kimkakati;

(xv) Kusimamia Mikataba ya Ushirikiano wa Kimataifa na Kikanda ili kuhakikisha kuwa watumishi wa umma wanapata fursa za ajira katika taasisi ambazo Tanzania ni mshirika;

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(xvi) Kuratibu na kufuatilia ajira za wageni katika utumishi wa umma na miradi ya kimkakati ili kuhakikisha pia kuwa wazalendo wanapata fursa ya kujifunza kama waambata kwa wataalamu hao wa kigeni;

(xvii) Kusimamia na kuwezesha Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania kutekeleza majukumu yake;

(xviii) Kutoa mafunzo kwa watumiaji wa Mfumo wa Utumishi/Watumishi Mtandao;

(xix) Kusimamia zoezi la Tathmini ya hali ya Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma kwa kutumia mfumo uliojengwa kwa ajili ya kukusanya, kuchakata na kuainisha mahitaji halisi ya watumishi kwenye Taasisi za Umma;

(xx) Kuendelea kutoa mafunzo ya namna ya kutumia Mfumo mpya wa HCMIS kwa Maafisa Utumishi/Tawala na viongozi wa Taasisi za Umma;

(xxi) Kuendelea na uidhinishaji wa taarifa za kiutumishi na mishahara kwenye Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Malipo ya Mishahara katika utumishi wa umma;

(xxii) Kufanya uhakiki wa watumishi kwenye Taasisi za Umma ili kuhakikisha kunakuwa na matumizi bora ya Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma sambamba na kusafisha na kuboresha taarifa za kiutumishi na mishahara kupitia Mfumo wa HCMIS;

(xxiii) Kujenga uwezo wa Maafisa TEHAMA na maafisa wanaoshughulikia malalamiko katika Utumishi wa Umma kutumia Mfumo wa Kidijitali wa Kushughulikia Malamiko ya Wananachi uitwao Sema na Waziri Utumishi/e-Mrejesho;

(xxiv) Kusimamia ajira za watumishi wa umma kwa kuajiri watumishi wapya 30,000 katika kada mbalimbali ambao wataigharimu Serikali kiasi cha **Shilingi 120,776,130,000**. Vile vile, utekelezaji wa zoezi la kuwapandisha vyeo **watumishi 120,210** ambao watalipwa kiasi cha **Shilingi 42,395,425,000** na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

watumishi 8,080 waliotengewa nafasi za kubadilishwa vyeo ambao wataigharimu Serikali kiasi cha **Shilingi 2,211,098,663** katika Mwaka wa Fedha 2022/23 kulingana na maelekezo yatakayotolewa;

(xxv) Kuchambua na kuhakiki madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi wa umma kwa kadiri yatakavyowasilishwa. Aidha, kiasi cha **Shilingi 103,883,257,000** kimetengwa kwa ajili ya malipo ya madai yatakayoidhinishwa;

(xxvi) Kukagua na kuidhinisha watumishi wapya wanaostahili kuingizwa katika Orodha ya Malipo ya Mishahara;

(xxvii) Kutoa vibali vya ajira mpya na mbadala ili kujaza nafasi stahiki kwenye taasisi mbalimbali za Umma;

(xxviii) Kuwezesha Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali na Mashirika ya Umma kuandaa Orodha ya Kazi na Maelezo ya Kazi ili kupata uwiano mzuri wa watumishi katika kutekeleza majukumu ya Taasisi husika;

(xxix) Kuendelea na uboreshaji wa michakato ya utoaji huduma na kuimarisha usimamizi wa Mifumo na Viwango vya utendaji kazi kwa kufanya ufuatiliaji pamoja na kutoa ushauri wa kitaalam katika Taasisi za Serikali ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wananchi;

(xxx) Kuendelea na ukamilishaji wa Mfumo Jumuishi wa Ufuatiliaji na Tathmini Serikalini kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ambao utauanganisha Mifumo ya Ufuatiliaji na Tathmini iliyopo katika Taasisi zote za Umma;

(xxxi) Kufanya Tathmini ya kina ya Utendaji kazi wa Wakala za Serikali ili kubaini utekelezaji wa malengo ya dhana ya uanzishaji wa Wakala hizo katika Utumishi wa Umma;

(xxxii) Uwezeshaji wa uandaaji na uhuishaji wa Miundo ya Maendeleo ya Utumishi katika Utumishi wa Umma;

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(xxxiii) Kuwianisha na kuoanisha mishahara na mipango ya motisha katika Utumishi wa Umma;

(xxxiv) Kusimamia utawala wa utumishi wa umma kwa kushughulikia mahitaji ya vibali vya uhamisho, kushikizwa, kuazimwa na likizo bila malipo kwa watumishi na baina ya waajiri mbalimbali katika Utumishi wa Umma;

(xxxv) Kuimarisha uwepo wa viongozi wenye sifa stahiki, weledi na maono ya utumishi wa umma wenye kuzingatia dira ya maendeleo na mikakati mbali mbali ya kitaifa kwa kupokea na kushughulikia mapendekezo ya nafasi za uteuzi, mikataba ya ajira na vibali vya kukaimu nafasi za uongozi kadiri maombi hayo yatakavyokuwa yanawasilishwa na waajiri mbalimbali;

(xxxvi) Kuimarisha upatikanaji wa taarifa (Kanzi data) za Viongozi wa Serikali waliopo kwenye nafasi na wanaoonesha mwelekeo na uwezo wa kukidhi uteuzi katika nafasi za uongozi; ili kuwa na viongozi wenye kukidhi matarajio ya utumishi wa umma na watanania;

(xxxvii) Kujenga uwezo wa Taasisi za Serikali katika kuandaa Sera za Kisekta zinazozingatia utafiti ili kuziwianisha na kuondoa migongano na urudufu wakati wa utekelezaji;

(xxxviii) Kufanya mapitio ya Sheria na Miongozo ya Kiutumishi kwa lengo la kuboresha utendaji kazi pamoja na kutoa miongozo ya kuimarisha Menejimenti ya Utumishi wa Umma kupitia nyaraka za kiutumishi;

(xxxix) Kuendeleza ufuatiliaji na uhamasishaji wa ujumuishwaji wa masuala ya Anuai za Jamii katika Utumishi wa Umma ili kuhakikisha kuwa makundi yote yanapata huduma zinazozingatia usawa. Aidha, maandalizi ya Mwongozo wa ujumuishaji wa masuala ya jinsia katika Utumishi wa Umma yataendelezwa;

(xl) Kuendelea na uhamasishaji wa uzingatiaji wa maadili kupitia vyombo vya habari na kuelimisha watumishi wa Umma na waajiri kuhusu umuhimu wa kupunguza malalamiko ya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wateja na kushughulikia ipasavyo malalamiko yanayowasilishwa;

(xli) Kuendelea kujenga uelewa wa wadau kuhusu Kanuni za Maadili ya Utumishi wa Umma;

(xlii) Kuendeleana ufuatiliaji wa uzingatiaji wa maadili katika Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikaliza Mitaa na taasisi nyingine za umma;

(xliii) Kukamilisha utafiti wa uzingatiaji wa maadili katika utumishi wa umma (Public Service Integrity Survey) kwa nia ya kubaini kiwango cha uzingatiaji wa maadili na kutoa ushauri wa uboreshaji unaozingatia taarifa sahihi za utafiti;

(xliv) Kuendelea na kampeni za uimarishaji wa uzingatiaji wa maadili kwenye taasisi za umma;

(xlv) Kuendelea kuhabarisha wananchi kuhusu huduma zitolewazo na Ofisi na namna ya upatikanaji wake kupitia njia mbalimbali za mawasiliano ikiwemo magazeti, redio, runinga, tovuti, mitandao ya kijamii, Gazeti la Serikali, majarida, vipeperushi na vitabu, mikutano ya wadau na semina;

(xlvi) Kuratibu maandalizi ya Mradi wa Kuboresha Utoaji Huduma katika sekta ya umma chini ya Shirika la Maendeleo la Dunia (UNDP);

(xlvii) Kuendeleza ujenzi wa jengo la Ofisi la ghorofa tano la Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora katika eneo la Mtumba - Dodoma; na

(xlviii) Kuendelea kutoa huduma kwa Viongozi wa Kitaifa Wastaafu (Viongozi 11 na wajane saba) kwa mujibu wa sheria.

B. CHUO CHA UTUMISHI WA UMMA (TPSC)

61. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/23 Chuo cha Utumishi wa Umma kimepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(i) Kutoa mafunzo ya kujiandaa kufanya mitihani ya Utumishi wa Umma kwa watumishi 950 ili kuwajengea uwezo wa utendaji kazi na kutoa huduma bora kwa wananchi;

(ii) Kutoa mafunzo ya Uongozi na Maendeleo, Menejimenti na Usimamizi wa ofisi kwa watumishi wa umma 5,315 ili kuendeleza stadi, weledi na ujuzi katika maeneo hayo. Vile vile, mafunzo hayo yatatolewa kwa njia ya mtandao kwa Watumishi wa Umma 2,500;

(iii) Kutoa Mafunzo ya Awali katika Utumishi wa Umma kwa Watumishi wa Umma 4,800 ili kujenga uelewa wa kitendaji wa Serikalini kwa waajiriwa wapya;

(iv) Kuwezesha Midahalo kwa washiriki wa ndani nan je ya nchi wapatao 800 ili kupunguza gharama za serikali kupeleka watumishi nje ya nchi na kubadilishana uzoefu wa kitaalam;

(v) Kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa washiriki 13,025 katika fani za Utunzaji wa Kumbukumbu, Uhazili na Utawala, Uhazili, Menejimenti ya Rasilimali Watu, Utawala na Manunuzi ya Umma;

(vi) Kutoa ushauri katika maeneo mbali mbali 15 ya kitaalam kwa Taasisi za Umma kwa ajili ya kutambua changamoto halisi za utendaji na kuchangia katika utoaji wa maamuzi yanayozingatia matokeo ya utafiti;

(vii) Kuratibu midahalo kwa njia ya mtandao katika maeneo 35 kwa Watumishi wa Umma na sekta binafsi;

(viii) Kuwezesha mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 7 wa Chuo cha Utumishi wa Umma katika ngazi za Shahada ya Uzamivu na Shahada ya Uzamili;

(ix) Kuendelea na ujenzi wa majengo katika Kampasi ya Singida awamu ya pili ambao utahusisha ujenzi wa Ukumbi kwa ajili ya shughuli mbalimbali za Chuo;

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(x) Kuanza ujenzi wa Ukumbi Dodoma katika kiwanja cha Chuo kilichopo eneo la NCC awamu ya kwanza. Ukumbi huo unatarajiwa kutumika kwa ajili ya mafunzo, midahalo na semina kwa Watumishi wa Umma;

(xi) Kuanza ujenzi wa uzio awamu ya kwanza katika Kampasi ya Tabora kuzunguka eneo la Chuo; na

(xii) Kufuatilia upatikanaji wa eneo katika Jiji la Mbeya kwa ajili ya ujenzi wa Kampasi ya Mbeya.

C. MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO (eGA)

62. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/23, Mamlaka ya Serikali Mtandao imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kuendelea kuiunganisha mifumo ya Taasisi za Serikali kwenye Mfumo wa kuwezesha mifumo ya Serikali kuwasiliana na kubadilishana taarifa (Government Enterprise Service Bus (GovESB) kwa kufuata mpango kazi;

(ii) Kusimamia na kutathmini hali ya usalama wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA, hatimaye kushauri maeneo ya kuboresha na kufuatilia utekelezaji wake ili kuhakikisha kuwa mifumo na miundombinu ya TEHAMA ya Serikali inafanya kazi na kutoa huduma kwa taasisi za umma na wananchi wakati wote kwa ufanisi na usalama;

(iii) Kujenga mifumo itakayoboresha utoaji wa huduma wa Taasisi mbalimbali za Serikali katika Utumishi wa Umma. Baadhi ya mifumo hiyo ni:

a. Mfumo Maalum wa Kusimamia Utoaji Huduma kwenye Zahanati na Vituo vya Afya (GoTHOMIS Lighter Version) – TAMISEMI. Lengo la mfumo huu ni kuongeza ufanisi katika usimamizi wa utoaji huduma katika Zahanati na vituo vya afya;

b. Mfumo wa Uendeshaji wa Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja – Watumishi Housing (WHC): Lengo la mfumo huu ni kuendesha kwa ufanisi uwekezaji wa pamoja;

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

c. Mfumo wa Kusimamia Mikopo ya Asilimia 10 kwenye Halmashauri kwa kushirikiana na TAMISEMI. Lengo la mfumo huu ni kusimamia mikopo ya vijana, wanawake na walemavu ili iweze kuwa na udhibiti na ilete tija;

d. Mfumo wa Kusimamia Shughuli za Mamlaka za Viwanja vya Ndege – TAA. Lengo la mfumo huu ni kusimamia utendaji na rasilimali za Mamlaka za viwanja vya ndege;

e. Mfumo wa Kusimamia Shughuli za Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali – Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali. Lengo la mfumo huu ni kuboresha utendaji kazi wa ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali;

f. Mfumo wa Usajili wa Wahandisi (awamu ya pili) – Bodi ya Usajili wa wahandisi. Lengo la mfumo ni kurahisisha usajili wa wahandisi na kuweza kutoa ripoti zinazohitajika kwa wakati;

g. Mfumo wa Tiketi za Kielektroni ulioboreshwa – Shirika la Meli Tanzania (MSCL). Lengo la mfumo ni kuongeza ufanisi na kuongeza mapato ya shirika kutokana na shughuli za usafirishaji;

h. Mfumo wa Usimamizi wa Manunuzi ya Umma – Wizara ya Fedha. Lengo la mfumo huu ni kuboresha manunuzi ya umma;

i. Mfumo wa Kusimamia Usambazaji wa Mbolea – TFRA. Lengo la mfumo huu ni kuongeza ufanisi katika kusimamia uagizaji na usambazaji wa mbolea nchini;

j. Mfumo wa Taarifa za Soko la Ajira (National Labor Market System) – Ofisi ya Waziri Mkuu. Lengo la mfumo huu ni kuwezesha kuwa na taarifa zote za ajira nchini, nafasi za kazi na kuweza kupata takwimu kamili za hali ya soko la ajira nchini; na

h. Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (awamu ya tatu);

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(iv) Kuendeleza utafiti na ubunifu katika matumizi ya teknolojia mpya za TEHAMA ili kuibua huduma mpya kwa umma kupitia TEHAMA na kuwezesha matumizi sahihi ya teknolojia mpya zinazoibuka;

(v) Kupanua Miundombinu ya Mtandao wa Mawasiliano wa Serikali (Government Network) ili kufikisha katika Wilaya zote nchini;

(vi) Kuziwezesha Taasisi 160 kutumia Mfumo wa Ofisi Mtandao (e-Office), hivyo kufanya Taasisi zinazotumia mfumo huo kufikia 300;

(vii) Kukagua mifumo ya kimkakati, kisekta na kitaasisi ili kuhakikisha kuwa imetengenezwa na inatumika kwa kufuata sheria, kanuni, viwango na miongozo iliyopo na kushauri maeneo ya kuboresha na kufuatilia utekelezaji wake;

(viii) Kusimamia, kuendesha na kuendeleza Mifumo na Miundombinu Shirikishi ya TEHAMA ya Serikali na Taasisi zake; hii ni pamoja na kusimamia na kuboresha vituo vya Kuhifadhi Mifumo na Taarifa za Serikali pamoja na vituo vya kujikinga na majanga;

(ix) Kuwajengea uwezo watumishi katika kusimamia mifumo na miundombinu ya TEHAMA katika Taasisi za Umma; pia kutoa mafunzo kwa watumiaji kuhusu matumizi sahihi na salama ya mifumo na miundombinu ya TEHAMA; na

(x) Kutoa ushauri wa kitaalamu na msaada wa kiufundi kwenye maeneo ya TEHAMA kwa taasisi za Serikali ili viwango na miongozo iweze kufuatwa, ili kuwa na matumizi ya TEHAMA yenye tija na kupunguza gharama.

D. WATUMISHI HOUSING INVESTMENT (WHI)

63. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/23, Watumishi Housing Investment imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

- (i) Kuendeleza mradi wa ujenzi wa nyumba 1,000 jijini Dodoma pamoja na mikoa mingine zikiwemo wilaya mpya;
- (ii) Kubuni na kutekeleza miradi ya nyumba za gharama nafuu katika Halmashauri mpya;
- (iii) Kujenga na kuuza viwanja 300 vilivyopimwa jijini Arusha;
- (iv) Kuendelea kuuza nyumba zilizojengwa na zitakazojengwa maeneo mbalimbali nchini;
- (v) Kuanzisha rasmi Mfuko wa Uwekezaji wa Pamoja wa FAIDA Fund;
- (vi) Kuendelea na shughuli za kikandarasi kwa kutoa huduma za ujenzi wa majengo katika taasisi mbalimbali za umma; Kutoa huduma za ushauri wa majenzi katika miradi inayoendelea na miradi mipya; na
- (vii) Kukarabati nyumba na miundombinu katika miradi ya WHC ya nyumba zilizopangishwa.

64. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23, Fungu 32: Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 47,611,581,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizi, **Shilingi 39,541,381,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 8,070,200,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

SEKRETARIETI YA AJIRAKATIKA UTUMISHI WA UMMA

65. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/23, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

- (i) Kusimamia na kuendesha michakato ya ajira ili kuwezesha waajiri kupata watumishi wenye sifa zinazotakiwa kwa mujibu wa miundo ya utumishi husika;

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(ii) Kushiriki kama Wataalam waalikwa kwenye usaili unaoendeshwa na Taasisi zinazotumia Sheria zilizokasimiwa kwa Taasisi husika;

(iii) Kuendelea kuimarisha Ofisi ya Sekretarieti ya Ajira Zanzibar kurahisisha michakato ya ajira kwa ajira za Muungano;

(iv) Kuanza ujenzi wa mfumo wa usaili wa mchujo kwa njia ya mtandao "Online aptitude test" mfumo huu utasaidia Serikali kupunguza gharama kwa kiasi kikubwa hasa gharama za uendeshaji wa saili za mchujo. Aidha mfumo huu utasaidia kuwapunguzia gharama zinazotumika wakati wa usaili kwani saili zitafanyika katika maeneo wanayotoka;

(v) Kuanza ujenzi wa mfumo wa kupima haiba za wasailiwa "psychometric testing system" ili kuiwezesha serikali kutambua haiba na tabia za wasailiwa kwa lengo la kuwasaidia waajiri kubaini maeneo ya kuwajengea uwezo waajiriwa wapya;

(vi) Kutoa taarifa na elimu kwa umma ili kukuza uelewa kuhusu shughuli zinazotekelezwa na Sekretarieti ya Ajira katika mUtumishi wa Umma.

(vii) Kuboresha mifumo ya usaili kuwa ya kisasa zaidi kwa kutumia TEHAMA.

(viii) Ununuzi wa vitendea kazi hususani magari ya viongozi na wafanyakazi ili kusaidia utekelezaji wa majukumu ya Taasisi kwa wakati.

(ix) Kuanza ujenzi wa jengo la Ofisi za Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma Jijini Dodoma.

(x) Kuongeza uwezo wa Taasisi kufanya usaili kwa kanda.

66. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha wa 2022/23, Fungu 67: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma inaomba kuidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 8,721,849,000**. Kati ya fedha hizo,

Shilingi 5,063,849,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 3,658,000,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

OFISI YA RAIS, TUME YA UTUMISHI WA UMMMA

67. Mheshimiwa Spika; katika Mwaka wa Fedha 2022/23, Tume imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kufanya ukaguzi wa kawaida katika Taasisi za Umma 150 na Ukaguzi Maalum katika Taasisi za Umma 10 kuangalia uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya usimamizi wa Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma;

(ii) Kufanya mikutano minne ya kisheria ya Tume kujadili na kutolea uamuzi rufaa, malalamiko, taarifa za ukaguzi na masuala mengine ya kiutumishi kadri yatakvypokelewa;

(iii) Kuandaa Taarifa ya Hali ya Utumishi wa Umma na Utekelezaji wa Majukumu ya Tume kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2021/2022 na kuiwasilisha kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(iv) Kuandaa mfumo wa TEHAMA kwa ajili ya kuongeza ufanisi kwenye ushughulikiaji wa rufaa na ukaguzi wa rasilimaliwatu;

(v) Kufanya utafiti kuhusu uendeshaji na usimamizi wa Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma;

(vi) Kuhuisha Miongozo miwili ya Tume kuhusu uzingatiaji wa masuala ya Ajira na Uwasilishaji wa Taarifa Tume na kuisambaza kwa Waajiri, Mamlaka za Ajira na Nidhamu;

(vii) Kuelimisha Taasisi za Umma na Watumishi wa Umma kuhusu majukumu ya Tume na uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Utumishi wa Umma; na

(viii) Ujenzi wa jengo la Ofisi za Tume Makao Makuu Dodoma.

68. Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza Mpango wa Mwaka wa Fedha 2022/23, Fungu 94, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Umma inaomba kuidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 5,981,824,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 5,681,824,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 300,000,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

OFISI YA RAIS, IDARA YA KUMBUKUMBU NA NYARAKA ZA TAIFA

69. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/23, Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa itatekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kukusanya taarifa, kumbukumbu na nyaraka mbalimbali zinazohusu historia ya nchi yetu kutoka Taasisi za Umma, Taasisi na watu binafsi;

(ii) Kufanya ukarabati wa nyaraka kongwe zilizohifadhiwa katika Ghala Kuu la nyaraka na zile zinazotarajiwa kukusanywa;

(iii) Kuimarisha uhifadhi wa kumbukumbu na nyaraka katika teknolojia ya kisasa kwa kuingiza nyaraka katika mfumo wa kidigitali wa kuhifadhi kumbukumbu na nyaraka (Digital Records Management and Preservation System) ili kurahisisha upatikanaji wake na kulinda nakala halisi;

(iv) Kuweka na kuhuisha mifumo ya utunzaji wa kumbukumbu katika Taasisi za Umma ili kuongeza ufanisi na tija katika utoaji wa huduma Serikalini;

(v) Kujenga uwezo wa Taasisi za Umma katika usimamizi wa kumbukumbu na nyaraka za Serikali kwa kuandaa mikutano na mafunzo kazi kwa watumishi wa umma kuhusu Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya utunzaji wa taarifa, kumbukumbu na nyaraka za Serikali;

(vi) Kufanya tathmini (appraisal) ya kumbukumbu tuli za Taasisi za Umma zilizohifadhiwa katika Vituo vya Kumbukumbu vya Idara ili kubaini zenye umuhimu wa kuendelea kuhifadhiwa na zile ambazo umuhimu wake wa matumizi umefikia ukoma kwa lengo la kuziteketeza kwa mujibu wa Sheria;

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(vii) Kukagua, kuchambua na kuhamisha kumbukumbu tuli kutoka katika Taasisi za Umma na kuzihifadhi katika Vituo vya Kumbukumbu vya Idara;

(viii) Kuwezesha Taasisi za Umma kutengeneza Miongozo ya kuhifadhi na kuteketeza kumbukumbu (Record Retention Disposal Schedule) kwa mujibu wa Sheria;

(ix) Kufanya Ukaguzi wa hali ya utunzaji wa kumbukumbu katika Taasisi za Umma;

(x) Kutambua, kukusanya, kutunza na kuhifadhi kumbukumbu na vitu vya Waasisi wa Taifa;

(xi) Kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa utunzaji na uhifadhi wa kumbukumbu na nyaraka katika maendeleo ya Taifa letu;

(xii) Kuimarisha utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka kwa kununua vitendea kazi na vifaa vya uhifadhi vikiwemo kuongeza mashubaka, scanner na magari maalumu ya kubebea nyaraka; na

(xiii) Kuanza ujenzi wa jengo la Utawala Makao Makuu Dodoma.

70. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha wa 2022/23, Fungu 4: Idara ya Kumbukumbu ya Nyaraka za Taifa inaomba kuidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 4,914,791,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizi, **Shilingi 3,504,791,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 1,410,000,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

MAJUMUISHO

71. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais ikiongozwa na Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiyo yenye dhamana ya maamuzi juu ya nchi na menejimenti ya Utumishi wa Umma ambayo ni nguzo muhimu

na mtambuka katika uendeshaji na uendelezaji wa nchi. Utumishi wa Umma umeendelea kutoa mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi yetu. Tunayo matarajio makubwa kuwa mchango wa watumishi wa umma katika maendeleo ya nchi yetu utaendelea kukua kwa kasi kubwa ili kuiwezesha nchi yetu kufikia uchumi wa kati wa kiwango cha juu.

72. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais itaendelea kuimarisha uwezeshaji wa vyombo vinavyosaidia kwenye maamuzi ya nchi, usalama na kuimarisha vita dhidi ya rushwa. Maadili kwa viongozi wote na watumishi wa umma yanatarajiwa kuchangia ipasavyo kwenye nchi kupata tija ya rasilimaliwatu na ufanisi katika matumizi ya rasilimalifedha wakati wote. Kati ya mambo ambayo Serikali itayapa kipaumbele ni usimamizi thabiti wa rasilimaliwatu na rasilimalifedha kwa kusisitiza uwajibaji wa hiari.

73. Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kufanya maboresho ya kisekta na mtambuka ili kuongeza tija na ufanisi katika utendaji wake. Wajibu wa Ofisi ya Rais ni kuhakikisha maboresho yanayofanywa katika nchi yetu hayana urudufu na yanaleta tija na ufanisi katika Utumishi wa Umma na kuwa chachu ya maendeleo. Aidha, itahakikisha kunakuwepo na utawala bora ulio imara kuanzia ngazi ya juu ya uongozi hadi chini. Katika kuimarisha uwazi Ofisi ya Rais itahakikisha wananchi wanapata taarifa sahihi kuhusu maamuzi ya Serikali na kuweka imara mifumo ya mrejesho wa utoaji huduma.

74. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa miundo na mgawanyo wa majukumu kwa mawaziri, utekelezaji kwa ujumla unajumuisha, Ofisi ya Rais Ikulu; Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma; Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma; Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma; na Ofisi ya Rais, Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa.

75. Mheshimiwa Spika, Mipango na Bajeti kwa Mafungu niliyoyataja yamezingatia vipaumbele vya Serikali ya Awamu ya Sita katika kuimarisha utendaji kazi wa Utumishi wa Umma,

uzingatiaji wa matumizi bora ya rasilimalifedha, maadili ya uongozi na kuongeza kasi ya kufanya maamuzi na kutoa huduma bora kwa wananchi na hivyo kuongeza tija na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali katika ngazi zote.

76. Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Mafungu yote yaliyo chini ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora imelenga kuwa na Utumishi wa Umma unaotoa huduma bora kwa haraka na staha, ukizingatia Katiba, Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo katika kujenga imani zaidi kwa wananchi na kuendana na kauli ya Rais, Mhe. Samia Suluhu Hassan, aliyoitoa 22 Aprili, 2021 wakati akilihutubia Bunge la 12 aliposema: ***'Tutawapima viongozi na watumishi kwa namna wanavyotimiza majukumu yao, hatutawaonea aibu viongozi na watumishi wazembe, wezi na wabadhirifu wa mali za umma. Tutaendeleza pia juhudi za kupambana na rushwa kwenye utumishi wa umma. Wajibu wa watumishi wa umma ni lazima uendane na haki zao'***. Katika kuendana na wakati, jitihada zaidi zitawekwa kwenye kujenga uwezo na mifumo ya kimenejimenti na utoaji huduma ikiwemo matumizi sahihi na salama ya fursa zinazopatikana katika utoaji huduma kwa TEHAMA ndani ya Serikali, hivyo tunataka kujenga utumishi wa umma wa kidijitali.

77. Mheshimiwa Spika, napenda kulikumbusha Bunge lako tukufu kuwa, Waziri mwenye dhamana ya menejimenti ya Utumishi wa Umma ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye katika hotuba zake amekuwa akisisitiza dhamira yake ya kushughulikia haki na masilahi ya Watumishi wa Umma. Hivyo, kabla ya kuomba fedha kwenye Bunge lako tukufu, naomba kueleza kuwa kilio cha masilahi na motisha kwa Watumishi wa Umma kinaendelea kufanyiwa kazi na Serikali sikivu ya CCM chini ya Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

78. Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza kwa kina utekelezaji wa majukumu kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 na Mipango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Fedha 2021/22 sasa naomba kuwasilisha rasmi mapendekezo ya maombi yetu kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 kwa muhtasari kama ifuatavyo:-

(i) Fungu 20: Ofisi ya Rais, Ikulu

Matumizi ya Kawaida	Sh.	29,828,203,000
Jumla	Sh.	29,828,203,000

(ii) Fungu 30: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri

Matumizi ya Kawaida	Sh.	577,206,673,000
Matumizi ya Miradi ya Maendeleo	Sh.	164,092,594,000
Jumla	Sh.	741,299,267,000

(iii) Fungu 33: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma

Matumizi ya Kawaida	Sh.	9,260,049,000
Matumizi ya Miradi ya Maendeleo	Sh.	3,470,000,000
Jumla	Sh.	12,730,049,000

(iv) Fungu 32: Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma

Matumizi ya Kawaida	Sh.	39,541,381,000
Matumizi ya Miradi ya Maendeleo	Sh.	8,070,200,000
Jumla	Sh.	47,611,581,000

(v) Fungu 67: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma

Matumizi ya Kawaida	Sh.	5,063,849,000
Matumizi ya Miradi ya Maendeleo	Sh.	3,658,000,000
Jumla	Sh.	8,721,849,000

(vi) **Fungu 94: Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma**

Matumizi ya Kawaida	Sh.	5,681,824,000
Matumizi ya Miradi ya Maendeleo	Sh.	300,000,000
Jumla	Sh.	5,981,824,000

(vii) **Fungu 04: Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa**

Matumizi ya Kawaida	Sh.	3,504,791,000
Matumizi ya Miradi ya Maendeleo	Sh.	1,410,000,000
Jumla	Sh.	4,914,791,000

79. Mheshimiwa Spika na Wabunge wenzangu, Jumla kuu ya Bajeti ninayoomba kwa mafungu yote yaliyo chini ya Ofisi ya Rais (Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora) kwa mwaka 2022/23, ni kama ifuatavyo:-

Jumla kuu - Matumizi ya Kawaida	Sh.	670,086,770,000
Jumla kuu - Matumizi ya Miradi ya Maendeleo	Sh.	181,000,794,000
Jumla Kuu kwa Mafungu yote	Sh.	851,087,564,000

80. Mheshimiwa Spika na Wabunge wenzangu, mwisho naomba kuwasilisha maombi haya ili muweze kuyajadili na kuyaidhinisha. **Ahsanteni kwa kunisikiliza, naomba kutoa hoja.**

Jenista J. Mhagama (Mb.)
WAZIRI WA NCHI – OFISI YA RAIS
(MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono. Ahsanteni sana, tutaendelea na utaratibu wetu.

Sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo. Aje atoe maoni ya Kamati yetu ya Bunge. *(Makofi)*

MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kuhusu Utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, ili kuliwezesha Bunge kufuatilia taarifa hii ipasavyo, naomba kutambulisha sehemu nne za Taarifa hii:-

Sehemu ya Kwanza yenye maelezo ya jumla, inabainisha misingi na Muundo wa Taarifa.

Sehemu ya Pili yenye ufafanuzi na uchambuzi, inachambua Taarifa ya Utekelezaji, Upatikanaji wa fedha na uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati.

Sehemu ya Tatu yenye Maoni na Ushauri, inakamilisha uchambuzi kwa kuonesha maoni na mtazamo kutokana na uchambuzi uliojenga misingi ya ushauri wa Kamati.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Sehemu ya Nne na ya mwisho yenye hitimisho, inamalizia taarifa kwa kulishauri Bunge kuhusu hoja ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, Msingi wa Kamati kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ni Masharti ya Kanuni za Bunge. Kifungu cha 6(4)(a) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, kinatambua jukumu la Kamati hii kufanya uchambuzi huo. Aidha, Kanuni ya 117(4) ya Kanuni za Bunge imeweka masharti yaliyotaka Taarifa ya Utekelezaji ya Makadirio ya Ofisi hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, ili kukidhi masharti hayo, tarehe 21 hadi 22 Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuhusu Utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Katika hatua hiyo, Kamati ilifanya Uchambuzi wa kina na matokeo yake ni Taarifa hii. Naliomba Bunge lako Tukufu liipokee taarifa hii, kujadili sambamba na Hoja ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu na Makadirio ya Mapato na Matumizi iliyochambuliwa na Kamati, inahusu utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kwa ajili ya Ofisi hii muhimu pamoja na Taasisi zilizo chini yake. Randama zenye taarifa hizi zinahusu Mafungu Saba yalivyotajwa katika Taarifa ya Kamati. Kwa mawanda hayo nitangulie kusema kuwa nitaisoma taarifa hii kwa muhtasari, lakini naomba taarifa yote kama ilivyowasilishwa mezani, iingie kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*).

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Bunge ilitoa siku zisizozidi tisa (9) kwa Kamati kufanya uchambuzi wa Taarifa za utekelezaji wa bajeti. Kanuni hiyo inatambua umuhimu wa kufanya ulinganisho kati ya utekelezaji wa bajeti unaoripotiwa na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata.

Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati ilizingatia Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Bunge na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti za Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Uchambuzi huo ulijenga msingi wa kulinganisha uzoefu uliopatikana kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na mipango ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022, ilikusudia kufanikisha utekelezaji wa mipango na majukumu ya Ofisi ya Rais, Menjimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Ili kuliwezesha Bunge kujiridhisha na mwenendo wa Matumizi unavyoakisi madhumuni ya kuidhinishwa kwa bajeti hiyo, Kamati ilidadisi utekelezaji wa mipango na majukumu ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kulijulisha Bunge hili kuwa kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa Bajeti umezingatia mipango na majukumu yaliyooombewa fedha. Kwa mfano, sehemu ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge na kupatikana, zimetumika kusimamia misingi yote ya Utumishi kwa kulinda maadili ya Utumishi wa Umma. Aidha, Ofisi hii ilitumia fedha zilizopatikana kusimamia na kuimarisha misingi ya utawala bora.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo, Kamati inampongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa usimamizi madhubuti wa jambo hili.

Kwa maoni yetu, hali ya usimamizi wa Utumishi wa Umma na kuimarika katika misingi ya utawala bora, imeipandisha zaidi Tanzania katika medani za utawala bora Afrika na duniani kwa ujumla.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Ofisi hii ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 183.358 sawa na asilimia 28.6 ya bajeti yake ya Matumizi ya Maendeleo. Mchanganuo wa kiasi hicho cha fedha kwa mafungu chini ya Ofisi hii umeoneshwa katika Jedwali Na. 01 ya Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati zinaonesha kuwa hadi Februari, 2022, Ofisi hii na Taasisi zilizochini yake ilipokea jumla ya shilingi bilioni 82.037 kwa ajili ya kugharimia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 44.7 ya bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa na Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Mchanganuo wa fedha hizo zilizoidhinishwa na kupatikana unaonekana katika Jedwali Na. 02 ya Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo umeonesha kwamba: -

(a) Hadi kufikia mwezi Machi, 2022, fedha zilizopokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ni asilimia 44.7 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kiasi hiki ni pungufu ukilinganisha na kiasi cha utekelezaji wa bajeti wa mwaka unaoisha.

(b) Upatikanaji wa fedha za Miradi ya Maendeleo kwa ujumla hautoi matumani ya kukamilika kwa miradi hiyo. Aidha, utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma unakabiliwa na upatikanaji hafifu wa fedha ikilinganishwa na miradi inayotekelezwa na taasisi nyingine.

(c) Licha ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa jumla wa miradi ya maendeleo kuwa hafifu, lakini imeonekana msukumo mdogo kwenye miradi ya maendeleo iliyotekelezwa na Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kwa uchambuzi huo, itakuwa vigumu kwa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma kutekeleza miradi ya maendeleo. Aidha, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka haina uwezo wa kukamilisha utekelezaji wa miradi hiyo kutokana na ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na taasisi zake hadi kufikia mwezi Februari, 2022 ilipokea kiasi cha fedha ambacho ni asilimia 69.6 ya bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Mchanganuo wa fedha zilizoidhinishwa na kupatikana kwa Taasisi zilizo chini ya Ofisi hii umeonekana katika Jedwali Na. 03 ya Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi unaonesha kwamba:-

(a) Mwenendo wa jumla wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida hadi mwezi Februari, 2022 ni asilimia 69.6. Hata hivyo, ulinganisho wa upatikanaji wa fedha kwa mafungu ya Ofisi hii unaonesha unatofautiana kwa kiasi kinachopokewa.

(b) Hadi mwezi Februari, 2022, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma ilipokea fedha iliyoidhinishwa kwa kiwango cha asilimia 89.8 ya bajeti yake ya Matumizi ya Kawaida. Kwa mwenendo huu, kuna uwezekano mkubwa wa kupata na kutumia fedha kama ilivyoidhinishwa na Bunge.

(c) Mwenendo wa upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida kwa ajili ya Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka hautoi matumaini. Hadi Februari, 2022, idara hii ilipokea asilimia 58.7 ya bajeti yake ya Matumizi ya Kawaida. Kwa hali hiyo, uendeshaji wa shughuli za Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka umeathirika kwa kiasi.

(d) Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma imepokea kiasi kidogo cha fedha za uendeshaji. Ulinganisho unaonesha kuwa shughuli za Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka hazipati uzito unaostahili.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(e) Mheshimiwa Spika, kwa uchambuzi huo, ni dhahiri uzoefu uliopatikana katika mwaka wa fedha 2021/2022 utafaa kutumika ili kukabiliana changamoto za upatikanaji wa fedha kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Kamati ilitoa maoni na ushauri katika maeneo 18. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa ushauri wa Kamati umezingatiwa. Mfano wa ushauri uliozingatiwa, unahusu Serikali kukamilisha usanifu na ujenzi wa Mfumo Maalum wa kuwezesha Mifumo ya Serikali kusomana na kubadilishana Taarifa. Utekelezaji ulioripotiwa unaonesha kuwa baadhi ya taasisi zimeunganishwa na Mpango Kazi wa kuhakiki Taasisi zote za Serikali zinaunganishwa katika Mfumo huu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuipongeza Serikali kwa kuzingatia sehemu kubwa ya ushauri uliotolewa, bado kuna umuhimu kwa Serikali kuujali ushauri unaotolewa na Kamati Bungeni. Kwa maoni ya Kamati, uzingatiaji wa ushauri wa Kamati unaiwezesha Serikali kukidhi matarajio ya wananchi wanaowakilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Kanuni za Kudumu za Bunge zimetambua umuhimu wa uzoefu unaopatikana katika mwaka wa fedha unaoisha ili kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata. Kamati imezingatia umuhimu huo na masharti ya kanuni za Bunge kwa kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu Makadirio ya Matumizi, Kamati imebaini ongezeko la bajeti la 16% ukilinganisha na Bajeti ya Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Uchambuzi wa Makadirio hayo kwa Taasisi zilizo chini ya Ofisi hii, unabainishwa katika Jedwali Na. 04 ya Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kwa kuthamini uzoefu uliopatikana katika utekelezaji wa Bajeti inayoisha, Kamati ilifanya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ulinganifu kati ya Makadirio hayo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na Bajeti iliyoidhinishwa na kupatikana kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Mchanganuo na ulinganifu uliofanyika unaonekana katika Jedwali Na. 05 ya Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kwa uchambuzi huu, Kamati imebaini yafuatayo:-

(a) Kwa ujumla Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 yameongezeka kwa 16% ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Hata hivyo, Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya Tume ya Utumishi wa Umma yamepungua kwa 13.4%.

(b) Makadirio ya Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma yameongezeka kwa kiasi kikubwa, ambacho ni 157.4%. Ongezeko hili linatokana na kutengewa fedha kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo inayohusu uboreshaji wa Mifumo.

(c) Ili kutathmini mwenendo wa utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Kamati ilichambua Makadirio ya Matumizi ya Kawaida, yaliyowasilishwa na mtoa hoja. Katika kufanikisha hilo, Kamati ilichanganua Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Mchanganuo huo unaonekana katika Jedwali Na. 06 la taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi umeonesha kwamba:-

(a) Kama ilivyo kwenye Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, Bajeti ya Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma imeongezeka kwa asilimia 19.4 ukilinganisha na bajeti iliyoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2021/2022.

(b) Bajeti ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Fungu 32 imepungua kwa asilimia 13.8.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(c) Kwa ujumla Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Taasisi zake yameongezeka kwa asilimia 20.4.

Mheshimiwa Spika, kwa uchambuzi huo ni dhahiri kuwa shughuli za usimamizi na uboreshaji wa Utumishi wa Umma pamoja na kusimamia misingi ya utawala bora zitatekelezwa kwa ufanisi zaidi. Hata hivyo, ufanisi huu utategemea kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua Makadirio ya Bajeti ya Miradi ya Maendeleo ya Ofisi hii na taasisi zake kwa mwaka wa Fedha 2022/2023 na kulinganisha na matumizi ya fedha kwa ajili hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Ulinganisho huo unapatikana katika Jedwali Na. 07 la taarifa.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi huo umeonesha yafuatayo:-

(a) Jumla ya fedha iliyoombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni sawa na 0.4% ya bajeti yote ya Taifa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

(b) Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni asilimia 21.2 ya bajeti ya Ofisi hii. Uwiano huo wa Matumizi ya Maendeleo kwa bajeti ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, unatofautiana na uwiano katika bajeti kuu kati ya bajeti ya Miradi ya Maendeleo na Matumizi ya Kawaida. Wakati kwa Ofisi hii uwiano wa Matumizi ya Maendeleo kwa Matumizi ya Kawaida ni 21.2% kwa 78.8%. Uwiano katika bajeti kuu ni 37.8% kwa 62.2%.

Mheshimiwa Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati. Baada ya maelezo hayo, naomba kukamilisha uchambuzi kwa kubainisha Maoni ya Kamati yaliyojenga mtazamo ambao ni msingi wa Ushauri wa Kamati. Maoni hayo ni kama ifuatavyo:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(a) Ushauri unaotolewa Bungeni kuhusu utekelezaji wa Mipango, Majukumu na Bajeti unahitaji kupewa nafasi stahiki ili kukidhi matarajio ya wananchi;

(b) Kuna umuhimu wa kufanikisha upatikanaji wa kiasi cha fedha za matumizi kama ilivyoidhinishwa na Bunge. Vinginevyo kuna hatari ya kukosekana kwa tija ya mipango inayokusudiwa kwa kipindi kinachohusika;

(c) Fedha kwa ajili ya majukumu na shughuli zilizohusu kuhifadhi Kumbukumbu Tuli, Utunzaji wa Kumbukumbu na Ofisi Mtandao, Utunzaji wa Nyaraka na Kuwaenzi Waasisi wa Taifa zisipopatikana ipasavyo, inaweza kuathiri uwezo wa Taifa kukidhi malengo yake; na

(d) Juhudi za Serikali kuimarisha misingi ya Utawala Bora na uzingatiji wa haki kwa Watanzania wote, Wanawake na Wanaume kwa kuzingatia na kuheshimu Katiba na Sheria ni jambo linalosukuma maendeleo halisi ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa maoni niliyobainisha kutokana na uchambuzi, naomba kutoa ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

(a) Serikali iendelee kuzingatia ipasavyo, ushauri unaotolewa Bungeni kuhusu utekelezaji wa mipango, majukumu na bajeti kwa madhumuni ya kukidhi matarajio ya wananchi.

(b) Serikali ihakikishe kuwa fedha inayoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Ofisi hii na taasisi zake inapatikana ipasavyo ili kufanikisha upatikanaji wa manufaa ya utekelezaji wa majukumu yaliyopangwa;

(c) Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa iwezeshe kifedha ili imudu na kuboresha utekelezaji wa majukumu yake ya kuhifadhi kumbukumbu tuli, kutunza kumbukumbu mbalimbali na Ofisi Mtandao, kutunza nyaraka pamoja na kuwaenzi Waasisi wa Taifa;

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(d) Serikali iendelee kuimarisha misingi ya Utawala Bora pamoja na kuboresha zaidi miundombinu, maendeleo ya watumishi na mifumo ya utendaji kazi katika Utumishi wa Umma sambamba na kuboresha mishahara na maslahi ya watumishi.

(e) Watumishi waendeleo kuhimizwa kuwa wazalendo kwa nchi yetu na kufanya kazi kwa uadilifu, bidii, weledi na maarifa kama msingi imara wa maendeleo;

(f) Ujenzi wa Ikulu ya Chamwino ukamilishwe kwa wakati kama ilivyokusudiwa;

(g) Serikali iweke mikakati inayotekelezeka ya kutumia rasilimali zake zinazojumuisha watu wake ambao kimsingi wana uwezo mkubwa, pia, Rasilimali nyingine za nchi.

(h) Serikali iendelee kutoa ajira zaidi ili kukabiliana na changamoto ya upungufu wa watumishi.

(i) Serikali iendelee kusimamia na kutoa mafunzo maalum mara kwa mara kwa Watumishi wa Umma ili kuwezesha utendaji kazi unaozingatia weledi na ustadi mkubwa.

(j) Serikali itengeneze kanzidata ya wanaofanyiwa usaili na kufaulu kwa lengo la kuwa na orodha ya wataalam wenye sifa wasioajiriwa ambao wanaweza kuajiriwa bila usaili iwapo itatokea nafasi za ajira.

(k) Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Mamlaka Serikali Mtandao (eGA), ya uandaaji wa mifumo ya kielektroniki inayofanikisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali, mamlaka hiyo iendelee kufuatilia ufanisi wa mifumo inayotengenezwa.

(l) Chuo cha Uongozi kihamasishwe uandishi wa tawasifu za viongozi waliofanya mambo yenye kuacha alama katika nchi yetu ili kuwaenzi. Aidha, Chuo kianze

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kuandika tawasifu ya Taifa kwa ajili ya vizazi vijavyo na kuweka taswira kwa nchi nyingine.

(m) Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI waone namna bora ya kushughulikia watumishi wa Halmashauri wanaofanya vibaya sehemu moja na kuhamishiwa sehemu nyingine.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inahusika na kufanikisha azma iliyodhihirishwa katika hotuba ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa kwenye Bunge lako Tukufu siku ya Alhamisi, tarehe 22 Aprili, 2021. Kwa kuzingatia hilo, Kamati imefanya uchambuzi na uchanganuzi kama ilivyoeleza. Aidha, Kamati inatoa maoni kutokana na uchambuzi huo na kukamilisha kwa kutoa ushauri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kufanya hivyo, sasa naomba kipekee niwashukuru kwa moyo wa dhati Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano wao na namna ambavyo wamejitoa kikamilifu kutekeleza ya majukumu ya Kamati. Hali hiyo inadhihirisha kwamba, Wajumbe wa Kamati hii wako tayari kulitumikia Bunge, Taifa na wananchi wake wakati wowote kwa uzalendo mkubwa. Kutokana na hivyo, ningetamani kuwatambulisha Wajumbe wote kwa kuwataja majina yao, lakini kutokana na ufinyu wa muda, naomba majina yao yabaki kwenye kumbukumbu rasmi za Bunge kama nilivyoomba hapo awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika, Wenyeviti wote wa Bunge kwa kazi kubwa na nzuri wanayofanya. Nitumie fursa hii pia kumshukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mheshimiwa Jenista Joackim Muhagama pamoja na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Deogratius John Ndejemi kwa ushirikiano mkubwa walioipa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru pia Makatibu Wakuu Dkt. Moses Kusiluka (Ikulu), Dkt. Laurean Ndumbo (Utumishi), Naibu Katibu Mkuu (Utumishi) Ndugu Exavia Daudi, kwa ushirikiano wao kwa Kamati wakati wa kuchambua taarifa ya Ofisi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, namshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Nenele Mwiambi, *ndc*, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge; Ndugu Athuman Hussein, *ndc*; Makatibu wa Kamati, Ndugu Gerald Magili, Ndugu Angelina Sanga, na Ndugu Sikudhan Mbinga. Kipekee namshukuru msaidizi wetu Ndugu Paulina Mavunde kwa kazi nzuri aliyofanya na Makatibu wote kwa uratibu wao mzuri wa shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kuandaa na kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja hivi punde.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

SEHEMU YA KWANZA

1.0 MAELEZO YA JUMLA

1.1 Utangulizi

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kuhusu Utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, ili kuliwezesha Bunge kufuatilia taarifa hii ipasavyo, naomba kutambulisha sehemu nne za Taarifa hii ambazo ni:-

(a) Sehemu ya **Kwanza** yenye maelezo ya jumla, inabainisha msingi na Muundo wa Taarifa;

(b) Sehemu ya **Pili** yenye ufafanuzi na uchanganuzi, inachambua Taarifa za Utekelezaji, Upatikanaji wa fedha na uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati;

(c) Sehemu ya **Tatu** yenye Maoni na Ushauri, inakamilisha uchambuzi kwa kuonesha maoni au mtazamo kutokana na uchambuzi unaojenga msingi wa ushauri wa Kamati; na

(d) Sehemu ya **Nne** na ya mwisho yenye hitimisho, inamalizia taarifa kwa kulishauri Bunge kuhusu hoja ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

1.2 Msingi wa Uchambuzi wa Kamati

Mheshimiwa Spika, Msingi wa Kamati kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ni Masharti ya Kanuni za Bunge. Kifungu cha 6 (4) (a) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, kinatambua jukumu la Kamati hii kufanya uchambuzi huo. Aidha, Kanuni ya 117(4) ya Kanuni za Bunge imeweka masharti yaliyotaka Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Ofisi hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, ili kukidhi masharti hayo, tarehe 21 hadi 22 Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuhusu Utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Katika hatua hiyo, Kamati ilifanya Uchambuzi wa kina na matokeo yake ni Taarifa hii. Naliomba Bunge lako Tukufu liipokee taarifa hii na kujadili sambamba na Hoja ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

1.3 Mawanda ya Uchambuzi

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu na Makadirio ya Mapato na Matumizi iliyochambuliwa na Kamati, inahusu utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kwa ajili ya Ofisi hii muhimu pamoja na Taasisi zilizo chini yake. Randama zenye taarifa hizo zinahusu Mafungu (Votes) saba ambayo ni:-

- (a) **Fungu 20:** Ofisi ya Rais, Ikulu;
- (b) **Fungu 30:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri;
- (c) **Fungu 32:** Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma;
- (d) **Fungu 33:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma;
- (e) **Fungu 67:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma;
- (f) **Fungu 94:** Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma; na
- (g) **Fungu 04:** Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa.

SEHEMU YA PILI

2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI

2.1 Ufafanuzi wa Jumla

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Bunge ilitoa siku zisizozidi Tisa kwa Kamati kufanya uchambuzi wa Taarifa za utekelezaji wa bajeti. Kanuni hiyo inatambua umuhimu

wa kufanya ulinganisho kati ya utekelezaji wa bajeti unaoripotiwa na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata. Kwa msingi huo, Taarifa hii inaripoti yafuatayo:-

(a) Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022; na

(b) Yatokanayo na uchanganuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

2.2 Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2021/2022

Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati ilizingatia Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Bunge na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti za Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kazi hiyo ilifanyika tarehe 21 na 22 Machi, 2022. Uchambuzi huo ulijenga msingi wa kulinganisha uzoefu uliopatikana kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na mipango ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Mambo yaliyochambuliwa ni Ukusanyaji wa Maduhuli, Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na Upatikanaji wa fedha kwa ajili ya Matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Uchanganuzi huo ni kama ifuatavyo:-

2.2.1 Utekelezaji wa Mipango na Majukumu ya Ofisi ya Rais

Mheshimiwa Spika, bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ilikusudiwa kufanikisha utekelezaji wa mipango na majukumu ya Ofisi ya Rais, Menjimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Ili kuliwezesha Bunge kujiridhisha na mwenendo wa Matumizi unavyoakisi madhumuni ya kuidhinishwa kwa bajeti hiyo, Kamati ilidadisi utekelezaji wa mipango na majukumu ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kulijulisha Bunge hili kuwa kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa bajeti umezingatia mipango na majukumu yaliyooombewa fedha. Kwa mfano, sehemu ya

fedha zilizoidhinishwa na Bunge na kupatikana, zimetumika kusimamia misingi yote ya Utumishi kwa kulinda Maadili ya Mtumishi wa Umma. Aidha, Ofisi hii ilitumia fedha zilizopatikana kusimamia na kuimarisha misingi ya Utawala Bora. Mfano wa usimamizi huo ni juhudi za Serikali kusimamia uzingatiaji wa haki kwa Watanzania wote, Wanawake na Wanaume kwa kuzingatia na kuheshimu Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo, Kamati inampongeza Mhe. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa usimamizi madhubuti wa jambo hilo. Kwa maoni yetu, hali ya usimamizi wa Utumishi wa Umma na kuimarika katika misingi ya utawala Bora, imeipandisha zaidi Tanzania katika medani za utawala Bora Afrika na Duniani.

2.2.2 Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Ofisi hii ilitengewa jumla ya Sh. **183,358,401,000.00** sawa na **asilimia 28.6** ya bajeti yake ya Matumizi ya Maendeleo. Mchanganuo wa kiasi hicho cha fedha kwa Mafungu yaliyo chini ya Ofisi hii umeoneshwa katika **Jedwali Na. 01**.

Jedwali Na.0 1: Mchanganuo wa kiasi cha fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kwa mwaka 2021/2022 kwa kila Fungu

FUNGU	TAASISI	KIASI	% ya Jumla
30	Sekretarieti Baraza la Mawaziri	171,858,401,000	93.7
33	S. Maadili viongozi	1,850,000,000	1.0
32	Utumishi wa Umma	7,650,000,000	4.2
04	Idara ya Kumb. na Nyaraka	2,000,000,000	1.1
JUMLA		183,358,401,000.00	100

Chanzo: Randama za Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, Taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati zilionyesha kuwa hadi mwezi Februari, 2022, Ofisi hii na Taasisi zilizochini yake ilipokea jumla ya Sh. **82,037,068,997.00** kwa ajili ya kugharimia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kiasi hicho ni sawa na **asilimia 44.7** ya Bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya Miradi ya Maendenelo inayotekelezwa na Ofisi hii kwa mwaka 2021/2022. Mchanganuo wa fedha hizo zilizoidhinishwa na kupatikana unaonekana kwenye **Jedwali Na. 02**.

Jedwali Na.0 2: Mchanganuo wa kiasi cha fedha

FUNGU	TAASI	KIASI KILUCHOIHINISHWA	% ya Jumla	KIASI KILUCHOPOKEWA	% ya jumla	% ya lengo
30	Sekretarieti Balaza la Mawaziri	171,858,401,000.00	93.7	78,559,889,830.00	95.8	45.7
33	Sekretarieti ya Maadili viongozi	1,850,000,000.00	1.0	74,510,000.00	0.1	4.01
32	Utumishi wa Umma	7,650,000,000.00	4.2	3,062,669,167.10	3.7	40.0
04	Idaraya Kumb. na Nyaraka	2,000,000,000.00	1.1	340,000,000.00	0.4	17.0
JUMLA		183,358,401,000.00	100	82,037,068,997.00		44.7

Chanzo: Uchanganuzi wa Taarifa kutoka Randama za Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ulioandaliwa na Kamati

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo umeonesha kwamba: -

(a) Hadi kufikia mwezi Februari, 2022, fedha zilizopokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ni **asilimia 44.7** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kiasi hicho ni pungufu ikilinganishwa na kipindi cha utekelezaji wa bajeti wa mwaka unaoisha. Hali hiyo inayoashiria kutokamilika kwa Mradi ifikapo mwezi Juni, 2022.

(b) Upatikanaji wa fedha za Mradi wa Maendeleo kwa ujumla hautoi matumani ya kukamilika kwa Miradi hiyo. Aidha, utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa na Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma unakabiliwa na upatikanaji hafifu wa fedha za kugharimia Miradi ikilinganishwa na Miradi inayotekelezwa na Taasisi nyingine.

(c) Licha ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa jumla wa Miradi ya Maendeleo kuwa hafifu, lakini imeonekana msukumo mdogo kwenye Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa na Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Miradi hiyo katika bajeti ilitengewa **asilimia 1** ya bajeti ya Miradi ya Ofisi hii lakini kwenye upatikanaji wa fedha, Miradi hiyo imepata **asilimia 0.1** ya fedha iliyopokelewa.

Mheshimiwa Spika, Kwa uchambuzi huo, itakuwa vigumu kwa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Aidha, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka haina uwezekano wa kukamilisha utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Hali hiyo ikiendelea, itapoteza maana ya Taasisi hizo kupanga utekelezaji wa mradi ya Maendeleo.

2.2.3 Uchambuzi wa Taarifa za Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma pamoja na Taasisi zake iliidhinishwa jumla ya Sh. **552,609,738,829.00** kwa ajili ya Matumizi Kawaida. Hata hivyo, taarifa zilionyesha kuwa, hadi kufikia Mwezi Februari, 2022, zilipokewa jumla ya Sh. **384,448,364,791.19** sawa na **asilimia 69.6** ya bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Mchanganuo wa fedha zilizoidhinishwa na kupatikana kwa Taasisi zilizochini ya Ofisi hii unaonekana katika **Jedwali Na. 03**.


Jedwali Na.03: Ulinganisho wa kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na kupokelewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida hadi Februari, 2022

TAASISI	MAKADIRO KWA MWAKA 2021/2022	KIASI KILICHOPATIKANA HADI MMEZI FEBRUARI, 2022	% YA MAKADIRO
OR -Ikulu	24,557,764,000.00	16,303,723,999.98	66.4
Sekretarieti Balaza la Mawaziri	467,921,917,000.00	325,350,798,801.90	69.5
Sekretarieti ya Maadili viongozi	7,366,921,000.00	4,661,073,244.47	63.3
Utumishi wa Umma	38,219,114,000.00	27,513,866,417.10	72.0
Sekretarieti ya Ajira	3,388,771,000.00	3,044,094,284.68	89.8
Tume ya Utumishi wa Umma	6,560,233,829.00	4,879,498,000.00	74.4
Idara ya Kumb. na Nyaraka	4,595,018,000.00	2,695,310,043.06	58.7
JUMA	552,609,738,829.00	384,448,364,791.19	69.6

Chanzo: Uchanganuzi wa Taarifa zilizomo kwenye Randama za Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi unaonesha kwamba:

(a) Mwenendo wa jumla wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya Matumizi ya kawaida hadi mwezi Februari, 2022 ni **asilimia 69.6**. Hata hivyo ulinganisho wa upatikanaji wa fedha kwa Mafungu ya Ofisi hii unaonesha kutofautiana kwa kiasi kinachopokelewa kama inavyoonekana katika **Mchoro Na. 01**.



Chanzo: Uchanganuzi wa data katika Jedwali Na. 03 kwa ajili ya kufanya ulinganisho

(b) Hadi mwezi Februari, 2022, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma ilipokea fedha iliyoidhinishwa kwa kiwango cha **asilimia 89.8** ya bajeti yake ya Matumizi ya Kawaida. Kwa mwenendo huo, kuna uwezekano mkubwa wa kupata na kutumia fedha kama iliyoidhinishwa na Bunge;

(c) Mwenendo wa upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida kwa ajili ya Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka hautoi matumaini. Hadi mwezi Februari, 2022, idara hii ilipokea **asilimia 58.7** ya bajeti yake ya Matumizi ya Kawaida. Kwa hali hiyo, uendeshaji wa shughuli za Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka umeathirika kwa kiasi.

(d) Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma imepokea kiasi kidogo cha fedha za uendeshaji. Ulinganisho unaonesha kuwa shughuli za Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na za Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka hazijapata uzito unaostahili kwa kupewa kiasi cha fedha pungufu ya **asilimia 65** ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa uchambuzi huo, ni dhahiri uzoefu unaopatikana katika mwaka wa fedha 2021/2022 utafaa kutumika ili kuzikabili changamoto za upatikanaji wa fedha kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

2.2.4 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati

Mheshimiwa Spika, wakati wa kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Kamati ilitoa Maoni na Ushauri katika maeneo Kumi na Nane (18). Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa ushauri wa Kamati umezingatiwa.

Mheshimiwa Spika, Mfano wa ushauri uliozingatiwa, unahusu Serikali kukamilisha usanifu na ujenzi wa Mfumo Maalum (Government Enterprise Service Bus, GovESB) wa kuwezesha Mifumo ya Serikali kusomana na kubadilishana Taarifa.

Utekelezaji ulioripotiwa unaonesha kuwa baadhi ya Taasisi zimeunganishwa na Mpango kazi wa kuhakikisha Taasisi zote za Serikali zinaunganishwa katika Mfumo huu. Aidha, viwango na Miongozo imeandaliwa kuwezesha ubadilishanaji wa Taarifa kuwa endelevu, wenye tija na usalama wa Taarifa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuipongeza Serikali kwa kuzingatia sehemu kubwa ya ushauri uliotolewa, bado kuna umuhimu kwa Serikali kuujali ushauri unaotolewa na Kamati Bungeni. Kwa maoni ya Kamati, uzingatiaji wa ushauri wa Kamati unawezesha Serikali kukidhi matarajio ya Wananchi wanaowakilishwa Bungeni.

2.3 Yatokanayo na Uchanganuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023

Mheshimiwa Spika, Kanuni za Kudumu za Bunge zimetambua umuhimu wa uzoefu unaopatikana katika mwaka wa fedha unaoisha ili kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata kama ilivyoelekezwa katika Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Bunge. Kamati imezingatia umuhimu huo na masharti ya Kanuni za Bunge kwa kuchambua mambo Makuu manne kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kama ifuatavyo:-

2.3.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Jumla ya Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora

Mheshimiwa Spika, kuhusu Makadirio ya Matumizi, Kamati ilijulishwa kwamba, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inaomba kuidhinishwa Matumizi ya Sh. **850,787,564,000.00** Kiasi hicho ni ongezeko la bajeti la asilimia **16** ikilinganishwa na Bajeti ya Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Uchanganuzi wa Makadirio hayo kwa Taasisi zilizo chini ya Ofisi hii, unabainishwa kwenye **Jedwali Na. 04**.

Jedwali Na.0 4: Mchanganuo wa Makadirio ya Matumizi ya Ofisi hii na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

FUNGU	TAA SISI	KIASI	% ya Jumla
20	OR –Ikulu	29,828,203,000.00	3.5
30	Sekretarieti Balaza la Mawaziri	741,299,267,000.00	87.1
33	Sekretarieti ya Maadili viongozi	12,730,049,000.00	1.5
32	Menejimenti ya Utumishi wa Umma	47,611,581,000.00	5.6
67	Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma	8,721,849,000.00	1
94	Tume ya Utumishi wa Umma	5,681,824,000.00	0.6
04	Idara ya Kumb. na Nyaraka	4,914,791,000.00	0.6
JUMLA		850,787,564,000.00	100

Chanzo: *Uchanganuzi wa Kamati wa Taarifa za Randama za Mafungu yote chini ya Ofisi hii*

Mheshimiwa Spika, kwa kuthamini uzoefu uliopatikana katika utekelezaji wa Bajeti inayoisha, Kamati ilifanya ulinganisho kati ya Makadirio hayo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na Bajeti iliyoidhinishwa na kupatikana kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Mchanganuo na ulinganisho uliofanyika unaonekana katika **Jedwali Na. 05**.

Jedwali Na.0 5: Mchanganuo wa Makadirio kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 ikilinganishwa na maombi ya fedha kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

TAASISI	BAJETI KWA MWAKA 2021/2022	FEDHA ILIYOPATIKANA		FEDHA INAOMBWA KWA MWAKA 2022/2023	ONGEZECO
OR –Ikulu	24,555,764,000.00	16,303,723,999.98	66.4	29,828,203,000.00	21.5
Sekretarieti Balaza la Mawaziri	639,780,318,000.00	325,350,798,801.90	69.6	741,299,267,000.00	58.6
Sekretarieti ya Maadili viongozi	9,216,921,000.00	7,366,921,000.00	79.9	12,730,049,000.00	38.1
Menejimenti ya Utumishi wa Umma	45,869,114,000.00	30,576,535,584.20	66.7	47,611,581,000.00	3.8
Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma	3,388,771,000.00	3,044,094,284.68	89.8	8,721,849,000.00	157
Tume ya Utumishi wa Umma	6,560,233,829.00	4,879,498,830.00	74.4	5,681,824,000.00	-13.4
Idara ya Kumb. na Nyaraka	4,595,018,000.00	1,899,707,956.97	41.3	4,938,791,000.00	7.5
JUMLA	733,966,139,829.00	389,421,280,457.73	69.4	850,811,564,000.00	16

Chanzo: Uchanganuzi wa Kamati wa Taarifa za Randama za Mafungu yote chini ya Ofisi hii

Mheshimiwa Spika, kwa uchambuzi huo, Kamati imebaini kama ifuatavyo:-

(a) Kwa ujumla Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 yameongezeka kwa **asilimia 16** ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Hata hivyo, Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya Tume ya Utumishi wa Umma yamepungua kwa **asilimia 13.4**.

(b) Makadirio ya Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma yameongezeka kwa kiasi kikubwa, ambacho ni **asilimia 157.4**. Ongezeko hilo limetokana na kutengewa fedha kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo inayohusu uboreshaji wa Mifumo.

(c) Pamoja na ongezeko la jumla la bajeti uzoefu uliopatikana kuhusu upatikanaji wa fedha kwa mwaka 2021/2022

unaonyesha kuwa ongezeko hilo linaweza lisiwe na tija iwapo fedha hazitopatikana kama inavyopangwa.

2.3.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ya Kawaida

Mheshimiwa Spika, Kamati ilizingatia kuwa Matumizi ya Kawaida yanahusu Gharama za Uendeshaji na Mishahara katika Ofisi hii na Taasisi zinazohusika. Ili kutathmini mwelekeo wa utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora katika kutoa huduma kwa Wananchi, Kamati ilichambua Makadirio ya Matumizi ya kawaida yaliyowasilishwa na Mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, katika kufanikisha hilo, Kamati ilichanganua jumla ya Sh. **850,787,564,000.00** zinazoombwa kwa Matumizi ya Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Uchanganuzi huo kwa kutumia njia ya majedwali, ulilenga kuona uwiano wa Matumizi ya Kawaida na Matumizi ya Maendeleo kwa kila Taasisi chini ya Ofisi hii. Aidha, ulinganisho wa Makadirio hayo kwa upande mmoja na bajeti iliyoidhinishwa na kupatikana kwa mwaka 2021/2022 ikililinganishwa na upatikanaji wa fedha kwa upande mwingine, ni miongoni mwa vigezo vya uchambuzi vilivyotumiwa na Kamati. Mchanganuo huo unaonekana katika **Jedwali Na. 06**.

Jedwali Na.0 6: Ulinganisho wa Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na upatikanaji wa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022

TAASISI	BAJETI KWA MWAKA 2021/2022	FEDHA ILIYOPATIKANA	MAOMBI KWA MWAKA 2022/2023	% OINGEZEKO
OR -Ikulu	24,557,764,000.00	16,303,723,999.98	29,828,203,000.00	21.5
Sekretarieti za laa la Wawaziri	467,921,917,000.00	325,350,798,801.90	577,206,673,000.00	23.4
Sekretarieti ya Vaa diti viongozi	7,366,921,000.00	4,661,073,244.47	9,260,049,000.00	25.7
Venejimenti ya Utumishi wa Jmma	45,869,114,000.00	27,513,866,417.10	39,541,381,000.00	-13.8
Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Jmma	3,388,771,000.00	3,044,094,284.68	5,063,849,000.00	49.4
Tume ya Utumishi wa Jmma	4,879,998,430.00	4,879,498,830.00	5,481,824,000.00	12.3
dara ya Kumb. na Nyaraka	2,571,018,000.00	1,559,707,956.97	3,504,791,000.00	36.3
JUMLA	556,555,503,430.00	383,312,763,535.10	669,886,770,000.00	20.4

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi umeonesha kwamba:

(a) Kama ilivyo kwenye Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, Bajeti ya Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma imeongezeka kwa **asilimia 19.4** ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka 2021/2022.

(b) Bajeti ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Fungu 32 imepungua kwa **asilimia 13.8**.

(c) Kwa ujumla Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Taasisi zake yameongezeka kwa **asilimia 20.4**.

Mheshimiwa Spika, kwa uchambuzi huo ni dhahiri kuwa shughuli za usimamizi na uboreshaji wa Utumishi wa Umma pamoja na kusimamia misingi ya utawala bora zitatekelezwa kwa ufanisi zaidi. Hata hivyo, ufanisi huo utategemea kwa

kiasi kikubwa na upatikanaji wa fedha. Bila shaka, Serikali itazingatia uzoefu uliopatikana katika utekezaji wa bajeti ya mwaka 2021/2022 kurekebisha changamoto za upatikanaji wa fedha.

2.3.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya utekezaji wa Miradi ya Maendeleo yanasaidia kutoa picha ya mahitaji ya kiasi cha fedha kwa ajili ya Miradi katika kila hatua. Makadirio hayo yanapolinganishwa na uzoefu uliopatikana kwa Mwaka wa Fedha unaoisha, husaidia kubainisha picha halisi na uwezekano wa utekezaji wa Miradi inayohusika. Kwa msingi huo, Kamati ilichambua Makadirio ya bajeti ya Maendeleo ya Ofisi hii na Taasisi zilizo chini yake na kulinganisha na Matumizi ya fedha kwa ajili hiyo kwa mwaka wa fedha unaoisha. Mchanganuo wa Makadirio hayo unaonekana katika **Jedwali Na. 07**.

Jedwali Na.0 7: Uchanganuzi wa Makadirio ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kwa Ofisi hii na Taasisi zake ikilinganishwa na Mwaka 2021/2022

TAASISI	BAJETI KWA MWAKA 2021/2022		MAKADIRIO KWA MWAKA 2022/2023	
	KIASI KILICHODHINISHWA	% YA KUPOKEA	MAKADIRIO	% ONGEZEKO
Sekretarieti Balaza la Mawaziri	171,858,401,000	45.7	164,092,594,000.00	-4.5
Sekretarieti ya Maadili viongozi	1,850,000,000	4	3,470,000,000.00	87.6
Menejimenti ya Utumishi wa Umma	7,650,000,000	40.03	8,070,200,000.00	5.5
Idara ya Kumb. na Nyaraka	2,000,000,000	17	1,410,000,000.00	-29.5
Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma	-	0	3,658,000,000.00	
	183,358,401,000	44.7	180,700,794,000.00	-1.4

Mheshimiwa Spika, uchambuzi umeonesha yafuatayo:-

(a) Jumla ya fedha inayoombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni **Sh. 180,700,794,000.00** sawa na **asilimia 0.4** ya bajeti yote ya Taifa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

(b) Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni **asilimia 21.2** ya bajeti ya Ofisi hii. Uwiano huo wa Matumizi ya Maendeleo kwa bajeti ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inatofautiana na uwiano katika bajeti kuu kati ya bajeti ya Miradi ya Maendeleo na Matumizi ya kawaida. Wakati kwa Ofisi hii uwiano wa Matumizi ya Maendeleo kwa Matumizi ya kawaida ni **asilimia 21.2** kwa **asilimia 78.8**, uwiano katika bajeti kuu ni **asilimia 37.8** kwa **asilimia 62.2**.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

3.1 Maelezo

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kukamilisha uchambuzi kwa kubainisha Maoni ya Kamati yanayojenga mtazamo ambao ni msingi wa Ushauri wa Kamati. Maoni hayo ni kama ifuatavyo:-

(a) Ushauri unaotolewa Bungeni kuhusu utekelezaji wa Mipango, Majukumu na Bajeti unahitaji kupewa nafasi stahiki ili kukidhi matarajio ya Wananchi;

(b) Kuna umuhimu wa kufanikisha upatikanaji wa kiasi cha fedha za Matumizi kama inavyoidhinishwa na Bunge. Vinginevyo kuna hatari ya kukosekana kwa tija ya mipango inayokusudiwa kwa kipindi kinachohusika;

(c) Fedha kwa ajili ya majukumu na shughuli zinazohusu kuhifadhi Kumbukumbu Tuli, Utunzaji wa Kumbukumbu na Ofisi Mtandao, Utunzaji wa Nyaraka na Kuwaenzi Waasisi wa Taifa zisipopatikana ipasavyo, inaweza kuathiri uwezo wa Taifa kukidhi malengo yake; na

(d) Juhudi za Serikali kuimarisha misingi ya Utawala Bora na uzingatiaji wa haki kwa Watanzania wote, Wanawake na Wanaume kwa kuzingatia na kuheshimu Katiba na Sheria ni jambo linalosukuma Maendeleo halisi ya Tanzania.

3.2 Ushauri wa Kamati

Mheshimiwa Spika, kwa Maoni niliyobainisha kutokana na uchambuzi, naomba kutoa Ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

(a) Serikali iendelee kuzingatia ipasavyo, Ushauri unaotolewa Bungeni kuhusu utekelezaji wa Mipango, Majukumu na Bajeti kwa madhumuni ya kukidhi mataraji ya Wananchi;

(b) Serikali ihakikishe kuwa fedha inayoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Ofisi hii na Taasisi zake inapatikana ipasavyo ili kufanikisha upatikanaji wa manufaa ya utekelezaji wa majukumu yaliyopangwa;

(c) Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa iwezeshe kifedha ili imudu na kuboresha utekelezaji wa majukumu yake ya kuhifadhi Kumbukumbu Tuli, Kutunza Kumbukumbu mbalimbali na Ofisi Mtandao, kutunza Nyaraka pamoja na Kuwaenzi Waasisi wa Taifa;

(d) Serikali iendelee kuimarisha misingi ya Utawala Bora pamoja na na Kuboresha zaidi miundombinu, Maendeleo ya Watumishi na Mifumo ya utendaji kazi katika Utumishi wa Umma sambamba na kuboresha Mishahara na maslahi ya Watumishi;

(e) Watumishi waendeleo kuhimizwa kuwa Wazalendo kwa nchi yetu na kufanya kazi kwa uadilifu, bidii, weledi na maarifa kama Msingi imara wa Maendeleo;

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(f) Serikali iendelee kutoa Ajira zaidi ili kukabiliana na changamoto ya upungufu wa Watumishi;

(g) Serikali iendelee kusimamia na kutoa mafunzo maalumu ya mara kwa mara kwa Watumishi wa Umma ili kuwezesha utendaji kazi unaozingatia weledi na ustadi mkubwa;

(h) Ujenzi wa Ikulu ya Chamwino ukamilishwe kwa wakati kama ilivyokusudiwa;

(i) Serikali iweke Mikakati inayotekelezeka ya kutumia Rasilimali zake zinazojumuisha Watu wake ambao kimsingi wana uwezo mkubwa. Pia, kutumia Rasilimali nyingine za nchi;

(j) Serikali itengeneze Kanzidata ya wanaofanyiwa usaili na kufaulu kwa lengo la kuwa na orodha ya Wataalamu wenye sifa wasioajiriwa, ambao wanaweza kuajiriwa bila usaili iwapo itatokea nafasi za ajira;

(k) Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) ya Uundaji wa Mifumo ya Kielektroniki inayofanikisha ukusanyaji wa Mapato ya Serikali, Mamlaka hiyo iendelee kufuatilia ufanisi wa Mifumo inayotengenezwa;

(l) Chuo cha Uongozi kihamasishe uandishi wa Tawasifu za Viongozi waliofanya mambo yenye kuacha alama katika nchi yetu ili kuwaenzi. Aidha, Chuo kianze kuandika Tawasifu ya Tanzania kwa ajili ya vizazi vijavyo na kuweka Taswira kwa nchi zingine; na

(m) Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI waone namna bora ya kushughulikia Watumishi wa Halmashauri wanaofanya vibaya sehemu moja na kuwahamishia sehemu nyingine.

SEHEMU YA NNE

4.0 HITIMISHO

4.1 Maelezo ya Kuhitimisha

Mheshimiwa Spika, kabla ya kumaliza taarifa hii, nilikumbushe Bunge lako Tukufu kuhusu mwelekeo aliouweka Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan, alipolihutubia Bunge hili tarehe 22 Aprili, 2021 kwa kusema:

Naomba kunukuu: "Tutawapima Viongozi na Watumishi kwa namna wanavyotimiza majukumu yao, hatutawaonea aibu Viongozi na Watumishi wazembe, wezi na wabadhirifu wa mali za Umma. Tutaendeleza juhudi za kupambana na rushwa kwenye Utumishi wa Umma. Wajibu wa Watumishi wa Umma ni lazima uendane na haki zao."

Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inahusika na kufanikisha azma iliyodhihirishwa katika kauli hiyo. Ni dhahiri kuwa, maombi ya fedha yaliyowasilishwa na Mtoa hoja kabla ya taarifa hii, yanalenga kuenzi na kutimiza kwa vitendo mwelekeo alioutoa Mheshimiwa Rais mbele ya Bunge, siku ya Alhamisi, tarehe 22 Aprili, 2021. Kwa kuzingatia hilo, Kamati imefanya Uchambuzi na uchanganuzi kama nilivyoeleza. Aidha, Kamati imetoa Maoni kutokana na uchambuzi huo na kukamilisha kwa kutoa Ushauri.

4.2 Shukurani

Mheshimiwa Spika, baada ya kufanya hivyo, sasa naomba kipekee niwashukuru kwa moyo wa dhati Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano wao na namna ambavyo wamejitoa kikamilifu katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Katika kipindi hiki cha kushughulikia bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Wajumbe walijitoa kikamilifu na kutekeleza majukumu ya uchambuzi kwa moyo na weledi wa hali ya juu, bila kujali

ufinyu wa muda uliotengwa ikilinganishwa na Mafungu mengi yaliyo chini ya Ofisi hii. Hali hiyo ni udhirisho tosha kwamba, Wajumbe wa Kamati hii wako tayari kulitumikia Bunge, Taifa na Wananchi wakati wowote kwa Uzalendo mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu wake ningetamani kuwatambua Wajumbe wote wa Kamati kwa kutaja majina yao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Abdallah Jafari Chaurembo, Mb – **Mwenyekiti**
2. Mhe. Dennis Lazaro Londo, Mb – **Makamu Mwenyekiti**
3. Mhe. Margaret Simwanza Sitta, Mb
4. Mhe. Mwantum Mzamili Zodo, Mb
5. Mhe. Dkt. Thea Medard Ntara, Mb
6. Mhe. Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mb
7. Mhe. Festo Richard Sanga, Mb
8. Mhe. Rehema Juma Migila, Mb
9. Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mb
10. Mhe. Mwatam Dau Haji, Mb
11. Mhe. Amandus Julius Chinguile, Mb
12. Mhe. Sebastian Simon Kapufi, Mb
13. Mhe. Michael Constatino Mwakamo, Mb
14. Mhe. Lazaro Justin Nyamoga, Mb
15. Mhe. Mwantakaje Haji Juma, Mb
16. Mhe. Omar Issa Kombo, Mb
17. Mhe. Shanif Jamal Mansoor, Mb
18. Mhe. Zacharia Paul Issaay, Mb
19. Mhe. Seif Salum Seif, Mb
20. Mhe. Constantine John Kanyasu, Mb
21. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis, Mb
22. Mhe. Tunza Issa Malapo, Mb
23. Mhe. William Vangimembe Lukuvi, Mb
24. Mhe. Prof. Palamagamba Aidan Mwaluko Kabudi, Mb

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumshukuru sana Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Jenista Joachim Mhagama (Mb), pamoja na Naibu Waziri wa nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Deogratius John Ndejemi (Mb), kwa ushirikiano mkubwa walioipatia Kamati wakati wa kuchambua Hoja aliyoiwasilisha. Nawashukuru pia Makatibu

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Wakuu Dkt. Moses Kusiluka (Ikulu), Dkt Laurean Ndumbaro (Utumishi), na Naibu Katibu Mkuu (Utumishi) Ndg. Exavia Daudi, kwa ushirikiano wao kwa Kamati wakati wa kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee namshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nanelwa Mwiambi, *ndc*, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg, Athuman Hussein, *ndc*, Makatibu wa Kamati, Ndg. Gerald Magili, Ndg. Angelina L. Sanga, na Ndg. Sikudhan Mbinga wakisaidiwa na Ndg. Paulina Mavunde, kwa uratibu wao mzuri wa shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kuandaa na kukamilisha Taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja hivi punde.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Abdalla J. Chaurembo (Mb)

MWENYEKITI

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA
UTAWALANA SERIKALI ZA MITAA**

21 Aprili, 2022

SPIKA: Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kwa maoni hayo ambayo umeyatoa kwa niaba ya Kamati; na kwa hivyo kwa niaba ya Bunge.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Waheshimiwa Wabunge, kwa utaratibu wetu, ninayo majina hapa ya Wabunge ambao wanatamani kuchangia siku ya leo kwenye hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. Tutaanza na Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, atafuatiwa na Mheshimiwa Janejelly James Ntate na Mheshimiwa Prof. Kitila Alexander Mkumbo ajjandae.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa kwanza katika Wizara hii. Kipekee sana nampongeza sana Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana katika Wizara hii. Sambamba naye nampongeza pia Naibu Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya bila kuwasahau Makatibu Wakuu wote wawili na Watendaji wote wa Wizara hii ambayo ni nyeti sana kwa kuhudumia shughuli mbalimbali za Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo ni mwaka mmoja tangu Mheshimiwa Rais alihutubie Bunge lako Tukufu, maana alihutubia Bunge hili tarehe 22 mwezi wa Nne 2021. Kwa hiyo, leo ni mwaka mmoja tangu hotuba yake aitoe ndani ya Bunge hili na katika mchango wangu nitapenda nianze na nukuu ambayo ameitoa wakati anahutubia Bunge. Alisema: *“Serikali itaendelea kutekeleza kwa vitendo dhamira yake ya kuwa Serikali anayoiongoza na itaendeleza jitihada za kuimarisha maadili, nidhamu, uzalendo, uchapakazi na uwajibikaji.” (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia aliahidi pia kusimamia haki na stahiki za watumishi wa umma na watendaji Serikalini ili kuongeza ari ya kufanya kazi kwa bidii na kukuza uwajibikaji wa hiyari katika utumishi wa umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ni ahadi ya Mheshimiwa Rais na mara zote Mheshimiwa Rais alikuwa anatembea katika vitendo vyake. Na tumeona, baada ya ahadi hii alianza kazi kubwa ya kwanza kupandisha madaraja jambo hili ambalo lilikuwa limesimama kwa muda mrefu sana tangu mwaka 2016/2017 lakini kwa mkupuo alikuja kupandisha madaraja

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

watumishi takribani 190,761. Hali kadhalika kuna watumishi wengine takribani 926,190 watapandishwa madaraja na wako katika hatua mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mchango wangu nilipenda pia kusema eneo moja kwamba katika upandishaji huu wa madaraja kwa mkupuo, tunashukuru kwamba una faida hii; kwamba tumewapandisha kwa mkupuo lakini katika ule mkupuo kuna wale ambao sasa walikuwa wamecheleweshwa sasa kwa kuwapandisha kwa mkupuo maana yake inabidi wale wachache ambao sasa wana sifa za ziada ambazo walicheleweshwa nao tuwabaini ili waweze kusongezwa mbele zaidi ya madaraja. Hii itasaidia pia kuwapatia stahiki zao kwa mujibu wa sheria na baadhi yao wengi wanakaribia kuelekea kustaafu. Maana yake ni kwamba hata mafao yao yaweze kupangwa kulingana na madaraja hayo mapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo tumeona pia upandishaji wa vyeo, kwamba tumeona wanaendelea kupanda vyeo katika nafasi mbalimbali; na sasa wanakaribia kufikisha watumishi takribani 25,000 ambao wamepandishwa nafasi mbalimbali katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, jambo hili linaonesha ile dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Rais ya kuongeza ari na uwajibikaji Serikalini, na hii pia inachagiza, ni sehemu ya motisha, ya watumishi ya kuendelea kujitoa na kuendelea kuwajibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nataka niseme moja ambalo ninaamini kabisa kwamba kwa ninavyomwamini Mheshimiwa Rais hawezi akaacha lipite hivi hivi; hili la kuhusu kupandisha mishahara ya watumishi wa umma. Hili ni jambo ambalo muda mrefu sana halijafanyiwa kazi, takribani sasa ni miaka sita. Lakini kwa ahadi hizi ambazo ameendelea kuzitimiza hata hili ninaamini siku ile ya Meimosi ambayo ndiyo aliyotoa ahadi na haya yote ameweza kuyatekeleza ndani ya kipindi cha mwaka mmoja naamini kabisa kwamba inawezekana kabisa kwa bajeti hii iliyotoka, Trilioni 36 mwaka 2021/2022 na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

hii ya mwaka 2022/2023 ambayo tunasoma takribani Trilioni 41 sitaki kuamini kwamba fedha zote hizi zinakwenda kwenye miradi, ninaamini kabisa kwamba na watumishi safari hii na wenyewe watatoka kifua mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo hili ni muhimu sana, kuongeza motisha ya wafanyakazi kupitia mishahara kwasababu kwanza tutambue watumishi hawa ni sehemu ya kodi za Serikali, kupitia mishahara yao Serikali inakusanya kodi; kwa hiyo tunapowaongeza maana yake pia tutaongeza kodi hapo baadaye kupitia mishahara ya watumishi, kwa hiyo kwa hali ilivyo sasa ya mfumuko wa bei na upandaji wa gharama mbalimbali za maisha, mimi naamini kabisa kwamba ni wakati sahihi kabisa kwa watumishi nao sasa kuweza kuonwa kwa jicho hili la huruma la Mheshimiwa Rais na wenyewe sasa waweze kupambana na hali hii ya kimaisha, lakini pia kuongeza tija na uwajibikaji katika utumishi wa umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo ningependa kulichangia ni katika fungu 40 ambalo sasa hili ni fungu maalum kwa ajili ya Ofisi ya Rais Ikulu; hili fungu ni muhimu sana. Na katika bajeti hii ambayo imepita tumetenga takribani Shilingi bilioni 24.5 na hadi mwezi Machi zimeshatumika bilioni 18.3. Hili ni eneo muhimu sana Waheshimiwa Wabunge, hizi ndio fedha ambazo zinamwezesha Rais kufanya kazi hizi kubwa ambazo tumeziona katika kipindi hiki kifupi. Hii ndiyo kazi kubwa ambayo zile trillion zilizokuja kwenye madarasa kwenye maji, kwenye afya na maeneo minjini yote zimetokana na fungu hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni vizuri sana tumtengee Rais fedha hizi za kutosha aweze kuzunguka maeneo mbalimbali katika dunia; lakini pia zimesaidia hata kukuza mitaji na uwekezaji, kwasababu tumeona hata hivi karibuni Mheshimiwa Rais alikuwa katika Falme za Kiarabu amefanya kongamano kubwa la *expo* kule ambako amekutana na wafanyabiashara na wawekezaji kutoka maeneo mbalimbali. Hii yote ni mitaji ambayo inatokana na kazi nzuri

sana ya fungu hili. Kwa hiyo fungu hili ni vizuri sana hata wakati wa kupitisha tupitisha kwa sauti kubwa ili sasa tumpe funguo Mheshimiwa Rais ya kwenda kututafutia mafungu mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halikadhalika Filamu ya *Royal Tour* ambayo ameizindua hivi karibuni kule Marekani, na tutaanza sasa uzinduzi wake katika Taifa letu, hili nalo ni eneo mahsusi sana la kimkakati kwa ajili ya kukuza utalii wa Watanzania. Tunaona kabisa kwamba dhamira njema hii ya Mheshimiwa Rais kupitia kazi ambayo ameifanya katika filamu ile yeye mwenyewe kuwa kama ndiye *tour guide* namba moja wa Taifa sasa iwe *wake up calls* kwa tasnia nzima ya utalii, lakini pia na Wizara nyingine zote kufungamanisha eneo hili la utalii, na pia kukuza uwekezaji na mitaji katika maeneo mengine kwa sababu sasa Tanzania inatangazika katika maeneo mbalimbali duniani kupitia hiyo *loyal tour*. Kwa hiyo hapa ndipo nilipotaka nielezee kumuhimu mkubwa sana wa fungu hili la 20 ambalo ni ofisi mahsusi ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Eneo la mwisho ambalo nilitaka kulichangia ni eneo la uhaba wa watumishi katika maeneo mbalimbali ya huduma za kijamii hasa elimu na afya. Tumeona kwamba kuna ahadi ya ajira mpya takribani 32,000. Tunaomba sana hivi ajira zitangazwe kwa haraka na zibainishwe vizuri, maana wametokea matapeli ambao wanachanganya vijana wetu. Kwa hiyo ni vizuri kwenye tovuti za Serikali mambo haya yawe hadharani ili wananchi waweze kupata fursa ya kuomba ajira hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Janejelly James Ntate atafuatiwa na Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo, Mheshimiwa Ester Amos Bulaya ajiandae.

MHE. JANEJELLY J. NTATE: Mheshimiwa Spika, ahsante; na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu kupata nafasi ya kuchangia kwenye bajeti ya Menejimenti ya Utumishi wa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Umma. Pia nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye alimwongoza Mheshimiwa Rais na kutuletea Jenista Mhagama kuwa Waziri wa Utumishi. Nasema hivyo nina maana gani, Mheshimiwa Jenista tumekuwa naye kwenye vyama vya wafanyakazi, lakini masuala mengi tulikuwa tukimwambia anasema lazima nishauriane na Waziri wa Utumishi, na sasa amepewa mtoto alee mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nifikishe salamu za watumishi wa Tanzania wakimpongeza Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan. Wanampongeza kwa sababu gani; kwa mwaka mmoja ametoa Shilingi bilioni 300 ili watumishi wapandishwe madaraja, ametoa Shilingi bilioni 23 ili watumishi walipwe malimbikizo ya mishahara yao. Amepunguza kodi kutoka asilimia tisa kwenda nane. lakini kwenye mfuko wa jamii amepeleka Trilioni 2.17 ili wastaafu walipwe. Hakika amejipambanua kwamba yeye maono yake ni kuendeleza maslahi watumishi wa Tanzania, Mungu ambariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwa msingi huu leo nitashauri, na ninajua Mheshimiwa Jenista haya utayachukua na utayafanyia kazi nakuamini. Ushauri wangu ni kwenye upandishwaji wa madaraja kwa watumishi. Mmesema mtaendelea na zoezi la kupandisha madaraja watumishi wa Tanzania lakini upandishwaji huu una mambo matatu yote yanaongelea kupandishwa watumishi.

Mheshimiwa Spika, kuna *Public Service Act Part II 6 (a)* inaongelea upandishwaji wa madaraja na ujazaji wa nafasi zilizo wazi, imetaja vigezo kabisa. Lakini mwongozo wa 2013 unaendana na *Public Service Act*. Sasa, kuna mwongozo wa mwaka 2019, huu ndio ulikuja na kuumiza watumishi na umeruvuga mambo fulani kwenye utumishi. Mwongozo huo unasema, mtumishi aliyeanza kazi kupanda cheo ni miaka mitano, mmoja kuthibitishwa kazini minne ya kusubiri; hii ni sawasawa na umri wa mtoto kuanza shule. Lakini aliye kazini miaka minne, aliyeenda masomoni muda wake umepotea, hata pandishwa. Sasa Mheshimiwa Jenista mnaenda kupandisha watumishi vyeo, nitaomba wakati

unakuja kuhitimisha uniambie mtatumia mwongozo upi kati ya hii mitatu. *(Makofi)*

Niende kwa watumishi ambao wanakuwa wamepewa teuzi za mamlaka ya Mheshimiwa Rais. Teuzi hizi zinapokoma watumishi hawa wanachelewa kupangiwa kazi, na kwa sababu hiyo kunakuwa kuna hasara mbili; kwa upande wa Serikali kunakuwa na hasara ya kulipa mshahara kwa mtu asiyefanya kazi; na Mungu amesema asiyefanyakazi asile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwa mtumishi mwenyewe binafsi anaweza kuwa na msongo wa mawazo, ulevi na huweza kufa kifo ambacho hakikupangwa na Mwenyezi Mungu. Hilo hilo nalo naomba uliangalie ili teuzi za watu hawa zikikoma basi wapangiwe sehemu za kazi mapema.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna watumishi ambao wanatolewa kwenye taasisi kuja kujaza nafasi kwenye Wizara za Serikali na Idara za Serikali, na hapa naomba mpaangalie sana. Watumishi wanaotoka kwenye taasisi wanakuja na mishahara mikubwa, anapofika kwenye Wizara au Idara mwingine ana mashahara kuliko hata Katibu Mkuu wake, sasa sijui hapa kumtuma kunakuwaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini la pili pale kunakuwa na watumishi ambao wameumia na wewe kuanzia vyeo vya chini mpaka wamefika vyeo vya juu. Sasa hao watumishi mnarudisha utendaji kazi wao nyuma. Lakini kama mngekuwa mnawachukua wao mkawapandisha kuwa wakuu wa Idara au wakuu wa Vitengo walio chini yao watafanya kazi vizuri sana ili nao waweze kupanda. Na kwa hili sitaficha, naipongeza taasisi ya Bunge, Bunge wameonesha mfano, Bunge watumishi wao, Wakuu wa Idara, Wakurugenzi, Katibu wao wamezaliwa humo humo kwa watumishi ambao wamewalea wenyewe. Hilo naomba ulichukue tulifanyike kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na niliwahi kuliuliza nikaambiwa *vetting* sasa huyu tangu akiwa cheo cha kwanza, anaenda

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mpaka anakuwa *principal* hizo *vetting* hazikuonekana? Zinaonekana wakati wa kujaza hiyo nafasi tu? naomba menejimenti ya utumishi wa umma hilo mliangalie.

Mheshimiwa Spika, kuna swala la *recategorization*, mnakwenda kufanya *recategorization*; na niliwahi kuuliza swali la msingi nikajibiwa lakini sikuridhika, na kiti cha Spika kikasema swali la Mheshimiwa Janejelly lina *logic* lakini mmemjibu mnavyoelewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kupunguza mshahara wa mtumishi ni adhabu kati ya adhabu tatu, lakini sasa huyu mtumishi amesoma watoto wake walikuwa wanakula mlo mmoja ili akajisomeshe anapomaliza anakuja kubadilisha kada mnamwambia tunakushusha na mshahara. Sasa kusoma imekuwa ni adhabu. Lakini niwaambie, hakuna anachokuwa anakwenda kuweka gharama, hata *wage bill* bajeti yake ni ile ile, nafasi yake mnaweza mkaweka hawa ajira mpya, mkaajiri, ikazibwa naye akabaki na mshahara wake. Mnapopunguza mshahara *pension* yake mmeipunguza, na kama Mungu ameamua kumchukua mirathi yake mmeipunguza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini nishauri kwenye ajira mpya, mnatangaza, wasomi wetu wanaomba wengi, labla nafasi 1000 wameomba 20,000 lakini kwenye usahili ule walioshinda labda ni 1,800 au 2,000. niwambe fungua *database*, hao 1,000 wape kazi. Sasa, ikitokea mnataka watumishi wengine wa kada ile ile nenda kwenye *database* peleka hao. Hii itatusaidia kuajiri kwa kufuatana na umalizaji wa vyuo; lakini hii ya kutangaza kila wakati, unakuta aliyemaliza elimu mwaka 2020 anapata ajira wa mwaka 2017 hajapata ajira, nalo naomba mliangalie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ukiyatekeleza hayo utakuwa umetutendea haki watumishi wa Tanzania na tunakuamini haya utafanya. Una kijana hapa anakusaidia, lakini pia wamekupa timu ya watendaji ambayo ninaiamini. Umeletewa Naibu Katibu Mkuu ambaye nimefanya naye kazi, alikuwa *boss* wangu. Naye haya nilipokuwa nikimwambia

alisema sina maamuzi, sasa amepewa maamuzi yupo menejimenti ya utumishi wa umma. Ninawaamini mkiyafanya haya mtakuwa mmemsaidia Mheshimiwa Rais, haya yote anayotaka kufanya kwa watumishi yafanyike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kuna jambo moja ambalo aliwaahidi watumishi, haya aliyaahidi Meimosi na ameyatekeleza lakini aliwaambia nanukuu; "Wanangu la mshahara naomba mnisubiri mwaka ujao wa fedha".

Mheshimiwa Spika, Ninaamini Mama kauli zake anaziishi kwa hiyo Watumishi wanasubiri Meimosi kuna jambo ambalo litatajwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja, ahsanteni sana. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na michango yetu; lakini niwakumbushe tu kuwa Mbunge unaruhusiwa kunukuu lakini ni vizuri unukuu kwa usahihi ili kumbukumbu zetu rasmi na rejea tena za Bunge zikae sawa sawa. Ni vizuri kunukuu kwa usahihi, mtu yeyote yule unayemnukuu, na hasa unapomnukuu Mheshimiwa Rais. Kama wewe ndivyo ulivyomuelewa wewe sema ulivyomuelewa ili watu wajue wewe umeamua kusema hivyo kwa kuelewa kwako. Lakini kama unamnukuu nukuu maneno halisi aliyoyasema kwasababu isije ikaonekana baadaye tukaanza kufuatilia huko Rais alisemaje kumbe hayo maneno uliyoyasema wewe hayapo, tutapata wakati mgumu kidogo. Kwa hiyo, unaposema unanukuu nukuu maneno halisi aliyoyasema yule unayemnukuu.

Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Prof. Kitila Alexander Mkumbo atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, Mheshimiwa Jerry William Silaa, ajiandae.

MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii; na mimi nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri na hasa matumizi ya tafiti kwenye hotuba yake, amerejea tafiti mbalimbali;

kwakweli ni hotuba ambayo imenifurahisha sana. La pili; mipango yote ambayo Mheshimiwa Waziri ameeleza ili iweze kutekelezwa kikamilifu itahitaji fedha; na moja ya chanzo cha fedha kikubwa katika nchi hii ni utalii. Ni kwasababu hiyo na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge wengine kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa ubunifu wake wa kuja na *The Royal Tour* ambayo baadhi ya wataalam wa utalii wametuambia kwamba ina nafasi ya kuongeza *volume* utalii katika nchi hii mara mbili au mara tatu. Hiyo itatuongezea uwezo wetu wa kuweza kujitegemea lakini hasa ku-*finance* mambo haya mengi ambayo Mheshimiwa Waziri wa Nchi ameeleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie maeneo mawili. Kwanza ni suala la hali ya utumishi wa umma nchini. Na niungane na nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge aliyemaliza kuongea kwa hotuba yake na mchango wake mzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, utumishi wa umma ndiyo injini ya utekelezaji wa sera na sheria ambazo tunazitunga humu Bungeni, ndiyo injini ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa, kwa hivyo lazima tuwaheshimu na kuwapa *recognition* ya kutosha watumishi wa umma. Na kuna kipindi kwakweli tunajisahau, tunajimwagia sifa sisi wenyewe wanasiasa tunasahau kwamba nyuma ya sisi kuna watumishi wa umma ambao wanafanya kazi kubwa ya wakati mwingine katika mazingira magumu. Mimi nichukue nafasi hii kuwapongeza sana watumishi wa umma wa nchi hii kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuendesha nchi yetu na Serikali yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, utumishi wa umma kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri una changamoto nyingi; lakini nataka niongelee changamoto moja kubwa ambayo tushirikiane namna ya kuitatua. Ni kuhusu suala la uhaba wa watumishi wa umma katika sekta mbalimbali. Wakati mwingine tukilizungumza tunaliweka katika kiwango pengine hakiakisi uhalisia. Hebu tuangalie, nitoe mifano katika sekta saba kama muda utaniruhusu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kwanza ni elimu. Kwa mujibu wa taarifa za Serikali ambazo nimezichambua kupitia bajeti hii, Walimu wa Sekondari na shule za Msingi mahitaji ya nchi hii ni 433,992, Walimu waliopo ni 258,291, upungufu ni Walimu 175,701 sawa na asilimia 40.

Mheshimiwa Spika, sekta ya afya. Tunahitaji 208,232, waliopo 98,987, upungufu 109,295 sawa na asilimia 52.5. Lakini ukitaka kuangalia tatizo kubwa zaidi nenda kwenye zahanati na vituo vya afya kwa sababu huko ndiko zaidi ya asilimia 70 ya wananchi wanatibiwa kwenye zahanati na vituo vya afya. Vituo vya afya na zahanati nchi hii vinahitaji watumishi 131,547, waliopo ni 48,579, upungufu 82,968 na asilimia 63.1 ni upungufu.

Mheshimiwa Spika, katika sekta ya maji afadhali kidogo ndiyo bora, watumishi 10,279 ndiyo mahitaji, Watumishi waliopo ni 9,207, upungufu ni 169 sawa na asilimia Moja tu ya upungufu. Kwa hiyo sekta ya maji tupo vizuri kwa kiasi cha kutosha. Kilimo (*productive Sector*). Tunazungumzia mahitaji ya Maafisa Ugani 20,000 waliopo ni 9,600, upungufu ni 13,400, sawa na asilimia 67 ya upungufu.

Mheshimiwa Spika, jumla kwa sekta hizi chache ambazo nimezitaja tunazungumzia tunahitaji Watumishi wa Umma 1,238,089, waliopo 679,955, upungufu ni 558,134 jumla ya upungufu ni asilimia 45 maana yake nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais ameeleza vizuri hapa kwamba Serikali mwaka huu itakwenda kuajiri na tumepata kibali cha *staff* 30,000 na tumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutoa kibali hicho. Lakini tunazungumzia 30,000 kati ya upungufu wa 679,955, maana yake tunakwenda kutatua tatizo kwa kiwango cha asilimia 4.4. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimefanya hesabu, *trend* ikiwa ni hii ili tuweze kutatua *gap* hii tutahitaji miaka 21, ili ku-*address* hii *gap* iliyopo *we need 21 years*. Ni wazi kwa saizi ya uchumi wetu ni wazi kabisa haitawezekana ku-*address* tatizo hilo kwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kutoa tu vibali. Ukisoma taarifa za Wizara mbalimbali wanaeleza changamoto ya ajira *solution* yake nini? Tumeomba kibali utumishi, yaani ndiyo *solution* inaishia hapo. (Makoni)

Mheshimiwa Spika, sasa nataka kutoa mapendekezo nikiamini kwamba kwa kweli hata iwe ni Serikali ya Marekani kwamba inaweza ikaajiri watumishi hawa tukaziba hii *gap* haitawezekana. *We need to think of alternative ways* na Mheshimiwa Waziri utusaidie, mje na mikakati mipya namna ya kutatua tatizo hili. Naomba nitoe mapendekezo manne.

Mheshimiwa Spika, moja, kwanza ifanyike *National Audit* ya Watumishi wa Umma. Nilipokuwa Katibu Mkuu Wizara ya Maji tuliambia kufanya *National Audit* ya Watumishi wa Umma tukaenda tukagundua kwamba kuna kazi zinafanywa na wafanyakazi wawili kwa kazi moja, ndiyo ikatusaidia ile ndiyo unaona upungufu katika Wizara ya Maji ni asilimia moja kwa sababu ya *National Audit* ambayo tulifanya. Serikali ifanye *National Audit* tupate mahitaji halisi ya Watumishi wa Umma. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pili, tutekeleze sera ya *D by D* kwa uhakika. Kwa mfano, kwa nini Serikari iajiri Maafisa Ugani? Kwa nini mapato ya mazao ya kilimo katika kijiji yabaki hapo wakaajiri wao, kwa nini tusitumie mtindo huo? Hiyo inaweza ikaangaliwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nadhani la mwisho tuweke mazingira mazuri kwenye sekta binafsi ili kwamba kwa mfano katika shule, asilimia Tatu peke yake ya shule ndiyo za sekta binafsi kwa shule za msingi zilizobaki ni za Serikali. Tukiweka mazingira mazuri watu binafsi wafungue shule nyingi zaidi za msingi wataajiri Walimu, hivyo hivyo katika sekta ya kilimo na zingine. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mwisho ni Sekta ya Madaktari. Madaktari wengi katika hospitali za binafsi wanatoka sekta ya umma, ni muhimu tuweke mazingira mazuri ili sekta ya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

umma ya afya iweze kuajiri watumishi wake badala ya kutumia watumishi wa umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie mchango wangu na eneo moja muhimu la haraka. Suala la bodaboda, machinga lipo katika ukurasa wa 42 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, tuelewe vizuri *structure* ya uchumi wetu ikoje, niwapeni mfano katika Jimbo la Ubungo sisi tunazo Kata Nane, Jimbo la Ubungo tuna bodaboda 4,891. Kimara 728, Mabibo 683, Makuburi 847, Makurumila 839, 655, 656, 645 na Ubungo 838. Kata ya Ubungo yenye bodaboda 838, bodaboda wanne wana *Masters*, bodaboda 21 ni *Graduate*, Digrii ya Kwanza, hiyo ipo katika Dar es Salaam huko wengi ni *Form Four*, *Form Six*, *Graduate*, kwa hivyo hii ni sekta muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wakuu wa Mikoa waelezwe na Mheshimiwa Waziri mtupe mtamko hapa, hii tabia ya kutoa matamko yakusumbua sekta binafsi yaishe. Tungetaka tamko hapa la Waziri atueleze kwamba anapiga marufuku bodaboda kupigwa marufuku kuingia Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi ina vipaumbe Sita, kipaumbele cha Sita kinazungumzia kuajiri wafanyakazi Milioni Nane kutoka sekta iliyorasmi na isiyorasmi tutapataje Milioni Nane tukianza kuwasumbua watu hawa? Hawa ndiyo ajira zetu hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuliahidi Dar es Salaam kwamba, tulitoa ahadi kwa bodaboda hamtapigwa marufuku tena kwenda katikati ya Jiji, sasa tupate tamko la Serikali kwamba hili tamko la jana ni la mwisho kusumbua bodaboda katika nchi hii, hawa ndiyo wenye uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa Kanuni zetu kwa sababu hiyo hoja ya watu wa bodaboda, hoja ya watu wa mchomoko sijui Kigoma na maeneo mengine wamekabidhiwa Serikali wao watalifanyia

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kazi. Kwa hivyo, kwa mujibu huo huo wa Kanuni zetu tuipe muda Serikali itakapotoa hiyo taarifa yake ndiyo mjadala utanzia hapo, kuhusu hoja hizi mbili za hawa bodaboda lakini pia wale wenye magari madogo kule Kigoma wanaitwa mchomoko.

Mheshimiwa Ester Amos Bulaya atafuatiwa na Mheshimiwa Jerry William Silaa, Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa ajiandae.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, nami niungane alipoishia Kaka yangu Profesa Kitila Mkumbo, ni kweli kuna uhitaji mkubwa wa watumishi katika Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mfano tu kwenye Halmashauri ya Mji wa Bunda, tuna upungufu wa watumishi zaidi ya 900, Halmashauri moja tu ya Mji wa Bunda. Sasa ukija Watendaji wa Mitaa wapo 38 mahitaji ni 80, upungufu 50. Ukija Walimu wa Msingi, mahitaji ni Watumishi 1,252, Watumishi waliopo ni 738, pungufu ni 514. Ukija Maafisa Ugani Kilimo mahitaji ni Watumishi 48, Watumishi waliopo ni 34, pungufu 14. Watumishi wa Afya mahitaji ni Watumishi 402, Watumishi waliopo ni 184, pungufu ni 218.

Mheshimiwa Spika, katika upande wa watalaam wa ujenzi mahitaji ya watumishi ni Tisa, waliopo ni watumishi watatu kwa Halmashauri moja tu ya Mji. Ukija Watendaji, Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Kata mahitaji ni 14 tunae Mmoja tu, Halmashauri ya Mji hiyo. Ukija Walimu wa Sayansi Na Hisabati; mahitaji 162 waliopo ni Walimu 88 na pungufu ni Walimu 74. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge hiyo ni Halmashauri moja Halmashauri ya Mji wa Bunda. Halmashauri imepata hati safi kwa uchache wa hao watumishi *imagine* mkitupa watumishi wa kutosha Mheshimiwa Jenista Dada Mkubwa mtupe wote 900 Mji wetu wa Bunda utakuwa kwenye hali gani? Tunahitaji watumishi wa kutosha. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, nimesoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri, nimesoma ukurasa kuanzia 55 nimeusoma vizuri, 52 mpaka 55, ukurasa wa 105 mpaka ukurasa wa 108 nina maslahi hapa. Mheshimiwa Waziri amezungumzia kulipa Shilingi Bilioni 91 ya malimbikizo ya madeni ya Watumishi wa mishahara 65,000 malimbikizo ya madeni ya mishahara kwa watumishi 65,000 Shilingi Bilioni 91.

Mheshimiwa Spika, ukisoma ripoti ya CAG yaani hii mpya *latest* Machi, 2022, watumishi wanawadai Shilingi Bilioni 430 ya malimbikizo ya muda mrefu, siyo mishahara peke yake kuna malimbikizo ya mishahara ya watumishi wapya, kuna malimbikizo ya watu waliopandishwa madaraja na posho za watumishi, lakini hapa mmelipa Shilingi Bilioni 91 peke yake, bado mnadaiwa Shilingi Bilioni 399 mnazilipa lini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimeona hapa mmetenga Bilioni 103, kutenga ni jambo lingine kulipa jambo lingine na hata hili mkifanikisha kulipa bado mtakuwa mnadaiwa Shilingi Bilioni 236. Je, mtazilipa lini? Siyo sawa Serikali kuendelea kudaiwa malimbikizo ya Watumishi ambayo ni haki yao ya msingi.

Mheshimiwa Spika, kwa mtindo huu ukiangalia unakuta mtumishi anaanza kuidai Serikali alipoajiriwa tu ana malimbikizo ya mishahara, haya akipandishwa madaraja bado lile daraja alilopandishwa haliendani na mishahara anaotakiwa kulipwa, bado ana malimbikizo. Haya, imefika tena kustaafu bado anaweza akaa miaka 20 hajalipwa kisa utaratibu wa mafao haujafanyiwa kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dada yangu Mheshimiwa Waziri naomba unisikilize hilo nimesema la madeni, bado wastaafu wetu wanacheleweshwa kulipwa mafao yao. Ukiuliza sababu ni kwamba majalada yao maandalizi ya mafao hayajafanyiwa kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe mfano mpaka tunavyoongea kwenye taarifa mpya ya CAG majalada 571 hayajafanyiwa kazi, kuanzia mwaka wa kwanza mpaka wa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

28. Mstaafu amestaafu waliokaa miaka mitatu ambao hawajalipwa ni 391. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kaanza kwenye *stress* za kucheleweshewa mishahara, kulundikiwa malimbizo anakutana nayo tena huku kwenye kulipwa kiinua mgongo chake, siyo sawa kwa watumishi wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, waliokaa miaka mitano hawajalipwa mafao yao baada ya kustaafu wako 59. Waliokaa Miaka Kumi ni Wastaafu 54. Miaka 20 wapo Wastaafu 17. Waliokaa miaka 15 ni Wastaafu 25. Waliokaa miaka 25 ni Wastaafu 18, Waliokaa miaka 28 ni Wastaafu Saba, jumla ni Wastaafu 571 ya wastaafu wa Taifa hili waliotumikia Taifa lao kwa jasho na damu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa huku hatuwapandishii mishahara, tukiwapandisha madaraja malimbikizo lukuki, tukiwaajiri malimbikizo lukuki, Serikali mnaanza kudaiwa na wafanyakazi wanapoajiriwa, wanapopandishwa madaraja na wanapostaafu hamuwalipi kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri naomba sana tuwatende haki wafanyakazi na watumishi wa Taifa hili ambao wanatumikia Taifa hili kwa jasho na damu na hawalalamiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa kuna kipindi wamekaa miaka Mitano hawajapandishwa mishahara wapo tu wanalijenga Taifa lao. Sasa Mheshimiwa Waziri hapa nimelizungumzia bado taasisi zako kuna taasisi 15 na Mheshimiwa Spika nakupongeza, taasisi yako inapeleka michango wengine hampeleki. Nitolee mfano shirika la reli hajjapeleka michango ya watumishi Shilingi Bilioni 99. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maji ndiyo wamekuwa sugu maana hata *penalty* hawalipi wanadaiwa *penalty* huko Shilingi Milioni 441 hawajapeleka. TRA wakusanya mapato pelekeni michango ya wafanyakazi. Bodi ya Mikopo, Mfuko wa Bima, nitaje na wengine?

WABUNGE FULANI: Taja! (*Makofi*)

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, pelekeni michango ya watumishi kwa mujibu wa Sheria ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, Serikali ndiyo wasimamizi lakini taasisi zenu zinaongoza kutopeleka michango na hii ina athari kwenye kiinua mgongo cha watumishi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kingine ninyi ndiyo mnachangia hii mifuko kufa, tuliwaomba hapa *actuarial valuation* hamjaleta, sasa CAG ameamua kufanya kwa mlango wa nyuma. Kwenye ripoti ya mwaka huu kwa mujibu wa Sheria ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2018 inasema mifuko walau iwe na ukwasi wa asilimia 40.

Mheshimiwa Spika, *PSSSF*, mfuko ambao ndiyo unaosaidia Watumishi wa Umma una ukwasi wa asilimia 22. Mlivyolipa kale kahela Shilingi Trilioni Mbili kwa hati fungani, kidogo ndiyo kamesaidia imefika asilimia 30 lakini bado ni chini ya sheria inavyotaka. Sasa nauliza na CAG amependekeza Shilingi Trilioni 2.45 iliyobaki mnaipila lini ili kuokoa huu Mfuko?

Mheshimiwa Spika, hii ni 399 bado ya madeni mengine. Sasa mkiangalia mzizi wote ninyi ndiyo mnatengeneza tatizo, ninyi ndiyo mnatupa ahadi hapa na bado hamtekelezi kwa wakati na bado wafanyakazi mfuko wao una hali mbaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivi mnawezaje kupata *guts* za kuwahamasisha sekta binafsi wapeleki michango wakati ninyi wenyewe hampeleki michango? Ninyi wenyewe hamlipi madeni. Sasa huu ni mfuko wa wafanyakazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu *NSSF* mna madeni sugu ya Shilingi Trilioni 1.5 Serikali hamjapeleka, Mheshimiwa Waziri naomba tuilinde hii mifuko tutimize wajibu wetu, tusaidie wafanyakazi wetu, *please!*

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*).

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Jerry William Silaa atafututiwa na Mheshimiwa na Mheshimiwa Mhandisi Ezra John Chiwelesa, Mheshimiwa Dkt. Alice Karungi Kaijage ajiandae.

MHE. JERRY W. SILAA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti hii ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako hili linafanya kazi kwa mujibu wa Ibara ya (63) (2), (3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inaipa mamlaka na madaraka kwa niaba ya wananchi kuisimamia na kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Spika, nimesikiliza kwa makini sana hotuba ya bajeti iliyosomwa hapa Bungeni leo na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, nimegundua yapo mambo makubwa ambayo Serikali Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ameyafanya kwenye utumishi wa umma. Mambo haya yamefanyika katika kipindi hiki cha mwaka mmoja ambapo Serikali Awamu ya Sita imekuwa madarakani.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana naamini si watumishi wa umma pekee lakini Watanzania wote walipata mshtuko kwa msiba wa kuondokewa na Rais wetu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli.

Mheshimiwa Spika, kazi iliyofanywa na Serikali ya Mheshimiwa Samia kwa mwaka mmoja, naamini imeleta matumaini makubwa kwenye sekta ya Utumishi wa Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yako maandiko kwenye *Quran* Tukufu iko sura alishushiwa Mtume Muhammad *(S.A.W)* Mwenyezi Mungu akitaka kumtia moyo na sura hii nitaisema

hapa. Sura inasema *walaak ahkirut kairulaka minaluula*. Bila shaka wakati ujao utakuwa ni bora zaidi kuliko wakati uliotangulia. Serikali ya Awamu ya Sita imefanya kazi kubwa. *(Makofi/Vicheko)*

MHE. MOHAMED SAID ISSA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Jerry Silaa ukae kuna Wabunge wawili wamesimama hapa. Mheshimiwa Mohamed.

MHE. MOHAMED SAID ISSA: Mheshimiwa Spika, naomba kumpa taarifa mzungumzaji kwamba hii aya ambayo ameinukuu, ameinukuu vibaya. Sasa kwa mujibu wa *Quran* Tukufu na kwa mujibu wa dini yetu ya Kiislam ukibadilisha herufi moja, umebadilisha maana. Kwa hiyo naomba kumpa taarifa kwamba aya hii inatamkwa *walal-akhiratu khairulaka minal uula*. *(Makofi)*

SPIKA: Haya sasa, Mheshimiwa Jerry Silaa hiyo ilikuwa ni taarifa ambayo nafikiri sasa hili jambo ili likae vizuri chukua yeye alivyoinukuu halafu iseme kwa tafsiri. *(Vicheko/Makofi)*

MHE. JERRY W. SILAA: Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana mtoa taarifa, Kiiarabu changu kidogo kimechanganyika. Kwa hiyo niombe kumbukumbu sahihi za Bunge zichukue kiarabu cha mtoa taarifa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema wakati huu umekuwa bora kuliko wakati uliotangulia? Ni kwa mambo makubwa ambayo yamefanyika kwenye utumishi wa umma. Kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri tumeona watumishi 190,781 wamepandishwa madaraja na Mheshimiwa Waziri ametueleza hapa kwamba watumishi wengine 92,619 watapandishwa madaraja kabla ya mwezi Juni mwaka huu 2022, ni kazi kubwa sana, tunaipongeza sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri vile vile kwenye Hotuba yake ameeleza kwamba wako watumishi 13,495 wamepata ajira mpya, maana yake nini? Wako Watanzania 13,495 waliokuwa tegemezi na leo nao wamekuwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wanategemewa kwa kupata mishahara kupitia utumishi wa umma. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, wako watumishi 21,127 wamefanyiwa *recategorization* kwenye kada zao za utumishi. Sasa maana sahihi ya *recategorization* nadhani Mheshimiwa Dullo utamtafsiria Babu Talle ili aelewe kazi kubwa iliyofanywa na Serikali hii ya Awamu ya Sita. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, yako mambo Serikali imefanya, siyo kwenye Wizara hii lakini yana *impact* kwenye Wizara ya Utumishi wa Umma. Serikali ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan imetoa *non cash bond* ya trilioni mbili kwa Mfuko wa Pensheni wa *PSSSF* ambayo imefanya Mfuko huu kuweza kulipa pensheni kwa wakati. Jana nimezungumza na Mkurugenzi Mashimba, leo tunavyozungumza hapa wastaafu wa mwezi wa tatu tayari wanalipwa pensheni zao, ni kazi kubwa sana imefanyika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alitoa agizo la kuongeza wanufaikaji wa Mfuko wa Bima ya Afya, wale wategemezi toka umri wa miaka 18 mpaka umri wa miaka 21. Hivi tunavyozungumza wako watu 77,345 ambao walikuwa wamevuka miaka 18 na ilimpasa mtumishi kama ni mtoto wake atoe pesa mfukoni kumuhudumia matibabu, leo wanahudumiwa na Mfuko wa Bima ya Afya na yenyewe ni jambo kubwa kwenye utumishi wa umma. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, yako mambo mengi kwa sababu ya muda niseme tu, Mheshimiwa Rais kwa kuthibitisha mapenzi yake na watumishi wa umma wa nchi hii amemteua mtu bingwa kabisa, mwanamke aliyehudumu ndani ya Bunge hili kwa muda mrefu kuliko akinamama wengin,e amekuwa Mbunge wa Viti Maalum lakini amekuwa Mbunge mbobezi wa Jimbo la Peramiho. Amepita Wizara ya Elimu anajua matatizo ya watumishi Walimu. Amekuwa *Chief Whip* hapa Bungeni na tumeona wote kazi yake. Amekuwa mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha Mapinduzi, siyo mwingine ni binti wa Katekista wa Peramiho, Mheshimiwa Jenista Joakim Magigi Mhagama ambaye watu wa namna

hii ndiyo wale King Kiba (Ally Kiba) aliwaimba kwenye kibao chake cha utu. Pamoja na upole na uzuri wake lakini amejaliwa utu na utulivu wa hali ya juu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imetangaza ajira mpya 32,604. Nimwombe Mheshimiwa Waziri, niombe Serikali ajira hizi ziende kuajiriwa kwa haki. Ningetamani sana ajira hizi 32,604 kama vile zigawanywe kama zile pesa za *TARURA* kila Jimbo lingepata. Nafahamu ziko sheria za Utumishi wa Umma, nia yetu ni kuona kwamba ajira hizi zikitoka maana nadhani kila Mheshimiwa Mbunge hapa ana meseji ya ajira hizi za 32,000. Ni ombi langu, ama ni ushauri wangu kwa Serikali ajira hizi zikitoka tuzione zimetapakaa nchi nzima kwa usawa. Tuone kwenye Majimbo yetu kama kweli ajira 32,604 basi kila Jimbo takribani watu 100 wawe wamepata ajira. Ikifanyika hivyo italetwa usawa kwa Taifa, italetwa uhimilivu kwa Taifa na itaondoa ile kero ya *unemployment* kwetu sisi sote kwa umoja wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, nilipita Tabora tarehe 12 Aprili nilikutana na mzee Ramadhani Ally Mkwande, yeye ni mstaafu wa *TTCL*. *TTCL* ilikuwa na mkataba na *NSSF* kulipa pensheni za watumishi wake na wao ni moja kati ya wale watumishi ambao bado wanalipwa shilingi 50,000 kwa mwezi, aliniomba nije kusema Bungeni na nimeona nimtendee haki. Tunaiomba Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ijaribu ku-*standardize* watumishi wote wafike kile kiwango cha shilingi 100,000 wanachopata *pensioners* wengine ili na wenyewe waweze kuendesha maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda la mwisho la kusema, niliongea kidogo pale kwenye Mfuko wa *PSSSF* kwenye ile *bond* ya *two trillion* aliyoitwa Mheshimiwa Rais kupitia Serikali yake. Niseme tu Kamati ambayo Bunge lako limekasimia kazi ya uwekezaji inasimamia Mifuko hii, kazi kubwa imefanyika lazima tuseme. Kazi kubwa imefanywa na Serikali kuweza kutengeneza *liquidity* kwenye Mifuko hii na kazi kubwa inaendelea kufanyika. Nikuombe na niliombe Bunge lako Tukufu, tuendeleo kuwatia moyo, tuendeleo kuikumbusha

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Serikali kwa adabu, lakini mwisho wa siku naamini *pensioners* wa nchi hii wataendelea kupata pensheni zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mhandisi Ezra John Chiwelesa atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage na Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate ajandae.

MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA: Mheshimiwa Spika, nai pia nikushukuru kwa nafasi hii. Nichukue nafasi hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo ameifanya ya kututangazia ajira hizi ambazo zinajaribu kutupunguzia *gape* la watu walioko mtaani na hatimaye kutusaidia kwenye ujenzi wa uchumi na halikadhalika kuwapa fursa Watanzania ya kushiriki ujenzi wa Taifa lao.

Mheshimiwa Spika, nadhani nimemsikiliza sana Mheshimiwa Waziri kwenye Hotuba, lakini vile vile taarifa yake aliyotoa kwa vyombo vya habari wiki hii iliyopita. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na msaidizi wake kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya. Vile vile niipongeze Serikali kwa ajira hizi mpya kwa sababu tumeona kwamba ajira hizi takribani 32,604 kwa mujibu wa taarifa zinaenda kuigharimu Serikali takribani milioni 26.297 na kwa mwaka ni bilioni 315. Hii ni hela nyingi sana ambayo sasa Serikali inaitoa irudi kwa wananchi na hatimaye isaidie mzunguko huko mtaani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunachokiona ni kwamba itatusaidia kupunguza ukali wa maisha na hatimaye vijana wetu ambao wamekuwa *stranded* kwa muda mrefu wataweza kupata ahueni halikadhalika waweze kwenda mbele zaidi.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri hasa kwa tamko ambalo amelitoa kuhusu mpango mzuri wa kufanya usaili katika Mwaka huu wa Fedha ambao unakuja hasa suala lile la kuweza kufanya usaili kutokea kwenye maeneo yale yale ambayo wananchi wapo kule. Nayasema haya Mheshimiwa Waziri kwa sababu vijana wetu

wamekuwa wanapata shida sana sana kupita kiasi, maana ilikuwa inafikia hatua mtu unajiuliza ni mwakilishi wa wananchi na mbaya zaidi hata hizi *interview* zimekuwa zinafanyika mara nyingi kipindi Wabunge tuko majumbani hatuko hapa. Walau hata tungekuwa hapa tungeweza kui-*feel* ile *pinch* ya kwamba vijana wako hapa. Unaita vijana 3,000 kuja kuwafanyisha *interview* hapa Dodoma ya kutafuta watu 400 au watu 600. Vijana ambao wamekaa miaka mitano bila ajira, vijana wamekaa miaka minne bila ajira, ila anapoitwa anaona matumaini yanakuja anaingia kwenye mikopo ya pesa, wengine wanauza mali walizonazo wanasafiri kuja Dodoma. Anafika hapa kati ya 4,000 uliowaita ni 300 tu ndiyo watakaochukuliwa au ni 400 ndiyo watakaochukuliwa. Wale vijana wengine 4,600 wanarudi wapi?

Mheshimiwa Spika, wamekuwa wanarudi na masononeko makubwa na mioyo yao inauma kwa sababu wanajiona kwamba hawana bahati, kusoma kwao ni kwa bure. Kwa hiyo ile hali pamoja na kwamba tunao ukali wa maisha ambao tulikuwa tunaendelea nao, ila ile hali ilikuwa inaleta manung'uniko huko mitaani na kuzidi kuleta chuki hata kuzidi kuichukua Serikali. Kwa hiyo mfumo huu ambao tunasema tunauleta leo, vijana wafanyiwe usahili huko kwao itatusaidia kutupunguzia vurugu nyingine ambazo zilikuwa zinatuletea kero kwa vijana wetu. Kwa sababu kama usahili utafanyika na mtu yuko Biharamulo, akafanyiwa usahili pale pale kwake alipo, haingii gharama kubwa sana kwa sababu bado ataendelea na shughuli zake ambazo anahangaika nazo na majibu yakija amekosa atakuwa na matumaini ya kujaribu tena *next time*.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa najiuliza, kama tunaweza kupeleka mitihani ya darasa la saba, tukapeleka mitihani ya kidato cha nne, tukapeleka mitihani ya kidato cha sita, wakaisimamia kule hatimaye ikarudishwa huku ikasahihishwa. Unamsafirisha mtu hapa ambaye hana ajira muda mrefu, aje tu hapa kufanya *written examination* haikuwa sawa kabisa. Kwa hiyo tumpungeze Waziri kwa hatua hiyo nzuri ambayo sasa inaenda kutengeneza *platform* nzuri kwa vijana wetu ili sasa waweze kutoka kwenye

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

maumivu yale ambayo walikuwa nayo, hatimaye waweze kusogea mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na haya yote yanayotokea, tungeomba sasa watu wa Sekretarieti ya Ajira wajitahidi zaidi, pamoja na kwamba watakuwa wanafanya huu mchujo hebu haki itendeke. Haki itendeke kwa sababu nyle nyote ni Wabunge humu ndani. Tuko Wabunge zaidi ya 390, kila Mbunge anawapiga kura hapa. Hata kama hamsemi lakini lazima meseji za vijana wetu tunazo na vijana wanalalamika. Wengine wanakwambia Mheshimiwa jaribu kutusaidia, ukimwambia kuna mfumo sasa guvu hivi, anakwambia hamna mbona wenzetu wamepitia sehemu Fulani na wamepata. Kwa hiyo kama kuna Wabunge *special* humu wanao uwezo wa kupita huko tujulishane ili na sisi tuje, lakini kama kuna *platform* ya haki kwa Wabunge wote, tunaomba huu mchakato ufanyike kwa haki ili vijana wajue kwamba tuko kwa ajili ya kuwawakilisha lakini hatuingilii mchakato wa usaili huko. Kwa hiyo tulikuwa tunaomba hilo jambo lijaribu kufanyika hivyo ili muweze kutusaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile tumieni ya *first in first out, FIFO* itumike Mheshimiwa Waziri. Kwa sababu kuna mtu mwingine kamaliza miaka mitano iliyopita unakuja unaajiri mtu aliyemaliza mwaka jana, kozi ile ile, kwa kigezo gani unamwacha yule kule aliyekuwa amemaliza kipindi cha nyuma? Wakati yule aliyekuwa amemaliza nyuma, hakupenda kutoku-*apply* ajira ni kwamba Serikali haikuwa imetoa ajira, kwa hiyo alikuwa hana pakwenda. Kwa hiyo fursa inapopatikana leo tumpe aliyekuwa ametangulia nafasi tuendeleo kujipanga kwa ajili ya wale ambao wanakuja leo. Kwa sababu umri wa kuajiriwa Serikalini nao unapita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu tumeona sasa hivi vigezo vingi sana, tumekuwa na vigezo vya miaka 18 mpaka 25 na hili jambo naomba tuliweke wazi hapa. Leo tuseme *conditions* nyingine ambazo zinawanyima fursa Watanzania tuziache. Katiba ya nchi hii inampa kila mtu haki ya kutokubaguliwa hasa anapotaka kushiriki shughuli za maendeleo za Taifa hili. Sasa unapokuja unatangaza nafasi

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ya kazi. Mimi nina *document* hapa, nina tangazo la kazi, hii ni *Public Service Recruitment Secretariat* tarehe 14 Aprili. Hizi wametangaza nafasi za Ngorongoro *Conservation* nyingi sana nafasi ziko hapa. Wametangaza madereva, wametangaza na wengine, huku chini sasa kwenye *condition; general conditions all applicants must be citizens of Tanzania with age between 18 and 25 years old for certificate and diploma, age 18 and 30 years for bachelor degree holders.*

Mheshimiwa Spika, hii sikatai wameweka *condition* hii, lakini nimerudi kwenye tangazo hapa, hii hapa Pasiansi Chuo cha Wanyamapori. Hiki Chuo ni cha Wizara ya Maliasili na Utalii, *age* waliyoweka hapa *applications* za mwaka jana ambao hawa wako shule leo wameweka mtu anayetakiwa aingie chuo miaka 18 mpaka 24. Sasa unajuliza mtu aliyeingia chuo na miaka 24 labda na miezi 11 au miaka 24 na miezi 10 anamaliza chuo akiwa tayari na miaka 25. Halafu *condition* ya ajira, wewe huyo huyo unayemiliki Wizara unampa *condition* ya ajira kwamba huyu mtu asizidi miaka 25. Unajuliza wewe mwenye chuo unayempa *condition* huyu umeongea na Wizara kwamba hili darasa lote mtaliajiri muda ule utakaokuwa umeisha? Huna hiyo *condition*, matokeo yake unaweka *condition* ambayo inazidi kuongeza maumivu kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kitu kibaya zaidi hii hapa wazazi wanalipa, ada milioni tatu, ada milioni nne, mzazi amejihimu kapeleka mtoto pale Chuo cha Wanyamapori. Mtoto anamaliza unamwambia kazidi umri. Chuo kina *conditions* zake, anayeajiri ana *conditions* zake. Hili jambo naomba tuliache. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni lazima tuwatendee haki Watanzania na tuwape fursa ya kuajiriwa. Kwa sababu hapa wangelikuwa wanafanya vizuri kama wanataka haya masharti ya miaka na nini, wawachukue *fresh from school*, wawasomeshe wenyewe kwenye kile chuo, wawapeleke tayari, hiyo hawatakuwa na kigezo kingine, lakini wasiache mzazi anapeleka mtoto wake pale, mtoto hujampa *condition*

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

hiyo, anamaliza chuo, yuko mtaani unaanza kumwambia miaka 25. Miaka 25 anaitoa wapi? Miaka minne hujajiri. (Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Ezra kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Esther Matiko.

T A A R I F A

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nataka nimpe Mheshimiwa *Engineer* Ezra anachokizungumza ni kweli, siyo tu kwenye maliasili, ajira zote ambazo Serikali inatangaza inaweka vigezo ambavyo vinaengu Watanzania wengi wasiweze kuajiriwa bila kuangalia uhalisia wa umri na lini anamaliza chuo. Siyo kwenye maliasili tu, ni sekta zote ambazo wanatangaza hata kwenye majeshi. (Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Mhandisi Ezra Chiwelesa, unaipokea taarifa hiyo?

MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA: Mheshimiwa Spika, naipokea.

Mheshimiwa Spika, labda sasa kwa kumalizia kwenye hili eneo ningeomba kama Bunge, sisi ndiyo tuna nafasi ya kuwasemea vijana hawa wa Kitanzania na wazazi hawa ambao wamepeleka watoto wao. Hii *condition* naomba tuiangalie upya, ifutike kama ni kusaili waite hata watu 10,000, watafute wawili lakini hawa wawili wanaowataka wawape fursa, kila mtu ajue kwamba nili-*apply* sikuzuiliwa kuliko hiki kinachofanyika leo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na hali nyingine pia tumeiona. *Recently*, kazi nyingi ambazo zimekuwa zinatangazwa Magezea, Polisi, Uhamiaji, *condition* mtu awe amepita JKT. Ni lini Taifa hili liliweka kigezo cha kupita JKT? Au ililetwa humu tukakubaliana kwamba sasa JKT kama JKT ndiyo *condition* turuhusu vijana wetu walioko mtaani waanze kwenda JKT na Serikali itupe nafasi ya kwamba vijana wote

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

walioko mtaani, wataweza kuwabeba kweli? Tukiruhusu vijana wote waliomaliza *form four* waje wajiunge na JKT tutaweza kuwabeba? Hatutaweza. Kwa hiyo hizi *conditions* nyingine tujaribu kuzitoa ili tutengeneze fursa sawa kwa vijana ambao wako huko kila mmoja aone na aweze kuitumia nafasi yake kushiriki kwenye kuleta maendeleo ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Alice Karungi Kaijage, atafuatiwa na Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate na Mheshimiwa Emmanuel Lekisho Shangai ajiandae.

MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kunipa nafasi ya kuchangia katika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Namshukuru Mwenyezi Mungu pia kunipa nafasi ya kusimama. Naendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa usimamizi mzuri wa Serikali yake yote mpaka tunaona jinsi ambavyo Wizara hii inafanya kazi kwa ufanisi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Jenista Mhagama pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Deo kwa kazi nzuri sana wakishirikiana na watendaji wote wa Wizara husika katika kufanikisha malengo ya kuboresha utumishi huu wa umma.

Mheshimiwa Spika, jukumu kubwa ambalo ofisi hii inalo ni kuhakikisha kwamba Utumishi wa Umma unaendelea kuzingatia suala zima la misingi ya utawala bora. Misingi ya utawala bora ni kufanya kazi kuzingatia sheria, sera na taratibu mbalimbali walizojiwekea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sitatofautiana na wenzangu wengi walionitangulia; Serikali Awamu ya Sita katika mwaka huu tunaomaliza imeonyesha dhamira ya dhati kabisa ya kuboresha maslahi ya Watanzania ambao ni Watumishi wa

Umma. Naepuka kurudia vyote walivyosema wenzangu kwa habari ya mishahara, upandishaji madaraja kufuta kodi ya Bodi ya Elimu ya Juu kwenye mishahara yetu, kupunguza kodi ya mshahara mpaka 8%, na mambo kadha wa kadha. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, suala zima la upandishaji wa madaraja, wamevunja rekodi kwa maana ya mambo yote ambayo ameahidi Mheshimiwa Rais kwenye mwaka ullopita kupitia bajeti yake, kwa asilimia kubwa sana yametokelezeka. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo yote mazuri yaliyotekelezeka, tunaendelea kutambua hali tete ya uchumi duniani unavyokwenda pamoja na adha mbalimbali za kivita. Pia tunatambua anguko la kiuchumi katika sehemu mbalimbali duniani, lakini pamoja na yote hayo, watumishi wa nchi yetu bado wanaendelea kuomba suala zima la upandishwaji wa mshahara kulingana na pato letu, basi liendeleo kuzingatiwa pale itakapowezekana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mishahara hii tunashauri itakapopandishwa pale itakapowezekana, basi iwe kama zamani, izingatie suala zima la *living wage*, yaani mtu mshahara wake umsaidie kupanga mwezi mzima kula tarehe moja mpaka tarehe 30. Kwa nini? Sasa hivi mtumishi wa kawaida anapata mshahara mpaka tarehe 10, 15 umekwisha. Hii inapelekea kumpa msongo wa mawazo na inasababisha magonjwa mbalimbali hasa yasiyoambukiza ambayo pia ni mtihani mkubwa kuyagharomia. Hata hivyo naipongeza Serikali kwa kujiandaa kuja na Mfuko wa Bima ya Afya kwa Wote. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, katika utawala bora ni kusimamia suala zima la sheria, sera na taratibu walizojiwekea waajiri na watumishi. Hii pia inajielekeza katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwamba Serikali na Chama cha Mapinduzi inatambua umuhimu wa vyama vya wafanyakazi ili kuleta mahojiano kati ya waajiri pamoja na waajiriwa kuboresha utumishi mahala pa kazi. (Makofi)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, tunashauri Wizara hii iendelee kusimamia kwa ukaribu utawala bora katika sehemu mbalimbali kati ya waajiri ili wafanyakazi wawe na uhuru wa kujiunga na vyama vyao bila vizuizi. Pia maslahi yao mbalimbali yaweze kuzingatwa na kusimamiwa kupitia vyama vyao, kwani mtu mmoja mmoja sio rahisi kuhudumiwa. Kwa hiyo, naomba Wizara izingatie kwamba mahali pa kazi pote, watumishi wawe na uhuru wa kujiunga na vyama vya wafanyakazi na Mabaraza yawe huru ili wafanyakazi waweze kufumuka na kueleza changamoto zao.

Mheshimiwa Spika, hakuna sheria inamruhusu mfanyakazi mmoja atoke na kuleta changamoto yake. Hii inapelekea migomo ambayo siyo halali. Kwa sababu vyama vya wafanyakazi ndiyo pekee vinaruhusiwa kuendesha mgomo. Sasa kama wafanyakazi hawapati nafasi ya kueleza mambo yao kwenye Vyama vya Wafanyakazi wataeleza wapi? Vyama vya Wafanyakazi vikipata tatizo vinapeleka kwenye Tume ya Usuluhishi na ikishindikana, kwenye Mahakama Kuu, kwenye Kitengo cha Kazi. Mahakama Kuu Kitengo cha Kazi inaweza kusema sasa nendeni kwenye mgomo.

Mheshimiwa Spika, natoa mfano wa madereva Tanzania. Madereva wana changamoto zao mbalimbali. Hivi ninavyozungumza na wewe kuna hatari ya mgomo, lakini ni kwa sababu waajiri wengi wamekuwa hawawapi uhuru wafanyakazi kujadili mambo yao kwa utaratibu. Hii inapelekea watu wachache kuanzisha migomo kinyume na utaratibu. Kwa hiyo, ofisi hii naishauri kupitia suala zima la utawala bora, basi isimamie masuala mazima ya wafanyakazi katika vyama vyao mahali pa kazi ili kuepusha misugvano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali, awamu iliyopita imetoa ajira za kutosha na sasa ziko ajira karibia 30,000. Kwa upande wa Idara ya Afya, mgawanyo wa ajira umekwisha. Mimi ninayo *document*, ajira zimeshagawiwa zote katika Wizara ya Afya, ila nina jambo moja nilisemee

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ambalo huwa nina *interest* nalo na nitakuwa sijawatendea haki nisiposema huku ndani.

Mheshimiwa Spika, nimezungumzia sana suala la Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili ya Mileembe. Nimesemea sana hili suala mbali ya upungufu wa watumishi, vifaa na kadhalika. Tunaishukuru Serikali sasa imepanua hospitali katika suala zima la magonjwa mahututi pamoja na *Emergence Department*. Pamoja na upanuzi huo, lakini katika mgawanyo huu ile Hospitali ya Mileembe haijapewa mtumishi hata mmoja. Ninashauri katika mgawanyo wa watumishi wa afya, hebu warudie tena, kwa sababu wako wanaojitolea katika hospitali hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii huduma ni nyeti, watu wengi wakienda kwenye ajira, ikifika wakati wa kusoma, wanaondoka, wanasoma kozi nyingine. Hawa-*specialize* kwenye suala zima la afya ya akili, lakini watu wanaojitolea wapo pale, sasa ajira zimetoka wameona pia Mileembe haijawa *located*. Kwa hiyo, nawashauri kama wenzangu kwamba suala zima la ajira tuliangalie kutokana na umuhimu wa sehemu husika.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia kabisa ni suala zima la ajira Wahadhiri wa Vyuo Vikuu. Nashauri kama inawezekana, Sekretarieti ya Ajira kama iwe kama zamani, iachie sasa vyuo viajiri *especially* watu ambao ni *academic staff*. Wanaweza wakaajiri *technical staff* lakini *academic staff* wawaachie kwa sababu TCU inashauri, angalau mtu mwenye GPA 3.5 aajiriwe, lakini Sekretarieti ya Ajira inasema 3.8. Kwa hiyo, unakuta Vyuo vya Umma vinakosa watu ambao wamewa-*train* wenyewe na wanawafahamu. Pamoja na kwamba wana GPA hiyo, lakini wanawafahamu kwamba uwezo wao ukoje. Angalau *academic staff* kama itawezekana Sekretarieti ya Ajira iwaachie basi vyuo waajiri wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia ikiwezekana, maprofesa wetu muda wao wa kustaafu uwe angalau miaka 60 ili wapewe mikataba baadaye ya kuendelea. Watu hawa ni watu

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wazima lakini wana *experience* kubwa na wameona mengi, siyo rahisi kukosea. Tunawahitaji kwenye vyo katika uboreshaji wa kupata Watanzania ambao wana ujuzi wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema machache hayo...

SPIKA: Mheshimiwa Kaijage, naona Mheshimiwa Dkt. Paulina Nahato amesimama. Ni taarifa, utaratibu ama nini? Washa kisemeo.

MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kumpa taarifa mchangiaji kwamba *academic staff* ambao wanafundisha, umri wao wa kustaafu ni miaka 65 na sio 60. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Kaijage, unaipokea taarifa hiyo?

MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE: Mheshimiwa Spika, siipokei. Nilikuwa nilikuwa nashauri kama itawezekana, waweze kustaafu *at age* ya 60, halafu waanze kupewa mikataba kuanzia 60 kwenda juu mpaka watakapochoka wenyewe, kwa sababu ni watu muhimu sana na wana uzoefu na uelewa mkubwa. (*Makofi*)

SPIKA: Sasa Mheshimiwa Kaijage ngoja tuliweke vizuri. Kwanza walikuwa wanastaafu miaka 60, Serikali ikapandisha mpaka miaka 65. Sasa kwa mchango wako, unataka Serikali irejeshe 60 halafu iwaachie mpaka huko mbele au ianzie hiyo 65 isogeze mbele?

MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE: Mheshimiwa Spika, ianzie 60 halafu waendele mpaka watakapo choka wenyewe, kwa mikataba lakini ndio wazo langu.

SPIKA: Ni sawa. Nilitaka tu niliweke sawa ili uwe umemwelewa huyo aliyekuwa anatoa taarifa. Kwa hiyo, endelea na mchango wako.

MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE: Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, atafuatiwa na Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai na Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, ajjandae.

MHE. DAIMU I. MPAKATE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami kutoa mchango wangu mdogo kwenye Wizara hii ya Utumishi ili nami mawazo yangu yachukuliwe.

Mheshimiwa Spika, moja, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunisimamisha kwa siku ya leo. Pili, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo anatuangaikia Watanzania ili kuleta maendeleo ya nchi yetu. Pamoja na shukrani hizo, nitachangia katika sehemu tatu. Sehemu ya kwanza ni suala la menejimenti kwa maana ya TAKUKURU, sehemu ya pili itakuwa ni *TASAF*, ya mwisho nitaungana na wenzangu kuomba suala la ajira.

Mheshimiwa Spika, utendaji wa TAKUKURU na ripoti yake sina mashaka nayo, lakini utendaji wake unakutana na vikwazo ambavyo tusipoviangalia kwa fedha nyingi zilizokwenda vijijini, usimamizi wake ni mdogo, kiasi kwamba ubadhirifu unaendelea kuwepo katika Halmashauri zetu katika nyanja mbili. Moja, TAKUKURU hawana watumishi wa kutosha katika maeneo yetu, ukizingatia maeneo yalivyokuwa makubwa, kunakuwa na watumishi watatu mpaka wanne. Kama ilivyo Tunduru na vijiji vyake, TAKUKURU wanashinda kutembelea miradi yote ya maendeleo ili kufuatilia kama utaratibu wa manunuzi na *force account* unatumika kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na tatizo la watumishi, hawana magari. Huwezi kutembea zaidi ya kilometa 18,776 kufuatilia miradi ambayo inatekelezwa na Halmashauri kama

magari hakuna. Kwa kweli jambo hili linafifisha jitihada za kujenga uchumi kwa maana ya miradi kutekelezwa kwa kiwango kinachotakiwa. *Force account* ina utaratibu wake, lakini wajumbe wengi kutoka vijijini hawaelewi. Inatakiwa *procedure* zile zifuatiliwe, zisipofuatiliwa, tunaweka nyanja kwa upande wa watumishi wa Halmashauri kufanya yale wanayoyataka, matokeo yake wale Wajumbe wanachofanya hakieleweki. Kama TAKUKURU watakuwa wanapitia miradi hii, hayo mambo mengine yatashindwa kufanyika kwa urahisi zaidi kwa sababu watakuwa wanaogopa muda wote watu wa TAKUKURU watakuja kuangalia utaratibu wa manunuzi unaendaje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali, pamoja na kazi nzuri wanayoifanya lakini bado kazi hii inatakiwa ifanywe kwa hali ya juu ili malalamiko yaliyoko vijijini yaweze kupungua na miradi yetu iende kwa kiwango kile ambacho kinatakiwa. Katika usimamizi wa miradi hii kwa upande mwingine maeneo yetu, malalamiko ya wananchi ni mengi, TAKUKURU wanakaa ofisini, hawatembe maeneo ya vijijini wakajue hizi changamoto kutokana na tatizo la magari na uchache wa wafanyakazi. Kwa hiyo, naomba ufuatiliaji ukamilike kwa maana ya kuongeza watumishi TAKUKURU pamoja na magari ili waweze kusimamia miradi ya maendeleo vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nilipenda nizungumzie ni suala la *TASAF*. Kwanza tumshukuru Rais kuendelea kuwasaidia wananchi wetu masikini, lakini mwaka huu utaratibu umebadilika kidogo ambao unaleta malalamiko na hauna tija kwa wanufaika wa *TASAF*. Tumesema hawa uwezo wao ni mdogo, *most of them* wanakuwa wanapata mlo mmoja au hakuna kabisa. Tunawaambia watalipwa kutumia simu. Kama ameshindwa kula kwa siku mara tatu, atakuwa na simu ya kupokelea hiyo pesa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, jambo hili limekuwa ni changamoto sana. Naomba ule utaratibu wa kupeleka fedha moja kwa moja kwa walengwa kwa kutumia magari,

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

basi uendelee, kwa sababu gharama yake ni ndogo kuliko kumwambia alete akaunti namba. Matokea yake analeta akaunti namba ya jirani yake; wakati wanaposti, jina linatofautiana ile pesa inakuwa haiendi. Jambo hili kwa kweli limekuwa ni kero kwa wanufaika wengi, hela zao zinachelewa kwa sababu ya kuambiwa apeleke akaunti namba.

Mheshimiwa Spika, pamoja na akaunti namba, mmeanzia utaratibu wa kulipa benki. Benki hiyo kwa shilingi 27,000/= au shilingi 40,000/= unamtumia benki, mtu anakaa zaidi ya kilometa 100, anachukuwa nauli kwenda na kurudi shilingi 15,000/= mpaka shilingi 30,000/= anafuata shilingi 40,000/=, tunawasaidia au tunawatesa?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Wizara iangalie suala la malipo ya *TASAF* kupitia simu yasiitishwe na suala la kupitia benki halina manufaa kwa wanufaika kwa sababu hata benki yenyewe ina makato ambayo inayolazimisha yule mnufaika naye mapato yake yaweze kupungua. Nadhani gharama ya benki ni kubwa zaidi kuliko kuwatuma watu kupeleka *cash* na *risk* yote iliyokuwepo, lakini ni nafuu zaidi kuliko kutumia benki na simu.

Mheshimiwa Spika, bado tunatakiwa tutoe elimu kwa hao wanufaika wa *TASAF*, wale wanaofanya kazi za kujitolea. Kama sio mnufaika, anapewa shilingi 24,000/=. Akienda kufanya kazi, kama kazini analipwa shilingi 12,000/=: siku anapokea huku, anapata shilingi 12,000/= na mwenzake anapokea shilingi 24,000/= anapewa shilingi 12,000/=. Hii inaleta malalamiko. Kwa hiyo, naomba waendelee kutoa elimu kwa maeneo yote, kwamba anayefanya kazi tofauti ya thamani, atalipwa kutokana na ile kama wanavyofanya wenzake ili kuhakikisha kwamba watu wanaendelea.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, kwenye *TASAF*, sifa kwa kweli imekuwa ni changamoto kubwa sana. Bado kuna malalamiko, wenye sifa wengi wameachwa katika wanufaika hawa. Kwa hiyo, naomba hizi sifa mzingatie kwa hali ya juu kwa sababu sifa hizi ni umasikini, lakini walio wengi ukienda kwa wanufaika, wanaoenda kupokea, unajua kabisa huyu

ana uwezo wa kufanya kazi. Bado hatujawa makini kwa asilimia kubwa kuhakikishwa kwamba wanufaika halali ambao ndiyo tunaokusudia hawapati; wanapata wale wajanja wajanja ambao kwa kweli wana uwezo wa kufanya kazi kwa namna moja au nyingine.

Mheshimiwa Spika, suala la ajira. Naipongeza Serikali kwa kutangaza ajira, lakini bado manunguniko ya hawa walimu au manesi ni makubwa. Kila wanapoomba huko vijijini, hawapati, wanapata wa mjini tu. Kama sheria inaruhusu, tugawe kama wanavyofanya wanajeshi. Mwezanagu ameongea vizuri sana pale, Jeshi la Wananchi, Polisi, Magezea, wanazigawa nafasi hizi kulingana na mkoa na Wilaya. Hizi nafasi ukizigawa kwa wilaya, nchi nzima hii wasomi wamejaa. Walimu siku hizi vijijini huko wanajitolea kwa hali ya juu, Wahudumu wa Afya, wako wengi, wamesoma, lakini inapotokea kuomba kwenye mtandao wanapata wa mjini tu, hawa wa vijijini sifa hawana?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaomba sana Serikali ilianganalie kwa hali ya juu kwa sababu huko vijijini tunakotoka wasomi wamejaa, walimu wamejaa. Tunaomba mwangalie; hizo kompyuta ziangalieni, zina macho. Wale tuliosoma kompyuta tunasema *garbage in garbage out*. Sasa isiwe ikawa inatokea *garbage in, garbage out*, wanatengwa; watu wa vijijini hawapati hizi kazi. Tunaomba mlianganalie mtutengee hizo nafasi kila mkoa kila wilaya ipate. Kila mtu hapa ana barua mifukoni mwao, tuwasaidie hawa watu tupunguze malalamiko ya ajira katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, sheria hizo kama haziruhusu, basi leteni turekebishe. Hao wenzetu wanaofanya kazi ya bodaboda wengi hata ukienda *Bolt*, sijui wapi, utakuta wasomi kabisa, watu wenye *degree* wanafanya kazi hiyo. Wameshakata tamaa, ndiyo maana wanaendesha bodaboda. Sasa tunaomba mjitahidi sana, katika hali ya kawaida, kwa kweli tuwajali watu wetu, hizi nafasi zigawiwe kwa uwiano ili kila eneo lipatikane wasomi ambao wanafanya kazi.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, hii itasaidia kitu kimoja; huko vijijini sasa hivi wasomi wenye *Degree* na *Diploma* wanachekwa kwamba wewe umepoteza muda wako, umenikuta hapa mimi na jambo fulani, kwa sababu amemaliza *Degree* yake, anarudi kijijini, naye analima au anaendesha bodaboda. Kuna faida gani? Kwa hiyo, wenzetu, wale wanavijiji wengine wanaona kama *model* ile siyo sahihi, kwamba kusoma unapoteza muda.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuwajali hawa watu wa vijijini ili waonekane kusoma ni mali. Waangalieni, waliomaliza 2015, 2016 na 2017 waajiriwe, kwa sababu hao ndio waliokuwa wengi na wengi wako vijijini. Hiyo mitandao kule inasumbua kidogo. Kama anashindwa kupata nauli ya kwenda mjini, atapataje hela ya kuweza kununua mtandao?

Mheshimiwa Spika, naomba sana Wizara iliangalie hili, kilio hiki ni kikubwa sana kwa wale wahitimu ambao wako vijijini.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara na ikiwa muda wetu utaruhusu, tutamalizia Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya.

MHE. EMMANUEL L. SHANGAI: Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Awali ya yote niwashukuru sana Wizara nzima kwa kazi nzuri wanayoifanya, wakiwepo watendaji wote, TAKUKURU Pamoja na Katibu Mkuu, mwalimu wangu Dkt. Laurean Ndumbaro na wote ambao wanafanya kazi hizo kwenye Wizara. Pia nipende kusema kwamba Wizara hii wanafanya kazi nzuri sana, na kuanzia Awamu hii ya Sita. Mimi nilikuwa Mwenyekiti wa Halmshauri nimeona kazi kubwa iliyofanywa watumishi kule wanaishukuru sana Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi cha nyuma watumishi walikuwa wanafanya kazi ili mradi tu, watumishi walipopandishwa vyeo pamoja na kubadilishiwa madaraja naona sasa wanafanya kazi kwa *morale*. Kwa hiyo niombe Wizara iendeele kufanya kazi hiyo. Nimeona kwamba mmepanga kuwapangisha watumishi wengine madaraja pamoja na kuwapandisha vyeo. Niombe kwamba tuendeele kutumia sheria zetu tulizonazo ili wasiwepo watumishi ambao wataachwa bila kupandishwa vyeo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na pia niombe Wizara, kwamba kuna watumishi wa kati tunafanya zoezi la kuwapandisha vyeo pamoja na madaraja, kuna watumishi ambao waliachwa niombe wizara mtoe nafasi tena kwa watumishi hao ili wapate nafasi kama watumishi wengine ndani ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwenye ajira ambazo zimetangazwa kuna maeneo ambako watumishi wamekuwa wakiondoka. Kwa mfano halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro mwaka jana walipoajiriwa walimu walijiriwa watumishi ambao ni walimu 10; walimu nane walikuwa wa shule za msingi na walimu wawili walikuwa ni shule za sekondari. Kwa bahati mbaya wale watumishi walishaajiriwa nyuma wakaacha ajira za Serikali. Kwa hiyo wakati wanaingizwa kwenye mfumo ilionekana kwamba wale watumishi hawawezi kuajiriwa tena. Kwa hiyo badala na halmashauri yetu kunufaika na watumishi 10 wale watumishi walirudishwa mpaka leo hawajulikani walipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niombe wizara kwenye ajira hizi tunaomba *replacement* ya zile nafasi 10 pamoja na watumishi wengine kwa sababu kwenye halmashauri yetu ya Ngorongoro watumishi wengi wanaondoka kwa sababu ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, na ili kutatua tatizo hili nishauri Wizara, kwamba tuangalie maeneo ya pembezoni. Nakumbuka siku moja Mbunge Mheshimiwa Kandege alizungumza kwa maeneo ya Nkasi na Rukwa na maeneo

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mengine; kwa miaka ya nyuma Serikali kupitia mradi wa Mkapa *Foundation* kuna maeneo kama haya ambayo walikuwa wanapewa motisha walikuwa wanaajiriwa na Mkapa *Foundation* ili watu kufanya kazi kwa mkataba wa Serikali. Jwa hiyo maeneo kama halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro na maeneo mengine ya pembezoni tuwape kipaumbele ili angalau maeneo yale wananchi nao wapate huduma.

Mheshimiwa Spika, Lakini kuna maeneo mengi sana mwaka 2017 Serikali iliwaondoa watumishi wa darasa la saba kwenye ajira. Wengine waliondolewa kwa haki na wengine waliondolewa kwa kuonewa. Nitoe mfano ya watumishi waliondolewa na mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro; watumishi wenyeji 63 wengi wao walijiriwa miaka 1993 na wengine walijiriwa kabla ya mwaka 2004 lakini wote waliondolewa kwenye ajira na inaonekana hilo kulikuwa na chuki kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi niombe Wizara ifanyie kazi malalamiko ya watumishi hao; na nimuombe Waziri, kwamba niwalete watumishi hao waje kuaonana na wewe pamoja na Katibu Mkuu ili mshughulikie matatizo yao, na wale wenye sifa warudishwe kazini.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna watumishi wengine wa Baraza la Wafugaji Ngorongoro, nao waliachishwa kazi. Kulikuwa na mkataba ambao Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro pamoja na Baraza la Wafugaji wallingia mabkubaliano kwamba wale watumishi wa Baraza la Wafugaji walitakiwa kuajiriwa na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro; lakini baadaye waliomba kibali utumishi; kiuhalisia walikuwa na bajeti lakini baadaye wakasema utumishi wamenyimwa kibali. Kwa kuwa tayari Baraza la Wafugaji ni taasisi ya Serikali iliyoanzishwa na Sheria ya Bunge hapa hapa; kwahiyo mimi nikuombe Mheshimiwa Waziri na watumishi hawa nao waangaliwe.

Mheshimiwa Spika, Serikali yoyote duniani ina kazi ya kuhakikisha kwamba huduma kwa wananchi zinatolewa. Na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ili watumishi nao waweze kufanya kazi ni lazima wawe na maslai mazuri ili waweze kufanya kazi masaha yote yanayotakiwa. Kwa hiyo niendeleo kuishauri Wizara, kwamba tuwaangalie watumishi, hasa kupokea malalamiko yao kwa wakati na kufanyia kazi kwa wakati. Unakuta kwamba kuna malalamiko yameletwa wizarani, mtu anasubiri miezi sita, sijui tunafanya nini mpaka miezi sita inapita bila kufanyiwa kazi? Tunatakiwa kwamba watumishi wanapoleta malalamiko yao yanatakiwa kufanyiwa kazi kwa *specified time*; siyo mtu anakuja Dodoma anatoka, Kikoma anatoka Arusha, kila wakati anakuja Dodoma hapati majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeona kwamba mmeanda mfumo wa kupokea malalamiko, lakini wakati mwingine watumishi hawapati majibu yao kwa wakati. Niombe Wizara kufanyia malalamiko kazi kwa wakati wale wahusika wapate majibu yao kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba niunge mkono kwa asilimia 100.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, atafuatiwa na Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya.

MHE. DKT. THEA M. NTARA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Na mimi niungane na wezangu kuwapongeza sana Mawaziri, ndugu yangu dada yangu Jenista pamoja na Naibu wake; jina lake la Kigogo ni gumu samahani sana. Niwapongeze kwa kazi nzuri nipo kwenye hiyo Kamati, kwa hiyo niwapengeze kwanza...

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, anaitwa Deogratius Ndejemi; kwa hiyo unaweza ukamwita Deo.

MHE. DKT. THEA M. NTARA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nikupongeze sana Mheshimiwa Deo kwa kazi nzuri unayofanya kwa kusaidiana na Mheshimiwa Jenista. Kwanza niwapongeze hasa kwa usikivu tukiwa kwenye Kamati. Ni Mawaziri wasikivu sana, maoni yetu mengi waliyachukua kwa uzito waliostahili.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, mimi nianze na suala moja ambalo tulizungumza kwenye Kamati na mlitoa ahadi; kuhusu *harmonization* ya mishahara kati ya wahadhiri na waendeshaji.

Mheshimiwa Spika, Katibu Mkuu alitoa ushahidi kwamba hilo suala tayari wanalifanya kazi. Sasa mimi niseme tu, liamenza muda mrefu, na mnasema hao watu walikuja kuwaona; hebu niombe sasa mlifanyie kazi ili huko kwenye vyuo watu wafanya kazi kwa upendo. Nililiseba, maana unakuta mhadhiri ana *master* na mwendeshaji ana *masters* lakini mishahara yao inakuwa tofauti mno kiasi kwamba ikapelekea watu kudharahuliana au kujengeana chuki. Kwa hiyo ni vizuri mkaangalia hilo suala lifike wakati sasa liishe.

Mheshimiwa Spika, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya hawa ni watumishi. Kwa muda mrefu wamekuwa wakipata *political fund* ya milioni tano ambayo ni ndogo sana. Mimi nilikuwa Mkuu wa Wilaya, hiyo milioni tano nilikuwa ninaiona; na Wakuu wa Mikoa milioni 20. Sasa ni muda mrefu Mkuu wa Wilaya au Mkuu wa Mkoa anakwenda na hicho kiwango.

Mheshimiwa Spika, mimi niwaombe wakae pamoja na TAMISEMI kuangalia kiwango cha huyu mtumishi kiwe angalau kipande. Mkuu wa Wilaya anakwenda mahali kwenye harambee huku hana hela, unakuta anatoa mia tano, mia tatu; na hiyo inawafanya wanaonekana wanyonge. Mkuu wa Mkoa anakwenda mahali anashindwa hata kutoa milioni moja. Sasa sijui Waheshimiwa Mawaziri *political fund* yao ni kiasi gani; lakini ningepomba hili litazamwe mkishirikiana pamoja na TAMISEMI kuona kwamba kwamba ifikie wakati sasa kile kwango kiongezeke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kingine nipongeze sana kazi waliyoifanya wala CAG kama alivyosema Prof. Mkumbo. CAG walifanya kazi nzuri sana kuangalia idadi ya watumishi katika shule za msingi. Sasa ile asilimia 41 ya upungufu ni kubwa mno. Kwa hiyo, cha kufanya hapa sasa ni kuangalia namna gani hao CAG nao waende kwenye vyuo, na wakifika

kwenye vyuo nako watoe hizi takwimu za upungufu wa watumishi. Sasa CAG akienda kwenye vyuo yeye anangaalia tu mambo ya *consultancy*; ajue vyuo na shule kazi yao ni ufundishaji na kujifunza. Kwa hiyo *a-base* kwenye kukagua vitu vinavyohusiana na ufundishaji na kujifunza. Kwa mfano anaenda pale Ardhi ili tujue watumishi wa pale ardhi wamepungua wangapi? Anacheki *workshops* zao zikoje, anacheki maabara; hivyo ndiyo vitu anatakiwa CAG atuambie ili tujue kabisa upungufu wa vituo hivyo katika vyuo vikuu na vyuo vya kati. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lingine, niwaombe Ofisi ya Utumishi kule Hai Mkoani Kilimanjaro tayari wametenga eneo la kujenga Chuo cha Utumishi wa Umma na wametenga muda mrefu. Sasa, niwaombe Ofisi ya Utumishi, lichukueni hilo Mheshimiwa Waziri ili muone kama mnaweza kuanza angalau na zile *process* za mwanzo, kwasababu ni muda mrefu hilo eneo limetengwa. Bahati nzuri kwenye kamati tuliwaambia mimi naona ingependeza kama mtalichukua hilo na kuona kwamba tunaongeza idadi ya vyuo vya utumishi kwa kuwasaidia watumishi kupata elimu na pia kuongeza vyuo vya aina hiyo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mimi baada ya hapo nikushukuru sana kwa leo naishia hapo. Ahsante sana. (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya.

MHE. LEAH J. KOMANYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kutoa mchango wangu katika hoja iliyopo mbele yetu. Nianze kwa kuipongeza Wizara kwa hotuba yao nzuri na kwa kazi nzuri wanazozifanya pamoja na ushirikiano wanaotupatia sisi Wabunge. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, niungane na wenzangu kuishukuru Serikali kwa namna inavyotekeleza Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi. Katika mwaka huu wa fedha ajira 44,000 zinaendelea kutekelezwa, na tayari ajira 11,000

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

zimeshatolewa lakini pia watumishi 92, 619 watapandisha vyeo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa nashauri kipaumbele kiangaliwe kwenye halmashauri zenye upungufu mkubwa wa watumishi ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Meatu ambayo upungufu wake upo juu sana kwa asilimia ikilinganishwa na upungufu wa kitaifa.

Mheshimiwa Spika, katika miaka mitano Halmashauri ya Meatu imekumbwa na uhaba mkubwa wa watumishi kwa sababu watumishi wengi wamekuwa wakihama. Ndani ya miaka mitano walimu 232 walihama huku halmashauri tukipokea walimu 39 tu. Vilevile waliokoma utumishi ikiwemo kustaafu ni walimu 156. Shule za Msingi Halmashauri ya Wilaya ya Meatu tuna upungufu wa walimu 930 sawa na upungufu wa asilimia 47 huku sekondari tukiwa na upungufu wa walimu 199 sawa na asilimia 42. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nishukuru kwa tangazo la Wizara ya Afya lililotolewa na *Professor* Abel Makubi kwamba angalau watumishi waweze kudumu kwa miaka mitatu kabla hawajaanza kuomba kwenda katika halmashauri nyingine kwa kuwa sisi halmashauri za pembezoni tumekuwa tukiathirika kabisa; na watumishi wanaporipoti na kuomba uhamisho. Kwa hiyo sisi halmashauri tunakuwa daraja la kupitia watumishi katika kupata ajira.

Mheshimiwa Spika, katika upande wa afya Halmashauri ya Wilaya ya Meatu tuna upungufu wa watumishi 675 sawa na upungufu wa asilimia 68. Hospitali ya Wilaya ya Meatu peke yake tuna upungufu wa watumishi 201 sawa na upungufu wa asilimia 64 huku zahanati zaidi ya nane zikiwa na mtumishi mmoja mmoja. Mtumishi akihama, akistaafu au akijifungua ile zahanati inafungwa.

Mheshimiwa Spika, tuiangalie kwa jicho la huruma Wilaya ya Meatu ambapo kama nilivyotaja zahanati nane zina mtumishi mmoja mmoja. Hospitali ya Wilaya ya Meatu zaidi ya miaka sita hatuna mtalaamu wa mionzi, (*X-RAY*) kiasi

kwamba inawalazimu wananchi kusafiri kwenda Shinyanga, Mwanza, na Bariadi. Hii inasababisha wananchi hao wanapata gharama na wengine kupata ajali wanapoelekea kwenda kupata kipimo cha X-RAY.

Mheshimiwa Spika, pia Wilaya ya Meatu hatuna Mhandisi wa Vifaa Tiba na hivyo kuisababisha halmashauri kuingia gharama kubwa kwa kuwaleta watalaamu kutengeneza vifaa hivyo. Mathalani kiliharibika kifaa cha kutoa dawa ya uzingizi, kiligharimu shilingi milioni nne kumleta fundi kuja kukitengeneza kifaa hicho. Kwa hiyo kama halmashauri tunaingia gharama kubwa na kutokutekeleza majukumu ya kutibu kwa sababu ya kukosa watalaamu hao. Kwenye ajira nimeona wahandisi wapo naomba Halmashauri ya Meatu tupatiwe mtaalamu mmoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niipongeze Serikali katika mfumo wake mpya wa taarifa za utumishi na mishahara. Mifumo hii inatengenezwa na Watanzania wenzetu na wazalendo wenzetu. Mfumo huu ukitumiwa vizuri utasaidia kupunguza tatizo la watumishi hewa kwa sababu mtumishi akistaafu ataondolewa moja kwa moja na mfumo.

Mheshimiwa Spika, nimuombe Waziri kuna changamoto ya mawasiliano kati ya Wizara ya Utumishi na Wizara ya Fedha. Mfumo wa *Lawson* unaonesha *wage bill* ipo chini lakini fedha inayotolewa hazina ipo juu ukilinganisha na *wage bill*. Kwa mfano; katika ripoti ya CAG iliyopita Halmashauri ya Wilaya ya Uyui ilipelekewa zaidi ya shilingi milioni 309 katika mishahara kutoka hazina zaidi ya *Lawson*, Kaliua milioni 209.9, Urambo milioni 149. Ni ukweli usiopingika, sababu ya msingi inayosababishwa hivi ni kufuta majina ya watumishi waliokoma utumishi ambapo tunachelewa kupeleka taarifa hazina. Udhaifu huu usipodhibitiwa utaibua upya mishahara hewa Serikalini (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba mwaka 2016 Serikali ilipoanzisha zoezi la kutafuta watumishi hewa kuna watumishi waliokuwa wamepata barua za kupandishwa madaraja ya mishahara yao na asilimia ndogo

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

waliweza kubadilishiwa; lakini kundi kubwa lilisitishwa kusubiri zoezi la kusafisha watumishi. Kundi hili lilikaa hadi mwaka 2017 na wengine mwaka 2018 ambapo walipewa barua mpya zikafutwa zile za zamani; kwa hiyo wamechelewa miaka miwili wakilinganishwa na wale wenzao waliopandishwa mwaka 2016. Waliopandishwa mwaka 2016 walipandishwa tena mwaka 2021 ilhali lile kundi la pili limeendelea kubaki hivyo hivyo na kusababisha manung'uniko kutoka kwa watumishi kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niombe Serikali sasa, kwamba, kwakuwa hawa watumishi hawakuwa na makosa isipokuwa lilikuwa ni zoezi zuri; watakapokuja kupandishwa wale wa 2021 wawachukue na wale wengine lile kundi lingine ili waweze kuwa-*balance*, maana yake athari yake itakuwa pia katika kiwango cha mshahara ambacho wanatakiwa kustaafu nacho.

Mheshimiwa Spika, zoezi hili lilisababisha pia wengine waliostaafu wasiweze kurekebishiwa mishahara yao. Kuna wengine walirekebishiwa mishahara yao lakini hawakuweza kulipwa mapunjo yao na hivyo kusababisha mafao yao kupigiwa hesabu kwa mishahara ya zamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi niombe Serikali yetu Sikivu, Wizara ya Fedha itoe mapunjo ya mishahara kwa waliostaafu. Tunafahamu sasa hivi hawana faili kwa Mkurugenzi na pia hawana faili popote; ni wao wenyewe kutafuta wabunge wao ili waweze kuwasaidia. Serikali iangalie kwa pamoja na iwalipe mapunjo yao ili yawekwe katika mafao na hivyo stahiki ya mafao yao wanayotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa uchangiaji kwa kipindi chetu cha kwanza kwa siku ya leo. Nitawataja baadhi ya wabunge watakaoendelea kuchangia mchana na nitawataja wale watakaoanza. Mheshimiwa Nicholas George Ngassa, Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi,

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya, Mheshimiwa Aidha Joseph Khenani wengine wataendelea kutajwa kadri muda utakavyokuwa unakwenda.

Waheshimiwa Wabunge katika michango iliyotolewa hapa Bungeni, niwakumbushe tena, na nasema siku zote, lugha ya mazungumzo wakati ni mwingine ni ngumu na kanuni zetu zinataka mtu achange bila kusoma. Kwahiyo wakati wa kutengeneza zile sentensi unaweza ukapitiwa na maneneo fulani hivi ama ili ukamilishe sentensi yako ukasema jambo fulani pengine ambalo hukuwa umelikusudia.

Sasa katika michango iliyotolewa hapa kuna namna fulani hivi wamezungumzwa vijana ambao wanajishughulisha na kilimo huko vijijini na kwamba wengine ni wasomi, wengine wamemaliza kidato cha nne, wengine cha sita, wengine wana stahada, wengine shahada na shahada zingine za uzamivu, wengine za uhamili na mambo kama hayo.

Sasa, sisi wote tunafahamu kuna juhudi nyingi na kubwa zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita kuhakikisha vijana wetu wanapata ajira kwenye kilimo na juhudi hizo zinapofanywa zinafanywa kwa wananchi wote si wasomi pekee wala si wale ambao tunafikiri pengine hawajasoma. Na kwa hivyo kilimo kisionekane kwamba pengine ni kazi ambayo wanafanya watu wa aina fulani hivi ambao hawana elimu kwa hiyo kuna watu mahali hivi wanawacheka. *(Makofi)*

Nafikiri kwa juhudi hizi zinazofanywa na Wizara ya Kilimo na Serikali yetu ya Awamu ya Sita zinaashiria kwamba hicho kichoko hakitakuwepo kwa sababu watu hawa watawezesha vizuri na watafundishwa vizuri, na sisi kama wabunge wakati wa michango yetu lazima tuoneshe mabadiliko hayo kwenye hii sekta ya kilimo ili kuwatia moyo vijana wetu ambao wanahitimu ngazi mbalimbali za masomo. Kwamba kilimo ni sehemu mojawapo ambayo wanaweza kwenda wakajajiri wao lakini pia wakaajiri watu wengine. Vivyo hivyo na maeneo mengine yote ambayo vijana wetu wanajajiri. Hata tunapowazungumzia hapa

vijana ambao wapo wamejiajiri kwenye bodaboda na Mheshimiwa Mbunge wa Ubungo ametoa hapa takwimu wao kuwepo kwenye hiyo kujiajiri kwenye hilo eneo la bodaboda haimaanishi pengine lile eneo hadhi ndogo kuliko elimu yao kwa sababu hawa watu walivyoenda kujiajiri huko maana yake kipo wanachokipata na wanatumia elimu yao kufanya hiyo biashara wanayoifanya. *(Makofi)*

Kwa hivyo, isije ikaleta hiyo picha kwamba pengine watu wanaojiajiri kwenye hayo maeneo wanakuwa wanatazamwa tofauti nanafikiri Mbunge wa Ubungo aliliweka vizuri kwamba hata hao wasomi sana tu wapo kwenye hilo eneo kuashiria kwamba mtu yoyote eneo ambalo anaona anaweza kujiajiri atafanya hivyo na hii itatuondolea kasumba ya kufikiri kwamba kila mtu lazima asubiri ajira za Serikali kwa sababu kama tulivyoona kwenye hii hotuba haitawezekana Serikali kuajiri kila mtu ambaye anahitimu na hivyo lazima Serikali itengeneze mazingira ya watu kujiajiri katika hizi sekta nyingine.

Kwa hiyo sisi Wabunge tusitume ujumbe kana kwamba hizo sekta nyingine pengine ni za watu wa hali fulani.

Waheshimiwa Wabunge sasa kabla sijasimama hapa alikuwa amesimama Mheshimiwa Lusinde akiomba mwongozo kuashiria kwamba kuna jambo ambalo limefanyika hapa ndani anataka kujua kama linaruhusiwa ama haliruhusiwi Mheshimiwa Lusinde. *(Makofi)*

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE Mheshimiwa Spika, nikushukuru kunipa nafasi niombe mwongozo wako kwa Kanuni ya 76 ambayo inaruhusu kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema.

Mheshimiwa Spika, tupo kwenye bajeti kuu ya nchi na kwa sasa tangu asubuhi mpaka saa hizi Waziri wa Fedha sijamuona humu na Wabunge wamekuwa wakichangia sana.

Mheshimiwa Spika, je, naomba Mwongozo wako kama ni sawasawa na hii michango ya Waheshimiwa Wabunge itachukuliwaje pale ambapo Wabunge wamezungumza kwa umakini mkubwa kuhusu Wizara ya Fedha na mhusika mkuu hayupo? Naomba mwongozo wako.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge amesimama hapa Mheshimiwa Lusinde akiomba mwongozo kwa mujibu ya Kanuni 76 ambayo inampa fursa Mheshimiwa Mbunge ya kuomba mwongozo ili ajue jambo ambalo limetokea Bungeni mapema kama linaruhusiwa ama haliruhusiwi.

Mheshimiwa Lusinde ameeleza kwamba yeye alivyotazama siku ya leo tangu asubuhi hoja ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora ilivyowekwa mezani na pia michango mbalimbali Waheshimiwa Wabunge wanayoitoa hajamuona Mheshimiwa Waziri wa Fedha na hiki ni kipindi cha bajeti.

Kwanza, kwa sababu ameomba mwongozo kama jambo hilo linaruhusiwa la Waziri wa Fedha kutokuwepo Bungeni wakati bajeti zikiendelea ndiyo inaruhusiwa kwasababu Waziri anaweza kuwa anamajukumu mengine ambayo haya tunayoyajadili ndiyo ambayo yanaweza yakatusaidia kufika sehemu fulani.

Waheshimiwa Wabunge kwanza leo yupo Naibu Waziri Fedha wengine pengine hawajamuona, Mheshimiwa Hamad Chande yupo humu ndani. Mheshimiwa simama kidogo ili watu wajue upo humu ndani. Kwa hiyo msiwe na wasiwasi hoja za Waziri wa Fedha yupo naibu wake anazichukua. Unaweza kukaa Mheshimiwa. (*Makofi*)

Hata hivyo, hata kama hata yeye asingekuwepo hapa ndani kwanza Waziri Mkuu alikuwepo ametoka kidogo kwaajili ya majukumu; kwa hiyo yote inaashiria Serikali ipo Bungeni. Lakini hapa ndani mnamuona pale kakaa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu ambaye anasimamia Bunge, Sera na Uratibu ambaye kimsingi shughuli zote zinazohusu

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Serikali humu ndani kile kiti pale ndicho kinakuwa kinachukua mambo yote. Kwa hiyo msiwe na wasiwasi. Lakini pia Waziri mwenye hoja yake iliyopo hapa mbele yupo kwa hivyo anazichukua hoja zote zinazozungumzwa katika kipindi ambacho hoja yake ipo mezani. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge msiwe na wasiwasi kwwa kuwa Spika wenu anawalinda na hoja zenu zinachukuliwa kwa uzito kabisa na hakutatokea namna ambayo hoja fulani haitapewa uzito kwa sababu Waziri fulani pengine hakuwepo kwa sababu hata hapa nimezungumza mambo ya kilimoilhali Waziri na Naibu Waziri hawapo lakini Serikali ipo Bungeni.

Kwa hiyo bidii wanayoifanya wanazozifanya wao kama sehemu ya Serikali wataendelea kufanya hivyo hata wasipokuwepo wao hapa kwanini kwa sababu utaratibu upo wa namna ya Serikali kupata taarifa lakini pia utaratibu mzuri upo wa namna Bunge tunavyowasiliana na Serikali kwenye hizi hoja.

Ukitaka kujua kwamba Serikali inafanyakazi na Spika wenu anawalinda hoja zenu zote hata usizomsikia Waziri hapa huwa zinajibiwa kwa maandishi, kwa hiyo msiwe na wasiwasi Waheshimiwa Wabunge.

Baada ya kuyasema haya Waheshimiwa Wabunge nasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa 10:00 leo.

(Saa 07:05 Mchana Bunge Liisitishwa hadi Saa 10:00 Jioni)

(Saa 10.00 Jioni Bunge Lilirejea)

Hapa Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikali Kiti

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI

HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais,
Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa
Mwaka wa Fedha 2022/2023**

(Majadiliano Yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Kwenye orodha naona tuna Mheshimiwa Nicholas George Ngassa, jiandae Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, jiandae Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi.

MHE. NICHOLAUS G. NGASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kufungua dimba mchana huu wa kuchangia Hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unapongelea masuala ya Utumishi wa Umma nchini na unapongelea masuala ya Utawala Bora wasaidizi Namba Moja wa Mheshimiwa Rais ni hizi Ofisi mbili, Ofisi ya Katibu Mkuu Kiongozi na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Hawa ndiyo *custodian* wa mambo yote yanayohusu utawala wa nchi yetu, ndiyo *custodian* wa mambo yote yanayohusu Utumishi wa Umma, pia ndiyo *custodian* wa nyaraka zote za Serikali katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mantiki hiyo nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Jenista Mhagama Dada yetu kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri wa hii Wizara. Lakini pia nimpongeze Kaka yetu Deo Ndejemi kwa kuwa Naibu Waziri.

Nimpongeze Mwalimu wangu Daktari Ndumbalo kwa kuendelea kuaminiwa kuwa Katibu Mkuu wa hii Wizara. Pia nimpongeze Xavier Daudi ambaye kwa sasa ni Naibu Katibu Mkuu wa hii Wizara ambae alikuwa ni Mtendaji Mkuu wa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Sekretarieti ya Ajira wakati na mimi naingia Serikalini mwaka 2011. Tunawatakia kheri katika kazi zenu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mchana huu nitachangia mambo matano ambayo ni mawazo yangu na ushauri na mapendekezo kwa Serikali ambayo naamini yatakuwa na mchango mkubwa katika kuboresha suala la Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ni mfumo wa kuomba ajira Serikalini. Tuna huu mfumo unaitwa *online application portal* ambao uko chini ya Sekretarieti ya Ajira. Kwa sasa tunavyo Vyuo Vikuu vingi nchini kwetu lakini pia vinatoa kozi na mafunzo mbalimbali. Mfumo wetu kwa sasa bado unawanyima haki baadhi ya Watanzania katika kuomba maombi ya kazi. Unakuta watu wamesoma kozi hapa nchini au nje ya nchi lakini wanapofika hatua ya kuomba maombi ya kazi unakuta kozi kwenye huu mfumo wetu wa kuomba kazi haupo. Naomba Mheshimiwa Waziri na Wasaidizi wako mkalifanyie hili ili kufungua wigo wa Watanzania wengi kuweza kuomba ajira zinazotolewa na Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo jingine katika mfumo huu ambalo linaonesha udhaifu wake ni wanapoandaa usaili wa waomba ajira. Unakuta wamesema tunahitaji watu wenye kozi zifuatazo, labda wanasema *Business Administration*, wanasema *Economics and other related courses* wale watu wanapoomba wakifika kwenye usahili wale watu walio-*apply* kwa kutumia *other related courses* siku ya usahili wanatolewa nje wanaambiwa kwamba kozi uliyoomba haihusiani na ajira uliyoomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ilitokea sana kwa watu wengi walipoomba kazi za *TRA* hivi karibuni walipofanya usaili. Mheshimiwa Waziri na Wasaidizi wako tunaomba pia mkalifanyie kazi hili jambo. Mfumo ufunguliwe, baadhi ya *selection* ziwe hata ikiwezekana mfumo uwe wa kuandika. Sasa hivi dunia ni ya sayansi na teknolojia watu wengi wamehitimu vyuo vikuu, wengine wamehitimu nje ya nchi.

Kwa hiyo unapokuwa na mfumo unapokuwa na zile kozi ambazo ni *common* tu zinazotolewa na vyuo vya nchini, matokeo yake unajikuta watanzania wengi tunawaacha nje katika mfumo huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambao ningependa kuchangia mchana huu ni suala la Watendaji Wakuu wa Taasisi, Mamlaka na Wakala kuendelea Kukaimu zaidi ya miezi sita. Mheshimiwa Waziri ukifanya utafiti, ukifanya *screening* katika Wizara, Idara na Mamlaka za Serikali, utakuwa bado kuna Watendaji Wakuu au Wakuu wa Idara au Wakurugenzi Wakuu bado wanakaimu na Kanuni zetu za kudumu za Utumishi wa Umma Toleo la 2009 zimeweka ukomo wa miezi sita, baada ya pale *vetting* inakamilika, mapendekezo yanakwenda kwenye mamlaka ya uteuzi kwa kupitia Wizara husika lakini kwa kuwa ninyi ndiyo Wizara kiongozi ni kama kiranja wa Wizara zingine kwa maana ya kwamba mna-*deal* moja kwa moja na mna-*link* moja kwa moja na Ofisi Namba Moja ya Ikulu kwa maana Ofisi Kuu ya Nchi. Kwa hiyo, tunawashauri jambo hili la upekuzi lisiwe kisingizio au kichaka cha kuchelewesha watu kuthibitishwa kazini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wanaokaimu zaidi ya miezi sita ni kinyume cha Kanuni za Utumishi wa Umma, ni kinyume cha Sheria ya Utumishi wa Umma wa nchi yetu. Tunaomba hili Mheshimiwa Waziri wewe Dada yetu ni msikivu utalisimamia vizuri na wale wenye sifa waendeleo kuthibitishwa na waweze kuwa-*full* katika nafasi zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ambalo ningependa kulichangia mchana huu ni suala la Watumishi wa Umma wanaojisomesha mafunzo ya muda mrefu. Mafunzo ya muda mrefu ni kama vile tunasema mtu amesoma digrii ya Kwanza, aliajiriwa akiwa na diploma ameenda kusoma digrii ya Kwanza amejijendeleza au alikuwa na digrii ya kwanza ameenda kusoma digrii ya pili, wanaporudi kazini kumekuwa na urasimu mkubwa sana katika kuwabadilisha madaraja lakini pia kuwabadilisha kada. Kwa mfano, kama mtu anahitaji kufanyiwa *re-*

categorization unakuta mtu alikuwa ni Katibu Muhtasi ameenda kusoma amepata *degree ya Human Resource* tuchukulie mfano rasilimaliwatu anatakiwa aje afanyiwe *re-categorization* awe *Human Resource Officer* lakini mpaka aje afike hiyo hatua atasugua sana miguu, atapambana sana na mabosi matokeo yake ni urasimu mtupu na inatengeneza mazingira ya rushwa katika Ofisi za Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Wizara mlisimamie hili jambo wale wanaostahili mpaka Mtendaji Mkuu au Mamlaka ya Ajira inapotoa kibali cha mtu kwenda kusoma maana yake imeshajiandaa. Sasa unapotoa kibali mtu akirudi kazini unanza kumfanyia urasimu tunakuwa hatuwatendei haki Watumishi wa Umma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la Nne ni suala la mikataba ya huduma kwa mteja. Maboresho katika *Civil Service* ambayo yalianza miaka ya 1995 wakati huo Katibu Mkuu Kiongozi alikuwa Martin Lumbanga, yalikuja na mapendekezo mengi ikiwepo suala la kuanzisha *Client Service Chatter* mikataba ya huduma kwa mteja. Sasa lengo hapa ni kuhakikisha mteja kwa maana ya kwamba ama Mtumishi ndani ya Taasisi au mteja anayetoka nje ya Taasisi kupata huduma ya viwango lakini kwa wakati, tunaomba hili Mheshimiwa Waziri mlisimamie.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila Taasisi ihakikishe wana mkataba kwa mteja na ioneshe huduma inayotoa, mteja atatumia siku ngapi kuipata. Kama akiwa anatakiwa kulipa malipo ya awali au amekamilisha maombi, *application* aambiwe siku 14 kama ni umeme utafungiwa ili kuwe hakuna ujanja ujanja wa kutafuta *link* na *connection*. Kama ni suala labda Mfumo wa Jamii au Hifadhi ya Jamii ukikabidhi maombi yako ndani ya miezi mitatu umepata fedha zako. Hii itasaidia sana kutoa malalamiko, itasaidia kutoa usumbufu kwa Waheshimiwa Wabunge katika kuhakikisha wanafuatilia mambo mbalimbali ambayo tu ni mfumo ungewekwa na yangekuwa yamerahisishwa katika kupatikana. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo jingine la tano na la mwisho ambalo ningependa kulichangia mchana huu ni suala la Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Katika historia ya nchi yetu mwaka 1984 Serikali ya kwanza ya Mwalimu Nyerere ilileta *Bill of Rights* humu Bungeni. Ndiyo ikawa msingi wakuwa na haki za binadamu katika Taifa letu na zikaingizwa katika hii Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Ibara ya 129 na Ibara ya 130 imeeleza majukumu ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, kwa ridhaa yako ningependa ninukuu mambo mawili ama matatu ambayo ningependa niyachangie kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma Ibara ya 130 Sehemu ya Kwanza, majukumu ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Jukumu Na. (b) Kufanya shughuli za kupokea malalamiko ya uvunjifu wa haki za binadamu kwa ujumla, kufanya uchunguzi juu ya mambo yanayohusu haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora, kufanya utafiti, kutoa na kueneza nchini elimu kwa umma kuhusu haki za binadamu na utawala bora na ikibidi kufungua mashauri mahakamani ili kuzuia vitendo vya uvunjifu wa haki za binadamu na kurekebisha haki inayotokana na kuvunjwa huko kwa haki za binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningepomba nichangie kwa kifupi. Hii Tume yetu ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwa sasa Mheshimiwa Waziri kama vile bado imelala. Tunaomba muende mkawaamshe kidogo hususani kwenye suala la kutoa elimu ya haki za binadamu na utawala bora kwa Watanzania. Mfano mzuri, ninyi chini ya ofisi yenu mnayo TAKUKURU. TAKUKURU wanajitahidi sana kutoa elimu kwa wananchi, wana vipindi kwenye Vyombo vya Habari, wanakwenda mpaka kwenye ma-*group* ya *WhatsApp* na hii mkiifanya tume ya haki za binadamu mfanye vizuri ndiyo itakuwa *shock absorber* mtapunguza hata yale maswali Mheshimiwa Rais yuko sehemu ana ziara unakutana na mabango ya wananchi wanalalamika. Unakuta Mheshimiwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Rais yuko amevalikwa kwenye sherehe za siku ya Mahakama au siku ya Sheria Duniani, Mama au Baba anatoka na bango amedhulumiwa haki zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii Tume itasaidia sana kupunguza migogoro, itasaidia kupunguza manung'uniko ya wananchi lakini kiujumla itawasaidia nyinyi Watendaji wa Serikali ndiyo maana *composition* yake imewekwa watu ambao wana weledi pia hata upatikanaji wao imeshirikisha vyombo vikubwa vya nchi, lengi likiwa ni kuweka watu ambao ni *credible* wataisaidia Serikali, watamsaidia Mheshimiwa Rais na watawasaidia ninyi katika uendeshaji wa kazi zenu za kila siku na kuzipunguzia taasisi nyingine shughuli kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, waamsheni, waambieni waingie *field* hawa siyo *Criminal Investigation Department* hawa ni *ombudsmen* hawa ni *watchdog* wa Serikali, watawasaidia na tutasonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tuna wageni, tuna wageni jioni. Kabla ya kuendelea, tunao wageni jukwaa la Spika, tuna mgeni wa Mheshimiwa Spika Ndugu Brenda Msangi ambae ni Afisa Mtendaji Mkuu *CCBRT*, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni Watano wa Mheshimiwa Maimuna Patan Mbunge, ambaye ni Watoto wake na Shangazi yake kutoka Jiji la Dar es Salaam, Ndugu Hellen Makota - Shangazi, karibu. Ndugu Justice Chiwango mtoto, Ndugu Beatrice Molle mtoto, Ndugu Brian Malisa mtoto na Ndugu Mary Mushi mtoto, karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rehema Juma, jiandae Godwin Emmanuel, jiandae Aida Joseph Khenani.

MHE. REHEMA J. MIGILLA: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kukushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia

hoja iliyopo mezani jioni hii. Awali ya yote nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai na upendeleo aliotupatia sisi wanadamu wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuwashukuru sana Viongozi wa Kamati yetu lakini pia Mawaziri ambao wanaiongoza Wizara hii ya Utumishi na Utawala Bora. Mimi nikiri kwanza ni Mjumbe wa kamati ya USEMI. Mawaziri hawa Dada yangu Mheshimiwa Jenista, Kaka yangu Mheshimiwa Deo Ndejembu na Watumishi wote walio chini ya Wizara hii, wanafanya kazi vizuri na wanatupa ushirikiano wa kutosha. Kwa sababu ya muda naomba niende haraka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza kuishukuru Serikali kwa mambo yote inayoyafanya juu ya watumishi wetu wa umma. Tumeona jitihada nyingi sana zimefanyika ili kuhakikisha hawa Watumishi wa Umma wanafanya kazi katika mazingira *very conducive*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona wafanyakazi sasa hivi baadhi wamebadilishiwa madaraja, wamelipwa madeni yao ya *arrears*, madeni ya likizo, matibabu na vitu vingi pia wamefanyiwa *re-categorization*. Hivyo ningependa sana kuishukuru Serikali kwa kuwa sikivu juu ya hawa watumishi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, panapokuwa na mazuri pia mabaya yanaweza yakawepo, nitajikita zaidi kwenye Jimbo langu. Jimbo langu lina raia ambao walikuwa wananchi wa Burundi. Wananchi hawa baadhi yao wamezaliwa Tanzania, wamesomea Tanzania na wanafanya kazi Tanzania. Raia hawa tuliwapa uraia, baada ya kuwapa uraia bado wanaendelea kufanya kazi kwa kibali. Tangu waanze kufanya kazi wengine wameanza mwaka 2003 mpaka leo hii hawa raia wanafanya kazi kwa mkataba. Walisainishwa barua ya mkataba mara moja tu lakini tangu hapo hawajapewa tena barua ya mkataba. Sasa sijajua wanafanya kazi kwa utaratibu upi?

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi hawa, ama watumishi hawa wanateseka sana. Hivi ninavyokwambia haki yao kama watumishi ni ile *Check Number* tu inayowapa mshahara. Hawana haki ya likizo, hawana haki ya pensheni na wakati huo huo kila mwezi wanakatwa pesa za *PSSSF*. Hawa wananchi hawana haki ya kushiriki kwenye Vyama vya Wafanyakazi lakini hawana haki ya kupata likizo ya uzazi, likizo maalum, lakini hawana haki hata ya kuweza kushiriki kwenye baadhi ya shughuli mbalimbali za Kitaifa kama sensa, sijui uchaguzi, hawana hiyo haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukumbuke kwamba hawa watu tayari wameshakuwa ni raia wetu, hivyo nikuombe sana Dada yangu, najua Wizara hii ni sikivu na ninyi ni wasikivu, kilio cha hawa wananchi, hawa watumishi wetu kwa sababu tumewakuza wenyewe, wamesoma kwenye vyo vyetu, wanayo mahitaji yao ya msingi sana, ninaomba Wizara na Serikali iyasikilize. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ambalo wanaomba hawa watumishi. Kwanza wapatiwe ajira ya kudumu, hii ajira waliyonayo haina *sustainability*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili kuna watu ambao walistaafu lakini mpaka leo kwa sababu walikuwa wanafanya kazi kwa mkataba hawajui hata pensheni zao watapa lini, ilihali kila mwezi walikuwa wanakatwa *PSSSF* inapofika wamestaafu hawana wanachoondoka nacho kama Mtumishi wa Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo wanahitaji hawa watu ni kupata stahiki kwa wale ambao wameshafariki, wale warithi wao, wajane, wagane, watoto basi waweze kupata stahiki zao ambazo alikuwa anazifanyia kazi huyo Mtumishi wa Umma. Ninakuomba sana najua Serikali yetu ni sikivu sana, kilio cha hawa watu naomba tukisikie kwa mikono miwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua hili suala nimeshaliongelea sana, najua Mheshimiwa Waziri na tangu

akiwa Mheshimiwa Mchengerwa nilishalifikisha sana na Mheshimiwa Jenista nimeshakufikishia na hata Katibu Mkuu Dkt. Ndumbaro nimeshamfikishia. Kwa sababu leo mpo *cabinet* yote najua kilio cha hawa wananchi kimefika tamati. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala jingine ni suala la uhaba wa watumishi hasa wa Kada ya Afya. Ni ukweli uliowazi kabisa watumishi wa Kada ya Afya hususani kwenye Majimbo ya Vijijini unakitisha mno. Kituo cha Afya au Zahanati unakuta ina Mtumishi mmoja tu. Mimi Kata ninayotoka Kata ya Ichemba kuna Zahanati pale Mtumishi mmoja tu ndiyo anafanya kazi pale. Sasa anapokuwa Mtumishi mmoja au wawili kiukweli utendaji wa kazi unakuwa ni mgumu. Mtu huyo huyo ahudumie familia yake lakini mtu huyo huyo anatakiwa ahudumie hawa wananchi. Sasa anapokuwa peke yake kuna mambo yanajitokeza mengi sana ambayo yanaweza kwa namna moja au nyingine yakamsababishia hata akafukuzwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachokuambia Mheshimiwa Waziri huko kijijini kwetu kuna utaratibu watumishi wa zahanati wanafanya kazi kuanzia Jumatatu mpaka Ijumaa tena kuanzia saa mbili mpaka saa kumi, kwa hiyo mgonjwa anapopatikana baada muda huo hana msaada.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia bado kuna unyanyasaji mkubwa sana unaofanywa na hawa watumishi kwa sababu ya uchache wao. Unakuta Mama Mjamzito anapofika pale anaambiwa kwamba hii ni mimba ya ngapi, akisema ya kwanza anaambiwa aende Hospitali nyingine. Lakini anaambiwa hayo ni kwa sababu Mtaalam wa kuzalisha pale hiyo mimba ya kwanza anakuwa pale hayupo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba hawa wataalam mnaowapeleka huko, utalam ni ukoje? Haiwezekani huyo mtaalam aliyosomea eti atuwekee masharti kwamba mimba ya kwanza kituo cha Afya, mimba ya pili mpaka ya tatu ndiyo zahanati pale. Hivi haya mafunzo ndiyo wanafanya hivyo kweli? Tunaomba sana hawa watumishi kwenye Kada ya

Afya tuwapeleke huko vijijini. Kwenye ajira hizi niombe sana watu wa vijijini tuongezewe watumishi wa Kada ya Afya. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala jingine ni kuhusu Mishahara na mabadiliko ya mishahara kwa watumishi. Kiukweli watumishi, hata mimi nilikuwa Mtumishi wana manung'uniko makubwa sana. Watumishi wa Serikali takribani miaka mitano iliyopita hawajawahi kupata nyongeza ya mishahara, maisha yao yamekuwa ni magumu sana, gharama za maisha zimepanda, lakini mishahara wao haupandi. Imefikia sasa hivi hata tamaa ya kufanya kazi imekwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii nimeshuhudia huko kwangu Mfanyakazi ana-*bet*, ukiuliza wanakuambia hali ngumu ya maisha. Wafanyakazi wanakopa mpaka songesha, wanakopa vikoba hebu ifikie mahali hawa wafanyakazi tuwaonee huruma jamani wana maisha magumu, mfumuko wa bei unawahusu, kodi, nyumba kila kitu matibabu jamani tuwaonee huruma hawa wafanyakazi, *this time* tuwaongezee mishahara. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni matumizi mabaya hasa ya ubadhirifu wa fedha. Sifa mojawapo ya mtumishi wa umma ni kuwa muadilifu katika kazi anayoifanya lakini wafanyakazi walio wengi tunaona wana ubadhirifu mkubwa sana wa madaraka yao. Hapa juzi kuna *crip* ime-*trend* sana hapa ya *temporary offices*, hivi kweli mtu anatomia milioni 100 kwa kujenga *temporary office* kiasi kwamba mpaka Waziri Mbarawa anawaambia TAKUKURU fanyeni kazi. Ina maana huyu mtu mpaka Mbarawa anasema TAKUKURU wafanye kazi hakuna *means* nyingine zilizomwangualia mpaka amefikia kufanya ubadhirifu wa kiasi hicho?

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu ninachoshangaa hawa wanaofanya ubadhirifu hivyo, hatuoni hatua za makusudi zikichukuliwa dhidi yao. Tunaona wengi akishagundulika na tatizo anaweza akahamishwa kituo,

anatolewa kituo A anakwenda kituo B. Hivi huyu ameshakuwa ni mwizi kwanza ukimtoa kituo A ukimpeleka kituo B ndiyo ataacha wizi? Huo wizi ataendeleza. Kwa hiyo, kuwahamisha sioni kama ni *solution* ya hawa wanaofanya ubadhirifu wa mali za wananchi. Wananchi wanalipa kodi kwa shida, maisha ni magumu halafu wao tu wanapiga, hapana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe ushauri kwa hao wanaofanya hivi, nafikiri hatua kali zichukuliwe dhidi yao. Isiishie tu kumsimamisha kazi au kumfukuza kazi; iendeleo aidha, wafungwe jela au hata wafilisiwe mali zao. Hivi mimi Rehema hapa nimekaa najua kabisa nina mchongo wa maana ambao najua mwisho wa siku nitasimamishwa tu kazi au nitafukuzwa kazi, si nitaiba? Nitaiba, halafu najua kabisa mwisho wa siku nitafukuzwa kazi lakini tayari nimeshatengeneza mchongo wa maana fedha ya maana. Kwa hiyo, akifikiria fedha yake ya kustaafu ni ndogo kuliko huo mchongo, nafikiria tuongeze adhabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Kunambi, jilandae Mheshimiwa Khenani.

MHE. GODWIN E. KUNAMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ningependa kwa dhati kabisa kwanza nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya katika kuleta maendeleo kwenye Taifa letu. Leo hii niseme kwa dhati kabisa, nimefarijika sana; kwa sababu moja tu, Bunge lililopita nilijenga hoja kwa habari ya jambo la *OPRAS*. Nilieleza mapungufu ya *OPRAS*; na nikaainisha mapungufu yote ya *OPRAS* na leo hii nasema nimefarijika kwa sababu Serikali Serikali hii ni sikivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hii ni sikivu kwa maana na nampongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Wizara ya Utumishi na Utawala Bora; amekwenda muda mfupi tu mama yangu huyu, muda mfupi tu, lakini tunaona Wizara inakuja na mabadiliko chanya kwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Taifa hili. Sasa kwa sababu hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, nampongeza pia Naibu Waziri, lakini nampongeza na Katibu Mkuu Dkt. Ndumbo, Mwalimu wangu kwa kweli kazi kubwa inafanywa na ni nzuri kwenye Wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze kwenye mchango wangu. Katika hoja yangu niliyoeleza hapo kuhusu *OPRAS*, wizara au Serikali imekuja sasa na mpango bora kabisa katika upimaji wa utendaji kazi wa Taasisi za Umma ambao naamini unakwenda kuweka tija kwa Taifa letu. Kwanza wamekuja na Mfumo wa *PEPMIS (Public Employees Performance Management Information System)*, mfumo huu ni mfumo ambao unakwenda kuwa mbadala wa *OPRAS* kwa maana ya kila mtumishi mmoja mmoja anakwenda kupimwa sasa, lakini haitoshi siyo tena kujaza makaratasi, sasa hivi ni mtandao. Kwa hiyo, tunaona watumishi wanakwenda kutendewa haki lakini watawajibika pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine wamekuja na mfumo mwingine wa *PIPMIS (Public Institutions Performance Management Information System)*. Mfumo huu, ni mfumo ambao unakwenda kuweka makubaliano baina ya Serikali na Taasisi zake. Jambo hili ni jema ndiyo maana nimesema nimefarijika sana siku ya leo. Sasa katika hili, nimeona nitoe maoni angalau mawili, ni jambo jema lakini nami niboresha kidogo kwenye maeneo mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mifumo hii yote miwili imetajwa kwa Kada ya Viongozi wa Kisera. Sasa Viongozi wa Kisera hawa ni kuanzia *level* ya Wizara, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na kadhalika. Sasa nashauri jambo moja, nashauri kwenye maboresho hayo hayo tuje na *KPI*, tuongeze *KPI*. *KPI* kwa maana ya *Key Performance Indicators*. *Key Performance Indicators* ni viashiria muhimu vya utendaji kazi; sasa hivi vitatusaidia hawa Wakuu wa Taasisi kwa mfano; Waziri lazima awe na *Key Performance Indicators*, kwa sababu tuna Mpango Mkakati wa Miaka Mitano na tuna Mpango Kazi wa Mwaka Mmoja. Tukimpa Waziri kwa mfano, Waziri wa TAMISEMI, akapewa *Key Performance Indicators*

za Mpango Kazi wa Mwaka mmoja alionao, kupitia Mpango Mkakati wa Miaka Mitano, anaweza kupimwa vizuri na Mheshimiwa Rais kuliko kuangalia sasa Vyombo vya Habari kama anakwenda ziara na nini, hii itasaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, halikadhalika kwenye maeneo haya wasimamizi wa Taasisi kwa maana ya viongozi wa kada za utendaji nao wapewe *key performance Indicators*. Wakurugenzi wa Halmashauri *Key Performance Indicators*, twende kwenye *level* ya ma-CEO wa Makampuni au Mashirika ya Umma *key performance Indicators*; ndani ya mwaka mmoja atatuletea mpango kazi wake na tutampima kupitia mpango kazi aliotulewa na mwisho wa mwaka atueleze kama ame-*perform* kwa kiwango gani, kama kuna mapungufu aeleze. Mamlaka ya Nidhamu itakuwa sasa na uwezo wa kutathmini kwamba huyu amefeli kwa sababu hatukum-*finance* au kwa sababu kitendea kazi au rasilimali fedha, amefeli kwa sababu ya uwezo wake. Mwisho wa siku watu wa-*vacate* ofisi wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati kabisa hii inakwenda kumsaidia Mheshimiwa Rais na nasema kwa dhati. Mheshimiwa Rais sasa hata kuwa na kazi ya kutafuta nani anafanya vizuri na hafanyi vizuri. Nampongeza tena Mheshimiwa Waziri, Mama yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nimesikia kidogo kwamba baadaye tutakwenda *biometric*, nadhani tusiishie tu hapo. Nilipokuwa hapa Dodoma Mkurugenzi wa Jiji nilianzisha mfumo mmoja, nilifunga camera ofisi zangu zote, kwa hiyo ilikuwa nikikaa ofisini naangalia Idara ya Ardhi nikiwa ofisini, nikiwa kwenye mkutano, nikiwa kwenye kikao chochote namwona mtumishi kwenye ofisi kama anamhudumia mwananchi au anafanya mambo mengine ambayo siyo kwa shughuli zake za kila siku. Kwa hiyo, nilikuwa na uwezo wa ku-*detect* kila mtumishi, popote nitakapokwenda, nikiwa nakunywa chai naangalia simu yangu, ofisi yangu ipo hapa. Ndiyo siri ya mafanikio hapa Dodoma! (*Kicheko*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisipoteze sana muda, leo hii nimefarijika sana, naunga mkono hoja na Mungu awabariki watu wa Wizara. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Khenani, jia ndae Mheshimiwa Stella Manyanya.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Namshukuru Mwenyezi Mungu na mimi kuchangia wizara hii ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. Nitambue michango ya Wabunge wote ambao wamezungumzia kuhusu ajira na changamoto ambazo zinawakuba watumishi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wengi wamezungumzia kuhusu ajira, nami nitashauri kidogo. Pamoja na kwamba changamoto ni ya nchi nzima, lakini changamoto hizi zinatofautiana kulingana na mazingira. Nkasi peke yake ina mapungufu ya watumishi 1939, Nkasi peke yake. Sasa tunaomba hii keki ya Taifa inavyogawanywa waangalie na mazingira ambayo yameathirika zaidi, sisi kuwa pembezoni mwa nchi isiyo kama kila kitu kinachokuja tunaangaliwa mwishoni; ni vizuri tuangaalie hii keki kwa mgawanyo mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajikita zaidi kwenye Utawala Bora. Tunapozungumzia neno lenyewe Utawala Bora tunazungumzia utawala wa sheria, demokrasia, utu na haki za binadamu. Nikiwa nazungumza hapa mimi ni Mbunge pekee niliyetangazwa kutoka Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tanzania Bara. Nisikitike kusema; nazungumza hapa tayari haya malalamiko ambayo nakwenda kuyazungumza nimeshazungumza na Waziri Mkuu na mimi ni Mbunge halali nilichaguliwa na kutangazwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ninapozungumza najua kwamba inapotokea *DC* kwenye eneo lake anamwakilisha Rais na Mkuu wa Mkoa anamwakilisha Rais kwenye eneo lake la mkoa. Leo ninapofanya mkutano kama

Mbunge wa Tanzania na mwananchi wa Tanzania, *DC* anaamrisha watumishi wote waliopo Wilaya ya Nkasi wasitoe ushirikiano. Waziri Mkuu anajua; nashukuru alinipa nafasi ya kunisikiliza, lakini hakuna jambo lolote limefanyika mpaka leo. Tunapozungumza demokrasi, ili uende kwenye Utawala Bora lazima tujue na hapa kuna haja niwashauri vizuri, tusirudi kwenye mambo yaliyotokea Arusha au Hai. Lazima kuwepo na chombo maalum kitakachokuwa kinafuatilia mwenendo wa hawa Ma-*DC* wetu na Wakuu wa Mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watumishi wa Umma wanapata mishahara kutokana na kodi za Watanzania bila kuangalia vyama vyao. Leo unapomzuia mtendaji, Mkuu wa Idara kwenda kwenye mkutano wa Mbunge aliyechaguliwa; naamini Waziri Mkuu kama ingekuwa mimi ni Mbunge wa CCM angekuwa amechukua hatua mpaka leo. Nazungumza kwa uchungu mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inafikia mahali naambiwa kwamba, Diwani kwa sababu katika Kata 17 kwenye Jimbo langu nina Madiwani wanne wa CHADEMA, 13 ni CCM na kwenda kwenye mkutano kutoa fedha Mfuko wa Jimbo anaambiwa Diwani wa CCM asishiriki mkutano wangu na wale walioshiriki wamepewa adhabu ya kutoa boksi tatu za marumaru. Leo mimi nimekuwa chanzo cha kujenga ofisi za Chama cha Mapinduzi? Kwa nini natendewa hayo kama Mtanzania? Utawala Bora uko wapi? Jambo hili halifurahishi hata kidogo kwenye Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kibaya zaidi ukiangalia Katiba yetu leo tunayoitumia, huyu anayeteuliwa kuwa *DC* kwa Mujibu wa Katiba anakwenda kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama. Hakuna chombo ambacho anakwenda kujifunza; anaweza kutumia kinywa chake kuondoa amani ya hilo eneo kwa sababu hajui mambo yanayohusu ulinzi na usalama. Kipindi cha nyuma walikuwa wanajitahidi wanawaandaa viongozi, leo wanachukua watu hawana sifa ya kuitwa Mwenyekiti wa Ulinzi na Usalama. Unapomwambia Mtumishi asiende kwenye Mkutano wangu

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

na mimi ni Mbunge nikitumia nguvu ya umma nini kinatokea?
(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upendo wa Taifa langu, niliombe tena Bunge, niombe tena Waziri Mkuu,

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Taarifa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naomba kutoa taarifa kwa Mheshimiwa Mbunge Aida Khenani, kwamba masuala haya ni ya kisheria. Tuna Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao inaainisha kinagaubaga kwamba kuna sheria ambazo zimetungwa zinazotoa mamlaka ya uendeshaji wa shughuli za Serikali. uteuzi wa Wakuu wa Wilaya unatokana na takwa la Kikatiba, lakini pia majukumu yao yameainishwa kwenye sheria ya *Regional Administrative Act*. Kifungu cha 14 na katika Sheria hiyo inaelekeza sifa za Mkuu wa Wilaya, lakini pamoja na hayo kuna *vetting* wanafanyiwa kwa hiyo hawachaguliwi tu ili mradi, kwenye masuala ya usalama wanajua.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, katika jambo ambalo amelizungumzia kuhusu *allegation* ya mambo ambayo ametendewa ya kiutawala katika wilaya yake; kama amekwisha kuwasilisha kwenye Mamlaka vivyo angesubiri sasa hatua ziweze kuchukuliwa kuliko kutuhumu tena mara mbili.

NAIBU SPIKA: Ahsante, dakika mbili zimekwisha. Je, unaipokea taarifa hiyo?

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Naibu Spika, namuheshimu sana kaka yangu na tulikuwa naye CHADEMA, afanye kazi anayojua amepewa na kuaminiwa na aliyemteua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kama changamoto ni Katiba ndiyo maana tunasema tunahitaji Katiba mpya. Tusifikiri Katiba Mpya kuhusu uchaguzi tuangalie na aina ya watu kama hawa ambao nawazungumzia leo. Kama shida ni Sheria au ni Katiba kuna haja sasa ya kuitazama Katiba mpya ambayo itakwenda kuleta mabadiliko ya kupata viongozi wanaokwenda kuendesha nchi kwa kufuata sheria, kanuni na utaratibu wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kushauri; la kwanza kuna haja ya kuwa na semina elekezi kwa hawa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya baada ya kuteuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu wa pili, kuna haja sasa ya kubadilisha *approach* ya kuwapata hao ma-DC na Wakuu wa Mikoa kuliko ilivyo sasa. Kama Mkuu wa Wilaya anaweza kwenda Kamati ya Ulinzi na Usalama na bado hana mafunzo yo yote yanayohusiana na ulinzi na usalama ni hatari kwa Taifa letu. Yamekuja kufahamika leo yaliyofanyika Hai, mambo yamesharibika, hatutaki yarudie. Nazungumza leo kama Mbunge wa Nkasi yanayoendelea kule kama msipochukua hatua kama Mbunge na mzaliwa wa pale; tutatumia nguvu ya umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimezungumza inavyowezekana, nimetoa taarifa inavyowezekana, lakini wapo kimya, naamini kama ni matatizo yake wachukue hatua ila kama wamemtuma watamuacha aendelee kufanya anayoyafanya leo. Sikukusudia kuzungumza haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye *TASAF*. Upande wa *TASAF* nimpongeze Waziri pamoja na Naibu wake; wamekuwa wasikivu sana, lakini kuna changamoto pia ya kupata wanufaika wa *TASAF*. Mwongozo ulivyo na watendaji kule chini hawafuati kama mwongozo unavyotaka. Wanapita Wenyeviti wa Serikali ndiyo wanaandika watu badala ya kwenda kupigiwa kura kwenye mkutano wa hadhara kwa kuwa wananchi wanafahamiana, wanajua nani ana sifa nani hana sifa.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kwenye *TASAF* hiyo, umekuwa sasa ni utamaduni kwa wale wanufaika kwa kuwa lengo ni kuwatoa kwenye umaskini, ile siku ambayo wanatakiwa wakapokee hiyo fedha ya *TASAF* wanalazimishwa kukatwa bima, nani aliwaambia bima inalazimishwa? Kama mtu anapewa 40,000; 70,000 anakatwa bima na kibaya zaidi, wengi wao wanaokatwa hiyo fedha ni wale ambao wapo kwenye msamaha wa matibatu wameshafikisha miaka 60. Kwa hiyo, hakuna tofauti na mwingine ambaye anaweza kuiba fedha za Watanzania. Kuna haja ya kuchukua hatua kwa watu ambao wamefanya hivyo.

MHE. STANLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Taarifa.

MHE. STANLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba hoja anayoizungumza ni kweli kabisa na ndiyo maana kwa sasa Serikali imekuja na *approach* mpya juu ya fedha za *TASAF* kuzielekeza kwenye miradi ya kimkakati kwa mfano barabara, zahanati, shule ili wanufaika wengi zaidi fedha hizi zikawasaidie na zisiwasaidie watu wachache kwa faida ya watendaji wasiokuwa waaminifu. Nakushukuru. (*Makoff*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Khenani, taarifa hiyo unaipokea?

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda naomba niendeleo naamini wenye changamoto hizo...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Khenani kwa mujibu wa kanuni zetu.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Naibu Spika, naikataa kwa sababu wanaopata shida...

NAIBU SPIKA: Wewe unasema siikubali, basi.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Naibu Spika, siikubali, naomba niendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumza haya kwa sababu mtu kama anajua umuhimu wa bima apewe elimu juu ya bima. Akipewa ile fedha yake anayeza maandazi akauze maandazi, azungushe ile fedha kwa sababu ndiyo lengo la kumtoa kwenye umaskini; kama alikuwa anaweza kula mlo mmoja aweze kula milo mitatu. Kwa namna nyingine kama anaweza kufanya biashara akazungusha akipata faida atakwenda kukata bima, wasiwalazimishe watu kukata bima na lengo la mfuko huu wa kusaidia kaya maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mazingira hayo ninayoyazungumza leo. Leo wamebadilisha utaratibu wa simu kwamba wale watu wanaotakiwa kunufaika na *TASAF* watumie simu, kama mtu hana uwezo wa kula milo mitatu anaweza kununua simu ya Sh.50,000? Anaweza kununua simu ya Sh.30,000? Nafikiri kuna haja ya kubadilisha *approach*, turudi kwenye lengo la kuwasaidia wananchi wetu kuwatoa kwenye umaskini kwenda angalau kwenye kiwango cha kati kwa kuwa ndiyo lengo la fedha hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mazingira hayo ambayo nimeyazungumza aidha watendaji wa Wizara ndiyo wanafanya vibaya huko chini, ni wajibu wa Wizara kufuatilia mwenendo unaoendelea huko chini, yawezekana wanachokiubiri siyo hicho kinachoendelea huko chini. Natambua wanafanya kazi kubwa sana, lakini haitakuwa na maana kama wanafanya kazi kubwa hapa ndani ya Bunge halafu huko chini maagizo yakienda hayatekelezeki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye hoja nyingine ambayo ni suala la kukaimu kwa hawa watumishi. Halmashauri ya Nkasi inaongoza kwa watu ambao wamekaimu zaidi ya miaka mitatu. wakati mwingine Wakurugenzi wanashindwa kuwapa utaratibu mzuri watumishi hawa na kupelekea kukosa haki zao za msingi. Kwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

sababu, kukaimu siyo shida sana, lakini je, wanakaimu kisheria? Wanapewa barua na Katibu Mkuu? Maana anaambiwa tu kaimu, mwisho wa siku anasema nadai fedha yangu, wanamwambia ulikaimu kinyume na utaratibu. Sasa kwa nini anakosa haki kwa kosa la watu wengine? Kuna haja ya ninyi kufuatilia vizuri ili haki za hao watumishi zipatikane.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kwa sababu ya muda, kustaafu siyo dharura. Toka mtu anaajiriwa, mnajua kwamba huyu mtu atastaafu. Labda mtu aliyekufa. Kwa hiyo, tuache visingizio... *(Makofi)*

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Manyanya, jiandae Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza, nianze kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa ajili ya yote. Pili, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa kazi kubwa anayofanya na tunamwomba afya njema ili aweze kuendelea kututumikia. Wakati huo huo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu na wananchi kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mengi yamezungumzwa, lakini kazi yetu sisi Wabunge tuliyopewa kwa mujibu wa Sheria na Katiba, ni kuwasemea wananchi kuwatetea na vile vile kuhakikisha kwamba tunakuwa na sheria nzuri zinazosaidia na mambo yote. Kwa misingi hiyo, kila mtu anapokuwa kwenye nafasi hii ya Ubunge lazima atimize wajibu huo kwa nguvu zake zote. Tunapozungumza, haijalishi jana nilikuwa nani au juzi nilikuwa nani? Leo mimi ni Mbunge, lazima niseme bila kuficha, ndiyo maana tunalindwa katika mazungumzo yote tunayosema humu Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitaanza kuzungumzia hali ambayo binafsi naiona siyo nzuri,

inayoendelea katika mitandao mbalimbali. Mitandao naichukulia ni sehemu rasmi ya taarifa, kwa sababu sisi wenyewe tumeshasema kwamba hata ushahidi wa kimitandao unaweza ukatumika hata Mahakamani. Hiyo ni kwa mujibu wa sheria. Kwa hiyo, nasema nini?

MHeshimiwa Naibu Spika, kuna hii hali ambayo inaendelea katika nchi yetu, nami kama mtu mzima ambaye Mwenyezi Mungu amenibariki nikaishi katika Awamu zote za Uongozi, nashangaa ninavyoona sasa hivi watu wanapenda kuendelea kutupiana maneno, wengine wakijaribu kuwasema viongozi waliopita, wengine wakijaribu kuwasema viongozi waliopo mambo mbalimbali, haileti afya kwa Taifa letu. Tuache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa hili lisingefika hapa leo bila uwepo wa wale viongozi waliopita. Taifa hili haliwezi kuendelea bila viongozi waliopo sasa. Kwa hiyo, badala ya sisi kushikamana kuangalia mbele tunakoenda, tunaendelea kupigana na tena wanaopigana wengine kuna chawa sijui wa watu wa zamani; kuna chawa wa watu wa sasa. Ukiangalia hawa wanaosema ni chawa, kwanza mimi neno lenyewe chawa linanitia kizunguzungu; maana yake chawa akiingia anaweza akakunyonya zaidi akakuharibia hata maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nasema hawa chawa wasaidie kuifanya nchi iende mbele. Hatutaki kutupasulia nchi yetu, hatutaki. Wote tunawataka wale wanaosifu yale mazuri ambayo yametufikisha hapa kutokea nyuma, na wanaosifu yale mazuri tunayoendelea nayo kwenda mbele. Hatutaki mambo ya ovyo. Nimeongea kama mtu mzima, ninao wajibu wa kupaza sauti kwa Taifa langu kwamba tunapoenda hatuko sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni la kuhusu watumishi. Wengi wamezungumza. Tunaongezea tu kuonesha uzito wa tatizo. Watu wanaoishi maeneo ya pembezoni wana gharama kubwa za kupata huduma kuliko walioko mjini. Inasikitisha, kama ambavyo tumesikia taarifa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mbalimbali, nami kwa Jimbo la Nyasa, kwa mfano, katika afya tuna watumishi 206 tu kati ya watumishi 800 wanaohitajita. Ni kama robo tu. Huyu mtumishi ambaye ataweza kuhudumia wale watu wote atakuwa wa aina gani? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hawa wananchi wanapokosa zile huduma muhimu wanatakiwa wazifuate mbali zaidi ambapo wanakutana na gharama ya nauli, gharama ya mihangaiko na gharama ya vifo. Hili hatuwezi kulivumilia. Kuna baadhi ya maeneo ya mjini humu kuna watumishi wengi. Kwenye shule kwa mfano, watu wanafikia kugawana vipindi, walimu wanne wanagawana kipindi kimoja, yaani somo moja wakati kule hakuna watumishi, kwa sababu gani? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tumeambiwa kuna ajira karibu 32,000 zitatolewa, lakini zote zitaishia mjini, hazitakwenda huko vijijini. Naomba kama kulikuwa na nia njema ya kusema kwamba tusiwe na ukabila, tuwe tunaajiri *centrally*, mimi naona hiyo kuajiri kati na yenyewe imeshakuwa ni tatizo, turudi tutafakari. Kuna wakati tulikuwa tunaajiri kupitia Serikali zetu hizi za Mitaa, lakini wengine wakawa kwenye Serikali Kuu. Baadaye tukasema hapana, tuweke mfumo ambao utawezesha wote kulipwa vizuri, pengine umesaidia kidogo, lakini bado matatizo ni mengi. Hivi kweli hata dereva mpaka unataka umwajiri wapi sijui, tumeambiwa hapa kwamba wataangalia utaratibu vizuri. Naona kuna mambo mengine *tunaya-complicate* pasipo lazima. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hali ya mishahara kwa upande wa madereva ni duni sana. Hata madereva wa kwenye Wizara mishahara yao siyo mizuri. Wakati tunapigia kelele mishahara ya watumishi wengine, hao madereva wanakesha usiku kucha. Naomba nao waweze kusaidiwa, waweze nao kupanda mishahara angalau itakayowezesha kupata *pension* inayoweza kuwasaidia zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende katika suala la kuondoa umasikini na hapo naiangalia *TASAF*. Hii *TASAF* tulikoanzia imefanya kazi nzuri, lakini nadhani sasa hivi tuiangalie zaidi. Kwa mawazo yangu ya kufikirika, nilifikiria kwamba pengine tuwachukulie hawa wanafunzi wanaohitimu, kwa mfano, hata ada walilipiwa, wanatakiwa sasa kwenda kufanya kazi, ajira hakuna. Kwa nini hili kundi la *TASAF* tusiliangalie upya katika kundi hili ambalo halina ajira na lina elimu tayari ya kuweza kufanya kazi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nafikiria kwamba wanapomaliza kwa mfano JKT kwa wale walioenda, au ambao hawajaenda; pengine tungewatawanya moja kwa moja kwenye maeneo ambayo wanaweza kutoa huduma, lakini wapangiwe angalau fedha ya kuweza kujikimu wakati wakipata zoezi hilo la kufanya kazi na wakati huo huo ikawa wanachangia katika kutoa huduma na kupata uzoefu ili baadaye waweze hata kama ni kujajiri wenyewe au kuajiriwa lakini angalau wanakuwa wamekaa hapo kwa muda fulani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kama kutakuwa na mfumo rasmi wa kutoa hizo ajira za muda, hasa katika Halmashauri zile ambazo mimi nasema kwamba ni za Ki-*TASAF*, maana yake kuna Halmashauri hazina mapato ya kutosha na zenyewe ziingie tu kwenye mfumo wa *TASAF*, ziweze kupewa huo msaada wa watumishi hata hao wa muda waweze kusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, katika kufanya hivyo, naamini kwamba itasaidia hata kuibua mambo mbalimbali yanayowezesha kutoa ajira zaidi. Kwa mfano, kutengeneza vikundi vya kuweza kutoa ajira katika hao wahitimu wa vyuo mbalimbali. Naona pamoja na kwamba tunasema kuna ajira binafsi, lakini ajira hizo binafsi hazijawa na mvuto. Hazijawekewa mfumo ambao unawasaidia. Hata Mungu akibariki, watu wamechangia hapa, pengine mama ikupendeze kutufikiria, watumishi; na hao je? Itawapendeza katika mfumo gani? Watasaidiwa katika mfumo gani? Angalau sisi tuko ndani, tunapata hizo kidogo tulizonazo, hao hawana kabisa na ndio kundi kubwa. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu mtu ambaye ameelimika, akiamua kuingia kwenye uhalifu anaweza hata kutumia *integration* katika kufanya uhalifu wake. Anajua hesabu zote, naye anaweza kujua kwamba atapata nini? Kwa hiyo, ni mambo ya hatari kuliacha hili kundi kubwa bila kuwa na hali halisi ya kulisaidia ili liweze kuajirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nasisitiza hayo na nikiomba kwamba rasilimali za Taifa hili siyo la kikundi cha watu au watu wachache. Rasilimali za nchi hii lazima zitumike kwa kadri inavyowezekana, kwa watu wote, kwa usawa unaostahili. Haiwezekani! Kwani mimi kuzaliwa kule kijijini kwangu ndiyo imekuwa nongwa? Nami nifikiriwe, watu wa maeneo ya vijijini wafikiriwe, wasaidiwe, wapunguziwe mateso yaliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama tulivyoanza katika masuala ya Vituo vya Afya, shule, twende zaidi, kuwe na fedha maalum ya kusaidia kuibua mambo mbalimbali ya kiuchumi maeneo hayo ili kuongeza ajira na utumishi ulio rasmi na usio rasmi. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, jia ndae Mheshimiwa Ally Kassinge, atafuatiwa na Mheshimiwa Isack Kamwele.

MHE. KILUMBE S. NG'ENDA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye bajeti ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. Kwanza kabisa napenda nichukue nafasi hii kwa dhati kabisa ya moyo wangu kumpongeza na kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mama yetu kipenzi, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayoifanya kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumza utawala bora. Kwa kadri tulivyofundishwa utawala bora una misingi

yake. Msingi wa kwanza wa utawala bora ni utawala wa sheria na hii ndiyo nyumba ya kutengeneza sheria, humu tulimo. Msingi wa pili wa utawala bora ni kuheshimu haki za binadamu, msingi mwingine ni mgawanyo wa madaraka (*check and balance*). Sasa mimi nilitaka angalau nipite kidogo kwanza katika kulitazama suala la utawala bora na hasa katika siku za karibuni tangu Rais wetu ameanza kazi rasmi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue nafasi hii kusema kwamba yalikuwepo mambo ambayo katika utendaji wa kawaida, wengi tulikuwa tunayalalamikia na tulikuwa tunataka yatazamwe; nayo ni haki za binadamu hasa katika suala zima la mtu kushtakiwa na *process* nzima ya mashtaka yake na hata kufikia Mahakama kutoa maamuzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nafasi hii, napenda kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ameonessa nia kubwa ya kusimamia misingi ya utawala bora. Inawezekana tukawa ni watu tunaosahau kwa haraka, lakini wapo watu walikuwa wamekaa rumande kwa makosa mbalimbali kwa muda wa miaka mitano, sita hadi miaka saba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais huyu amekuja kusema hapana, haiwezekani, huu siyo msingi wa utawala bora. Amefika mahali ametaka upande wa mashtaka uangalie kama watu hawa hakuna ushahidi wa kutosha waruhusiwe wawe huru. Wamekuwa huru wakiwemo viongozi wa madhehebu ya dini, wafanyabiashara na wananchi mbalimbali. Hata wale waliokuwa wamefunguliwa mashtaka, wengine wamefika mahali wamesema, wayatazame hayo mashtaka na upande wa mashtaka ukajiridhisha kwamba baadhi ya watu wanaweza wakafika mahali wakaachiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wanasiasa wako walionufaika kutokana na uamuzi huo wa Serikali, akiwemo Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo,

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe. Napenda wenzangu tuisahau mambo haya mema yanayofanywa katika kuimarisha misingi ya utawala bora. Nami hapa napenda niendeleo kuwatia shime Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu wa Wizara hii, najua ni watu wazuri, wachapakazi wazuri, lakini endeleeni kusimamia misingi hii ya utawala bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka ieleweke vizuri kwamba jukumu mlilopewa la utawala bora linakwenda zaidi ya Wizara yenu, kwa sababu mambo yanayohusu utawala bora mengine yanafanywa hata na Wizara ambayo siyo Wizara ya Utumishi na Utawala Bora. Ukienda Wizara ya Mambo ya Ndani, wanasimamia mambo mengi sana ya utawala bora; na huko mkiacha, watachafua sifa ya Wizara yenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru niliwahi kumsikia mzee wetu Mheshimiwa George Huruma Mkuchika akiwa Waziri wa Wizara hiyo, siku moja akiwaambia Wakuu wa Wilaya kwamba jamani, mnapofika mahali mkaanza, nitakuweka ndani, nitakuweka ndani, mkamate mweke ndani, hamchafui *image* ya Wizara nyingine, mnachafua ya Wizara yangu mimi ya Utawala Bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, nawajua ninyi ni watu mahiri, watu wasikivu, watu wanyenyekevu na marafiki wakubwa wa wananchi na Wabunge, nawaomba sana muwe na wivu mnapoona Wizara nyingine katika kutekeleza majukumu yake inakiuka misingi ya utawala bora. Usifike mahali mkakaa kimya mkasema haya yako kwenye Wizara nyingine. Wawe ni Ma-DC wawe ni Ma-RC wawe Watendaji wa Kata, sijui wa vijiji, wakikosea misingi ya utawala bora, wanachafua *image* ya Wizara yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka tunacho chombo hapa cha Kupambana na Kuzuia Rushwa (PCCB). Chombo hiki kimeendelea kufanya kazi yake vizuri ingawa sisi wenyewe ndio tunakikamata mikono na miguu ya kufanya

kazi. Tuliongeza makosa ya rushwa kutoka makosa saba mpaka kufikia 24, lakini katika makosa yote hayo ni kosa moja tu ndilo ambalo Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa inaruhusiwa kulipeleka moja kwa moja Mahakamani. Makosa mengine yote ni lazima wapeleke Ofisi ya Mashtaka, yaende kwa *DPP*, ndiyo yapate kibali kwenda Mahakamani. Huku ni kuwashika miguu na mikono Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri wakati sasa umefika, mje hapa na Miswada ya Sheria inayowaongezea nguvu *PCCB* kufanya *prosecution* ya kesi zao nyingine za makosa ya rushwa Mahakamani moja kwa moja. Kwa mfano, leo tuna matumizi ya nyaraka kwa udanganyifu, yaani wapo watu ambao wanafanya manunuzi, wanatoa risiti feki, wanaziweka katika matumizi ya Serikali na wanachukua fedha nyingi ya Serikali. Hili ni moja ya kosa, lakini *PCCB* hata wakimkamata mtu huyu ni lazima wapeleke kwenye Ofisi ya Mashtaka ya Serikali ili iende kwa *DPP* kupata kibali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la ufujaji na ubadhirifu...

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Taarifa.

T A A R I F A

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa anayechangia kwamba kwa mujibu wa Kifungu cha 22 cha Sheria ya *National Prosecution Service Act*, Sura ya 430, Mkurugenzi wa Mashtaka ameendelea kuwateua Maafisa wote wenye sifa ndani ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kuendesha mashtaka pale anapoonana inafaa; na amekuwa akifanya hivyo kila mwaka.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Ng'enda, unaipokea taarifa?

MHE. KILUMBE S. NG'ENDA: Mheshimiwa Naibu Spika, nimeipokea na ninadhani inaboresha mchango wangu. Nataka madaraka hayo ya *DPP* yaondoke ili hawa watu wa *PCCB* waweze kwenda moja kwa moja. Ni nzuri na ninashukuru kwamba hiyo ni hatua muhimu, lakini tunataka madaraka haya, mpaka upeleke kwa *DPP* au *DPP* ndio amteue, hapana. Tufike mahali *PCCB* iwe na uwezo wa kukamata na kupeleka Mahakamani moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya hilo, kuna matumizi mabaya ya madaraka na yamefika mahali yanahujumu uchumi wa Taifa letu kwa kiasi kikubwa sana. Wapo watu wamefika mahali wanatumia vibaya madaraka katika kutoa *tender* na vitu vingine. Unaangalia rushwa ya mtu kupokea na kutoa, lakini hii ndiyo rushwa mbaya zaidi. Rushwa nyingine zimefika mahali majengo yanajengwa chini ya kiwango. Tuwaruhusu *PCCB* na tuwaongezee nguvu; na ikiwezekana tuwaongezee vile vile wataalam, maana sasa hivi unakuta mtu wa kufanya *valuation* ya majengo yuko Makao Mkuu. *PCCB* Kigoma wakiwa na tatizo, wamwombe kutoka Makao Makuu. Tuwaongezee nguvu ili ikiwezekana watu hawa wapatikane katika maeneo ya Mikoa na waweze kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ambalo nataka kulizungumzia ni suala la utumishi; upandishaji wa madaraja watumishi. Naomba sana Mheshimiwa Waziri, hebu angalieni kwenye Halmashauri zetu, kumekuwa na matatizo makubwa. Maafisa Utumishi wetu kwenye Halmashauri wanafika mahali hawawapendekezi baadhi ya watumishi wenye haki ya kupandishwa madaraja. Inatokea hivi na inafika mahali mpaka mnakwenda mwaka wa fedha umempita; na wanafanya hivyo wakati mwingine kwa hila; wakati mwingine mpaka watazamwe tazamwe ndiyo waweze kuwapendek0eza. Kwa hiyo, wapo watumishi wenye haki ya kupandishwa madaraja ambao hawapandishwi kwa

sababu tu Maafisa Utumishi kwenye Halmashauri hizo hawatekelezi wajibu wao ipasavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, jiandae Mheshimiwa *Engineer* Kamwelwe, jiandae Mheshimiwa Kakunda.

MHE. ALLY M. KASSINGE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu, lakini nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa juhudi ya kazi ambayo anaendelea kuifanya, na kubwa zaidi kwa kutuletea dada yetu mahiri katika Wizara hii ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; akisaidiana na mdogo wangu Mheshimiwa Ndejembu, ambaye ninamfahamu kikazi yuko vizuri na kwa maana hiyo, Wizara hii imepata watu wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza kuchangia nikumbushe waliopewa dhamana ya Wizara hii ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; kwamba, ofisi hii ni ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa kingereza *Public Service Management*. Kwa Kiswahili fasaha kabisa hii *management* ni usimamizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa masikitiko sana niseme kwamba, maeneo yafuatayo yanaharibu taswira ya ofisi hii au ya Wizara hii ya eneo lake la usimamizi, badala yake inaonekana kana kwamba, ni Wizara ya kuleta shida kwa watumishi wa umma. Nikianza nae neo la wanaopata nafasi za uteuzi wa Rais, maafisa wakuu ndani ya Serikali na maafisa waandamizi ndani ya Serikali; wanatekeleza majukumu yao mpaka pale mamlaka ya uteuzi inaposema basi, wakapumzishwa kwenye majukumu hayo, ofisi hii imeendelea kuwatelekeza kwa muda usiojulikana. Huu ni msiba mkubwa na inasikitisha sana. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais Kikatiba ana mamlaka ya kufanya uteuzi maeneo mbalimbali katika idara na taasisi mbalimbali ikiwemo kwenye majeshi, lakini ikiwemo hata humu Bungeni anateuwa humu Bungeni. Na pale ambapo uteuzi wa Rais unapokoma taasisi husika inawarudisha kwenye majukumu yao mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kama ingekuwa Waheshimiwa Wabunge wanaopata bahati ya kuteuliwa na Rais kuwa Mawaziri au Manaibu Waziri na pale ambapo utumishi wao wa uwaziri au unaibu Waziri unakoma ikaonekana kwamba, na Ubunge wao umekoma hapo ingekuwa msiba mkubwa, lakini kwa utumishi wa umma imekuwa ni kinyume chake. Utumishi wao wa uteuzi unapokoma wamebaki wakitelekezwa kwa muda usiojulikana. Nalizungumza hili kwa masikitiko makubwa na ionekane sasa kupitia Bunge hili mabadiliko na marekebisho na maboresho yafanyike katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais alipofanya mabadiliko katika kada za wakurugenzi, watendaji wa Halmashauri, makatibu tawala wa wilaya kwa maana ya *ma-DAS*, pamoja na wakuu wa wilaya, wateule hawa walioachwa kwenye majukumu yao wapo ambao wamekaa bila majukumu yoyote kwa miezi mitatu, wengine miezi mitano, wengine miezi nane, wengine miezi tisa. Sasa kiutumishi huku kupumzishwa kwao kwa miezi mitatu, minne, mitano, mpaka tis ani nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kanuni za utumishi wa umma za mwaka 2003, kanuni ya 96 na ya 97, likizo inatajwa kama vile likizo ya mwaka, likizo ya uzazi, *sabbatical leave* na likizo nyinginezo. Sasa hawa waliokaa miezi tisa nje ya majukumu walikuwa kwenye likizo gani, watwambie?

Mheshimiwa Naibu Spika, na katika eneo hili nipongeze Mheshimiwa Dada yangu Mheshimiwa Jenista alivyoingia tu kwenye ofisi ameanza kushughulikia tatizo hili. Na ninayo amani kupata taarifa kwamba, watumishi wote

sasahivi wamerudi kwenye majukumu yao ikiwemo wakurugenzi, ma-DAS, pamoja na wakuu wa wilaya, lakini itakapofika wakati wa kupitisha mafungu hapa nitamuhitaji Mheshimiwa Waziri aje atoe maelezo hawa watumishi walikuwa kwenye likizo ipi na stahili zao ni zipi kwa muda wote ambao walikuwa nje ya utumishi wa umma? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo linaharibu taswira ya Wizara hii ni kucheleweshwa kwa mafao ya wastaafu pamoja na kucheleweshwa kwa kulipwa stahiki za wastaafu, gharama za kufungasha mizigo kwenda makwao. Vilevile wapo watumishi ambao wanastaafu kinyume na madaraja ambayo wanatakiwa wastaafie na kwa maana hiyo, wanakuwa wanaidai Serikali mapunjo. Mbaya zaidi unalipwa kwa mshahara wa nyuma kuliko ule ambao walitakiwa staafie. (*Makofi*).

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nachangia bajeti mwaka jana nilieleza kilio cha walimu wangu wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa, nilitaja wachache kwa uwakilishi wa wengine, na ninarudia tena kuwataja. Walimu hawani pamoja na Hadija Nasoro Bungurumo, Salima Khamis Kaisi, Omari Ahamadi Mcheluya. Watumishi hawa wamestaafu tangu mwaka 2020 bado pamoja na kuwasemea hapa hawajalipwa mafao yao ya kufungasha mizigo, hawajalipwa tofauti zao za mshahara, kwa maana ya mapunjo ya malimbikizo au *arrears*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaamini Serikali yangu ya Chama Cha Mapinduzi ni Serikali Sikivu ni Serikali makini. Inakuwaje wanyonge hawa tunawasemea hapa Bungeni halafu Serikali haichukui hatua? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, matarajio yangu hii itakuwa ni mara ya mwisho ya kuwasemea watumishi hawa. Kwa umahiri wako Mheshimiwa Waziri uliyepewa dhamana...

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Taarifa.

T A A R I F A

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nilitaka nimpe Taarifa mzungumzaji kwamba, sio wastaafu tu ndio hawapewi fedha za kufungasha na kwenda, bali hata ambao bado wanaendelea na kazi wanaohamishwa kituo kimoja kwenda kingine hawalipwi, wanaweza wakahamishwa hata vituo vitatu bila kulipwa mpaka wanastaafu hawajalipwa hizo hela ambazo walikuwa wanahamishwa wakati wakiendelea kufanya kazi. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ally, Taarifa unaipokea?

MHE. ALLY M. KASSINGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nimeipokea. Na ni maeneo ya kurekebisha katika Ofisi hii ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala lingine ni kuchelewa kufanyika kwa maamuzi kwa watumishi wenye mashauri ya kinidhamu. Ukiangalia sheria na kanuni za utumishi wa umma, ndani ya miezi mitatu inatakiwa mashauri ya kinidhamu yawe yamehitimishwa, mtumishi awe amejua kwamba, anayo hatia na kwa maana hiyo atatumikia adhabu yake au hana hatia, atarudishwa kwenye majukumu yake. Lakini kwa masikitiko makubwa niseme tu kwamba, wapo baadhi ya watumishi wamekaa zaidi ya mwaka mashauri yao ya kinidhamu hayajaamuliwa. Sasa hii ni kinyume kabisa na sheria ambazo tunazitunga hapahapa Bungeni na Serikali ina jukumu la kuzisimamia sheria hizi. Kama tunazitunga na Serikali ndio msimamizi tunatagemea nani akazisimamie? Nani atatoa haki kama si Serikali ambayo ndio inaleta miswada ya kurekebisha au kutunga sheria hapa Bungeni? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe taarifa tu kwamba, kuna walimu 48 Tanzania Bara waliombewa kibali cha kurudi kazini tangu mwezi Juni, 2021. Narudia, walimu 48 wameombewa kibali cha kurudi kazini baada ya mashauri

yao kuwa yamehitimishwa tangu mwezi Juni mwaka 2021 lakini mpaka leo mashauri haya yako kwenye ofisi hii ambayo bajeti yake tunaendelea kuijadili. Niombe, mtakapochukua hatua za kuwarudisha kazini watumishi hawa kwa upungufu mkubwa wa watumishi, hasa kada ya walimu tulionao, hawa waleteni Kilwa, mimi nitawapokea. Narudia, waleteni Kilwa tukawapangie majukumu tuna upungufu mkubwa wa walimu kule wakatummikie Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho ni kuhusu motisha kwa kada ya walimu. Walimu, hebu tuangalie ugumu na uzito wa majukumu yao; katika hali ya kawaida inaonekana kama walimu kazi yao kubwa ni kufundisha tu, lakini hapana, walimu hawa kwanza ni walezi wa watoto wetu. Hata pale ambapo watoto wameshindikana kule kwa walimu watoto wananyoosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni nani hajapitia mikononi mwa walimu katika Bunge hili? Hakuna; lakini walimu hawa tumewakumbuka kwa utaratibu gani katika motisha?

Mheshimiwa Naibu Spika, kada zingine wana *allowance* kulingana na majukumu na uzito wa kazi zao kama vile *responsibility allowance*, *on call allowance* pamoja na *rational allowance*. Sasa hawa walimu ambao wanatumia muda wa ziada kuandaa masomo, kuandaa *scheme of service* ya muhula mzima au mwaka mzima na shughuli hizi wanazifanya nyumbani. Kama ni mama anaacha baba amelala yeye anaandaa *scheme of work*, kama ni baba anaacha mama amelala yeye anaandaa *scheme of work*. Tunachukua hatua gani za kufikiria kuwapa motisha hawa walimu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna kuandaa *lesson plan*, nje kabisa ya ufundishaji wenyewe. Baada ya hapo unaandaa *lesson notice*, baada ya hapo unaanza kumfuatilia mwanafunzi mmoja baada ya mwingine. Hebu tufike mahali tupime majukumu mazito ya kazi ya walimu wetu hawa ambao kwa uzalendo mkubwa wanaitumikia nchi yetu na ndio zao la sisi sote na kwa maana hiyo, tuwakumbuke

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

katika motisha. Kama madaktari na sekta ya afya wanapata *on call allowance* wanapofanya kazi ya ziada...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Ahsante. *(Makofi)*

MHE. ALLY M. KASSINGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa muda. Na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kamwelwe, Mheshimiwa Kakunda, Mheshimiwa Aloyce Andrew Kwezi wajiaandae, na tutamalizia na Mheshimiwa Benaya Kapinga.

MHE. ENG. ISACK A. KAMWELWE: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii ya Utumishi na Utawala Bora. Samahani nina kikohozi kwa hiyo, sauti yangu sio nzuri sana, lakini nitajitahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kuendelea kujalia amani nchi yetu, lakini ameendelea kutupa pumzi Watanzania na Wabunge ili tuendeleo kutekeleza majukumu yetu ya kibunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipongeze sana viongozi wa Wizara hii, nikianza na Mheshimiwa Waziri Jenista Mhagama, Naibu wake Mheshimiwa Deo Ndejemi, Makatibu Wakuu wakiongozwa na Ndugu Ndumbaro pamoja na watendaji wote. Wizara hii ni Wizara inachunga watu, Ndugu Ndumbaro ni mtaratibu na ni mtu mwenye hekima na anaishi kwa utaratibu na yuko makini sana. Kumchunga binadamu inabidi uwe na akili ya ziada kwa hiyo, nawapa hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze sana Wizara hii kwa hotuba nzuri, hotuba makini na imechambua vizuri kuhusu masuala ya utumishi. Misingi ya uongozi wa nchi yetu

ililetwa na waasisi wa nchi hii akiwemo baba wa Taifa, Hayati Julius Kambarage Nyerere pamoja na Mzee Karume. Walitoa matamshi yao ya uongozi kwamba, ili nchi hii iweze kuendelea inahitaji ardhi, watu, siasa safi na uongozi bora. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, uongozi bora tunauona kwa Rais wetu mpendwa. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Awamu ya Sita, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, katikati ya bajeti ya 2021/2022 alifanya jitihada za kutafuta fedha Shilingi trilioni 1.3. Baada ya kuileta fedha ile akaipeleka Kamati ya Bajeti, Kamati ya Bajeti wakaona hii sio *size* ya Waziri wa Fedha aliyezoea kupanua vifungu, hii hela ni ya kupanua ukomo wa bajeti. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha ililetwa hapa na Wabunge tukapitisha kwa hiyo, sheria hapo ukiangalia utawala bora umetekelezwa. Fedha, bajeti ikaongezeka kutoka trilioni 36 mpaka trilioni 37.94 tunampongeza sana Mheshimiwa Rais. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sasa angalia miongozo ambayo imetolewa na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, bajeti yam waka huu wa fedha 2021/2022 makusanyo ya ndani walikuwa wamepanga kukusanya Shilingi trilioni 17. Hadi *quarter* ya tatu TRA walishakusanya trilioni 16. Na kwa ukusanyaji huu wa trilioni 1.84 kwa mwezi ina maana kwamba malengo yatafikiwa na yatapitwa, haijawahi kutokea ni kwa mara ya kwanza tutaona kwamba bajeti inakusanywa kwa asilimia 100. Nampa hongera sana Mheshimiwa Rais. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na changamoto za kiuchumi wa dunia zinazoendelea bado Mheshimiwa Rais ameendelea kupambana kupanua vyanzo vya mapato. Ni hapa juzi tu mnaona jinsi ambavyo anaongoza suala la kampeni ya masuala ya utalii kupitia *Royal Tour*. Matokeo yake unaona bajeti tunayojadili leo ya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mwaka ujao wa fedha sasa tutaingia kwenye Shilingi trilioni 41. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizi zilizotolewa za Uvico na mimi nishukuru kwamba, jimbo langu lilipata 3,467,110,000 lakini zimefanya nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, zimejenga madarasa ya sekondari pamoja na madarasa ya shule shikizi. Kwa upande wa nchi nzima fedha hizi zimejenga zahanati na kujenga vituo vya afya na hospitali za wilaya. Maana yake ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba, *activities* zimepanuka. *Activities* zikipanuka maana yake zinahitaji watumishi, lakini kutokana na kazi aliyoifanya Mheshimiwa Rais wetu kwamba, ameongeza fedha mpaka za kuajiri. Niipongeze sana hii Wizara kwa kuajiri kwa kuweka mpango. Kwanza wameshatangaza nafasi za kuajiri watu elfu 11, lakini na sasa wataajiri nafasi za watu elfu 32; na Mheshimiwa Waziri ametuonesha maoteo ya mwaka ujao pengine wa fedha, wanaweza wakatangaza tena nafasi elfu 30. Hongera sana, kweli hapa tunaona siasa safi na uongozi bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wenzangu wamesimama kila mtu akasema kwake kuna upungufu kiasi gani wa wawatumishi. Mimi katika Halmashauri yangu ya Mlele nina upungufu wa watumishi 915. Kati ya hao walimu ni 149, lakini wahudumu wa afya ni 546, watendaji wa vijiji 8, lakini kada nyingine ni wahasibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasahivi tutakwenda kujadili ripoti ya *CAG* na mimi ni Mjumbe wa Kamati ya *PAC*. Wakati mwingine hizi hati zenye mashaka na hati chafu zinaletwa kwa sababu ya watu kutokuwa na weledi. Niombe sana na kushauri, kwamba hii kada ya wahasibu na hasa wahasibu wenye *CPA*, wenye *degree* pamoja na hizi diploma; na kwa sababu, kwenye bajeti kumewekwa fedha za *skill development* hawa wakifanyiwa semina nzuri nina hakika kabisa kwamba, hizi hati chafu na hati zenye mashaka zitapungua. Na zinapopungua ndivyo tunavyompa moyo

zaidi Mheshimiwa Rais wetu, ili aweze kutekeleza majukumu yake kwa furaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kutokana na hali yangu ya sauti hii, sikupanga kuongea mengi, lakini nimalizie tu kwa kusema kwamba, naunga mkono hoja. Nashukuru sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Joseph Kakunda, jandae Mheshimiwa Aloyce Kwezi na tutamalizia na Mheshimiwa Kapinga.

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwanza nianze na pongezi, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo anatomia mbinu mbadala kuitangaza nchi huko duniani na kutuletea faida kubwa sana Watanzania. Na hivi karibuni tu mtaanza kuona faida ya ile *Royal Tour* ambayo imezinduliwa wiki iliyopita kule marekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili nimpongeze sana Waziri na timu yake kwa jinsi ambavyo amewasilisha vizuri hotuba yake hapa Bungeni, lakini vilevile kwa namna walivyojipanga kuboresha mambo mbalimbali katika utumishi wa umma na utawala bora. Kwenye hotuba tunaambiwa hapa kwamba, Serikali itaboresha upimaji wa utendaji, lakini vilevile wanaanzisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ambao utaunganisha watekelezaji wote kuanzia Serikali za Mitaa mpaka Serikali Kuu. Hapo kwa kweli, nawapongeza sana, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi mchango wangu umejikita hasa kwenye maeneo matatu, mawili hasa. Katika kupima utendaji tunapima nini? Na katika ufuatiliaji na tathmini tunafuatilia nini? Na tunatathmini nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo mengi sana ambayo yanafanyika katika hayo maeneo mawili lakini kwa muhtasari unaweza ukayachanganya changanya ukaweka katika sehemu tatu kubwa.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya kwanza tunapima uelewa au kwa Kiingereza wanaita *clarity*, uelewa wa nini, tunapima uelewa wa sera, uelewa wa sheria, uelewa wa kanuni, uelewa wa miongozo mbalimbali inayotolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama watumishi wanaelewa vizuri Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu, Miongozo tunategemea kwamba wasikosee, tunategemea kwamba akija mkaguzi yoyote akute kila kitu kiko vizuri. Sasa kama uelewa uko chini basi tiba yake ni mafunzo kazini, kwa nini? Inawezekana huyu mtu alikuwa anaelewa sera zamani, alikuwa anaelewa sheria, anaelewa kanuni, anaelewa taratibu lakini kuna wakati anasahau. Kwa hiyo ni muhimu kumkumbusha kupitia mafunzo kazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ni kweli kwamba kila Wizara, kila Taasisi itakuwa na bajeti yake ya mafunzo, bajeti hiyo ni kubwa kiasi gani na itatoa itatoa mafunzo gani, hii Wizara ndiyo inatakiwa iratibu. Wizara hii inatakiwa iratibu mafunzo yote yanayofanyika huko kwenye Wizara mbalimbali na Taasisi mbalimbali ili kuhakikisha kwamba watumishi wanauelewa wa kutosha wa nini wanatakiwa kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaenda sehemu ya pili nikumbushe mafunzo umuhimu wake, wale watu wa dini wanajua kwamba Bibilia iliretemka zamani sana Quran iliteremka zamani sana, lakini karibu kila siku watu wanakumbushwa maandiko ya dini, vilevile hata Serikali inatakiwa lazima kukumbushana masuala hayo ambayo nimeyatamka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili ni mazingira wezeshi ya kazi au waingereza wanasema *conducive environment*. Kuna vipengele vitatu hapo, kipengele cha kwanza kabisa ni rasilimali fedha. Hapa Bungeni tunapitisha bajeti kwenye Wizara mbalimbali, kwenye Taasisi mbalimbali, kwenye Idara mbalimbali tunapitisha bajeti hapa, lakini ni kiasi gani bajeti ile inateremka kwa watekelezaji inatakiwa ipimwe. Sasa hiyo kwenye ufuatiliaji na tathmini hiyo ni lazima

iwe mada kubwa kabisa katika kazi, fedha imeenda kiasi gani, imepokelewa lini imetumikaje, imetumika kwenye kazi gani? Kuna ufanisi gani umepatikana? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili ni rasilimali watu. Kama hatuna rasilimali watu wa kutosha kwa maana ya idadi ya watumishi inayojitosheliza tusitegemee ufanisi wa kazi. Kwa hiyo, eneo hili nalo lazima lifuatiliwe vizuri na lipimwe. Kwa mfano, katika Jiji la Dar es Salaam Jiji ambalo linaongoza kwa ulipaji wa kodi hapa nchini, kama *TRA* pale Dar es Salaam wanahitaji watumishi 1,500 halafu kwa sasa hivi wako 700 ina maana ni chini ya 50% usitegemee ufanisi mzuri wa *TRA*. Ndiyo maana juzi wameongeza watumishi 300 kwa ajili ya Kariakoo tu peke yake, hili suala la idadi ya watumishi ni la muhimu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu la Sikonge nina vijiji 71, katika vijiji 71 nina *VEO* ambao ni *substantive*, ambao wameajiriwa Serikalini ni *VEO* 30, ina maana sina *VEO* 41! Unategemeaje ufanisi wa kazi kwenye Serikali za Mitaa namna hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu mwezi Agosti, mwaka jana Halmashauri yangu imeomba kibali Utumishi cha kuajiri watumishi 821 hadi leo hatujapata kibali hata cha mtumishi mmoja ukiacha wale wengine ambao wanakuja kupitia Wizara zingine, kupitia TAMISEMI, kupitia Afya na kupitia Wizara zingine. Tumeomba watumishi 821 hatujapata hata mmoja. Kwa hiyo, ufanisi wetu kwa kweli huwezi kuupima vizuri kama tuna shida ya watumishi namna hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipengele cha tatu tunapima uwepo na matumizi ya vitendeakazi *working gear*, vifaa gani vinahitajika ili watumishi waweze kufanyakazi kwa ufanisi. Kwa hiyo, Wizara hii tunaitegemea ifuatilie na kipengele hiki, vifaa gani vitendea kazi gani vinahitajika ili watumishi wafanye kazi zao kwa ufanisi, kama tunategemea ufanisi mzuri ni muhimu kipengele hiki kiwekewe nukta na Waziri Mheshimiwa Jenista Mhagama. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tatu ambayo tunaipima ni umahiri au weledi wa kazi (*competence*). Najua hiyo kengele ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, *competence* huwa hatuipimi kwa idadi ya vyeti alivyonavyo mtumishi. Unaweza ukakuta mtu ana-*PhD* lakini anashindwa weledi wa kazi na mtu ambaye ana cheti. Kwa hiyo, weledi wa kazi tunaupima kwa namna mtu ambavyo anatumiza majukumu yake ndani ya wakati halafu ana ripoti matokeo ya kazi yake, anayaripoti kwa mkubwa wake ndani ya kabla hajaulizwa, huyo ndiyo anafanyakazi zake kwa weledi. Lakini mtu ambaye kila siku ni wa kusukuma Sukuma, mtu ambaye kila siku lazima aulizwe ndiyo atoe taarifa, huyo siyo mweledi kwenye kazi. Kwa hiyo, tunapompima mtumishi kama ana weledi wa kutosha kwenye kazi tunapima je anaipenda kazi yake? *Positive attitude* kwenye kazi, lakini kinyume chake hapo sasa kuna utoro, kuna uzembe na mengine mengi sana. Kwa hiyo *competence* hujengwa zaidi na mambo yale mawili ya kwanza niliyoyataja yaani uelewa pamoja na mazingira wezeshi, kama uelewa na mazingira wezeshi ni duni huwezi kutegemea watumishi wawe mahiri kwenye kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ndiyo misingi mikuu ya kupima utendaji na vilevile kupima kama kweli tunafuatilia vizuri taasisi zetu na kama tunafuatilia Serikali vizuri. Tumeshauri mara nyingi lakini mimi leo nimefarijika sana hapa, kwa jinsi ambavyo Waziri ametamka hapa Bungeni kwamba sasa Serikali inaenda kuandaa mfumo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathmini, hii kitu namna hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Sasa Mheshimiwa Aloyce Kwezi, jiandae Mheshimiwa Kapinga.

MHE. ALOYCE A. KWEZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nami naomba niwe ni miongoni mwa wale watu ambao wanatoa pongezi kwa Serikali yetu ya Chama cha

Mapinduzi, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mheshimiwa Jenista Mhagama, nampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri Ndugu yangu Deo na nisisahau timu nzima inayoongozwa na Katibu Mkuu wa Utumishi Dkt. Ndumbaro. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa kuchangia lakini nianze kuwasilisha kero ambazo wananchi na watumishi wa Jimbo la Kaliua wamenituma. Awali ya yote wamenituma nianze kwa kuwashukuru sana Wizara hii ya Utumishi kwa kuanza kulipa malimbikizo ya mishahara kwa kiwango kikubwa sana. Tunawashukuru sana kwa kweli kwa mwezi Februari peke yake watumishi wa Jimbo la Kaliua mmelipa milioni 400. Pia mmelipa baadhi ya fedha ya uhamisho, nilikuwa napenda nikumbushe hapo Serikali yangu sikivu kwamba Halmashauri ya Kaliua pesa ambazo tunadai *arrears* pamoja na madai mengine ya utumishi yanafika shilingi bilioni 1.3.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba tuangalie jinsi gani tunavyokwenda tulipe awamu kwa awamu ili wale watumishi wawe na mazingira mazuri sana ya kufanyakazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nakuja na ushauri na ushauri wangu nataka kidogo tuelewane sehemu moja na kwenda ku-*challenge* sehemu ya *harmony*. Ninawashauri wa-*harmonize scheme* kwa maana ya kwamba tofauti ya mishahara kati ya Serikali Kuu, Serikali za Mitaa pamoja na Taasisi za Serikali. Mishahara ya Taasisi imekuwa ni mikubwa sana tofauti kabisa na mishahara ya watumishi wa Serikali Kuu au watumishi wa Serikali za Mitaa, sasa Wizara ambayo inaandaa hii *Scheme of Service* ni hii moja, hivi inakuwaje Afisa Utumishi au Mchumi aliyeko kwenye Halmashauri wanahudumia karibu watumishi 3000, 4,000 na huku wamesoma pengine miaka mitatu *Degree* yao, wanafanya kazi vizuri, inakuwaje mtu wa kwenye taasisi ambaye anasimamia watumishi 100 hawa wa Serikali Kuu na Halmashauri wanalipwa mishahara wanaanzia kima cha chini

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

cha 750,000 wale *graduate*, lakini wale wa taasisi kule wanakwenda kuanzia 2,000,000 na kidogo huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashauri hapa hebu fanyeni *job evaluation*, ukubwa wa majukumu, yaani mimi niongoze watumishi 100, nilipwe mshahara mara mbili ya huyu ambaye anaanza, tulisoma *UDSM* pamoja au Mzumbe au *whatever* na ninafanyakazi vizuri na pengine mimi niko kwenye mazingira magumu zaidi. Hiki kitu nawashauri mkiangalie kwa kina kwa sababu madhara yake ni makubwa sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watumishi wengi kutoka *Local Government* Halmashauri zetu wanakimbia kwenda kwenye Taasisi wakifuata keki nzuri. Hili jambo lazima tuwaambie vizuri kwa sababu tusipowashauri sisi tunakosea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kasinge alichangia vizuri pale nimemwelewa sana, alikuwa anagomba hii miundo kwa sababu huyo ni Afisa Utumishi zaidi ya miaka kumi, sasa haya tunayowaambia ndiyo ambayo tunayaona tunayaishi. Kwa hiyo, tunaomba mkiangalie jambo hili hii tofauti ya mishahara imekuwa ni kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo nilikuwa najjuliza hivi sasa hivi tunapoajiri tumeacha kufuata muundo wa utumishi wa umma? Kama tunafuata muundo wa utumishi wa umma nilikuwa najjuliza juzi juzi, mimi najua mtendaji wa kata kwa mfano anapoajiriwa utakuta pengine awe na Diploma au Shahada ya Maendeleo ya Jamii ya Fedha, Usimamizi wa Fedha, Utumishi, Mipango na mambo mengine. Lakini sasa hivi hapa katikati unachukua mtu ambaye kamaliza *Education* unamuweka Mtendaji wa Kata, Sekondari zetu huku ziko wazi hivi huu muundo! Nawaambia hili la wazi ndugu zangu sitaki kuwaficha, muundo tunaosimamia hapa nadhani mmeuboresha ni wa 2002 maboresho yakafanyika 2013 kwa wale *WEOs* hawa Watendaji wa Kata na Vijiji.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nilikuwa nashauri hivi tutawapandishaje vyeo hawa maana yake akitoka WEO II anategemea kwenda WEOI, au kwenda *Senior or whatever* huko mbele, sasa anapokwenda lazima kuna sifa zinakuwepo pale, hiki kitu ni nini? Nadhani hatu-*utilize resources* vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashauri muangalie mapema ili huko mbele tusije tukawekeana kelele zisizokuwa na sababu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nalishauri linahusiana na uhamisho. Utumishi wanapozunguka kwenye maeneo ya kwetu wanatuambia kwamba Mkurugenzi, Afisa Utumishi sijui taasisi gani, pitisha ila shauri kwamba lina upungufu wa hivi na hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, unakuta watumishi wanapoleta zile barua Mkurugenzi anapitisha anashauri kwamba nashauri hapa watumishi ni wachache, wakifika huku mna-*authorize* wanaondoka, sasa wanaondoka kwa wimbi kubwa matokeo yake Mjini ni wengi, Halmashauri zetu ziko hoi! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawaambia hili jambo ni la kweli. Muundo kwa mfano, Maendeleo ya Jamii kwenye Wilaya Ikama inataka pale Makao Makuu wawepo angalau wanne au watano. Jimbo la Kaliua Kata hata moja sina Maendeleo ya Jamii hata Mmoja, hawa wananchi wanaelimishwaje hebu niambieni? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kaliua ina Kata 28, hakuna Afisa Maendeleo ya Jamii kwenye Kata hata mmoja! Hii mikopo tunawafanyaje? Ni nani anahamasisha shughuli za maendeleo? Waje kwenye kamati hizi huku za LAAC sijui USEMI sijui wapi tunawabana, ooh! sijui nini, lakini Ikama huku kwa nini hatuifuati vizuri, kwa nini hatujaajiri vizuri huko?

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira nyingi Mheshimiwa Waziri zimekuwa zinakuja sasa hivi ni karibu mimi nasema ni

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ajira mbadala (*replacement*), ndiyo zimetoka nyingi lakini zile ajira zenyewe kwa mujibu wa Ikama mimi nina watumishi labda 2,000 lakini mahitaji yangu ni watumishi 4,000, hawa watumishi fuateni kutoka kwenye *source* kule, sisi ndiyo tunapata shida kule kwamba ukizunguka hapa Mganga Mkuu yuko wapi, ukizunguka hapa Mhudumu hamna, ukizunguka zahanati fulani ameenda kujifungua, miezi mitatu wananchi wa Kaliua wanahudumiwa na nani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa kulishauri na naliona ni la msingi sana mimi nilikuwa naomba mafunzo, hebu tufanye mafunzo kwa watumishi hasa wale waajiriwa wa mara ya kwanza. Nafasi zenu zile za uteuzi unamteua Mkurugenzi hajui hata *mail box* hajui kwamba inatakiwa itoke siku hiyo, anaanza kujifunza *folio* ni nini, anaanza kufanya hivi....

(*Hapa Mhe. Aloyce A. Kwelizi alionesha mfano*)

MHE. ALOYCE A. KWEZI: Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ni vitu gani? Hebu tuweke watu ambao ama wapelekeni mafunzo jamani kama zamani, wiki mbili, wiki tatu, akitoka kule anajua kwamba huyu Mkuu wa Wiaya ni mkubwa kwangu, huyu ni mdogo wangu, *chain of command* ikoje, haya ya shuleni ya moja kwa moja, haya yanakuja kufanya huku anaonekana anapwaya sasa, kwa sababu wale Wakuu wa Idara walioko pale wako imara kuliko Mkurugenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mmoja nawapa mfano wa kweli mimi sitaki kuwadanganya, kuna mmoja alipoambiwa yeye Mkurugenzi ni mamlaka ya uteuzi alichokifanya, kwanza akawaandikia Wakuu wa Idara wote anawatengua Vyeo! si mamlaka ya uteuzi? Kumbame sahau mamlaka ya uteuzi lazima a-*consider* Madiwani huko, alipopiga simu nikamwambia futa hizo barua haraka Mzee unatuaibisha, sijui mnanielewa? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hayo mambo mngekuwa mnawapa kozi haya yangetokea haya? Wanaingia mle wanafikiri wenyewe pengine ni wakubwa

hata kuliko Mwenyekiti wa Halmashauri, wakubwa kuliko *DC* lakini hawajui kwamba hii ni *chain* leo wa juu anaongea na wa chini vizuri, wa chini anaongea na hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kulishauri jambo moja kubwa sana, pale kwenye ule mlundikano wa vyeo, sasa hivi wanafurahi Watumishi wamepanda vyeo sana ni kweli, lakini ule mlundikano ambao umetokea sasa iko hivi, yaani Mtumishi ambaye alikuwa amepanda mara ya mwisho 2013 anakuja kupanda 2017 au 2018 anakutana na yule *junior* ambaye amekuja amefundisha kazi kakaa naye na nini, sasa hivi wote wako kwenye *class* moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashauri muangalie kama *possible* mnaweza mkarudi kwenye ule mfumo wa zamani kurekebisha hili tatizo kwa kutumia *accelerated promotion* kwamba, wewe hapa kwa kweli hata unajua na ingine ni aibu.

NAIBU SPIKA: Ahsante.

MHE. ALOYCE A. KWEZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunamalizia sasa na Mheshimiwa Benaya Kapinga.

MHE. BENAYA L. KAPINGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kufunga dimba siku ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote na mimi niungane na Wabunge wenzangu kuishukuru sana Serikali hii ya Awamu ya Sita kwa kazi nzuri inayoendelea kufanya katika nchi yetu. Ninamshukuru sana na nimpongeze Waziri Dada yangu Mheshimiwa Jenista Mhagama, amekuja muda mfupi katika Wizara hii lakini sasa hivi amejenga matumaini makubwa kwa watumishi. Watumishi wengi wanayo imani sana, ninamshukuru Naibu wake lakini nimshukuru pia Katibu Mkuu Dkt. Laurine Ndumbaro pamoja na Wasaidizi wake wanafanyakazi nzuri sana. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kuishukuru na kuipongeza Serikali kwa kibali kile cha ajira 32,000. Nina uhakika wamsema wenzangu hapa na hasa wale wa Majimbo ya vijijini na mimi natoka kijijini, hali yetu kule tunajua watumishi wako pungufu sana, tuna uhaba mkubwa sana wa watumishi. Nitolee mfano tu, iko shule ina Walimu Watatu na miongoni wao mmoja anaondoka, shule hiyo inabaki na Walimu Wawili. Kwa hiyo, nina uhakika sasa kwa kibali hiki cha watumishi 32,000 na mimi shule zangu kule zitapata watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia na zahanati zangu zitapata watumishi, lakini pia na hospitali itapata watumishi, naishukuru sana na ninaipongeza Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na Mheshimiwa Kasinge, nchi yetu inaongozwa kwa Katiba na Katiba hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetoa haki kwa Watanzania wote, haki ya kushiriki siasa, kwa maana ya kuchagua na kuchaguliwa, vilevile imetoa haki ya kufanya kazi na imetoa haki ya kuajiriwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2020 tulikuwa na Uchaguzi Mkuu katika nchi yetu, kuna Watumishi ambao walienda kushiriki kwenye uchaguzi ule, baadhi ya watumishi hawa walikuwa wateule wa Rais, kulikuwa na Wakuu wa Mikoa, kulikuwa na Wakuu wa Wilaya, lakini kulikuwa na watumishi wasiokuwa wanasiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Katiba hii hakuna raia wa Tanzania aliyezuiwa kushiriki siasa hakuna! Wananchi wote wameruhusiwa kwa mujibu wa Katiba hii kushiriki siasa. Kwa bahati mbaya sana mwaka ule wako wananchi raia wa nchi hii baada ya kuingia kwenye siasa walisitishwa haki yao ya kufanya kazi. Utaratibu ule haukubaliki kabisa kwa mujibu wa Katiba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Serikali hii ya Awamu ya Sita ilichukua hatua baada ya kusikia kilimo cha Wabunge wa Bunge hili kwamba utaratibu ule ulikuwa

siyo sahihi, watumishi wale wengi kama siyo wote wamarejeshwa kwenye nafasi na sasa wanaendelea na kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, uko Waraka wa mwaka 2014 unaosema uko wazi kabisa kwamba, mtumishi wa umma ataondolewa kwenye utumishi atakapoteuliwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwamba yeye ni nani sasa anashiriki uteuzi au uchaguzi wa katika maeneo yake ya siasa. Upo ule waraka umeeleza vizuri sana, lakini lililofanyika mwaka ule limeenda tofauti sana na waraka ule.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu kuchukua fomu tu alisitishiwa ajira, alisitishiwa kufanyakazi, tulikiuka sana Katiba hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, watumishi wale wamerudi, walirudi baada ya kukaa nje ya kazi kwa zaidi ya miezi wengine Saba, wengine Sita, wengine Nane. Mwendangu amehoji hapa wale watumishi walikuwa likizo ipi? Kwa sababu bado wana haki zao, kushiriki siasa hakumuondolei mtu haki ya kufanya kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nami naungana na mwenzangu Serikali kwa vile tayari tumewarudisha wale watumishi kazini, tunafahamu miezi kadhaa walikuwa hatuelewi kama walikuwa likizo au ilikuwa ni kitu gani lakini miezi kadhaa wana madai yao, kwa hiyo ningepomba maelezo yatolewe hapa na Serikali ule muda ulikuwa ni kitu gani. Nadhani kwa sababu Serikali hii sikivu na Mheshimiwa Jenista wewe ni msikivu utakuwa na majibu mazuri yanayoenda kuwatia moyo wale watumishi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni suala la hii *recategorization*. *Recategorization* ni kitu kizuri sana kina manufaa pande zote. Kina manufaa kwa mtumishi lakini kina manufaa pia kwa upande wa Serikali. Imekuwa hivyo vizuri inafanyika lakini kwa bahati mbaya sana kuna baadhi ya Taasisi inapofanyika hii *recategorization* ina wanyanyasa au inawaonea watumishi.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, mtumishi ameenda kusoma, mtumishi yuko kwenye nafasi fulani mahala Fulani, Taasisi inaona upungufu wa Idara Fulani, inamtoa mtumishi kutoka Idara aliyokuwa anafanyia kazi, anarudi kufanyakazi hapa kuimarisha ile Idara lakini mwisho wa siku anapunguzwa mshahara anakuja kuanza *as if* anaanza leo ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili siyo sahihi sijui, lakini ikibidi kama kwell mtumishi yule ameomba mwenyewe sawa, lakini sasa Idara au Taasisi inamhamisha kutoka Idara fulani inamrudisha hapa ili aendane na muundo wanamuondolea mshahara aanze tena upya! Ningependa Serikali itoe tamko hapa watumishi ambao Idara au Taasisi ndiyo iliyohitaji abadilishwe mfumo basi wale wasianze upya wasianze katika *level*/ile ya kwamba anaanza ajira, wahame na mishahara yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Waziri atakapokuja kusema hapa na mimi nitashika shilingi kama hiyo kauli sitaisikia. Kuna orodha ya watumishi wako hapa, wameondoka kwenye Idara fulani wamepelekwa kwenye Idara fulani wakaenda wakawashushia mishahara yao. Leo hii yule mtumishi alikuwa na mkopo, ana mkopo wa *Loan Board* anaenda kufanyakazi anarudi hana kitu kabisa! Si ndiyo tunafundisha watu kuiba hapa, tunafundisha watu ufisadi si ndiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Serikali tuliangalie hili, suala hili la *recategorization* ni zuri mno likifanyika na mtu akahama na kamshahara kake hivi nani anaumia? Hakuna kitu cha kuumia hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona niseme hili na nalisema kwa uchungu sana kwa sababu lina maumivu mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu nyingine ni ile ya uhakiki wa wale watumishi Darasa la Saba na hii naomba niliseme kwa upole. Ninatambua tuliwaondoa baadhi ya watumishi kwenye ajira, lakini ukienda kuwasakiliza baadhi ya

watumishi hao sababu inayoonekana kwamba wali-*forge* vyeti, baadhi ya watumishi hawa ni Walinzi, anakuambia kabisa mimi sikuwahi *sign* hicho kitu, mimi nimekikuta tu kwenye *file* yangu mimi sihusiki, ninaorodha ya watumishi 12 wana malalamiko hayo kwamba wao kama wao na ukiangalia zile *documents* zao unaona kabisa miandiko iko tofauti, sasa ni nani alibadilisha taarifa zile?

Ninaomba Serikali kwa unyenyekevu mkubwa na kwa sababu Rais wetu anasimamia haki na mara kadhaa amesema yeye ni mpenda haki, ningeomba sana kwa unyenyekevu mkubwa, tufanye uhakiki wa watumishi hawa, ikithibitika siyo basi warejeshwe kazini, yapo malalamiko ya wazi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante kwa mchango wako mzuri na kwa kweli umetumia dakika zako vizuri, umechangia *issue* moja tu, umeeleweka vizuri na naamini Serikali wamekuelewa. Hata juzi Mheshimiwa Anatropia alichangia habari ya ngozi tu, alijikita kwenye ngozi tu. Waheshimiwa Wabunge, utamkuta mtu stakabadhi ghalani yeye, korosho yeye, mbolea yeye, barabara yeye, kwa hiyo utakuta anajichanganya mwenyewe baadaye. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, Katibu wa Bunge ameomba niwatangazie kuwa kesho siku ya Ijumaa tarehe 22 kutakuwa na *Iftar* itakayoandaliwa na Benki ya *NMB* katika Viwanja vya Bunge eneo la maegesho ya magari jirani na kituo cha afya. Waheshimiwa Wabunge wote pamoja na Watumishi wa Bunge wanaombwa kuhudhuria *Iftar* hiyo itakayoanza Saa Kumi na Mbili Jioni.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hilo, naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho Saa Tatu Asubuhi.

(Saa 11.45 Jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 22 Aprili, 2022 Saa Tatu Asubuhi)